

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 14 Mei, 2019**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE. HAWA S. MANIFUNGA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

Taarifa ya Msemadi Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Kuhusu Wizara ya Viwanda na Biashara juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa. Katibu tuendelee.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Leah Jeremla Komanya, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swalii lake.

Na. 220

Mchakato wa *“Capital Development Grant Assessment”*

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza:-

Moja kati ya vigezo vya *“Capital Development Grant Assessment”* ni namna Halmashauri inavyoweza kutoa taarifa kwa wananchi juu ya mtiririko wa fedha ambazo Serikali imipeleka katika Halmashauri na miradi iliyokusudiwa kutekelezwa:-

(a) Je, kwa nini mchakato huo ulisitishwa?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kurejesha mchakato huo ambao utakuwa ukiongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali nchini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-**

Mheshimiwa mwenyekiti, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Leah Jeremia Komanya, Mbunge wa wa viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upimaji wa Halmashauri ulikuwa ni kigezo cha kuziwezesha Halmashauri kupata ruzuku ya maendeleo isiyo na masharti (*Local Government Development Grant*) kuanzia mwaka 2005. Miongoni mwa vigezo vilivyozingatiwa ni kuwepo kwa uwazi katika mapokezi na matumizi ya fedha kwenye ngazi ya Vijiji, Kata na Mitaa kwa kuhakikisha mapato na matumizi yanabandikwa kwenye mbao za matangazo. Mradi huo ulitekelezwa kuititia fedha za wafadhili ambapo Serikali pia ilikuwa na mchango katika fedha hizo. Mradi huo ulifikia ukomo mwaka 2013, baada ya wafadhalii kujitoa na Serikali kuendelea kutekeleza mradi huo kuanzia mwaka 2014/2015 na 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutoa ruzuku ya maendeleo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuziwezesha kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali zikiwemo afya na elimu. Wananchi wanachangia nguvu kazi na vifaa mbalimbali kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi hiyo. Serikali inakubaliana na wazo la kuzipima Halmashauri katika matumizi ya ruzuku hiyo inayotolewa na Serikali kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hilo liko kwenye mjadala ndani ya Serikali ili kuona namna bora ya kulitekeleza katika kuhakikisha kunakuwa na uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha zinazotolewa na Serikali kwenye Halmashauri hadi ngazi ya vijiji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leah Komanya, swalii la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nilikuwa na maswali madogo mawili ya nyongeza. Ni hatua zipo

zilizochukuliwa kwa Wakurugenzi walioshindwa kufikia malengo ya ukusanyaji mapato; kuchangia asilimia 40 katika miradi ya maendeleo; na kuchangia asilimia 10 kwa akina mama, watu wenye ulemavu na vijana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, katika nafasi za Wakuu wa Idara zilizo wazi Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha zinajazwa na watumishi wenye sifa za kuwa Wakuu wa Idara ili kuwepo na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za maendeleo ukizingatia Serikali inapeleka fedha nyingi sana katika miradi ya maendeleo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Leah Jeremia katika swali lake, anataka kujua ni hatua gani zimechukuliwa kwa Wakurugenzi na Watumishi wengine ambao wameshindwa kupeleka asilimia 40 na asilimia 10 kama ambavyo ndivyo ilivyo maelekezo ya Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba hata hivi karibuni Mheshimiwa Waziri wa Nchi alitoa taarifa ya tathmini ya makusanyo ya Halmashauri mbalimbali na Halmashauri ya kwanza mpaka za mwisho zimetajwa na alitoa muda ambao Halmashauri watachukua hatua kurekebisha mapato hayo na kila Mkurugenzi amepaswa kujieleza na kuonesha mikakati hiyo. Kwa hiyo, hatua zinachukuliwa na wana maelekezo mahususi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ni kweli kwamba kuna fedha zimetengwa asilimia 40 ili ikaendeshe miradi ya Halmashauri. Tumetoa maelekezo, sisi viongozi wa Wizara hii, sisi Manaibu wenzake na Watendaji wengine, tukifanya ziara kwenye Halmashauri zetu, pamoja na kwenda kukagua fedha kutoka Serikali Kuu, ni lazima pia kila Halmashauri itupeleke kwenye mradi mmojawapo ambao ni *own source*; fedha ambazo wamekusanya kutoka kwa wananchi,

zimefanya miradi? Hii ni ili tuwe na *connection* kati ya fedha ambayo inatolewa kama kodi, lakini pia na miradi ya maendeleo, kweli jambo linafanyaika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili ni kweli kwamba kuna maeneo mengi wako Wakuu wa Idara na Vitengo wanakaimu na tumetoa maelekezo kufanyike utaratibu, wale ambaao wana sifa wathibitishwe kazini na wale ambaao hawana sifa waondolewe ili tuwe na watu ambaao kimsingi wana uwezo wa kufanya maamuzi. Kwa sababu ni kweli kwamba kama mtu anakaimu, wakati mwingine amekaimishwa na Mkurugenzi, akipingana naye katika mambo fulani, anamwondoa anamweka mtu mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunataka watu wawe na uwezo, wakaelezee Idara, wawe na mipango na pla waweze kubuni kwa sababu ofisi ni ya kwake.. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Bonnah Moses Kaluwa, Mbunge wa Segerea aulize swalii lake. Mheshimiwa Mariam Kisangi, kwa niaba ya Mheshimiwa Bonnah Kaluwa.

Na. 221

### **Umuhimu wa Kujenga Daraja la Seminari - Segerea**

**MHE. MARIAM N. KISANGI (K.n.y. MHE. BONNAH M. KALUWA)** aliuliza:-

Barabara ya Segerea Sheli kuititia Seminari, Stakishari Polisi kwenda kutokea Majumba Sita ni suluhisho la Msongamano wa magari yanayopita barabara ya Segerea - Tabata kutokea barabara ya Mandela, lakini kwa sasa barabara hiyo haipitiki kwa kuwa daraja la Seminari liliondoshwa na maji ya mvua mwaka 2013.

Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kujenga daraja la Seminari ili kuondoa tatizo hilo na kurahisisha huduma kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba nijibu swali la Mheshimiwa Bonnah Moses Kaluwa, Mbunge wa Segerea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja la Seminari Segerea liko katika barabara ya Majumba Sita Stakishari yenyeye urefu wa kilomita 2.93. Hapo awali usanifu wa kujenga daraja hili ulishafanyika. Hata hivyo, ipo changamoto inayotokana na mto kutanuka, hivyo inahitajika kufanyika stadi ya kina na mapitio ya usanifu wa awali ili kupata mahitaji halisi ya ujenzi wa daraja kutokana na changamoto hiyo. Mara baada ya kukamilika kwa mapitio ya usanifu na tathmini ya gharama, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kujenga daraja hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2019/2020 *TARURA* imepanga kufanya usanifu wa kina wa daraja hilo ili kujua gharama halisi kwa maana ya *cost estimates* zinazohitaji kulijenga. Namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira wakati Serikali inachukua hatua hizo muhimu kwa ajili ya kutatua tatizo la kukosekana kwa daraja hilo. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa matatizo ya daraja la Segerea ni ya muda mrefu sana na kila wakati liko katika upembuzi yakinifu; na kwa kuwa Serikali sasa inataka

kufanya tena usanifu kupidia *TARURA*; mimi nauliza swali: Je, kwa nini *TARURA* sasa wasianze kujenga hilo daraja la Segerea badala ya kuanza tena upembuzi yakinifu ili kuwasaidia wananchi wa Segerea ambao wanapata shida sana kutokana na ukosefu wa daraja lile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa matatizo wanayopata wananchi wa Segerea yanafanana kabisa na yale wanayowapata watu wa Jangwani pale maeneo ya Magomeni: Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha daraja la Jangwani ili kuondoa matatizo ya kufunga barabara ile wakati wa mvua nydingi kila wakati? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi maswali yote mawili yanafanana. Adha ambayo tunaipata kutokana na lile daraja ambalo mto unahama, lakini na swali lake la pili kuhusiana na daraja la Jangwani ambalo linajaa maji kila muda, naomba Mheshimiwa Mbunge arejee katika siku moja ambayo nilijibu hapa, kwamba jumla ya shilingi bilioni 260 zimetengwa kwa ajili ya kuanza usanifu na kuhakikisha kwamba tunapata suluhu ya kudumu kuhusiana na Mto Msimbazi. Pia akubaliane name, kama ambavyo tunaweza tukafanya makosa tukajenga hilo daraja, baada ya muda likawa linaendelea kujaa, ndiyo maana tumemwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira kama ambavyo nimetoe majibu katika jibu langu la msingi, kwamba ni vizuri tukafanya usanifu wa kina kujua hasa tatizo ili ujenzi ukikamilika tuwe tumepeata suluhu ya kudumu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaynabu Vulu, Mheshimiwa Komu.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Kwa kuwa

swali la msingi linahusu muunganiko wa daraja na barabara; na kwa kuwa sote tumeshuhudia kwa macho au kupitia vyombo vya habari jinsi Mji wa Dar es Salaam ulivyoharibika kwa mafuriko; na kwa kuwa ujenzi wa madaraja na barabara umechangia kuhakikisha kwamba usafiri umekuwa siyo mzuri kwa watoto wetu, kwa watu wazima na kwa wagonjwa kutokana na mafuriko yaliyokuwepo: Je, Serikali itachukua hatua gani za dharura kuhakikisha mafuriko hayo hayataendelea tena na hayatatokea; na kuhakikisha Mji wa Dar es Salaam unarudi kama ulivyokuwa hapo awali? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sisi sote ni mashuhuda kwamba mvua ambazo zinanyesha Dar es Salaam sasa hivi ni nyingi sana ambazo hatukuzitarajia. Kwa hiyo, kwanza ni sisi wote kushiriki kuhakikisha kwamba tunapambana na tabianchi ambayo inaleta mwongezeko wa mvua ambazo hatuwezi kuzitarajia. Sasa tunafanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kipekee nichukue fursa hii kupongeza *UDART* jinsi ambavyo wamekuwa wakipambana na hali hii pale ambapo maji yanakuwa yamezidi, tunalazimika kusimamisha usafiri ili kusijie kukawa na madhara makubwa, lakini *immediately* zinafanyika juhudi za kuhakikisha maji yale yanaondolewa na usafiri unarejea kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge, ni ukweli usiopongika, kwa mvua ambazo zinanyesha sasa hivi; na bahati nzuri watabiri wa hali ya hewa walitufahamisha kwamba mvua zinatarajiwa kunyesha nyingi sana, kwa hiyo, hakuna namna ambavyo tunaweza tukasema tutafanya kuzuia mvua kwa sababu ni *calamity* ambayo inaweza ikatokea muda wowote. Kwa hiyo, tuwe na subira, hali ya Dar es Salaam itarudia katika

hali yake baada ya mvua hizi kukoma kama ambavyo wametuambia. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Komu, swali fupi la nyongeza.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunpa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kule Moshi Vijiji kwa asili kabisa hali ni mbaya sana wakati wa mvua kwa sababu ya aina ya udongo ambao uko kule, lakini hali ni mbaya zaidi katika Kata ya Arusha chini kule *TPC* katika kijiji cha Chemchem ambacho kimetengwa na Mto Kikavu ambao wakati wa mvua kunakuwa hakuna mawasiliano kabisa na sehemu nyingine zozote za Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka mwaka 2012, daraja hilo la Chemchem la hapo kwenye kivuko cha Mto Kikavu limekuwa likitengewa fedha, lakini ujenzi mpaka kesho haujaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri, ni lini mtakuja kuwaunganisha watu wa Chemchem na wenzao wa huko Tanzania? (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kijiji ambacho Mheshimiwa Mbunge anakitaja kwangu mimi ndiyo nakisikia. Katika swali la msingi sikutarajia swali la kutoka huko ambako Mheshimiwa Komu anasema. Ni vizuri sasa nimwambie Mheshimiwa Mbunge, baada ya kipindi hiki cha maswali na majibu ni vizuri tukawasiliana tujue uhalisia ukoje ili tuweze kutatua tatizo ambalo lipo. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Sawa kabisa Mheshimiwa Waziri, ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, swali fupi la nyongeza.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwe Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba niongeze swali dogo la nyongeza, kwamba kule kwangu kuna barabara ya kutoka Waama mpaka Masusu na hatimaye mpaka kule Lalaji na barabara nyingine ya Maskaroda na kwenda Lambo na kwenda Dareda ambapo zinaunganisha wananchi na hospitali na nilishatoa ombi: Je, Serikali inasemaje ili kunisaidia na watu wale ambao wana kilomita 20 kwenda kwenye hospitali wapate namna ya kufika? Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo fupi la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata fursa ya kwenda Jimboni kwa Mheshimiwa Dkt. Nagu kutatua mgogoro wa kijiji na tukafanikiwa kuutatua mgogoro ule. Ingekuwa vizuri sana Mheshimiwa Nagu kama ungeniambia tukapata na fursa ya kwenda kutembelea huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba huduma ya usafiri na hasa kwenda hospitali kama ambavyo yeye amesema kwenye swali lake, ni vizuri tukawasiliana na Meneja wa *TARURA* tujue nini hasa ambacho kinatakiwa kifanyike ili wananchi wetu waendelee kupata huduma na hasa ya kwenda hospitali. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Ester Alexandra Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 222

### **Kupandisha Hadhi Kituo cha Afya Dongobeshi**

**MHE. ESTER A. MAHAWE** Aliuliza:-

Halmashauri ya Mbulu haina Hospitali ya Wilaya hivyo wananchi wa Kata za Gidhim, Yayeda, Ampatumat

hutembea umbali mrefu kufuata huduma katika kituo cha Afya Dongobeshi.

(a) Je, ni lini Serikali itapandisha hadhi Kituo cha Afya Dongobeshi ili kiweze kuwahudumia wananchi wa Mbulu Vijijini na kupunguza msongamano katika Hospitali ya Rufaa ya Hydom?

(b) Je, ni lini Serikali itaongeza Watumishi wa Afya, dawa na vifaa tiba katika kituo hicho cha afya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swalii nyongeza ya Mheshimiwa Ester Mahawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwe Mwenyekiti, Kituo cha Afya Dongobeshi kilianzishwa mnamo mwaka 1974 kipo kata ya Dongobeshi, kinahudumia jumla ya wakazi takribani 30,000 wa Tarafa ya Dongobeshi na wakazi wa maeneo jirani wakiwemo wananchi wa Kata za Gidhim, Yaeda na Amputamat.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa kituo hiki, Serikali kwa nyakati tofauti imekuwa ikitoa fedha kwa lengo la kuboresha miundombinu pamoja na huduma za afya zitolewazo kwenye kituo hiki. Mwezi Machi, 2018 Serikali ilitoa kiasi cha shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ambayo ujenzi wake umekamilika hivi karibuni. Majengo hayo ni wodi ya Mama na Mtoto (*Maternity and Pediatric Ward*), jengo la upasuaji, jengo la maabara, nyumba moja ya mtumishi na jengo la kuhifadhi maiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuongeza idadi ya watumishi katika Kituo cha Afya cha Dongobeshi. Mwaka wa fedha 2017/2018 watumishi sita wapya wameajiriwa na kufanya kituo kuwa na jumla ya watumishi 37. Aidha, Serikali imetuma fedha bohari Kuu ya

Dawa (*MSD*) jumla ya shilingi milioni 320 zikiwa ni kwa ajili ya kunua vifaa tiba, hadi sasa vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni 37 vimepelekwa kituoni hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2018/2019, jumla ya shilingi bilioni 1.5 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu inayojengwa katika Tarafa ya Dongobesh. Kukamilika kwa hospitali hii kutaondoa msongamano kwenye Hospitali ya Hydom. Kwa kuwa, Hospitali ya Wilaya inajengwa katika eneo la Dongobesh hakuna sababu ya Kituo cha Afya kilichopo sasa kupandishwa hadhi kuwa hospitali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Mahawe.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini pia niipongeze Serikali kwa kutuletea fedha hizo shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya unaoendelea hivi sasa, lakini pamoja na majibu haya mazuri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwanza kabisa kuna msongamano mkubwa bado katika Kituo hiki cha Afya cha Dongobesh kwa sababu ya huduma ambayo si nzuri sana kwenye zahanati zetu. Je, ni nini kauli ya Serikali wakati tukisubiri kukamilika kwa ujenzi ambao ndio kwanza umeanza wa Hospitali ya Wilaya ambao utapunguza msongamano kwenye kituo hicho cha afya kupeleka huduma ya vifaa tiba pamoja na watumishi kwenye zahanati zinazozunguka Kituo hiki cha Afya cha Dongobesh?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Tarafa ya Yaeda Chini haina kituo cha afya. Je, ni lini Serikali itapeleka Kituo cha Afya katika tarafa ya Yaeda Chini ambayo mioundombinu yake migumu na huko ndiko wanakoishi wenzetu Wahadzabe? Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ester Mahawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, tupokee pongezi za kutoka kwa Mheshimiwa Esther. Nilipata fursa ya kwenda Kituo cha Afya Dongobesh na pia nikapata fursa ya kushiriki kuzindua ujenzi wa Hospitali ya Dongobesh kwa maana ya Hospitali ya Wilaya. Kipekee naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge Mahawe pamoja na Mheshimiwa Flatey Massay kwa ushirikiano mkubwa pamoja na wananchi wao katika kuhakikisha kwamba, huduma za afya zinaboreshwaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swalii lake anaongelea juu ya suala zima la kupeleka watumishi katika zahanati ili kusiwe na msongamano. Wewe ni shuhuda. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumepeleka maombi ya ajira elfu 15 kwa ajili ya watumishi wa Kada ya Afya kwa kadri kibali kitakavyopatikana, naomba nimhakikishie Mbunge na huko nako hatutawaacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swalii lake la pili, anaongelea juu ya suala zima la kujenga Kituo cha Afya katika Tarafa ya jirani ambako wanaishi jamii ya Wahadzabe ambaao wanauhitaji mkubwa. Naomba aendelee kuiamini Serikali tumeahidi tunatekeleza na naamini na yeye anaridhika na mwendo ambaao tunaufanya katika kujenga vituo vya afya. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii dogo la nyongeza. Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri amefika na Serikali imetupa fedha ya kujenga hospitali ya wilaya, lakini Mheshimiwa Waziri atakumbuka tulimsimika

kama Mzee wa Mbulu Vijiji na akatuahidi atatupatia Kituo cha Afya kile cha Maretadu na maombi yako kwake. Ndugu yangu awaambie watu wa Maretadu je, kituo cha afya kitaletewa fedha lini? Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatei Massay, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muungwana ahadi ni deni. Naomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuiamini Serikali kama ambavyo tumepeleka fedha katika Kituo cha kwanza cha Dongobesh, tukapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya wilaya, halikadhalika tutahakikisha kwamba, pale nafasi inapopatikana hatutasahau kwa sababu tumeahidi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Chatanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Devotha Minja.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Mgombezi ina zahanati na Kata ya Mtonga ina zahanati ambayo ina wakazi wengi, hasa ikizingatiwa kwamba, kuna mashamba ya m Konge. Je, watakuwa tayari sasa kutusaidia kupandisha hadhi Zahanati ya Mtonga pamoja na Zahanati ya Mgombezi ili viwe vituo vya afya, hasa ikizingatiwa kwamba, kuna watu wengi sana ambao wana shughuli za m Konge kule? Nashukuru sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mary Chatanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba, tunajenga vituo vya afya vyenye ramani na hadhi ya kufanana na vituo vya afya. Pale ambapo zahanati ambayo imejengwa ina hadhi ya kulingana na vituo vya afya hatusiti kufanya hivyo, lakini tunafanya kwa kuzingatia kwamba, ramani ile ambayo vituo vya afya vinajengwa na zahanati hiyo ifanane na ramani hizo, lakini pia hata ukubwa wa eneo; inahitaji eneo lisilopungua ekari 15 kuwa na kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sina uhakika katika zahanati ambazo Mheshimiwa Mbunge anaongelea zina maeneo na ramani ya kufanana na vituo vyetu vya afya? Tutafanya vile baada ya kujiridhisha kwamba, vigezo vyote vimetosheleza, kama ambavyo kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama kuna zahanati ambazo tumezipandisha hadhi kuwa vituo vya afya baada ya kuridhika kwamba, matakwa yote ya kituo cha afya yanakamilishwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Devotha Minja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro ambayo inahudumia wagonjwa 500 kwa siku, hospitali hii kwa miezi minne hivi sasa haina kipimo cha *full blood picture*, hospitali hii kwa miezi minne haina *oxygen*, hospitali hii kwa miezi minne haina *film*, wagonjwa wakienda kupima *x-ray* wanapewa *CD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufahamu Serikali ina mpango gani wa haraka wa kusaidia hospitali hii iweze kutoa huduma kwa wagonjwa? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Devotha Minja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina taarifa ya hili ambalo analolisema sasa hivi, lakini nimwombe Mheshimiwa Mbunge baada ya kikao hiki tuweze kulifuatilia na kuhakikisha kwamba, hiyo huduma ambayo ni ya msingi kwa wagonjwa iweze kupatikana katika Hospitali hii ya Rufaa ya Morogoro.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea sasa na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 223

### **Stahiki za Wafanyakazi**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza:-

Je, Serikali inatumia Sheria ipi kutowapa wafanyakazi stahiki zao zinazohusu kupandishwa madaraja na ongezeko la mwaka (*Annual Increment*) kwa wakati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Barua ya Katibu Mkuu – Utumishi yenyewe Kumbukumbu Namba CAC. 45/257/01/E/83 ya tarehe 9 Septemba, 2013 kuhusu upandishwaji wa vyeo kwa madaraja kwa watumishi wote nchini wa umma huzingatia vigezo muhimu sana kama vile sifa za kitaaluma, uzoefu wa kazi, utendaji mzuri wa kazi kwa maana ya *OPRAS*, tange au ukubwa kazini kwa maana ya *Seniority*, uwepo wa ikama na bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka husika wa fedha, vilevile bila kusahau nidhamu na mwenendo wa mtumishi huyo wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ile ya E. 9(1) ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009, Toleo la Tatu, nyongeza ya mwaka ya mishahara haipaswi kuombwa au kudaiwa na watumishi wa umma bali Serikali ndio yenye uamuzi wa kutoa au kutokutoa nyongeza hiyo. Hivyo, katika utumishi wa umma hakuna sheria inayoainisha kwamba, mtumishi anatakiwa kupata nyongeza ya kawaida ya mshahara kwa kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya E.2 ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009 viwango vya mshahara ikiwa ni pamoja na nyongeza ya mshahara kwa kila mwaka kwa maana ya *annual increment* hupangwa kulingana na uwezo wa Serikali kulipa. Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali ilitoa nyongeza ya mshahara ya kila mwaka kwa maana ya *annual increment* kwa watumishi wote wa umma kuanzia mwezi Novemba, 2017. Vilevile Serikali imewaelekeza waajiri wote kuendelea na upandishwaji vyeo kwa watumishi 193,166 waliokasimiwa katika ikama ya bajeti ya mwaka 2017/208 kuanzia tarehe 1 Mei, 2019 na barua zinaendelea kuingizwa kwenye mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahimize watumishi wote wa umma kufanya kazi kwa bidii na weledi ili kuleta tija katika utumishi wa umma na Serikali itaendelea kutoa nyongeza ya mshahara pamoja na kuboresha mazingira ya kazi kadri uwezo wa Serikali kulipa utakavyoruhusu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tunza Malapo. Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Suala la kupandishwa madaraja linaambatana na ongezeko la mishahara. Serikali hii ya Awamu ya Tano imekuwa haipandishi watu madaraja kwa wakati, mtu anakaa mpaka miaka sita, saba, hajapandishwa madaraja. Nataka tu kujua Serikali iko tayari kuwalipa wale watu *arrears* zao kwa ile miaka ambayo hawakupandishwa madaraja kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, Mheshimiwa Waziri amesema wafanyakazi wafanye kazi kwa bidii. Hivi kweli anafikiri unaweza kumkamua ng'ombe maziwa kama humpi chakula cha kutosha? Nakushukuru. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tunza Malapo, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kipekee nimpongeze sana kwa jinsi ambavyo anafuatilia masuala yote ya watumishi wa umma nchini. Hata hivyo, naomba niseme kwamba, katika upandishwaji wa madaraja tuna madaraja ya aina tatu, kuna kupandishwa kwa madaraja kwa maana ya *salary increase*, kuna *annual increment* na kuna *salary promotion*, lakini katika suala la upandishwaji wa madaraja Serikali ilitoa tamko hapa wiki tatu zilizopita kwamba, kuanzia Mei Mosi mwaka huu (2019) Serikali inatarajia kupandisha madaraja, vyeo, watumishi zaidi ya 193,000. Hilo zoezi limeshaanza, lakini vilevile mwaka 2017/2018 Serikali ilishalipa *annual increment* zaidi ya bilioni 72.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile naomba niseme kabisa kwamba, Walimu walishalipwa zaidi ya bilioni 37, lakini kada nyingine za utumishi wa umma walishalipwa zaidi ya bilioni 35, lakini malimbikizo ya mshahara zaidi ya bilioni 75 zimelipwa. Isitoshe tu, lakini zaidi ya wastaa fu waliokuwa wanaidai Serikali wameshalipwa zaidi ya bilioni tisa na hawa wastaa fu ni zaidi ya 1,800. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili ni kwamba, Serikali inawajali sana watumishi. Sio lazima iwe katika nyongeza tu ya mshahara, lakini vilevile tukumbuke kwamba, Serikali ndio *guarantor*, watumishi wanapotaka kujenga nyumba, watumishi wanapotaka kufanya mikopo, kuna bima za afya zote hizo ni sehemu ya motisha. Kwa hiyo,

naomba niseme kabisa Serikali inawajali watumishi katika njia mbalimbali na hata katika kupanda madaraja hiyo imeshaanza kutekelezwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Mollel, atafuata Mheshimiwa Masoud.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nampongeza dada yangu Mheshimiwa Mary Mwanjelwa kwa majibu mazuri yaliyokwenda shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali la nyongeza. Kwa kuwa, Serikali iliwafukuza watumishi ambao walighushi vyeti au hawakuwa na vyeti vya kidato cha nne na kati ya hao watumishi ambao walifukuzwa ni kwamba, walikopa katika benki zetu na mpaka sasa hawajui hatima yao na wengine wamekufa na wengine wamekimbia nyumbani kwa sababu, benki zinawafuata mpaka nyumbani. Nataka kujua kwa sababu, wakati wanachukua Serikali ndio ilikuwa *guarantor* wao. Sasa je, nini Kauli ya Serikali kwa benki ambazo zinawasumbua hawa watumishi na hawana jinsi ya kuweza kurudisha hizo fedha? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la mdogo wangu, Mheshimiwa Amina Mollel, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Serikali Mei, 2016 ilienda kwenye zoezi la kusitisha upandishwaji wa madaraja na vilevile kusimamia hilo zoezi zima la vyeti feki, lakini sio vyeti feki tu hata watumishi hewa. Tukumbuke kabisa kwamba, wakati najibu hapa swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Tunza Malapo nimesema Serikali inakwenda mbali zaidi katika kuwajali watumishi kwenye motisha hata katika kuwapatia *guarantor* mbalimbali ikiwemo na mikopo ya benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tukumbuke watumishi hawa walikuwa ni halali, walikuwa ni watumishi halali na ndio maana Serikali inakuwa ni *guarantor*. Sasa kama wewe tayari umeshafukuzwa na hiyo tunasema ni *crime* kwa maana hiyo, sisi tunazingatia tu kwa yule mtumishi ambaye ni halali, Serikali itamjali, Serikali itakuwa ni *guarantor* pamoja na mambo mengine ya motisha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nina swali moja dogo la nyongeza. *Annual increment* ipo kisheria, kutowapatia wafanyakazi *annual increment* kunasababisha wakati atakapostaafu kupungua, kupunjwa kwa mafao yao sambamba na kupungua kwa *pension* zao za izeeni na wanasesma kwamba, hii awamu ya kuwasaidia wanyonge na maskini.

Je, hawaoni sasa kuendelea kutowapatia *annual increment* wafanyakazi hawa wanaendelea kuwapunja, kuwadhulumu wanyonge hawa na lini Serikali wataacha tabia hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Masoud, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie tena kujibu kile nilicho jibu kwamba, suala la *annual increment* mwaka 2017/2018, Serikali imeshalipa *annual increment* kwa watumishi wote wa umma bila kujali kada zozote. Pia nimesema imelipa zaidi ya bilioni 72, lakini sio kwamba, Serikali inawapunja ni sehemu ya mtumishi wa umma kupata motisha; tena nilitegemea kaka yangu hata angeshukuru kwamba, Serikali inawajali watumishi na ndio maana imeweza kuongeza hiyo mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme jibu langu nilishalijibu, Serikali inawajali watumishi na ndio maana mwaka 2017/2018 imelipa zaidi ya bilioni 72. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mary Mwanjelwa, Naibu Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mbunge wa Nyamagana, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Shangazi.

Na. 224

**Kufungwa kwa Local Channels Kwenye Baadhi ya Ving'amuzi Nchini**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI (K.n.y. MHE. STANSLAUS S. MABULA)** aliuliza:-

Serikali kupitia Mamlaka ya *TCRA* wamefungia *Local Channels* kuonekana kwenye baadhi ya ving'amuzi hapa nchini, mfano *Azam Tv, DSTV* na vinginevyo.

(a) Je, Serikali haioni kwa kufanya hivyo imewanyima wananchi fursa ya kujua mambo yanayoendelea kwenye Taifa lao?

(b) Je, ni lini Serikali itatoa muafaka wa jambo hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana, lenye Sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa wananchi kupata fursa ya kujua mambo yanayoendelea kwenye Taifa. Kwa misingi hiyo, imetoa leseni zenye masharti tofauti ikiwemo leseni ya *public*, yaani utangazaji wa umma ambapo matangazo huruhusiwa kurushwa kwa watoa huduma wenye *must carry*. Hivi sasa matangazo ya umma ni *TBC 1* na *TBC 3* maarufu kama *Safari Channel*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha makampuni yanayomiliki visimbusi au ving'amuvi vya *DSTV*, *Zuku* na *Azam* hayakustahili kutoa huduma ya kubeba *channel* za ndani zisizolipiwa, yaani *free to air local channels*, kutokana na masharti ya leseni zao. Utoaji wa huduma za maudhui kuitia visimbusi vyao uko kwenye mfumo wa kukidhi soko la kimataifa na maudhui yake kuwa ya kulipia. Masharti ya leseni hizo na mfumo mzima wa miundombinu ya utangazaji husika yamelenga soko la kimataifa na hutofautiana na masharti ya leseni za watoa huduma za maudhui ya ndani ya nchi. Kuruhusu *channels* za ndani kuoneshwa kwa kutumia leseni za matangazo ya kimataifa kutazifanya *free to air local channels* kuwa za kulipia badala ya kuonekana bure.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuitia *TCRA* imefanya jitihada ikiwa ni pamoa na kukaribisha maombi ya leseni ya kubeba maudhui ya *channels* za ndani, yaani *multiplex operator*, kutoka kwa wanaohitaji kutoa huduma yakiwemo makampuni ya *Azam*, *DSTV* na *Zuku* ili yaweze kupata leseni stahiki na kuweza kutoa huduma za kubeba au kuonesha maudhui ya ndani kuitia visimbusi vyao. Kwa sasa *TCRA* inashughulikia maombi yaliyopokelewa ili iweze kushauri kuhusu utoaji wa leseni stahiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi, swali la nyongeza, atafuata Mheshimiwa Sophia.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoa na majibu ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 18(d) haki ya kupata taarifa ni haki ya msingi kabisa na imetajwa kwenye Katiba na Tanzania siyo kisiwa kwa maana kwamba tunatakiwa na sisi mambo yetu yafahamike kimataifa.

Je, Serikali haioni kwamba kuziuia hasa Azam kuonesha matangazo haya ni kunyima fursa ya habari za ndani kujulikana kimataifa? (*Makofii*)

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima kuwa wazalendo ni kupenda vya nyumbani na hawa Azam tumeona wakifanya kazi kubwa sana ya kuelimisha Taifa na kutoa taarifa mbalimbali za kijamii na mara nyingi hata matangazo ya Live ya Mheshimiwa Rais yanaonekana kuitia Azam.

Sasa Serikali ina mkakati gani mahsusini wa kuangalia hizi sheria na kanuni ili kuweza kuruhusu *Azam TV* iweze kuruka ndani na kuweza kuonekana katika ving'amuhi hivi tupate taarifa za *channel* zote za ndani zioneckane katika *Azam TV*. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rashid Shangazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana kwa kuwa amekuwa ni mmoja kati ya wadau wa tasnia ya habari kwa jinsi anavyofuutilia masuala haya ya visimbusi au ving'amuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kujibu maswali yake mawili ni kwamba ni kweli tunakiri kwamba kila Mtanzania anayo haki ya kupata habari na ndio maana kuitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania tulitengeneza utaratibu wa kutoa leseni za aina mbalimbali kwa watoa huduma za

matangazo kuweza ku-*apply*. Watu wa *StarTimes*, *Ting* na *Continental* wali-*apply* leseni ambazo zinawawezesha kuonesha *free to air channels* lakini Azam, Zuku na wengine wali-*apply* leseni ambazo zinawaruhusu kuonesha matangazo kwa njia ya kulipia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama Serikali tuliwaambia kabisa madhara au faida ya kuchukua leseni za aina hiyo ambazo hata gherama ya ulipiaji kwa mwaka ni tofauti. Azam waliamua kuchukua ile ya kimataifa kwa sababu walitaka mtu anayetaka kuona habari kupitia Azam aweze kulipia; kitendo cha wao kuanza kuonyesha *channels* za *free to air*, zile ambazo zinamruhusu mwananchi yeoyote hata kama hela imeisha kwenye king'amuvi aone, haikuwa ni sehemu ya masharti ya leseni yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa swali lake la pili, nimuondoe wasiwasi kwamba kati ya watu walio-*apply* leseni za kuonesha na *free to air channel* Azam wapo na nimuondoe wasiwasi kwamba jana wamepokea hiyo leseni na wametuhakikishia kama Serikali kwamba ndani ya miezi saba watakuwa wameshajenga *DDT* eneo lote la nchi yetu kwa ajili ya kurusha hizo *channels* za bure. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi ya swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TCRA* imeruhusu *TBC* kama *TV* ya Taifa kuonekana kwenye ving'amuvi vyote, lakini *TCRA* inaisimamia vipi *TBC* kuweza kuonyesha habari kwa uhakika na bila upendeleo kwa vyama vyote na wananchi wote? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Waziri nilikuona unataka kujibu.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana

Mheshimiwa Naibu Waziri Mhandisi kwa majibu mazuri sana aliyotoa kwa maswali aiyoulizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa swali la nyongeza napenda niseme tu kwamba *TBC* kama vituo vyote vya kitaifa duniani vina hadhi ya *must carry ambayo* kila kisimbusi lazima kibebe, kwa hiyo, siyo kitu cha Tanzania tu, kipo duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, hili ni suala la maudhui; suala la maudhui upande wa *TBC* ni wazi, kama una maudhui yako tafadhalii peleka *TBC*. Hakuna upendeleo wowote unaofanyika, wewe kama unaamini ni upendeleo ni shauri yako, lakini leta maudhui yako yaoneshwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba nikusitizie, kama kuna mtu hapa ana wasiwasi maana wengi wanaongea hawajawahi hata kupeleka maudhui, nileeteni mimi kama hayo maudhui hayataoneshwa. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa njema ni vyema zikawa na sauti, leo asubuhi kuanzia saa 12.00 *TBC* haikuwa na sauti kabisa na hakuna namba yoyote iliyokuwa inaonesha pale tupige kwa dharura wale ambao tuna ving'amuzi vya *Azam TV*.

Je, Mheshimiwa Waziri anatuambia nini na wakati walipokuja kurudi kutupatia sauti saa 1:10 asubuhi hawaku-apologize? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo la nyongeza.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa hata mimi mwenyewe nimeona hiyo hitilafu ikitokea leo, lakini siyo leo tu imekuwa ikitokea mara kwa mara kwa sababu *TBC, television* yenu ya Taifa sasa hivi ipo katika programu ya mageuzi makubwa sana kiteknolojia ndiyo maana muonekano wa *TBC* sasa hivi ni bora kupita miaka iliyopita nyuma na naomba ndani ya mwezi mmoja mtaona hata *background*, nyuma ukiangalia *TBC* chaitatofautiana sana na *CNN*. Kwa hiyo, kaa mkao wa kuangalia *Television* ya Taifa. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Habari, tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 225

### **Kunufaisha Kagera na Uchumi wa Kijiografia**

**MHE. HALIMA A. BULEMBO** Aliuliza:-

Mkoa wa Kagera una hekta 1,593,758 zinazofaa kwa kilimo na ni mkoa pekee unaopakana na nchi nyingi za *EAC* hivyo Kagera inaweza kuwa Kituo cha Biashara cha *EAC*.

Je, Serikali ina mpango gani mahsuswi wa kuifanya Kagera ifaidike na uchumi wa kijiografia?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera ni mkoa pekee hapa nchini unaopakana na nchi nyingi za Afrika Mashariki ambazo ni Uganda, Rwanda na Burundi. Ili kuuwezesha mkoa huu kunufaika na fursa za kijografia, Serikali inatekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati ikiwa ni pamoja na mradi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa, kipande cha Isaka-Rusumo chenye urefu wa kilometra 371, ukarabati wa barabara ya Lusahunga – Rusumo yenyeye urefu wa kilometra 91, Mradi wa Umeme Vijiji Awamu ya Tatu, mradi wa kuzalisha umeme wa megawati 80 katika Mto Rusumo na Mradi wa Vituo vya Pamoja katika mipaka ya Rusumo na Mutukula kwa ajili ya kuimarisha shughuli za kibashara na nchi jirani za Rwanda na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao ya wakulima wa Kagera na bidhaa za baadhi ya viwanda vyetu vya kusindika mazao ya killmo, mifugo, uvuvi na misitu vinafaldika kimasoko na jiografia ya Mkoa wa Kagera. Baadhi ya viwanda vinavyonufaika na jiografia ya mkoa ni pamoja na *Kagera Fish Co. Ltd.* na *Supreme Perch Ltd.* vinavyosinika minofu ya samaki, *Ambiance Distillers Tanzania Ltd.* kinachozalisha vinywaji vikali, *Bunena Development Co. Ltd.*, *NK Bottling Co. Ltd.* na *Kabanga Bottlers Co. Ltd.* vinavyozalisha maji ya kunywa na kiwanda cha Mayawa kinachosindika *wine* ya *rosella* na *juice*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na utekelezaji wa miradi ya kimkakati, Serikali kupitia Mamlaka ya Biashara (*Tan Trade*) ilitoa mafunzo ya kuhamasisha kuanzishwa kwa vikundi vya kurasimisha biashara mipakani katika vituo vitatu vilivyopo katika Mkoa wa Kagera. Vituo hivyo ni pamoja na Kabanga, Rusumo na Mutukula vinavyopakana na nchi za Burundi, Rwanda na Uganda kwa mtiririko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine, mafunzo hayo yalilenga kuwajengea wananchi uwezo wa kutumia fursa za kiuchumi zilizopo katika mipaka yetu na nchi jirani za Burundi, Rwanda na Uganda. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima swalii la nyongeza.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri kabisa na pili nimefurahi kusikia Mheshimiwa Waziri ametambua kuwa Mkoa wa Kagera ndiyo mkoa pekee nchini unaopakana na nchi nyingi za Afrika Mashariki. Mkoa wa Kagera unapakana na nchi nne za Afrika Mashariki kati ya tano kwa maana ya Burundi, Rwanda, Uganda, Tanzania yenye ambayo Kagera imo na hata Kagera inaifikia Kenya kwa kupitia Ziwa Victoria.

Ni kwa nini sasa Serikali isione kuna umuhimu wa kuufanya Mkoa wa Kagera kuwa kituo kikubwa cha biashara Afrika Mashariki? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, kwa hivi sasa Mkoa wa Kagera ndiyo mkoa pekee unaolima na kuzalisha kahawa nyingi nchini na hata tafiti zimeonesha hivyo kwamba Mkoa wa Kagera unazalisha asilimia 65.6 mpaka sasa, lakini kumekuwepo na malalamiko mengi ya utoroshwaji wa kahawa kutoka Mkoa wa Kagera kwenda Uganda.

Ni lini sasa Serikali itajenga mnada wa kimataifa Mjini Bukoba ili kahawa zote za maeneo ya Maziwa Makuu ziuzwe Mjini Bukoba? Nakushukuru. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo mafupi ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swalii la pili la nyongeza la Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge jinsi anavyowapigania wakulima wa kahawa wa Mkoa wa Kagera, hii inaonesha namna gani alivyokuwa jirani na watu wa Kagera. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali kwa kutambua umuhimu wa Mkoa wa Kagera kwenye uchumi wa Taifa hili na hasa uzalishaji wa kahawa kama alivyosema, inazalisha zaidi ya asilimia 40 ya kahawa yote nchini, lakini ndiyo mkoa unaoongoza kwa kilimo cha kahawa aina ya Robusta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumeshapanga sisi kama Serikali kwamba kuanzia msimu wa mwaka huu tutakuwa na minada ya kanda kwenye kanda zote nne za uzalishaji wa kahawa hapa nchini; kwamba tutakuwa na mnada wa Kanda Kagera, Kilimanjaro, Nyanda za Juu na kule Ruvuma. Pia nimtoe wasiwasi kwa mujibu wa takwimu na hali halisi ilivyo, kahawa yote ya Mkoa wa Kagera asilimia zaidi ya 90 inauzwa katika soko la moja la moja (*direct export*) na mpaka sasa tunapoongea, wakulima hasa Chama Kikuu cha Ngara kimeshaanza kuleta makubaliano hayo, kahawa yote imeshauzwa imebaki tu asilimia 10 ambayo ndiyo itaenda kwenye mnada. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gashaza.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza halijajibwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima ameshajibu Mheshimiwa Waziri majibu.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wilaya ya Ngara ni sehemu ya Mkoa wa Kagera na ni Wilaya inayopakana na nchi mbili kwenye Mpaka wa Rusumo kwa maana kupakana na nchi ya Rwanda na mpaka wa Kabanga kupakana na nchi ya Burundi. Kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, kwenye mipaka hii kuna vituo vya

pamoja vya forodha, lakini ipo fursa ya masoko ambayo hatunayo sasa na hivyo kupelekea wananchi wetu washindwe kufanya biashara katika maeneo haya ya mipakani.

Je, Serikali ipo tayari kutenga fedha kwa ajili ya kujenga masoko maeneo hayo ikiwezekana *shopping malls* ili kunufaika na fursa hii? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Halima Bulembo na swali lingine la Mheshimiwa Gashaza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na swali la Mheshimiwa Halima Bulembo kuhusu kujenga kituo kikubwa cha biashara cha Afrika Mashariki katika Mkoa wa Kagera, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba Serikali yetu ipo katika mpango mkakati wa kujenga kituo kikubwa cha kibiashara pale katika eneo la Nyakanazi ambapo soko hili litawenza kufikiwa na wananchi wetu wa mikoa inayozunguka Kagera, lakini pia nchi za DRC, Burundi, Rwanda na Uganda wote watakuwa na fursa ya kufika pale Nyakanazi kwenye kituo kikubwa hiki ambacho Serikali yetu kwa kushirikiana na Halmashauri zetu imeanga kukijenga kuanzia sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye swali la Mheshimiwa Gashaza kuhusu Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kujenga masoko haya pale Rusumo na Kabanga, nilifika pale Kabanga na kuona hali halisi ilivyo na tayari upo mradi ambaao unaendelea wa ujenzi wa soko la kimataifa pale Kabanga ambapo naamini ndani ya miaka miwili litakuwa limekamilika na wananchi wetu watakuwa wamefikiwa ili wawze kuuza mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo, kule Rusumo pia Serikali ipo kwenye mpango wa kuhakikisha tunaanzisha

soko ili kuhakikisha sasa wananchi wetu wa Kagera wananaufaika na jiografia yao ya kupakana na nchi zilizozunguka. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, naamini Mheshimiwa Halima jibu umepata sasa hivi. Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako sasa aulize swali lake.

Na. 226

### **Ujenzi wa Mradi wa Maji – Makambako**

**MHE. DEO K. SANGA** Aliuliza:-

Serikali ilikopa fedha za mkopo nafuu kutoka Serikali ya India kwa ajili ya miradi 26 ya maji ikiwemo Mji wa Makambako.

Je, ni lini mradi huo wa maji utanza na kukamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepata mkopo wenyewe masharti nafuu wa dola za Marekani milioni 500 kutoka Serikali ya India kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji katika miji 28 kwa upande wa Tanzania Bara na mradi mmoja upande wa Zanzibar. Utekelezaji wa miradi hiyo umegawanyika katika awamu mbili; awamu ya kwanza ni usanifu na awamu ya pili ni ujenzi wa miradi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Wizara imefikia katika hatua za mwisho za kumpata mtaalam mshauri kwa ajili ya kuandaa ripoti (*detailed project report*). Baada ya ripoti ya mradi kukamilika, Wizara itaendelea na hatua ya kutafuta wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa miradi. Ujenzi wa miradi hiyo unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wa kukamilika miradi hiyo utajulikana mara baada ya usanifu kukamilika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Sanga, Mheshimiwa Balozi Adadi.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 11 Aprili, 2019 kwa kuwa Waziri aliapa mbele ya wananchi wangu na mbele ya Rais alipokuja tarehe hiyo. Je, ni lini mradi huu utaanza na ni mwezi gani utaanza ili wananchi wangu waendelee kuwa na imani kutokana na kiapo alichokifanya siku ile? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, siku ile kulikuwa na changamoto ya Mradi wa Ngamanga, kwa kuwa siku ile ilionekana ni lazima wataalam wabaki pale ili waweweze kutatua tatizo hili; ni lini sasa hatua zilizochukuliwa ili kutatua mradi huu wa Ngamanga? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Sanga kwa kazi kubwa sana anayoifanya katika Jimbo lake la Makambako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kabisa Mheshimiwa Rais alivyofanya ziara na Mheshimiwa Waziri wetu alitoa *commitment* ya kuhakikisha mradi huu

utatekelezeka haraka. Nataka nimtoe hofu kabisa sisi kama Wizara tumejipanga na tunatambua kabisa agizo la Mheshimiwa Rais kwamba tukishindwa kutekeleza mradi huu, tutatumbuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara ya Maji hatupo tayari kutumbuliwa, tutafanya kuusaini mkataba ule haraka ili utekelezaji wa miradi ya maji miji hii 28 utekelezwe kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa katika mradi ule wa Ngamanga, tulishatuma wataalam wetu na tumeshaangiza mabomba, kuna kazi inaendelea naamini ndani ya muda mfupi utakamilika na wananchi wake watapata maji safi, salama na yenye kuwatoshaleza. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Balozi Adadi.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mji wa Muheza ni mojawapo ya sehemu ambazo zitafaidika na mradi huu kutoka India. Vile vile wakati wananchi wa Muheza wanasubiri mradi huu ambaao ni mkubwa, upo mradi mwengine wa kutoa maji katika Mji wa Pongwe na kuleta Muheza Mjini. Mradi huu umefikia asilimia 70 na tumebakiza asilimia 30 tu ili wananchi wa Muheza waanze kupata maji ya uhakika. Tatizo ni uchakavu wa mabomba ambayo yako pale Mjini Muheza. Nataka kujua, ni lini Serikali itaruhusu mabomba yale yaanze kufumuliwa na kazi hiyo ianze kufanyika ili maji hayo yaweze kuunganishwa kuja Mjini Muheza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, amekuwa mfuutiliaji mkubwa sana, hususan katika suala zima la utatuzi wa maji katika Jimbo lake la Muheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Balozi Adadi ameshakutana na Mheshimiwa Waziri na tumeshakubaliana kwamba sasa ile kazi ya kuhakikisha tunaondoa yale mabomba inafanyika mara moja. Nami kama Naibu Waziri tutalismamia katika kuhakikisha ile kazi inaanza na wananchi wake waweze kupata maji safi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuuliza, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa mradi mkubwa wa kuboresha upatikanaji wa maji katika Jimbo la Rombo kadiri ya mpango ambao tumeupeleka Wizarani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Mbunge, amekuwa akiuliza swali la Rombo mara kwa mara na tumeshakubaliana tutakwenda Rombo, lakini kikubwa tunashukuru kwanza Bunge lako Tukufu limetuidhinishia kiasi cha shilingi bilioni 610 katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo kwa wananchi wa Rombo kupata maji safi, salama na yenye kuwatoshaleza. (Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale, Mbunge wa Kilwa Kaskazini.

Na. 227

**Kufanya Tathmini Miradi ya Maji Chini ya Benki ya Dunia – Kilwa Kaskazini**

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE** aliuliza:-

Benki ya Dunia imefadhili miradi ya visima kumi (10) katika kila wilaya nchini:-

Je, Serikali imefanya tathmini kujua asilimia ya miradi iliyofanikiwa na ambayo haikufanikiwa; na kwa ile ambayo haikufanikiwa, Serikali haioni haja ya kuingiza fedha ili kukamilisha miradi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale, Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016, Wizara ya Maji ilifanya tathmini ya kina nchi nzima ili kujua idadi ya visima vyote vilivyochimbwa kwa Awamu ya Kwanza ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji katika Halmashauri zote Tanzania Bara. Idadi ya visima vilivyochimbwa ni 1,485. Kati ya hivyo, visima 990, sawa na asilimia 67 vilipata maji na visima 495 sawa na asilimia 33 vilikosa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo visima vyake vilikosa maji Serikali ilitumia vyanzo vingine mbadala kama vile chemchemi, mito, maziwa au kujenga mabwawa ili kuhakikisha maeneo yaliyopewa kipaumbele katika mpango wa vijiji 10 yanapata huduma bora ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali imeanzisha Mfuko wa Maji wa Taifa ambao unalipa miradi yote iliyochelewa kukamilika na miradi mipya inayoendelea kujengwa katika Halmashauri zetu. Lengo ni kuhakikisha huduma bora ya maji kwa kila mwananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngombale, halafu Mheshimiwa Bungara

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa mradi wa Mingumbi – Miteja ambao umekamilika, Kijiji cha Njia Nne ambacho kimepitisha na mradi huo hakikupata maji: Je, Serikali sasa iko tayari kusambaza maji kwa Kijiji hiki cha Njia Nne ili kuondokana na tatizo la maji ambalo liko pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; mwaka 2017, Wakala wa Serikali (*DDCA*) ilifanya mkataba na Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa kuchimba visima virefu 21, lakini mpaka sasa wamechimba visima vitatu tu katika vijiji 18. Sasa je, *DDCA* iko tayari kuchimba visima virefu hivyo, au nini sababu zilizowafanya *DDCA* wasichimbe visima virefu katika Viji ya Nampunga, Chumo, Mtundo wa Kimwaga, Nandembo, Kibata, Kinjumbi, Somanga na Marendego?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anafahamu nia ya Serikali yetu. Zaidi ya shilingi bilioni 4,668 ziliwekezwa pale katika kuhakikisha tunatekeleza Mradi wa Maji wa Mingumbi na Miteja katika jitihada za kutatua tatizo la maji. Nataka nimhakikishie kwamba nia ya Wizara yetu ni kuhakikisha Watanzania wanapata maji safi na salama. Tutafanya *extension* ili wa Kijiji kile cha Njia Nne nao waweze kupata maji safi na salama katika kuhakikisha tunamtua mwana mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala zima la uchimbaji wa visima, tulitenga kiasi cha shilingi milioni 456 katika kuhakikisha zaidi ya vijiji 19, ikiwa Kilwa Kusini na Kilwa Kaskazini vinapata huduma ya maji. Tuliwapa kazi hiyo *DDCA*, wamefanya kazi, lakini kulikuwa kuna ucheleweshaji mkubwa. Sisi kama viongozi wa Wizara tumeshamwondoa Mkurugenzi yule wa *DDCA* maana yake kulikuwa na ucheleweshaji. Yote hii ni kuweka mtendaji ambaye ataendana na kasi ya kuhakikisha tunatatua tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Ngombale, sisi kama Wizara ya Maji

tutahakikisha kwamba visima vilivyobaki vinachimbwa kwa wakati na wananchi wake waweze kupata maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selemani Bungara, halafu Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu hayo kuhusu Wilaya ya Kilwa, lakini Wilaya ya Kilwa kwenye Hospitali ya Wilaya kuna uhaba mkubwa wa maji: Je, Serikali inatuambia nini kuhusu jambo hili la Hospitali ya Wilaya kupata maji ya uhakika na salama?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bungara kwa swali fupi la Kibunge. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, sisi kama Serikali na Mheshimiwa Mbunge anatambua, ni mionganini mwa jithada ambazo tunazifanya katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji katika Jimbo lake la Kilwa Kusini. Yupo katika mpango wa miji 28, lakini kama unavyotambua, suala la hospitali ni suala la dharura sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubaliane na Mheshimiwa Bungara tukutane baada ya saa saba ili tuwasiliane na wataalam wetu tuangalie ni namna gani tunaweza tukawapatia wananchi wake huduma haraka katika suala zima la maji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja na nyongeza. Kwa kuwa Serikali ilikuwa na mpango wa kuchimba visima vya maji katika Vijiji vya Ng'hambi, Kiegea, Kazania na Chimaligo; na fedha zilitengwa, visima havijachimbwa? Mheshimiwa Waziri unaweza kuwaeleza wananchi wa vijiji hivyo fedha hizo zilikwenda wapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge. Kiukweli amekuwa mfuatiliaji mkubwa sana katika suala zima la maji. Ukimwona mtu mzima analia, ujue kuna jambo Mpwapwa. Sasa nataka nimhakikishie, kwanza nipo tayari kwenda Mpwapwa, lakini kuzifuatilia hizi fedha katika kuhakikisha zinafanya kazi na wananchi wake waweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali fupi la nyongeza.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa utekelezaji wa miradi ya maji unategemea na mpango wa fedha, natambua kuna baadhi ya Wakandarasi bado hawajalipwa fedha zao: Je, ni lini sasa Mkandarasi ambaye anatekeleza mradi wa Mji Mdogo wa Ilula katika Jimbo la Kilolo atapatiwa malipo yake ili wananchi wa Ilula waache kupatiwa migao ya maji mara kwa mara? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwapigania akina mama na Watanzania hususan katika suala zima la maji. Kikubwa, utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha. Kama unavyoona, gari haliwezi kwenda bila mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tulikuwa tunadaiwa takribani zaidi ya shilingi bilioni 88 na Wakandarasi, lakini tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na Wizara ya Fedha, wametupatia fedha zote shilingi bilioni 88 ambazo tulikuwa tunadaiwa na Wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, katika mradi wake ule wa Ilula kwa Mheshimiwa Mwamoto, Kilolo pale, tumeshamlipa zaidi ya shilingi bilioni moja. Tunataka zile fedha tulizomlipa sasa awekeze pale katika kuhakikisha anakamilisha mradi na wananchi wa Ilula waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatolesheleza.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mafupi yenye kueleweka. Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 228

### **Elimu ya Uraia na Haki za Binadamu**

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI** aliuliza:-

Ibara ya 13(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kwamba "Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria"; lakini kumekuwa na kiwango cha juu cha matukio na kesi zinazohusu kuvunjwa kwa haki za kiraia kwa kufanywa na vyombo vyaya dola:-

(a) Je, kwa kipindi cha mwaka 2010 – 2015 ni kesi ngapi zimefunguliwa Mahakamani kuhusu madhara yanayofanywa na vyombo vyaya dola dhidi ya raia, na huchukua muda gani hadi kutolewa hukumu?

(b) Je, kesi hizo zimekuwa zikigharamiwa kwa kiasi gani kutoka Mfuko wa Fedha za Umma tangu mwaka 2010 – 2015?

(c) Je, Serikali inafanya jitihada gani kuhakikisha wananchi wake pamoja na vyombo vyaya usalama wanapata elimu ya uraia?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka 2010 – 2015 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora hajafungua kesi yoyote Mahakamani kuhusu madhara yanayofanywa na vyombo vya dola dhidi ya raia. Tume imekuwa ikipokea malalamiko ya uvunjwaji wa haki za binadamu dhidi ya vyombo vya dola na kuyashughulikia kwa kufanya uchunguzi wa kawaida, usikilizwaji hadharani na kufanya usuluhishi na upatanishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbinu hizi zimeonekana kuwa na mafanikio makubwa katika kuwapatia wananchi haki yao wanayostahili, hivyo kutokuwa na umuhimu wa kufungua mashauri Mahakamani. Ikumbukwe kuwa ufunguaji wa mashauri Mahakamani ni hatua ya mwisho iwapo njia nyingine zote zimeshindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimeeleza, kwa kuwa Tume haijawahi kufungua kesi yoyote ya haki za binadamu katika Mahakama zetu kwa kipindi cha mwaka 2010 – 2015, hivyo basi, hakuna gharama zozote za ufunguaji wa mashauri Mahakamani zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka 2010 – 2015, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imefanya jitihada mbalimbali ili kuhakikisha wananchi pamoja na vyombo vya usalama wanapata elimu ya uraia. Jitihada hizo ni pamoja na kuelimisha Umma kuitia vyombo mbalimbali vya habari, mikutano, maadhimisho, machapisho na warsha mbalimbali katika kipindi cha 2010 hadi 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya vipeperushi na vijitabu 40,638, makala 18,300 za Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu, majarida yaliyowekwa kwenye tovuti ya Tume ni matano, vipindi vya redio na televisheni ni 115 na kufanya mikutano na wananchi kuhusu haki za binadamu

na hasa katika kumiliki ardhi kwenye mikoa 21 ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika kipindi cha kuanzia 2015 hadi sasa, jitihada hizi zimeendelea kufanya na Wizara yangu Waheshimiwa Wabunge na Bunge hili kwa ujumla kwamba haki zitakuwa zinatendeka na kwamba tunaendelea kubuni mbinu na mikakati mbalimbali itakayowezesha kuendelea kuwafikia wananchi wengi iwezekanavyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware, halafu Mheshimiwa Mwakajoka.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na majibu niliyoletewa na Serikali ni dhahiri kuwa suala hili bado halijawekewa mkazo na bado wananchi wanapata shida wakiwa mikononi mwa vyombo vyoma dola. Sasa Serikali haioni ni wakati sasa wa kujifanya tathmini mahususi na kuja na mikakati thabiti ili wananchi wa Taifa hili wapate kuwa na kusimamia haki zao? Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tathmini ni muhimu na ni endelevu. Wizara yangu inaendelea kufanya hivyo na kusisitiza kwamba Tume ya Haki za Binadamu inafanya hiyo. Pia ninapenda kusisitiza kwamba suala la haki za binadamu lazima iwe ni sehemu ya utamaduni wa Taifa; na kufanya ni sehemu ya utamaduni wa Taifa itabidi tutengeneze mkakati wa somo la Haki za Binadamu liingie katika mitaala ya shule zetu zote na katika ngazi zote. Somo la Haki za Binadamu na Utawala Bora liwe ni sehemu ya lazima kwa mafunzo yote ya vyombo vyetu vyoma usalama. Kama ni ulinzi, kama ni Polisi, Usalama wa Taifa au Uhamiaji, iwe ni sehemu muhimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Askari wetu wanaoshiriki katika vikosi nya kulinda amani duniani huwa wanapewa kozi ya haki za binadamu kwa wiki sita na Umoja wa Mataifa. Umoja wa Mataifa na Taasisi mbalimbali za Kimataifa ziko tayari kuisaidia Tanzania kuweka Chuo cha Haki za Binadamu ambacho kitatengeneza mitaala katika shule mbalimbali. Hiyo nimehakikishiwa na ninadhani inaweza kutokea tukishachukua maamuzi. Watu wako tayari kutusaidia ili haki za binadamu na utawala bora iwe ni sehemu ya utamaduni wa Taifa hili. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kila mwananchi wa Tanzania ana haki ya kulindwa na Serikali yake na sasa hivi kumetokea wimbi kubwa sana kwenye Nchi ya Afrika Kusini, wageni wanauawa, wanatekwa, wanachomwa moto na wanateswa sana. Je, Serikali ya Tanzania imechukua hatua gani kuwalinda Watanzania wote ambao wako Nchini Afrika Kusini kwa kipindi hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakajoka, hilo ni suala la kidiplomasia. Kwa hiyo...

**MBUNGE FULANI:** Ajibu.

**MWENYEKITI:** *No, ye ye ni Waziri wa Katiba na Sheria. Kwa hiyo, tuwaachie wenyewe Wizara ya Mambo ya Nje.*

**MBUNGE FULANI:** Yupo mwenye Wizara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Kabudi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivoyosema, suala hilo ni la Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje

na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Ni suala ambalo limekuja mahali pasipokuwa pake kwa sababu bado ipo siku ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na linaweza kuwa ni swali ambalo linajitegemea. Hata hivyo, msizoze, acha kuzoza. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwanza ninapenda kusema kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Afrika ya Kusini zina mahusiano mazuri sana ya kindugu na ya muda mrefu. Ndiyo maana nichukue fursa hii pia kumpongeza Cyril Ramaphosa kuchaguliwa kuwa Rais wa Afrika Kusini; na *inshallah* tukijaliwa tutahudhuria kuapishwa kwake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la usalama wa Watanzania siyo wa Afrika ya Kusini tu, usalama wa raia wa Tanzania popote walipo ni jukumu la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhakikisha Watanzania popote walipo wapo salama. Kwa hiyo, suala hilo linafutiliwa na Serikali ya Afrika Kusini yenye imeniandikia Nchi zote za Afrika; moja, kuomba radhi kwa yale yote yanayotokea nchini mwao ambayo yanaonekana kuwa ni ya ubaguzi na yanayoifanya Afrika ya Kusini ioneckane ni nchi ambayo haikumbuki ilivyosaidiwa na Waafrika wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali ya Afrika ya Kusini yenye imetuletea andiko kuititia Ofisi ya Ubalozi kuomba radhi kwa yale ambayo yanatokea. Nasi tunachukua hatua moja ya kuhakikisha raia wote waliko Afrika Kusini wako salama; na wale ambao watapata matatizo tumewaambia watoe ripoti kwenye balozi zetu ili hatua za kuwalinda na usalama wao kuwepo zichukuliwe. Kwa hiyo, hilo ndilo jibu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa Wabunge, naamini Serikali haiwezi kukaa kimya ikiwa kama hilo tatizo lipo na ninaamini litashughulikiwa tu kama lipo kweli.

Tunamalizia swalii la mwisho; Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Maulid Said Mtulia, Mbunge wa Kinondoni, aulize swalii lake.

Na. 229

### **Kipato Duni kwa Kazi za Sanaa**

**MHE. MAULID S. A. MTULIA** aliuliza:-

Vijana wetu wanafanya kazi za sanaa nzuri sana lakini kipato wanachokipata hakilingani na ubora wa kazi zao:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia vijana hawa kupata stahiki ya kazi zao?

(b) Je, sera na sheria zinasaidiaje wasanii wetu kumililiki na kunufaika na kazi zao za sanaa?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Maulid Said Mtulia, Mbunge wa Kinondoni, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Utamaduni ya Mwaka 1997 inaelekeza kuanzishwa kwa chombo cha kusimamia hakimiliki ambayo ni sehemu muhimu ya dhana pana ya haki bunifu (*intellectual property*). Hivyo, mwaka 1999 ikatungwa Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki ambayo chini yake maslahi ya watunzi wa kazi za Sanaa, watafsiri, watayarishaji wa kuhifadhi sauti, wachapishaji na kadhalika yanalindwa kisheria na chombo cha kusimamia haki hizo, yaani Chombo cha Hakishiriki Tanzania (*COSOTA*).

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swalii hilo.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA  
MICHEZO alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maulid Said Mtulia, Mbunge wa Kinondoni, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997 inaelekeza kuanzishwa kwa chombo cha kusimamia haki miliki ambayo ni sehemu muhimu ya dhana pana ya haki bunifu (*intellectual property*). Hivyo, mwaka 1999 ikatungwa Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki ambayo chini yake maslahi ya watanzi wa kazi za sanaa, watafsiri, watayarishaji wa kuhifadhi sauti, wachapishaji, na kadhalii yanalindwa kisheria na chombo cha kusimamia haki hizo yaani Chama cha Hakishiriki Tanzania (*COSOTA*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, sera na sheria vipo kulinda maslahi ya wasanii lakini tatizo ni uelewa mdogo wa wasanii wenyewe kuhusu haki zao na ulinzi wake kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na tatizo hilo, Serikali kupitia Bodi ya Filamu Tanzania na Baraza la Sanaa la Tanzania imetoa elimu kwa wadau 5,200 kuhusu masuala ya hakimiliki, hakishiriki, mikataba na makubaliano kupitia mafunzo ya kuwajengea uwezo ili wawe walinzi wa kwanza wa kazi na haki zao kwa kuingia mikataba yenye maslahi. Aidha, Serikali imeandaa mikataba ya mfano ya kutumiwa na wadau wa sanaa pale wanapohitaji. Mikataba hii imewekwa katika lugha nyepesi za Kiswahili na Kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe wito kwa wadau wa sanaa kuhakikisha wanasajili kazi zao *COSOTA* ili kulinda na kuweka mazingira mazuri yatakayovirahisishia vyombo va kisheria kusimamia haki zao. Hata hivyo, Serikali inaendelea na mchakato wa kuifanya mabadiliko Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa ya mwaka 1984 ili iendane na mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wasanii walioingia mikataba mibovu bila kujua, Serikali iliunda Kamati ya kupitia mikataba isiyo na tija katika wasanii na makampuni ambapo jumla ya mikataba kumi na moja (11) ilipitiwa na baadhi ya kampuni zimeridhiana na zimeanza kulipa kiasi cha fedha kwa wasanii au familia zilizowasilisha malalamiko yao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtulia.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanzu kabisa nitoe shukrani zangu za dhati kwa majibu mazuri ya Serikali. Vilevile niendelee kuhimiza Serikali kwamba mabadiliko ya Sera na Sheria ya Bodi ya Filamu yafanyike kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa wasanii wetu wamedhulumiwa kazi zao na wasambazaji walikuwa wanawaingiza mikataba kama wasimamizi badala ya wamiliki wa kazi; kwa kuwa sheria ipo kulinda haki za wasanii; na kwa kuwa nchi za wenzetu mfano Nigeria iliwhi kutoa tamko kuhakikisha kazi zote za wasanii umiliki urudishwe kwa wasanii wenyewe, je, Serikali yetu ya Tanzania iko tayari sasa kutoa tamko kuhakikisha wale wote waliodhulumu kazi za wasanii umiliki unarudi kwa wasanii wenyewe ili waweze kunufanika? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa wasanii wetu wanaendelea kuzalisha kazi nzuri kabisa; na kwa kuwa walaji wengi katika jamii wanahitaji kuendelea kuziona kazi za wasanii na katikati yake kuna ombwe kubwa kwamba wasanii, waandaaji na walaji hawaonani, je, Serikali ipo tayari kuja na suluhisho kuhakikisha kazi za wasanii zinafika kwa walaji ili wasanii waepukane na kutembeza *CDmkononi* wao wenyewe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

## **NAIBU WAZIRI WA HABARI UTAMADUNI, SANAA NA**

**MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Said Mtulia, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni kwa jinsi ambavyo amekuwa akipambania maslahi ya wananchi wa Kinondoni, ukizingatia kwamba wasanii wengi walioko katika jiji la Dar es Salaam wanaishi katika Wilaya yake ya Kinondoni. Kwa hiyo, nampongeza sana kwa kupambania maslahi ya wasanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na swalı lake la kwanza ambapo ametaka kujuua kama Serikali tuna mpango gani wa kurejesha zile hakimiliki ambazo zimechukuliwa kutoka kwa wasanii. Kama ambavyo nimejibu kwenye jibu langu la msingi kwamba kwa Sheria ya Hakimiliki ya mwaka 1999 ambayo tunayo sasa hivi inatoa haki na uhuru kwa msanii mwenyewe kuamua ni namna gani ambavyo atataka kuuza haki yake. Kama akitaka kuuza kazi zake zote kwa maana kwamba anauza pamoja na ile *master* ya kazi yake au kuuza baadhi kazi zake. Kwa hiyo, ni suala la msanii mwenyewe kuamua anataka kuuza kazi zake kwa njia gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi kama Serikali kwa kutambua kwamba suala hilo limeleta mchanganyiko mkubwa sana na halina maslahi kwa wasanii, kitu ambacho tunafanya kwanza ni kutoa elimu kwa wasanii kuweza kutambua haki na thamani ya kazi zao, kwa sababu tumeona madhara makubwa sana ambayo yamekuwa yakiwapata wasanii pale ambapo wanauza mpaka umiliki wa zile kazi zao. Kwa hiyo, tunaelimisha wasanii kwanza waweze kutambua kwamba kazi zao zina thamani, ukiiza leo kazi yako pamoja na *master* ni kitu ambacho kitaendelea kutumika miaka mingi matokeo yake hayatakuwa mazuri kwa miaka ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaendelea kutoa wito kwa wasanii wote nchini Tanzania kwanza kutambua thamani ya kazi yao na kuona kwamba siyo jambo jema kuuza mpaka umiliki wa kazi zao. Hata hivyo, kwa sheria ambayo tunayo inatoa haki kwa msanii kuamua ni namna gani ambavyo atauza kazi yake. Kwa hiyo, sisi kama Serikali

hatuwezi kutoa kauli ya moja kwa moja kwa sababu sheria imewapa uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikija kwenye swalii lake la pili ambalo amezungumzia kuhusu tatizo la usambazaji, ni kweli kwamba kwa miaka ya hivi karibuni tasnia yetu ya sanaa imekumbwa na changamoto nyingi ikiwepo suala la usambazaji. Kama ambavyo tunajua tatizo la usambazaji kwa miaka ya hivi karibuni liliisababishwa na kukosekana kwa kazi ambazo zina ubora na ubunifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usambazaji ni biashara kama biashara zingine. Kwa hiyo, sisi kama Wizara tunaamini kwamba hakuna mfanyakia biashara atawekeza mtaji wake kwenye biashara ambayo anaamini kwamba haiwezi kumpa faida hapo baadaye. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tunaendelea kutoa wito kwa wasanii kwanza kutengeneza kazi ambazo zina ubora na zitaleta ushindani kwenye soko lakini zitavutia wasambazaji wengi kuja kuwekeza mitaji kwenye kazi zao hiso.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwa sababu tunajua kwamba sasa hivi pia kuna mabadiliko ya sayansi na teknolojia na tumeshuhudia wasanii wengi sana wamehama kutoka kwenye mfumo wa kusambaza kazi zao kwa njia ya *CDwanatumia* njia ya mtandao. Kuna msanii anaitwa Wema Sepetu, kwenye filamu yake ya *Heaven Sent*. amefanya vizuri sana, amesambaza kazi yake kwa njia ya mtandao na mauzo yamekuwa mazuri. Kwa hiyo, nitoe wito kwa wasanii sasa waangalie namna gani ambavyo wataenda mbele zaidi kwa mabadiliko haya ya sayansi na teknolojia ili waanze kusambaza kazi zao kwa njia ya kimtandao.

**MWENYEKITI:** Kwa namna ya pekee Mheshimiwa Profesa Jay, swalii fupi la nyongeza.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi ya kuuliza swalii dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasanii wa Tanzania changamoto yao kubwa sana na namba moja ambayo inawakabili ni wizi wa kazi zao. Tumekuwa tukiona kazi zao zikiuzwa kwa holela kwenye maeneo mbalimbali lakini Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki, Na.7 ya mwaka 1999 imeonekana kuwa haina meno wala haiwasaidii wasani wa Tanzania. Je, ni lini Serikali italeta sheria hii hapa Bungeni ili tuweze kuifanya mabadiliko ili wasanii wa Tanzania ambao wanaleta sifa kubwa kwa Tanzania kwa kupitia sanaa yao waweze kufaidika na kazi zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Profesa Jay kwa swali nzuri la nyongeza kwa sababu yeye pia ni msanii, kwa hiyo, anatambua changamoto ambazo zinawakumba wasanii nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna changamoto kubwa sana ya suala la wizi ya kazi za sanaa, lakini sisi kama Wizara tumechukua hatua kadhaa. Hatua mojawapo ni kuhakikisha kwamba tunawahamasisha wasanii waweze kusajili kazi yao *COSOTA* ili pale ambapo wanapata matatizo iwe rahisi kuweza kusaldiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile amezungumzia changamoto kubwa ya sheria, tukiri kwamba hii sheria ina upungufu lakini Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki ipo kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara, kwa hiyo, kama Wizara ambacho tunafanya sasa hivi ni kuhakikisha kwamba kitengo hiki cha *COSOTA* kinahama kutoka Viwanda na Biashara kuja kwenye Wizara yetu ya Habari ili tuangalie ni namna gani ambavyo tutaifanyia marekebisho sheria hii. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, muda wetu wa maswali umeisha na sasa ni muda wa matangazo na nitaanza na wageni waliopo Bungeni asubuhi

hii. Nitaanza na wageni waliopo kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika amba ni wageni watano wa Mheshimiwa Spika kutoka *HAWA Foundation* amba wamekuja Bungeni kutambulisha miaka kumi ya kipindi cha *Wanawake Live* amba ni Ndugu Joyce Kiria - Mkurugenzi; Ndugu Elizabeth Mwakinga -Meneja wa Mradi; Ndugu Hellen Baja - Afisa; Ndugu Prosper Njau - Afisa; Ndugu Amen Ntangu - Mwalimu wa Ujasiriamali. Karibu sana wageni wa kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

Wageni 73 wa Mheshimiwa Joseph Kakunda ambaye ni Waziri wa Viwanda na Biashara amba ni Dkt. Binilith Mahenge - Mkuu wa Mkoa wa Dodoma; Prof. Joseph Buchweishaija - Katibu Mkuu; Ndugu Ludovick Nduhiye - Naibu Katibu Mkuu Viwanda; Dkt. Edwin Mhede - Naibu Katibu Katibu Biashara na Dkt. Adelhem Meru - Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Vipimo Nchini (WMA). Karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Wageni wengini wa Waziri ni Dkt. Ng'wanza Kamata Soko - Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara ya Tanzania; Prof. Humphrey P.B. Moshi - Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya Ushindani; Prof. Makenya Maboko - Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*); Prof. Esther Ishengoma - Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE); Dkt. Samwel Nyantahhe - Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*) na Prof. Patrick Makungu - Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wengine wa Waziri ni Ndugu John M. Lyanga - Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA); Dkt. Godfrey Simbeye - Mkurugenzi Mtendaji wa Sekta Binafsi Tanzania; Bw. L.C. Tenga – Mkurugenzi Mtendaji (CTI); Dkt. John Ulanga - Mkurugenzi Mkazi (*TMEA*); na Ndugu Mohamed Kiliwa - Mkurugenzi Mtendaji Kiliwa Group. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Wageni wengine ni wa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya amba

ni Mwalimu Juliana Godfrey na M.V. Bimbinga kutoka *High School* ya Kilakala. Karibuni sana katika Bunge letu. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, kulikuwa na wageni wa Jukwaa la Spika nilikuwa sijawamalizia, kuna Ndugu Octavia Mshiu -Kaimu Rais wa *TCCIA*. Pia wameambatana na Wakurugenzi wakuu wa Idara na Vitengo na Maafisa wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. (Makofi)

Wageni wengine ni wa Mheshimiwa Joseph Kakunda ambao ni familia yake ambao ni Mhandisi Kalunde Malale (mke wake); Ndugu Rahma Mkambo (shemeji yake) na Ndugu Malunga Mwakibete (Ndugu yake). Karibuni sana familia hii ya Mheshimiwa Kakunda. (Makofi)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kuna Wageni 12 wa Wabunge wa Wilaya ya Ilala, Jijini Dar es Salaam, Madiwani 12 ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Maadili ya Manispaa ya Ilala wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Manase John Mjema. Karibuni sana Madiwani wetu kutoka huko Ilala. (Makofi)

Wageni 6 wa Mheshimiwa Mwitwa Waitara (Mb), Naibu Waziri wa TAMISEMI ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Tarime Mkoani Mara. (Makofi)

Mgeni wa Mheshimiwa Jumaa Aweso, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambaye ni ndugu yake kutoka Pangani, Mkoani Tanga, Ndugu Ronald Moses. Karibu sana Bungeni. (Makofi)

Wageni 53 wa Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, kutoka Wilayani Muheza Mkoani Tanga wakiongozwa na Katibu wa CCM wa Wilaya, Ndugu Mohamed Moyo. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Adadi, wakiwasilishwa na Katibu wa CCM, Ndugu Mohamed Moyo. (Makofi)

Wengine ni wageni 15 wa Mheshimiwa Mary Chatanda ambao ni Viongozi wa Umoja wa Vijana kutoka

Korogwe, Mkoa wa Tanga wakiongozwa na Ndugu Lwiza Maungu. Karibuni sana wageni wetu wa Mheshimiwa Mary Chatanda. (*Makofi*)

Wageni 67 wa Mheshimiwa Agnes Marwa ambao ni Madiwani, Wenyevit na Makatibu wa UWT kutoka Wilayani Musoma, Mkoa wa Mara. Karibuni sana akina mama kutoka Mkoa wa Mara. (*Makofi*)

Wageni 31 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ambao ni Wanakwaya ya VCC *Praise and Worship Team* - Kanisa la *Assemblies of God*. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Mariam Ditopile ni mjasiriamali anayemiliki kiwanda kidogo cha *furniture* kutoka Mkoa wa Dar es Salaam ambaye ni Ndugu Leila Salim Machaeke. Karibu sana dada, hongera kwa kazi. (*Makofi*)

Wageni wawili ni wa Mheshimiwa Flatei Massay ambao ni Daktari kutoka Hospitali ya Haydom kutoka Babati, Mkoani Manyara Dkt. Emmanuel Boa na mpiga kura wake kutoka Mbulu Vijijini, Mkoani Manyara ambaye ni Ndugu Adam Getagno. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Wageni 19 wa Sophia Mwakagenda ambao ni Mtume Joseph Goliama na timu yake ya huduma kutoka Moshi Mkoa wa Kilimanjaro. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Sophia. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Kanal (Mst) Masoud Ali Khamis ambao ni Ndugu Ezekiel Shamakala na Ndugu Hawa Dalonya. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Kuna wageni ambao wapo hapa Bungeni leo kwa ajili ya mafunzo ni Wajumbe 100 kutoka Kongamano la Wanaume, Jumuiya Kuu ya Wabaptist wa Tanzania wakiongozwa na Mch. Anthony Mlyashimba. Karibuni sana Bungeni. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo lingine la mwisho, Wabunge wote wa imani ya Kikristo wanatangaziwa kuhudhuria Ibada katika Chapel ya Pius Msekwa, leo siku ya Jumanne, tarehe 14 Mei, 2019, saa saba mchana. Aidha, katika ibada hiyo Mtume Joseph Goliama, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Urejesho wa Maadili ya Taifa (TUMATA) atahudumu. Kwa hiyo, Wakristo wote mnakaribishwa hapo Pius Msekwa saa saba kamili mchana.

Katibu, tuendelee.

**WABUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kutokana na umuhimu wa shughuli za leo sitapokea mwongozo wowote kwa mujibu wa Kanuni ya 5. Tunaendelea, Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Viwanda na Biashara**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Waziri wa Viwanda na Biashara ili awasilishe hotuba ya bajeti ya Wizara yake kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Karibu sana Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda Biashara na Mazingira ambayo ilichambua bajeti ya Wizara Viwanda na Biashara, Fungu 44 na Fungu 60, tarehe 26 na 27 Machi, 2019, Jijini Dodoma, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji ya mpango na bajeti ya mwaka 2019/2020 na kuitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake imara, wenye uzalendo na mapenzi kwa Tanzania na Watanzania. Pia nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa miongozo yao thabiti inayolenga kuhakikisha maslahi na maendeleo kwa Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukupongeza wewe binafsi na uongozi wa Bunge kwa ujumla Spika, Naibu Spika na Wenyeviti kwa kuliongoza na kulisimamia vema Bunge letu. Pia naipongeza na kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira chini ya Mwenyekiti wa Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, Mbunge wa Mvomero na Makamu wake Mheshimiwa Kanali (Mst) Ali Khamis Masoud, Mbunge wa Mfenesini na Waheshimiwa wajumbe wote wa Kamati, ushauri na maelekezo yao yamekuwa muhimu sana kwa utendaji kazi wa Wizara yangu na kwa Watanzania kwani yamekuwa yakichochea kasi ya maendeleo ya viwanda na biashara nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya waliochaguliwa kupitia Uchaguzi Mdogo ambao ni Mheshimiwa Christopher Kajoro Chiza, Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mheshimiwa James Kinyasi Millya, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mheshimiwa Pauline Phillipo Gekul, Mheshimiwa Ryoba Chacha Marwa na Mheshimiwa Abdallah Ally Mtalea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri wapya kwa kuteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, nimshukuru Mheshimiwa Charles Mwijage, Mbunge wa Jimbo la Muleba, aliyekuwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa ushirikiano anaonipa hadi sasa. Nikiri kuwa wakati akiongoza Wizara hii aliweka misingi ambayo ni chachu katika kuendeleza sekta ya viwanda na biashara nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapa pole familia, ndugu, wananchi na jamaa, kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani (Profesa Maji Marefu) aliyekuwa Mbunge wa Korogwe Vijiini. Nawapa pia pole nydingi Waheshimiwa Wabunge waliopata misiba ya kufiwa na wazazi, watoto na wanafamilia wa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, natoa pole kwa Watanzania waliokubwa na kadhia na majanga mbalimbali, kama vile ajali za majini, barabarani na majanga mengine yanayofanana na hayo. Nitoe pole maalum kwa wawekezaji wenye viwanda, biashara na sekta binafsi kwa ujumla kwa hivi karibuni kuondokewa na viongozi muhimu kwenye sekta binafsi hususan Marehemu Dkt. Reginald Mengi na Mhandisi Aloyce Mwamanga. Tunamuomba Mungu awape uvumilivu, ujasiri, faraja na nguvu wafiwa wote na kwetu sote atuwezeshe kuendeleza mikakati muhimu waliyokuwa wakiisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii pia kuwashukuru viongozi na watendaji wote wa sekta binafsi hususan Baraza la Taifa la Biashara Tanzania, Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania, Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania, Chama cha Wafanyabiashara Viwanda na Kilimo Tanzania, Baraza la Kilimo Tanzania, Chama cha Wadau wa Ngozi Tanzania, Chama cha Wafanyabiashara Wanawake na Vikundi vyat Biashara Ndogo (VIBINDO) kwa michango yao

katika kuendeleza sekta ya viwanda, biashara masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo. Kwetu sisi, hao ni mionganoni mwa wadau wetu muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru viongozi na watumishi wenzangu Wizarani wakiwemo Naibu Waziri Mheshimiwa Mhandisi Stellah Manyanya, Katibu Mkuu -Profesa Joseph Buchweishaija, Naibu Katibu Mkuu – Ndugu Ludovick Nduhiye, Naibu Katibu Mkuu - Dkt Edwin Mhede, Wakuu wa Idara, Wakuu wa Vitengo, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na watumishi wote kwa kujituma wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba sasa niwasilishe kwa ufupi mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu kwa kipindi cha mwaka 2018/2019 na makadirio ya mapato na matumizi kwa kipindi cha mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2018/2019, utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara unazingatia vipaumbele vyaya dira ya Taifa ya Maendeleo, Malengo Endelevu ya Maendeleo, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Ilani ya Uchaguzi ya CCM, Mpango wa Maendeleo wa Mwaka na Maelekezo ya Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda, Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo, Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo na Sera ya Taifa ya Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019, Wizara ya Viwanda na Biashara, iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 143.33 kati ya hizo shilingi bilioni 100.02 ni za maendeleo na shilingi bilioni 43.3 ni za matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019, Wizara imesajili miradi mipy ya viwanda 304. Kati ya hiyo miradi 107 ilisajiliwa chini ya Kituo cha Uwekezaji (TIC); miradi mitatu ilisajiliwa chini ya Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kuzalisha Bidhaa kwa Mauzo ya Nje (EPZA) na miradi 194

ilisajiliwa moja kwa moja na *BRELA*. Miradi hiyo inatarajiwa kuongeza jumla ya ajira 11,793.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhudumia maendeleo ya viwanda vidogo nchini, SIDO imeendelea kutoa mitaji midogo, mafunzo, ushauri katika uendeshaji pamoja na kuzalisha na kusambaza teknolojia ambapo katika mwaka 2018/2019 zimevezesha kuanzishwa viwanda vipyta vidogo 1,400 vilivyozaajira 4,200. Hadi sasa inakadiriwa kuwa sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo inatoa ajira kwa Watanzania zaidi ya milioni 8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya utendaji vilivyoanzishwa na Sheria ya EPZA. Tangu Mamlaka ya EPZA vilivyoanzishwa hadi sasa imetoa leseni za viwanda 169 vilivyowekeza mitaji yenye thamani ya dola za Marekani billioni 2.2 ambayo imetoa ajira za moja kwa moja viwandani 56,312. Aidha, mauzo ya bidhaa nje ya nchi yenye thamani ya dola za Marekani billioni 2.242 yamepatikana. Katika mwaka 2018/2019, Mamlaka ya EPZA imesajili viwanda vitatu vyenye mitaji ya thamani ya dola za Marekani milioni 45.7 vinavyotoa ajira mpya 815.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vilivybinafsishwa na ambavyo havikubinafsishwa. Kati ya viwanda 156 vilivybinafsishwa viwanda 42 vinafanya kazi vizuri sana, viwanda 46 vinafanya kazi kwa kiasi cha kuridhisha (*satisfactory*), viwanda 20 vimefutwa kwenye daftari la orodha ya viwanda kwa sababu ubinafsishaji wake ulifanywa kwa kuza mali moja moja. Viwanda vingine 48 wamiliki waliouziwa wameshindwa kuvientesha kwa mujibu wa mikataba ya mauziano na hivi sasa tayari viwanda 16 vimerejeshwa Serikalini na wamiliki wa viwanda 32 wamepewa notisi inayowataka kuwasilisha mipango ya kuviendozea kabla ya tarehe 31 Mei, 2019 vinginevyo vitarejeshwa Serikalini mara moja ili vitafutiwe wawekezaji wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya viwanda ambavyo vimesharejeshwa Serikalini vimebainika kuwa

nyaraka za viwanda hivyo zilitumika kuchukulia mikopo mikubwa mno ukilinganisha na thamani iliyotumika wakati wa binafishajhi na wakopaji wengine hawajalipa mikopo hiyo na baadhi yao wameshindwa kukabidhi nyaraka za viwanda hadi sasa.

Napenda kuchukua nafasi hii kuwatahadharisha wahusika wote walio ndani na nje ya nchi kwamba kwa kufanya hivyo walitenda kosa la kuhujumu uchumi, nawaonya kwamba wahakikishe wamemalizana na mabenki kwa kulipa mikopo yao yote ifikapo tarehe 31 Mei, 2019 vinginevyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa. Aidha, nimeagiza ifanyike tathmini ya viwanda 13 ambavyo havikubinafsishwa ili kuhakikisha ndani ya mwaka ujao vyote vinafufuliwa ili vifanye kazi kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vipyta vinavyomilikiwa na Serikali. Kiwanda cha Viuadudu cha Kibaha kinachomilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 huzalisha na kusambaza dawa za kuua viluwiluvi na wadudu ikiwemo mbu ambao husababisha ugonjwa wa malaria nchini na magonjwa mengine ikiwemo dengue. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto imeagiza lita laki mbili zenyet thamani ya shilingi bilioni 2.64 na TAMISEMI imeagiza viuadudu vya shilingi bilioni 8.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aidha, nchi za Angola na Eswatini zimeonyesha nia ya kununua viuadudu vyenye thamani ya shilingi bilioni 13.053. Natoa wito kwa taasisi nyingine na watoa huduma wengine ikiwemo mahotelii wanunue viuadudu hivyo ili wanyunyize kwenye maeneo yao ili kuua kabisa mbu na mazalia yao na hatimaye kutokomeza kabisa magonjwa kama malaria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Matrekta aina ya URSUS. Mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili, 2019, *NDC* imewezesha kuunganishwa jumla ya matrekta 536 katil ya viambata vya matrekta 822 vilivyopokelewa kutoka Poland. Aidha, matrekta 399 yameuzwa mikoa mbalimbali nchini

yakiambatana na majembe ya kulimia 399 na majembe ya kusawazisha 186.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa viwango kwa bidhaa zinazosalishwa viwandani ndani ya nchi. Hadi kufikia Aprili, 2019, *TBS* ilitayarisha na kukamilisha jumla ya viwango vypa 195. Kati ya hivyo, viwango 26 ni vya uhandisi mitambo, viwili vya uhandisi umeme, 20 ni viwango mtambuka, 31 ni viwango vya kemikali, 20 ni viwango vya nguo na ngozi, 18 vya ujenzi, 9 vya mazingira, 14 vya madini na 55 ni vya sekta ya kilimo na chakula. Aidha, *TBS*ilitoa leseni 191 za nembo ya ubora zikiwemo leseni 29 zilizotolewa kwa wajasiriamali wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa ubora wa bidhaa kutoka nje. Katika kipindi cha Julai 2018 hadi Aprili 2019, *TBS*ilitoa jumla ya vyeti vya ubora 25,605 kwa shehena za bidhaa zinazotoka nje ya nchi na vyeti vya ubora kwa magari 30,580 yaliyokidhi viwango. Bidhaa zisizokidhi viwango huteketezwa au kurudishwa zilikotoka ili kulinda viwanda vya ndani na afya za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa bidhaa bandia na hafifu. Hadi kufikia Desemba 2018, Tume ya Ushindani ilikuwa imekamata makontena 82 kwa kukiuka Sheria ya Alama za Bidhaa ikiwemo kuingiza nchini bidhaa bandia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya kimkakati. Mradi wa Mchuchuma na Chuma cha Liganga. Miradi ya Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga, inatekelezwa na Kampuni ya *Tanzania China International Mineral Resources Ltd.* ambayo ni ya ubia kati ya Serikali ya Tanzania kupitia *NDC* na *Sichuan Hongda Group* ya China. Maandalizi yote muhimu ya kuanza ujenzi wa miradi hiyo ikiwemo leseni za uchimbaji madini, vyetu vya mazingira, vibali vya kutumia maji ya Mito ya Katewaka, Mchuchuma na Lupali vilishatolewa tangu mwaka 2014. Mradi huo unganishi ulifuzu kupata hadhi ya mwekezaji mahiri na hivyo kupewa vivutio maalumu vya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo wakati mradi ukiwa tayari kuanza utekelezaji Julai 2017, mwekezaji aliomba vivutio vipyta vya ziada. Wakati majadiliano yanaendelea kuhusu vivutio hivyo vya ziada, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha Sheria Na. 5 Na. 6 za ulinzi wa maliasili za nchi ili kukidhi matakwa ya Ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Azimio la Umoja wa Mataifa Na. 1803. Kulingana na sheria hizo mbili; yaani *Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, 2017* na *Natural Wealth and Resources Contract Review & Re-Negotiation of Unconscionable Terms Act, 2017*, mikataba yote ya nyuma ya aina hiyo ilitakiwa kupitiwa upya ukiwemo mkataba kati ya NDC na *Sichuan Hongda*. Mchakato wa kupitia upya mkataba huo uko katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Matairia cha Arusha. Utafiti wa kina wa kitaalamu wa jinsi ya kufufua Kiwanda cha Matairia cha Arusha, umeshauri kiwanda hicho kifufuliwe kwa ubia wa Serikali na sekta binafsi. Baada ya matangazo kutolewa kupitia tovuti ya NDC wawekezaji mbalimbali walijitokeza ikiwemo Kampuni ya *SAYINVEST Overseas (T) Ltd.* ambayo kiwango cha mtaji walichosema watawekeza na kiwango cha ajira kwenye andiko lao kinakubalika. Hati ya makubaliano ya awali kati ya NDC na *SAYINVEST* ilisainiwa mwezi Januari, 2019 na taratibu zingine za kukamilisha makubaliano ziko katika hatua za mwisho. Makubaliano hayo yatahusisha pia uendeshaji wa Mashamba ya Mpira ya Kalunga na Kilui na kuwapatia miche wakulima wadogo watakaokuwa tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Magadi Soda Engaruka. Mradi wa uchimbaji magadi soda katika Bonde la Engaruka, Wilaya ya Monduli, unaohusu ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha magadi soda tani 1,000,000 kwa mwaka kwa ajili ya matumizi ya viwanda hususan vya dawa, vioo na sabuni, utafiti wa kina au *technical economic study* utakaojumuisha utafiti wa maji safi (*detailed hydrological study*), mazingira na upembuzi yakinifu umeanza kufanyika.

Utafiti huo ndiyo utakaoelekeza namna mradi huo utakavyotekelawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kurasini *Logistic*. Mradi wa Kurasini *Logistic Park* wenye eneo la ukubwa wa ekari 62 ni kwa ajili ya Kituo cha Biashara na Viwanda. Hivi sasa kampuni za *IPP Automobile Ltd.* na *GF Trucking Ltd.* zimewasilisha maandiko ya nia ya kujenga viwanda vya kuunganisha magari na wametakiwa kuwasilisha sasa maandiko kamili ya miradi yao ili ifanyiwe tathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya kisekta kuendeleza viwanda. Tunayo mikakati mitatu, mkakati wa kwanza ni Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Alizeti wa mwaka 2016. Mkakati huu una lengo la kuhakikisha viwanda vya kukamua mafuta alizeti vinapata malighafi ya kutosha kwa kuongeza uzalishaji wa alizeti na kuboresha teknolojia za kusindika mafuta ya alizeti. Kama *CAMARTEC*, *TEMDO* na *SIDO* wamefanya uchambuzi wa mahitaji ya teknolojia za kupandia na kusindika mafuta katika mikoa mbalimbali na baadhi ya zana na teknolojia zimeanza kutengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwagine ni Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Ngozi na Bidhaa za Ngozi. Mkakati huu wa mwaka 2016 umelenga kuandaa viwango vya ubora vya bidhaa za ngozi ikiwemo viatu, kuimarisha Taasisi ya Teknolojia ya Ngozi (Mwanza) kwa kuipatia vifaa vya kufundishia utengenezaji viatu, kutoa mafunzo ya usanifu na utengenezaji viatu na kuondoa ushuru wa forodha kwa malighafi na vipuri vinavyoingizwa nchini kutoka nje vinavyotumika kutengenezea bidhaa za ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkakati wa Pamba hadi Mavazi wa mwaka 2016. Mkakati huu unalenga kuendeleza zao la pamba kuanzia hatua ya kuchambua pamba, kusokota nyuzi, kufuma nyuzi, kutengeneza vitambaa na kushona mavazi. Mkakati utachochaea uanzishwaji wa viwanda vinavyotoa huduma kukamilisha mavazi hususan utengenezaji wa vifungo, lebo na zipu. Utekelezaji wa mkakati huo umefanikisha ufufuaji wa Kiwanda cha Nguo

cha Afritex cha Tanga ambacho kilifungwa kwa muda mrefu na ufuufuaji wa kinu cha kuchambua pamba cha Manonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusitisha matumizi ya mifuko ya plastiki. Baada ya Serikali kusitisha uzalishaji na usambazaji wa mifuko ya plastiki nchini ifikapo tarehe 31 Mei, 2019, Wizara yangu imeendelea kuvishawishi viwanda 15 vinavyozalisha mifuko mbadala nchini viongeze uzalishaji sambamba na kukaribisha wawekezaji wapya kuwekeza kwenye utengenezaji wa mifuko mbadala, rafiki wa mazingira isiyio na madhara ya kiafya. Kiwanda cha kutengeneza Karatasi cha Mufindi kilichopo lringa kimeagizwa kitengeneze karatasi za kutosha ambazo ni malighafi muhimu kwenye viwanda vyta kutengeneza mifuko mbadala ya karatasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo, maeneo ya majengo ya uwekezaji wa viwanda vidogo na biashara ndogo. Katika kipindi cha mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuhamasisha utengaji wa maeneo kwa ajili ya shughuli za viwanda vidogo na biashara ndogo kwenye mikoa na wilaya. Hadi sasa Mkoa wa Mbeya umetenga eka 464, Mkoa wa Morogoro eka 16,022, Mkoa wa Rukwa eka 1,154 na Mkoa wa Mara eka 10,054 na mikoa karibu yote inaendelea na zoezi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa za masoko. Wizara kupitia *TANTRADE* na *SIDO* imekuwa ikiendesha maonyesho ya biashara kwa wajasiriamali ili wapate fursa za kuonyesha bidhaa zao na kupata masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Wajasiriamali. Katika mwaka 2018/2019, jumla ya mikopo 1,706 yenye thamani ya shilingi bilioni 3.164 imetolewa kwenye miradi iliyozalisha ajira 3,691.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhamasisha viwanda na biashara ndogo. Katika mwaka 2018/2019, Wizara yangu kupitia program mbalimbali za *SIDO* iliwezesha uanzishwaji wa viwanda vidogo 607. Serikali imeendelea kuimarisha *SIDO*

kwa kujenga majengo ya wajasiriamali kwenye Mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Mara na Mtwara na majengo ya ofisi Geita, Katavi, Simiyu na Chato. Aidha, vituo vya teknolojia vya Lindi, Shinyanga na Kigoma vimeboreshwa kwa kuwekwa mitambo mipyä ya kuchakata mazao ya korosho, michikichiki na mazao mengine kwa thamani ya shilingi bilioni 935. Vilevile Serikali imetoa shilingi bilioni 1 ili kuongeza majengo Mtwara, Kigoma na Ruvuma katika kuboresha tija na mazingira mahali pa kazi viwandani. Pia program ya kazi imevipatia mafunzo viwanda 23 katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Manyara, Mara, Morogoro, Mwanza na Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya biashara. Mwenendo wa bei wa bidhaa za viwandani kwa wastani katika mwaka huu ulikuwa ukipanda wakati wastani wa bei za mazao umekuwa ukishuka. Mathalani bei za nondo ya milimita 16 imepanda kutoka wastani wa Sh.32,500 mwaka 2017/2018 na kufikia wastani wa Sh.37,579 kwa mwaka 2018/2019, hilo ni ongezeko la asilimia 15.6. Hali hii inatokana na uhitaji mkubwa wa bidhaa husika katika soko.

Vilevile katika mwaka 2018/2019, bei ya mazao makuu ya chakula hususan mahindi, maharage na mchele zimeshuka kwa viwango tofauti ikillinganishwa na msimu wa 2017/2018. Kwa mfano, wastani wa bei ya jumla ya mahindi kwa gunia la kilo 100 ulipungua kutoka Sh.52,445 msimu wa 2017/2018 hadi kufikia shilingi 43,483 msimu wa 2018/2019 ikiwa ni upungufu wa asilimia 17. Kushuka kwa bei kulisababishwa na kuongezeka kwa mavuno nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara na bidhaa kutoka nje kwenye kipindi hicho hasa kutoka nchi za China, Japan na India. Biashara baina ya Tanzania na nchi za China, India na Japan ambapo biashara kubwa za uagizaji zinatoka huko, kwa ujumla umekuwa na urari hasi kutokana na kuagiza bidhaa zenye thamani kubwa kuliko mauzo yanayofanywa kwa mazao na bidhaa za Tanzania kwenda katika nchi hizo. Kwa mfano, mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda India, mwaka 2018 yalikuwa dola za Marekani milioni 734.27 ikillinganishwa na uagizaji wa bidhaa kutoka India yenye

thamani ya dola za Marekani milioni 1,218.07, hiyo ni urari hasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhusiano wa kibashara kati ya Tanzania na nchi nyingine duniani. Wizara imeendelea na hatua za kujipanga katika kutimiza matakwa ya utekelezaji wa Mkataba wa Uwezesaji Biashara wa Shirika la Biashara la Dunia (*World Trade Organization*), Mkataba wa Uwezesaji Biashara *Trade Facilitation Agreement* unaweka mfumo wa kisheria, mwongozo na msukumo wa Kimataifa kwa nchi wanachama kwenye kutatua changamoto za ufanyaji biashara.

Aidha, mkataba huo pia unaweka utaratibu wa pamoja katika kushughulikia masuala ya uwezesaji biashara miongoni mwa nchi wanachama wa *WTO*. Mkataba huo ulianza kutumika rasmi tarehe 22 Februari, 2017 baada ya kuridhiwa na nchi wanachama 112 kati ya wanachama 164 wa *WTO*. Aidha, hadi kufikia tarehe 27 Februari, 2019, nchi wanachama 141 zilikuwa zimeridhia mkataba huo. Hii ina maana nchi wanachama 23 ikiwemo Tanzania hazijaridhia mkataba huo ingawa taratibu za uridhiwaji mkataba huo nchini zimeshaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usajili wa makampuni, majina ya biashara, alama za biashara na huduma ya leseni za viwanda, leseni za biashara na hakimiliki ubunifu. Mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao (*Online Registration -ORS*) unaopatikana kuititia tovuti ya *BRELA* unalenga kuwezesha kutoa huduma kwa njia ya mtandao ili kumfikia mteja popote alipo, hivyo, kupunguza muda na gharama za usajili na kuiwezesha Serikali na wadau wengine kupata taarifa za usajili kwa haraka na kuweka kumbukumbu na taarifa sahihi. Mfumo huo umeunganishwa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*) kwa ajili ya utambuzi wa uhakika wa wamiliki wa Wakurugenzi wa kampuni husika.

Pia mfumo umeunganishwa na *TRA* ambapo namba ya cheti cha kampuni ni sawa na ile namba ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa mfumo huo umewezesha balada ya kusajiri makampuni 6,918 majina ya biashara 11,582, alama za biashara na huduma 4,117 hataza 28 na leseni za viwanda 166. Aidha, barua za kuomba taarifa 18,838 na vilevile taarifa za majalada 4,257 zimeshughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea na jitihada za kurahisisha mazingira ya kufanya biashara nchini kuititia utaratibu wa mikutano mbalimbali ambayo imekuwa ikizikutanisha Wizara za Kisekta, Taasisi ya Serikali pamoja Vyama vya Wafanyabishara ili kuainisha na kujadiliana namna bora ya kuondoa vikwazo mbalimbali vya biashara ikiwemo vya kodi na visivyo vya kodi. Mikakati na Mbinu za kuweka mazingira rafiki ya ufanyaji biashara nchini imeanishwa kwenye kitabu cha *blue print* ambapo rasimu ya mpango kazi wa utekelezaji wake imekamilika na utekelezaji wa *blue print* utaanza mwezi Julai, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutambua changamoto zinazowakabiri wafanyabiashara wa viazi mviringo, hususan kukosekana kwa vifungashio vinavyokubalika kutoka maeneo uzalishaji kwenda sokoni, sheria inawataka wazalishaji na wasafirishaji wa viazi mviringo kutumia vifungashio maalum ambavyo kwa bahati mbaya havipatikani sokoni. Kwa sababu ya changamoto hiyo, tumesimamisha kwa muda utekelezaji wa kanuni sheria hiyo hadi hapo utaratibu utakapoweka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa stakabadhi ghalani ni utaratibu wa biashara unaowezesha bidhaa kuhifadhiwa ghalani na stakabadhi kutolewa kwa mwenye mali inayothibitisha umiliki wake, thamani, aina, idadi na ubora au daraja. Stakabadhi ya ghalbani ni hati inayoweza kutumika kama dhamana kumwezesha mmiliki kupata mkopo kutoka taasisi za fedha. Hivyo, mfumo umewezesha benki za biashara kushiriki katika ununuzi na uuzaaji wa mazao kwa kuwa urejeshaji wa mikopo ni wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, manufaa yaliyopatikana kuititia mfumo wa Stakabadhi Ghalani ni pamoja na

kuimarika kwa usimamizi wa ubora, hifadhi bora ya mazao na kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa wakulima na hivyo kuwapa fursa kuuza kwa wakati na kwa bei nzuri. Manufaa mengine ni ongezeko la bei kwa mkulima kutokana na ushindani katika soko na ongezeko la ujenzi wa maghala ya kuifadhia mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio ya mfumo huo, kumekuwa na changamoto kwa viwanda vyatubu na ndani hususani katika kupata malighafi kwa bei shindani kwa mali ghafi kwa mazao yanayopatikana katika mfumo huo. Katika kushughulikia changamoto hiyo Serikali inaandaa utaratibu mahsusutu utakaowezesha viwanda vyatubu na ndani kupata malighafi kwa uhakika ili viweze kuwa shindani katika soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu biashara na masoko mipakani, tumeendelea kuimariisha biashara ya masoko mipakani kwa mipaka yetu yote. Mpaka sasa vituo tisa vimeanzishwa katika mipaka baina ya Tanzania na nchi wanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki pamoja na nchi ya Zambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maonyesho ya biashara ya ndani na nje nchi yameendelea kuwa nyenzo muhimu ya ukusanyaji wa biashara inayochochea maendeleo ya viwanda kwa kufungua fursa za masoko ya ndani na nje na kuvutia uwekezaji. Aidha, maonyesho hukutanisha wauzaji na ununuzi wa bidhaa na huduma pamoja na kuwezesha kubadilishana taarifa za biashara na huduma ikiwemo kuingia katika miadi ya biashara na bidhaa. Jukwaa hili huwawezesha wazalishaji na wafanyakishara kupata mwaya wa kupokea maoni ya moja kwa moja kutoka kwa watumiaji wa bidhaa au huduma, hivyo kupata mawazo mapya, kuwezesha ubunifu, kubadilishana uzoefu, kuendeleza bidhaa, kuongeza ubora na hatimaye kuwezesha bidhaa za Tanzania kuwa na ushindani katika soko la ndani kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaanda Sera ya Taifa ya Ubora

inayolenga kusimamia masuala yote ya ubora nchini sambamba na kulinda afya ya mlaji, wanyama, mimea na mazingira kwa ujumla. Pia sera hii inatarajiwa kuwa mwongozo wa mtangamano wa miundombinu ya Taifa ya ubora ambayo ni *Metrology, Standardization, Accreditation, Conformity* na *Market Surveillance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtangamano huo unakusudiwa kuondoa mwingiliano baina ya taasisi zinazojihusisha na masuala ya ubora. Aidha, Sera ya Taifa ya Ubora itatoa mwongozo katika makubaliano na Shirika la Dunia la Biashara, hasa vikwanzo vya kiufundi vya biashara na matumizi ya vikwazo vya kulinda afya ya mimea na wanyama (*SPS*). Hadi sasa nchi kadhaa Barani Afrika zimeshaanda Sera ya Ubora ikiwemo pamoja na Namibia, Nigeria na Rwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki cha Marrakeshi. Tanzania ni nchi wanachama iliyyoridhia *Convention* ya Shirika la Kumiliki Ubunifu Duniani (*World Intellectual Property Organization*) mwaka 1983 iliyoanza kutumika mwaka 1979. Tarehe 27 Juni, 2013 Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa Wipo uliofanyika Mjini Marrakesh Morocco ambao ulipitisha itifaki inayowezesha kupata na kuzalisha kazi za maandishi kwa watu wasioona, uoni haffiu ulemavu unaofanya mtu kushindwa kusoma kwa njia rahisi wa mwaka 2013. Itifaki hiyo imeanza kutekelezwa tarehe 30 Septemba, 2016 baada ya masharti ya kuanza kutumika kutimia kwa maana ya idadi ya nchi ya wanachama kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania haikuweza sahihi kwa kipindi hivyo ili kuweza kujipa muda wa kupata maoni kutoka kwa wadau wa ndani. Mwaka 2018/2019 Wizara imeandaa waraka ili kupata ridhaa ya Serikali na Bunge kwa Watanzania kuijunga na itifaki hiyo. Itifaki hiyo inatoa fursa ya upendeleo na upekee kwenye sheria za hakimiliki ili ziruhusu uzalishaji, usambazaji na kuwezesha upatikanaji wa kazi zinazochapishwa kuwa katika mfumo rafiki kwa walengwa waliotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niwasilishe mwelekeo na vipaumbele vya sekta vya viwanda na biashara kwa mwaka 2019/2020. Mwelekeo wa Sekta na Biashara unarejea kifungu cha 112 hadi 122 kwenye kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika malengo, kuna kuimarisha sekta binafsi kama *engine* ya kujenga uchumi wa viwanda. Ujenzi wa uchumi wa viwanda ikiwa ndiyo ajenda kuu ya Serikali ya Awamu ya Tano, natambua umuhimu wa kufungamanisha sekta za uchumi kwa kushirikisha sekta binafsi na za Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtazamo na mwelekeo huu mkuu utaendelea kuweka mbele nafasi ya sekta binafsi kwa *engine* ya uchumi na Serikali kuendelea kuweka mazingira rafiki na wezeshi ili kuhakikisha wadau wote wanatoa mchango unaohitajika katika ujenzi wa uchumi kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji katika viwanda na biashara, utekelezaji wa *blue print* unaangaliwa kuwa sehemu kubwa ya tiba ya changamoto ambazo zinawatatiza sekta binafsi. Hivyo ni mategemeo ya Serikali kuona sekta binafsi itachukua nafasi yake na kuchangamkia fursa zilizopo, kuzalisha na kutoa huduma ikiwa ni hatua muhimu ya kutambua jitihada zinazofanywa na Serikali katika kutatua matatizo wanayokabiliana nayo kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea kujenga uchumi wa viwanda, ni mtazamo wa dhamira ya Serikali kuwa sekta binafsi kwa kutumia vivutio na maboresho yanayofanywa, itajielekeza zaidi katika kujenga viwanda vinavyoongeza thamani mazao yanayozalishwa nchini ili kuondokana uuzaji wa mali ghafi nje ya nchi na hivyo kuwa soko la kwanza la uhakika kwa wazalishaji wa mazao nchini.

Aidha, sekta binafsi inategemewa kujenga viwanda vinavyotoa ajira kwa wingi na vile vinavyozalisha bidhaa zinazotumiwa na Watanzania walio wengi ambavyo

vitachangia kukuza soko la ndani na hivyo kuwa dirisha la mwendelezo wa soko letu la nje. Vile vile Serikali itahakikisha inashirikiana na sekta binafsi katika kuendelea kuwezesha upatikanaji wa maeneo ya uwekezaji yenyewe miundombinu ili kuvutia uwekezaji zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jithada zinafanywa na kuimarisha taasisi za kuendeleza uwekezaji, taasisi za utafiti, maendeleo ya teknolojia na mafunzo na taasisi za ushindani na udhibiti wa ubora wa bidhaa na huduma ili kuchangiza zaidi maendeleo ya ujenzi wa uchumi unaonufaisha wadau wote. Matumizi ya mifumo rasmi katika minyororo ya thamani, kama vile matumizi ya mfumo wa stakabdhi ghalani katika manunuzi, vituo vya maalum ya mauzo na kadhalika, utaimarishwa na kutumika kwa kiwango cha juu. Katika kufanya hivyo, chachu ya ulinzi wa viwanda na mlaji utakuwa kichocheo muhimu katika biashara nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha mazingira ya biashara na kuongeza ushindani wa biashara na kuhakikisha ubora wa bidhaa na huduma, Serikali imekamilisha na sasa inaendelea kuboresha mifumo ya usajili wa kampuni na majina ya biashara na kuhakikisha leseni za biashara za daraja A zinazotolewa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (*BRELA*) na daraja B zinazotelwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kupitia mfumo wa kielektoniki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kukamilika kwa mfumo wa Dirisha la Taifa la Biashara (*National Business Portal*) ambao ndio unatoa leseni za biashara, Wakala imeanza kutoa mfunzo kwa Maofisa Biashara na wa TEHAMA wa Halmashauri zote nchini ili waweze kuwahudumiwa wananchi vizuri zaidi. Mafunzo hayo yatafanyika kwa Maafisa Biashara na Maafisa TEHAMA wa mikoa na wilaya zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia itaendelea kufanya kaguzi kwa bidhaa zinazofungashwa kwenye maeneo ya mipaka ya Holili, Namanga Mtukula, Sirari, Kasumulo, Horohoro na Tunduma. Aidha, kaguzi hizi pia zitahusisha bandari za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na

Kigoma. Vilevile kaguzi za bidhaa zinazofungashwa kwenye maeneo ya viwandani ambapo ni pamoja na bidhaa za vyakula, vilainishi, saruji, rangi, mitumba, maziwa, mabati, nondo na vinywaji baridi vitaendelea kufanyiwa ukaguzi kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Viwango Tanzania litaendelea kuandaa viwango muhimu katika kilimo, chakula, uhandisi na viwango vya vifungashio mbalimbali na pia litaendelea kusimamia viwango vya Kitaifa kwa kutumia mifumo iliyopo ya kuhakiki ubora. Aidha, shirika litaendelea kutoa leseni za nembo za ubora kwa wajasiriamali wadogo wanaozalisha bidhaa mbalimbali zinazotokana na mazao na bidhaa za kilimo, mifugo na misitu na bidhaa kutoka sekta nyingine za uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile shirika litaendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali na wadau mbalimbali katika zana nzima ya kuzingatia mifumo ya ubora ili kuzalisha bidhaa zenye ubora. Mafunzo na semina hizo zitatolewa kwa wajasiriamali wadogo pamoja na wadau mbalimbali katika mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaratibu ushirikiano wa taasisi za udhibiti ambazo ni Shirika la *TBS*, Shirika la Viwango Zanzibar, *TRA*, *GCLA*, *EWURA*, *SUMATRA*, *TFDA*, *FCC*, *NEMC*, *NIT*, *TPA* na Jeshi la Polisi katika kusimamia ubora wa bidhaa hasa zinatoka nje kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa lengo la kuhakiki na kuthibitisha ubora ili kulinda viwanda vya ndani na afya za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kufanya uchunguzi katika makubaliano yanayofifisha ushindani (*anti competitive agreements*) katika eneo hilo uchunguzi utafanyika katika sekta zote zinazoonyesha kuwa na makubaliano ya kufifisha ushindani ambazo ni pamoja na Sekta ya Michezo, Mpira wa Miguu, kuhusu haki za kutangaza mechi za mpira wa miguu, Sekta ya Mawasiliano kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Nchini na Sekta ya

Biahsara na Kilimo kama sekta ndogo ya tumbaku ambayo imeonyesha kuwa na matumizi mabaya ya nguvu ya soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele ya Wizara yangu kwa mwaka 2019/2020 ni: moja, kuendeleza miradi ya kimikakati; pili, kuendeleza uraslimishaji wa viwanda na biashara ndogo za kati; tatu, uongezaji thamani wa mazao ya kilimo na mali ghafi nyingine na kuunganisha masoko; nne, kutekeleza mfumo wa udhibiti wa ufanyaji biashara nchini (*blue print*); tano, kuimarisha utafiti na teknolojia kwenye sekta za viwanda na biashara; sita, kuimarisha udhibiti na ushindani katika soko kwa ajili ya kuivilinda viwanda vya ndani na kukuza biashara; saba, uendelezaji wa maeneo maalum ya uwekezaji wa viwanda; kuendeleza biashara na majadiliano ya kibiashara ya Kimataifa na ujenzi wa Ofisi ya Wizara katika Mji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2019/2020, malengo mahususi ya Wizara kwa Sekta ya Viwanda, viwanda vidogo, biashara ndogo na masoko yameainishwa kwa kina katika kifungu cha 124 hadi 128 kwenye hotuba yangu ambayo nimeisambaza rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo mahususi ya taasisi za kisekta zilizo chini ya Wizara kwa mwaka 2019/2020 zikiwemo taasisi za kuendeleza uwekezaji, taasisi za utafiti, maendeleo ya teknojia na mafunzo na taasisi za ushindani na udhibiti wa ubora wa bidhaa na huduma yameanishwa kwa kina kuanzia kifungu cha 129 hadi kifungu cha 144 kwenye kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Mapato na Matumizi na Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2019/2020. Mapato ya Serikali katika mwaka 2019/2020, Wizara yangu inatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 14,300,000/= kutokana na uuzaaji wa nyaraka za zabuni na makusanyo mengine. Kati ya hizo, shilingi 5,300,000/= zitakusanywa kwenye Fungu 44 na shilingi 9,000,000/= zitakusanywa katika Fungu 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maombi ya fedha, kwa mwaka 2019/2020, Wizara ya Viwanda na Biashara inaomba kutengewa jumla ya shilingi 100,384,738,648/=. Kati ya hizo, shilingi 48,884,738,648/= ni za matumizi ya kawaida na shilingi 51,500,000,000/= ni matumizi ya maendeleo. Aidha, katika Bajeti hiyo, shilingi 79,149,452,000/= ni za Fungu 44 – Viwanda na shilingi 21,235,286,648/= ni za Fungu 60 - Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru tena washirika wetu wa maendeleo zikiwepo nchi rafiki ambazo ni Austria, Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Sweden, Uhlanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi. Aidha, tunayashukuru Mashirika ya Kimataifa ikiwa ni pamoa na ARIPO, Benki ya Dunia, CFC, DANIDA, DFID, EU, FAO, IFAD, JICA, Jumuiya ya Madola, KOICA, SIDA, Taasisi za Umoja wa Mataifa kama UNCTAD, UNDP, UNIDO, UNWOMEN, USAID, WIPO, TMEA, SADC na WTO. Vilevile, nashukuru taasisi zote, Sekta binafsi, taasisi zisizo za kiserikali CBOs na FBOs kwa kuendelea kwa kuwa sehemu muhimu ya wadau wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihitimishe kwa kuwashukuru tena Watanzania wote, wadau na washirika wa maendeleo wote kwa jithada na ushirikiano wanaotupatia katika kutekeleza azma ya ujenzi wa uchumi wa viwanda. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara yenye anuani [www.mit.go.tz](http://www.mit.go.tz)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa shabaha ya kumbukumbu, naomba kitabu changu cha hotuba ya bajeti na Makadirio ya Mapato Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2019/2020 chote kiwekwe kwenye Hansard kwa ajili ya kumbukumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge Iako liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi Wizara ya Viwanda na Biashara ambapo mapato ni shilingi 14,300,000/= na matumizi ya jumla ya shilingi 100,384,738,648/= kwa mwaka 2019/2020 kama ilivyoainishwa kwa kina kwenye kifungu cha 145 na 146 kwenye kitabu hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
(*Makofi*)

**HOTUBA YA WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA  
MHESHIMIWA JOSEPH GEORGE KAKUNDA (MB.),  
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA  
MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2019/2020 - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## **1.0 UTANGULIZI**

**1. *Mheshimiwa Spika;*** Kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara Fungu 44 (Viwanda) na Fungu 60 (Biashara) tarehe 26 na 27 Machi, 2019 Jijini Dodoma, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mipango na Bajeti kwa Mwaka 2018/2019. Aidha, naliomba Bunge lako likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2019/2020.

**2. *Mheshimiwa Spika;*** Naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake imara, wenye uzalendo na mapenzi kwa Tanzania na Watanzania. Pia, nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; pamoja na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi; Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; kwa miongozo yao thabiti inayolenga kuwahakikishia maslahi ya kimaendeleo Watanzania walio wengi.

**3. *Mheshimiwa Spika;*** Napenda kuchukua nafasi hii, kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika kwa kuliongoza

na kulisimamia vema Bunge Ietu. Pia, naipongeza na kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Suleiman AhmedSaddiq,MbungewaMvomero(CCM), naMakamuwake Mheshimiwa Kanali Mstaafu Ali Khamis Masoud, Mbunge wa Mfenesini (CCM) na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati. Ushauri na maelekezo yao yamekuwa muhimu sana kwa utendaji wa Wizara yangu na kwa Watanzania, kwani yamekuwa yakichochea kasi ya maendeleo ya Viwanda na Biashara nchini. Vilevile, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya waliochaguliwa kuitia chaguzi ndogo ambao ni Mheshimiwa Christopher Kajoro Chizza(Mb.) Jimbo la Buyungu; Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer (Mb.) Jimbo la Monduli; Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara (Mb.) Jimbo la Ukonga; Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava (Mb.) Jimbo la Korogwe Vijijini; Mheshimiwa Zuberi Mohammed Kuchauka (Mb.) Jimbo la Liwale; Mhe. James Kinyasi Millya (Mb.) Jimbola Simanjiro; Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi (Mb.) Jimbo la Ukerewe; Mheshimiwa Paulina Philipo Gekul (Mb.) Jimbo la Babati Vijijini; Mheshimiwa Ryoba Chacha Marwa (Mb.) Jimbo la Serengeti; na Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea (Mb.) Jimbo la Temeke.

**4. *Mheshimiwa Spika***; Nitumie fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri wapya kwa kuteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali. Kwa namna ya pekee; nimshukuru Mheshimiwa Charles J. Mwijage, Mbunge wa Jimbo la Muleba Kaskazini, aliyekuwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa ushirikiano anaonipa hadi sasa. Nikiri kuwa wakati akiongoza Wizara hii; aliweka misingi ambayo ni chachu katika kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara nchini.

**5. *Mheshimiwa Spika***; Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapa pole familia, ndugu, wananchi na jamaa kwa kuondokewa na wapendwa wetu, Mheshimiwa Stephen Hillary Ngonyani "Profesa Maji Marefu"; aliyekuwa Mbunge wa Korogwe Vijijini. Nawapa pia pole nyingi Waheshimiwa Wabunge waliopata misiba ya kufiwa

na wazazi, watoto au wanafamilia wa karibu. Vilevile, natoa pole kwa Watanzania waliokumbwa na kadhia ya majanga mbalimbali kama vile ajali za majini, barabarani na majanga mengine yanayofanana na hayo.

**6. Mheshimiwa Spika;** Naomba kutumia fursa hii pia kuwashukuru viongozi na watendaji wote wa sekta binafsi; hususan Baraza la Taifa la Biashara Tanzania (Tanzania National Business Council - TNBC); Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (Tanzania Private Sector Foundation - TPSF); Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (Confederation of Tanzania Industries - CTI); Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture - TCCIA); Baraza la Kilimo Tanzania (Agriculture Council of Tanzania - ACT); Chama cha Wadau wa Ngozi Tanzania (Leather Association of Tanzania - LAT); Chama cha Wafanyabiashara Wanawake (Tanzania Women Chamber of Commerce - TWCC); na Vikundi vyta Biashara Ndogo (VIBINDO); kwa michango yao katika kuendeleza Sekta za Viwanda, Biashara, Masoko, Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Kwetu sisi, hao ni mionganoni mwa wadau muhimu sana kwani ndiyo injini ya uchumi wetu.

**7. Mheshimiwa Spika;** Hotuba hii ya Bajeti ninayoivasilisha leo ni matokeo ya uratibu na ushirikiano mzuri wa viongozi wenzangu katika Wizara, akiwemo Naibu Waziri Mheshimiwa Mhandisi Stella M. Manyanya (Mb.) Jimbo la Nyasa; Katibu Mkuu, Prof. Joseph R. Buchweishaija; Naibu Katibu Mkuu – Viwanda, Ndugu Ludovick J. Nduhiye; Naibu Katibu Mkuu - Biashara, Dkt. Edwin P. Mhede (PhD); Wakuu wa Idara, Vitengo, Taasisi na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake. Napenda kuwashukuru na kuwapongeza kwa kujituma na kuonesha daima utayari wa kuboresha mbinu na mikakati ya kisekta kwa vitendo. Aidha, namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na wachapishaji wengine kwa kuchapisha machapisho mbalimbali ya Wizara na Taasisi kwa wakati.

**8. Mheshimiwa Spika;** Baada ya maelezo hayo ya awali, naomba sasa nielezee kwa ufupi mapitio ya Bajeti na utekelezaji wa Malengo ya Bajeti ya Wizara yangu kwa kipindi

cha mwaka 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa kipindi cha mwaka 2019/2020.

## **2.0 MAPITIO YA FEDHA ZA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2018/2019**

### **2.1 Misingi inayozingatiwa katika Kutekeleza Bajeti ya Wizara**

**9. Mheshimiwa Spika;** Wizara ya Viwanda na Biashara katika mwaka 2018/2019 imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo Endelevu ya Maendeleo (Sustainable Development Goals - SDGs), Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Mwaka 2016/2017-2020/2021, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015 - 2020; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/2019 na Sera za kitaifa ambazo ni pamoja na Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda (SIDP, 1996 - 2020); Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo (2003); Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (2008) na Sera ya Taifa ya Biashara (2003). Majukumu ya Wizara hutekelezwa na Idara, Vitengo na Taasisi zilizo chini ya Wizara ili kuwafikia walengwa na kuwapa huduma stahiki kwa wakati. Aidha, Wizara inafanya marejeo ya Sera hizo ili ziendane na matakwa ya wakati.

### **2.2 Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2018/2019**

**10. Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka 2018/2019, Wizara (Fungu 44 & 60) iliyodhinishwa matumizi ya jumla ya **Shilingi 143,334,153,648**. Kati ya hizo, fedha za Matumizi ya Maendeleo ni **Shilingi 100,024,525,000 na Shilingi 43,309,628,648** za Matumizi ya Kawaida. Aidha, Wizara iliyodhinishwa kukusanya jumla ya Shilingi **20,006,300,000** (inayojumuisha Fungu 44 **Shilingi 5,300,000** na Fungu 60 **Shilingi 20,001,000,000**) kutokana na ada za leseni, uuzaji wa nyaraka za zabuni, marejesho ya mishahara endapo mtumishi ataacha kazi na faini kwa kukiuka Sheria ya Leseni ya Biashara.

## 2.3 Fedha Zilizopokelewa

**11. Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia mwezi Aprili, 2019, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 43,375,340,491** kati ya hizo, Shilingi **30,855,056,831.42** kwa Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 12,520,283,660** kwa Matumizi ya Maendeleo. Aidha, jumla ya **Shilingi 8,990,341,969.04** zilikuwa zimekusanywa kama maduhuli.

## 3.0 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA BAJETI KWA MWAKA 2018/2019

### 3.1 SEKTA YA VIWANDA

#### Usajili, Uratibu na Usimamizi wa Ujenzi wa Viwanda

**12. Mheshimiwa Spika;** Majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara ni kusimamia na kuratibu ujenzi wa viwanda sambamba na kuhakikisha kuwa bidhaa zinazozalishwa zinapata masoko ya ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2018/2019, jumla miradi mipy 304 imesajiliwa. Kati ya hiyo, miradi 107 ilisajiliwa chini ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), miradi 194 ilisajiliwa na kupewa leseni na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na miradi mitatu (3) ilisajiliwa chini ya Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kuzalisha Bidhaa kwa Mauzo ya Nje (EPZA). Miradi hiyo inatarajiwu kuongeza jumla ya ajira 11,793. Aidha, SIDO imeratibu na kuhudumia viwanda vidogo vipyta 1400 vilivyotoa ajira 4,200. Hadi sasa, inakadirikiwa kuwa sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo imetua ajira kwa zaidi ya watanzania milioni 8.

**13. Mheshimiwa Spika;** Moja ya majukumu ya SIDO ni kuhudumia viwanda vidogo na vya kati. Katika kutekeleza jukumu hilo SIDO inatoa mitaji midogo, mafunzo, ushauri katikauendeshajipamojanateknolojiazakutumia. Teknolojia hizo huzalishwa ama kutafutwa na SIDO na kusambazwa kwa wajasiriamali wanaoendesha viwanda kulingana na mahitaji yao. Teknolojia hizo zimewesha uanzishwaji wa viwanda sambamba na urahisishaji wa kufanya kazi zingine hususan katika maeneo ya kilimo na ufugaji. Aidha, SIDO inatunza

kumbukumbu za viwanda vidogo na vidogo sana wanavyovihudumia na vinavyopatikana katika maeneo ya mikoa waliyomo ikishirikiana na Halmashauri.

**Hali na Utendaji wa Viwanda Vilivyoanzishwa kwa Sheria ya EPZ/SEZ**

**14. Mheshimiwa Spika;** Tathmini ya uwekezaji kwa viwanda chini ya Mamlaka ya EPZ na SEZ tangu Mamlaka ya EPZ kuanzishwa imeonesha mafanikio makubwa nchini. Hadi kufikia mwezi Septemba 2018, EPZA imetua leseni za kuanzisha viwanda kwa kampuni 169 zilizowekeza mitaji yenye thamani ya Dola za Marekani Bilioni 2.219, ambayo imetua ajira mpya za moja kwa moja viwandani 56,312; ambapo Mauzo ya bidhaa Nje ya Nchi yenye thamani ya Dola za Marekani Bilioni 2.242 yamepatikana. Katika mwaka 2018/2019, Mamlaka ya EPZ imesajili makampuni matatu (3) ya uwekezaji ambayo yanawekeza mitaji yenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 45.7 na manufaa kwa watanzania ni pamoja na ajira mpya 815.

**15. Mheshimiwa Spika;** Pamoja na changamoto ya miundombinu wezeshi katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji chini ya Mamlaka ya EPZ, ujenzi wa viwanda katika maeneo mbalimbali ya EPZ na SEZ unaendelea. Kwa mfano, viwanda 10 vinaendelea kujengwa na kimoja (African Dragon Enterprises Limited) kimeanza uzalishaji na kimechangia mapato ya zaidi ya Shilingi Bilioni 7.96 katika kipindi cha Desemba, 2018 hadi Februari, 2019 katika eneo la Mradi wa Bagamoyo SEZ. (*Kiambatisho Na. 1*)

**16. Mheshimiwa Spika;** Utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu wezeshi wa eneo la *Mtwara Free Port Zone (MFPZ)* umeanza kwa kushirikiana na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mtwara (Mtwara Urban Water and Sanitation Authority – MTUWASA) pamoja na TARURA; kwa kutumia fedha zilizotolewa na Serikali kiasi cha Shilingi 3,954,071,314. Kwa mujibu wa mpango kazi wa utekelezaji wa Mradi, MTUWASA wanatarajiwaka kukamilisha Mradi wa kipeleka maji eneo la *MFPZ* ifikapo Julai, 2019. Aidha, TARURA wamekamilisha usanifu wa barabara za eneo hilo na taratibu za kumpata Mkandarasi zinaendelea.

## **Viwanda Vilivyobinafsishwa**

**17. Mheshimiwa Spika;** Kuhusu hali ya viwanda 156 vilivyobinafsishwa, viwanda 88 vinafanyakazi na viwanda 68 havifanyi kazi. Kati ya viwanda 88 vinavyofanya kazi, viwanda 42 vinafanya kazi vizuri sana; 46 vinafanya kazi kwa kiasi cha kuridhisha (satisfactory); viwanda 20 vimefutwa kwa sababu ubinafsishwaji wake ulifanywa kwa kuuza mali moja moja na vingine kuruhusiwa kubadili matumizi. Viwanda vingine 48 wamiliki wameshindwa kuviendesha kwa mujibu wa mikataba ya mauziano na hivi sasa tayari viwanda 16 vimerejeshwa Serikalini na viwanda 32 wamepewa notisi ya kuwasilisha mipango ya kuviendeleza kabla ya tarehe 31 Mei 2019 vinginevyo vitarejeshwa Serikalini mara moja ili vitafutiwe wawekezaji wengine. Baadhi ya viwanda ambavyo vimesharejeshwa Serikalini vimebainika kuwa nyaraka za viwanda hivyo zilitumika kuchukulia mikopo mikubwa mno ukilinganisha na thamani iliyotumika wakati wa ubinafsishaji na wakopaji wengine hawajalipa mikopo hiyo na baadhi yao wameshindwa kukabidhi nyaraka za viwanda. Napenda kuchukua nafasi hii kuwatahadharisha wahusika wote walio ndani na nje ya nchi kwamba kwa kufanya hivyo walitenda kosa la kuhujumu uchumi wa nchi. Nawaonya kwamba wahakikishe wamemalizana na mabenki kwa kulipa mikopo yao yote ifikapo tarehe 31 Mei, 2019 na Serikali haitaongeza muda huo ambao ndio muda wa mwisho kuleta maelezo yanayoeleweka Serikalini kuhusu viwanda hivyo, vinginevyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wote watakaokaidi.

## **Viwanda ambavyo Havikubinafsishwa**

**18. Mheshimiwa Spika;** Viwanda 13 havikubinafsishwa kutokana na sababu mbalimbali na hivyo kuendelea kuwa mali ya umma chini ya Msajili wa Hazina. Baadhi ya viwanda hivyo vinavyofanya kazi kwa kusuasua na vingine havifanyi kazi kabisa (**Kiambatisho Na.2**). Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) tunaendelea kutafuta wawekezaji wapya wenye nia ya kuwekeza kwa maslahi mapana ya maendeleo ya nchi yetu.

## **Viwanda Vipyta Vinavyomilikiwa na Serikali Kiwanda cha Viuadudu cha Kibaha**

**19. Mheshimiwa Spika;** Serikali inamiliki Kiwanda cha Viuadudu cha Kibaha kwa asilimia 100 kuperitia NDC. Kiwanda hicho kina umuhimu mkubwa katika kupambana na ugonjwa wa Malaria nchini. Kiwanda kinazalisha na kusambaza dawa za kuua viluwiluvi na wadudu ikiwemo mbu ambapo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeagiza lita 200,000 zenye thamani ya Shilingi Bilioni 2.64, na tayari imelipia lita 60,000. Aidha, TAMISEMI kuperitia Halmashauri mbalimbali nchini imetenga Shilingi bilioni 8.9 kwa ajili ya kununua viuadudu kutoka kiwandani. Vilevile, nchi za SADC mfano, Angola na Eswatini zimeonesha nia ya kununua viuadudu kutoka katika kiwanda hicho vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 13.053. Pia, NDC inafanya mazungumzo na Wizara ya Kilimo ili kiwanda hicho kizalishhe dawa za kuua wadudu katika zao la pamba.

### ***Mradi wa Matrekta aina ya URSSUS***

**20. Mheshimiwa Spika;** NDC imeendelea kuunganisha matrekta aina ya *URSSUS* na zana zake na ujenzi wa kiwanda kipyta cha kuunganisha matrekta katika eneo la TAMCO Kibaha. Mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili, 2019 jumla ya matrekta 822 yalikuwa yamepokelewa kutoka nchini Poland na kati ya hayo matrekta 536 yalikuwa yameunganishwa. Kati ya hayo, matrekta 399 yalikuwa yameuzwa mikoa mbalimbali nchini yakiambatana na majembe ya kulimia 399 na majembe ya kusawazisha 186. Hadi mwishoni mwa Aprili 2019, jumla ya ekari 85,464 zilikuwa zimelimwa kwa kutumia matrekta hayo.

### **Udhibiti wa Viwango vya Bidhaa Zinazozalishwa Viwandani Ndani ya Nchi**

**21. Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka 2018/2019, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) lilipanga kuratibu utayarishaji wa viwango vipyta 400 kutoka sekta mbalimbali. Hadi kufikia mwezi Aprili 2019, jumla ya viwango vipyta muhimu 195 vinavyohusu kilimo, chakula, uhandisi na vifungashio

mbalimbali vilitayarishwa na kukamilika. Kati ya viwango 195 vilivyokamilika, viwango 26 ni vya Uhandisi Mitambo (Mechanical), viwili vya Uhandisi Umeme (Electrical), 20 ni Mtambuka (General Techniques), 31 ni vya Kemikali (Chemical), 20 vya Nguo na Ngozi (Textile and Leather), 18 vya Ujenzi (Building & Construction), tisa vya mazingira (Environmental), 14 vya madini (Mining) na 55 vya Sekta ya Kilimo na Chakula (Food and Agriculture).

**22. Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha mwaka 2018/2019, TBS iliendelea kusimamia viwango vya kitaifa kwa kutumia mifumo iliyopo ya kuhakiki ubora (Certification Schemes) na kutoa leseni za Nembo ya Ubora ya TBS. Hadi Aprili 2019, jumla ya leseni 191 zilitolewa. Kati ya leseni hizo, 29 zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo wanaozalisha kashata, mafuta ya kula, pombe, unga wa ngano, maji ya kunywa, tindikali ya betri, mvinyo, siagi ya karanga, kripsi za maembe na kripsi za ndizi. Leseni zilizosalia 162 zilitolewa kwa wajasiriamali wa kati na wakubwa.

#### **Udhhibit wa Viwango vya Bidhaa za Viwandani Zinazozalishwa Nje ya Nchi**

**23. Mheshimiwa Spika;** Shirika la Viwango Tanzania limeendelea na jukumu la kudhibiti ubora wa bidhaa zinazotoka nje ya nchi. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Aprili, 2019 jumla ya vyeti vya ubora (*Certificate of Conformity-CoCs*) 25,605 vimetolewa kwa shehena za bidhaa zilizotoka nje ya nchi baada ya kukaguliwa na kukidhi ubora kabla ya kuingia nchini. Aidha, jumla ya vyeti vya ukaguzi wa magari 30,580 yaliyokidhi viwango vimetolewa. Bidhaa ambazo hazikukidhi viwango ziliteketezwa au kuwaamuru waagizaji kuzirudisha nchi zilikotoka. Baadhi ya bidhaa zilizoteketezwa ni pamoja na nguo za ndani kilogramu 517, mashuka vipande 4,500, mabati vipande 303,572, vilainishi lita 1,050, *bolti* 720, kalamu katoni 143, *mathematical set* katoni 630, *tomato paste* katoni 100, kufuli dazeni 152 na bidhaa mbalimbali za vyakula na vinywaji baridi katoni 360. Serikali kupitia taasisi zake za udhibiti itaendelea kufanya ukaguzi na upimaji wa bidhaa kutoka nje ili kulinda viwanda vya ndani kutokana

na ushindani usio wa haki pamoja na kulinda afya za watanzania.

### **Udhibiti wa Bidhaa Bandia na Hafifu Kutoka Ndani na Nje ya Nchi**

**24. *Mheshimiwa Spika***; Hadi kufikia mwezi Desemba, 2018 Tume ya Ushindani ilikuwa imefanya kaguzi 153 katika Bandari ya Dar es Salaam na Bandari Kavu (ICDs) zilizopo Dar es Salaam ili kubaini, kukamata na kuteketeza bidhaa bandia kabla hazijaingia sokoni. Katika kaguzi hizo, makasha (containers) 1,536 yamekaguliwa na katika makasha hayo, makasha 82 yamekamatwa kwa kukiuka Sheria ya Alama za Bidhaa ya Mwaka 1963 na marekebisho yake. Bidhaa zilizokamatwa katika kaguzi hizo ni pamoja na vifaa vya ujenzi, miswaki, vifaa vya umeme, viatu, vipuri vya magari na vyombo vya nyumbani.

**25. *Mheshimiwa Spika***; Katika mwaka 2018/19, Tume ya Ushindani imefanya kaguzi za kushtukiza 18 zilizofanyika jijini Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na katika Mikoa ya Shinyanga na Tabora na kukamata bidhaa bandia ikiwemo viatu, pombe kali na wino wa vitarakishi. Bidhaa nyingine zilizokamatwa ni vipuri vya magari na mafuta ya kupaka mwilini. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 55 ya Kanuni za Alama za Bidhaa ya Mwaka 2008 na marekebisho yake, inayompa mamlaka Mkaguzi Mkuu kuharibu au kugawa bidhaa zilizokamatwa, Tume imegawa pampu za maji nne na vifaa vya muziki (spika nane) kwa Chuo cha Polisi Tanzania.

### **Mapitio ya Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda (1996 – 2020)**

**26. *Mheshimiwa Spika***; Wizara imeanza kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda (1996-2020). Mapitio hayo yanakwenda sambamba na mapitio ya Mkakati Endelevu wa Maendeleo ya Viwanda (Integrated Industrial Development Strategy – IIDS 2025), ambapo kwa mujibu wa Mpango Kazi inatarajiwa zoezi hilo kukamilika ifikapo Juni, 2020. Mara baada ya kukamilika kwa Sera pamoja na Mkakati wake, Wizara pia itafanya mapitio ya

Sheria ya Usajili na Leseni za Viwanda ili iweze kukidhi mahitaji ya sasa.

### **Kujenga Uwezo wa Wizara na Taasisi Zake**

**27. Mheshimiwa Spika;** Moja ya vipaumbele vya Wizara ni kuziwezesha Taasisi zake na kuzijengea uwezo kwa kuimarisha rasilimali watu, kutoa vitendea kazi na ujenzi wa miundombinu. Kwa mwaka 2018/2019, maeneo yaliyoimarishwa ni kama ifuatavyo:

- i. Wizara imerejea Muundo wa Taasisi ya TEMDO na CAMARTEC ili kuwezesha utekelezaji wa malengo balimbali ya kisekta na kitaifa;
- ii. TEMDO wameimarisha rasilimali watu kwa kuapeleka baadhi ya watumishi katika mafunzo ya muda mfupi (watumishi 42) na muda mrefu (watumishi 7);
- iii. Kuimarisha majengo na uwezo wa karakana na ofisi za usanifu za TEMDO kwa kuzipatia mashine, kompyuta na vifaa mbalimbali ambavyo vitasaidia kufanya usanifu, ubunifu, uendelezaji wa teknolojia na utoaji huduma katika sekta ya viwanda kwa lengo la kukuza na kuendeleza uchumi wa viwanda;
- iv. CAMARTEC imeimarisha rasilimali watu kwa kuongeza nafasi za ajira 16, na pia kuimarisha miundombinu ya kufanya utafiti na kuongeza uwezo wa kufanya utafiti na uendelezaji wa teknolojia;
- v. Wizara imeendelea kuimarisha uwezo wa TIRDO kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ya utafiti na kutoa huduma za ushauri wa kitaalam viwandani kwa kuitengea bajeti kiasi cha Shilingi Bilioni 3 kwa mwaka 2018. Bajeti hiyo imeliwezesha Shirika kuajiri watafiti wapya; kuanza kujenga maabara mpya ya mafuta na gesi itakayoongeza uwezo wa Shirika katika kutoa huduma za kitaalam kwenye sekta hizo. Aidha, TIRDO imewezeshwa kuboresha maabara zake za chakula kwa kuziwezesha kupata ithibati ya kimataifa (accreditation);

vi. Wizara imeajiri watumishi 6 na kupokea watumishi 4 wa kada mbalimbali waliohamia na hivyo kuongeza tija na ufanisi katika utendaji kazi wa kila siku; na

vii. Wizara imewapeleka katika mafunzo ya muda mrefu watumishi 17 na watumishi 9 katika mafunzo ya muda mfupi. Watumishi hao wako katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

### **Miradi ya Kimkakati Kuelekea Ujenzi ya Viwanda Mama**

#### **i) Mchuchuma na Chuma cha Liganga**

**28. *Mheshimiwa Spika***; Miradi ya Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga inatekelezwa na Kampuni ya *Tanzania China International Mineral Resources Limited* ambayo ni ya ubia kati ya Serikali kupitia NDC na *Sichuan Hongda Group ya China*. Maandalizi yote muhimu ya kuanza ujenzi wa miradi hiyo ikiwemo, leseni za uchimbaji madini, vyeti vyaa mazingira, vibali vyaa kutumia maji ya mito ya Katewaka, Mchuchuma na Lupali vilikwishatolewa tangu mwaka 2014. Mradi huo unganishi ulifuzu kupata hadhi ya Mwekezaji Mahiri (*Strategic Investors Status*) na hivyo kupewa vivutio maalum vyaa uwekezaji. Hata hivyo, wakati mradi ukiwa tayari kuanza utekelezaji mwezi Julai, 2017 Mwekezaji aliomba vivutio vyaa ziada.

**29. *Mheshimiwa Spika***; Wakati majadiliano yanaendelea kuhusu vivutio hivyo vyaa ziada, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha Sheria Na. 5 na 6 juu ya Ulinzi wa Maliasili za nchi (Permanent Sovereignty over Natural Resources) ili kukidhi matakwa ya Katiba Ibara ya 27 na Azimio la Umoja wa Mataifa (United Nations Resolution 1803 (XVII)). Kulingana na Sheria hizo mbili; *Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, 2017* na *Natural Wealth and Resources Contract Review & Re-Negotiation of Unconscionable Terms Act, 2017*, mikataba yote ya nyuma ya aina hiyo ilitakiwa kupitiwa upya ukiwemo Mkataba kati ya NDC na *Sichuan Hongda Group*. Mchakato wa kupitia upya mkataba huo unaendelea.

**30. Mheshimiwa Spika;** Katika mwezi Julai, 2018 Wizara kupitia NDC ilifanya uhakiki wa taarifa ya uthamini wa ardhi na mali za wananchi watakaopisha ujenzi wa miradi ya Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga kwa kushirikiana na Mthamini Mkuu wa Serikali na taasisi zingine za Serikali. Jumla ya Shilingi Bilioni 11.037 zinatakiwa kulipwa ikiwa ni fidia kwa wananchi 1,145 kwa maeneo yote ya mradi.

**ii) Kiwanda cha Matairi Arusha**

**31. Mheshimiwa Spika;** Utafiti wa kina wa kitaalam wa jinsi ya kufufua Kiwanda cha Matairi Arusha (kilichokuwa GTEA) uliishakamilika na Tamko la Serikali la kuhamishia mali za Kiwanda NDC lilitolewa mwezi Desemba, 2018. Baada ya matangazo kutolewa kupitia tovuti ya NDC, wawekezaji mbalimbali wamejitokeza ikiwemo Kampuni ya *SAYINVEST Overseas (T) Ltd* ambayo imeonesha nia ya dhati ya kuwekeza katika uzalishaji wa matairi nchini. Kiwango cha mtaji walichoweka kwenye andiko pamoja na kiwango cha ajira kwa watanzania hususan wakazi wa Arusha kinatoa mwelekeo wa kukubalika. Tayari Hati ya Makubaliano ya Awali (MOU) kati ya NDC na *SAYINVEST Overseas (T) Ltd* umesainiwa tarehe 5 Januari 2019 na taratibu zingine za kukamilisha makubaliano ziko katika hatua za mwisho.

**iii) Kuendeleza Mradi wa Mashamba ya Mpira Morogoro na Tanga**

**32. Mheshimiwa Spika;** NDC imeendelea kupanda miche mipya ya Mpira takribani 85,250 katika eneo la wazi katika shamba la Kalunga ambapo mpaka kufikia Desemba, 2018 hekta 155 zilikuwa tayari zimepandwa. Pia, NDC inasimamia uvunaji wa Mpira unaozalishwa kwa sasa katika shamba hilo. Wavamizi katika Shamba la Mpira la Kalunga wameondolewa.

**33. Mheshimiwa Spika;** Taratibu za kulichukua Shamba la Kihuhwi lililopo Muheza mkoani Tanga kutoka kwa msimamizi *Coast Water Project Limited* kutokana na usimamizi mbovu wa shamba tayari zimekamilika. Shirika linakarabati majengo

yaliyopo shambani hapo ili kuanza uzalishaji wa Mpira kwa muda wakati taratibu za kutafuta mbia wa muda mrefu zikiendelea. Taratibu za kuhamishia umiliki wa mashamba kwenda NDC kutoka CHC zilikwisha kamilika kupitia GN. Na. 266 katika Gazeti la Serikali Toleo Na. 29 la Julai 17, 2015. Aidha, taratibu za kupata hati za mashamba hayo kwa jina la NDC zinaendelea. Shirika linaandaa Upembuzi Yakinifu kwa ajili ya mashamba ya mpira utakaotoa mwongozo wa namna bora ya kuyaendesha mashamba hayo, ili kuongeza ufanisi na faida kwa Shirika na Serikali kwa ujumla.

#### **iv) Mradi wa Magadi Soda Engaruka**

**34. *Mheshimiwa Spika;*** Mradi wa Uchimbaji Magadi Soda katika Bonde la Engaruka, Wilaya ya Monduli unahusu ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha magadi soda tani milioni moja kwa mwaka kwa ajili ya matumizi ya viwanda hususan vya dawa, vioo na sabuni. Utafiti wa kina (*techno-economic study*) utakaojumuisha utafiti wa maji safi (*detailed hydrological study*), mazingira (ESIA), na upembuzi yakinifu (*feasibility study*) umeanza kufanyika.

#### **v) Kurasini Logistic Park**

**35. *Mheshimiwa Spika;*** Mradi wa Kurasini Logistic Park wenyewe eneo la ukubwa wa ekari 62 ni kwa ajili ya Kituo cha biashara na viwanda. Hadi sasa, Serikali imelipa fidia ya Shilingi Bilioni 101 kwa ajili ya kufidia wananchi 1,019. Hivi sasa, Kampuni za IPP Automobile Ltd na GF Trucking Ltd zimewasilisha maandiko ya kuonesha nia "*Expression of Interest*" ya kujenga viwanda vya kuunganisha magari na wametakiwa kuwasilisha maandiko kamili ya Mradi wao.

### **MIKAKATI YA KISEKTA YA KUENDELEZA VIWANDA**

#### **i) Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Alizeti**

**36. *Mheshimiwa Spika;*** Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mafuta ya Alizeti wa mwaka 2016 una lengo la kuendeleza mnyorowathamaniwazaola Alizeti na kutatuachangamoto zinazokabili mnyororo huo. Hadi sasa, Programu ya Pamoja

ambayo utekelezaji wake unaratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na kushirikisha Wizara mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Rais – TAMISEMI; Wizara za Viwanda na Biashara; Kilimo; Maji; Mifugo na Uvuvi na Fedha na Mipango imeandaliwa. Juhudi za kuhakikisha kuwa mbegu bora za Alizeti zinapatikana kwa wingi ili kuwezesha Viwanda vinavyosindika mbegu za Alizeti vinapata malighafi ya kutosha ili viongeze uzalishaji zinafanyika chini ya uratibu wa Wizara ya Kilimo.

**37. *Mheshimiwa Spika***; Mkakati huo pia umewezesha kuandaliwa kwa andiko kuhusu Viwango na Matakwa ya WanunuzikatikaSokolaAfrikaMashariki, Indianalakimataifa (*Standards and Buyer Requirements in East Africa, India and International Markets*) ili kuwaongoza wazalishaji wa mafuta ya alizeti kuzalisha mafuta yenye viwango vinavyokubalika kwenye masoko hayo. Andiko hilo liliandaliwa na mafunzo kutolewa kwa wasindikaji kwa kushirikiana na Mradi wa *Supporting Indian Trade and Investment for Africa* (SITA). Aidha, uboreshaji wa kuendeleza teknolojia ya kusindika mafuta ya Alizeti unaendelea kuhamasishwa kupitia taasisi za teknolojia na utafiti zilizo chini ya Wizara.

**38. *Mheshimiwa Spika***; Kituo cha CAMARTEC kimefanya uchambuzi wa mahitaji (needs assessment) ya teknolojia katika mikoa mbalimbali na kubuni zana 50 za kupandia mazao ya kilimo ikiwa ni pamoja na zao la Alizeti. Aidha, zana kwa ajili ya kuvuna na kukamua mbegu za Alizeti zilitengenezwa na CAMARTEC, TEMDO na SIDO na kusambazwa kwa wakulima na wasindikaji katika Mikoa mbalimbali.

**39. *Mheshimiwa Spika***; Mfuko wa Maendeleo ya Nchi za Jumuiya ya Ulaya (EDF 11) ulifadhili upatikanaji wa Masoko ya mafuta ya Alizeti kupitia maonesho yaliyofanyika mwezi Julai, 2018 Dar es Salaam, Tanzania na mwezi Agosti, 2018 Nampula, Msumbiji. Mfuko huo pia ulifadhili upatikanaji wa vifaa vya Maabara kwa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ili waweze kutoa huduma kwa Sekta ya Mafuta ya Alizeti. Juhudi hizo zinalenga kuwapatia fursa wasindikaji wa mafuta ya Alizeti kuingia kwenye masoko ya Kitaifa na Kimataifa.

**ii) Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Ngozi na Bidhaa za Ngozi**

**40. Mheshimiwa Spika;** Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Ngozi wa mwaka 2016 umejikita katika kuendeleza mnyororo wa thamani wa zao la Ngozi. Utekelezaji wa Mkakati huo unahamasisha usindikaji wa Ngozi hadi hatua ya mwisho ili Ngozi hizo zitumike katika kuzalisha bidhaa mbalimbali za Ngozi ndani ya nchi. Utekelezaji wa mkakati huo umefanikisha: Kuandaliwa kwa miongozo ya viwango vya ubora kwa Viwanda vinavyosindika Ngozi na vinavyotengeneza Viatu na namna ya kupanga madaraja ya Ngozi ghafi na zilizosindikwa hadi hatua ya mwisho; Kuimarishwa kwa iliyokuwa Taasisi ya Teknolojia ya Ngozi (TILT) Mwanza ambayo kwa sasa inatumiwa na Chuo cha Teknolojia cha Dar es Salaam (DIT) Kampasi ya Mwanza (DIT Mwanza) kwa kupatiwa vifaa vya kufundishia utengenezaji Viatu; Kutolewa mafunzo ya utengenezaji Viatu kwa vijana 800 kwa Mikoa ya Tanzania Bara na Visiwani; Kutolewa kwa mafunzo kwa njia ya mtandao (*e-learning*) ya usanifu wa Viatu; na Kuondolewa kwa ushuru wa forodha kwa malighafi na vipuri vinavyoingizwa kutoka nje vinavyotumika kutengenezea bidhaa za ngozi na viatu.

**iii) Mkakati wa Pamba hadi Mavazi**

**41. Mheshimiwa Spika;** Mkakati wa Pamba hadi Mavazi wa mwaka 2016 unalenga kuendeleza mnyororo wa thamani wa zao la Pamba kuanzia hatua ya kuchambua Pamba (ginneries), kusokota Nyuzi (spinning), kufuma Nyuzi (weaving), kutengeneza Vitambaa (finishing) na kushona Mavazi (garments). Uongezaji thamani wa Pamba hadi Mavazi utachochea uanzishwaji wa Viwanda vinavyotoa huduma (*auxiliary industries*), vikiwemo Viwanda vya kutengeneza Vifungo, Lebo na Zipu. Utekelezaji wa mkakati huo umefanikisha yafuatayo: -Kiwanda cha Nguo cha Afritex (T) Ltd cha Tangaambacho kilifungwa kwa muda mrefu sasa kimeanza kufanya kazi na Kinu cha Manonga, Tabora kimefuliwa na kimeanza kuchambua Pamba.

## **Chuma na Bidhaa za Chuma**

**42. Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2006 hadi 2018, matumizi ya bidhaa za chuma nchini yameongezeka kutoka tani 226,000 hadi kufikia tani 912,000 kwa mwaka, ikiwa ni ongezeko la asilimia 303.54. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2018, nchi yetu ilikuwa na viwanda 25 vya kuzalisha chuma na bidhaa za chuma. Viwanda vya kuzalisha Chuma na Bidhaa za Chuma hapa nchini vipo katika makundi mbalimbali yanayojumuisha nondo, mabati, mabomba, misumari, sen'yenye na kadhalika. Kati ya hivyo, Viwanda vya kuzalisha nondo vipo 16 vyenye uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 1,082,700 kwa mwaka, wakati uzalishaji halisi ni tani 240,336 kwa mwaka, sawa na asilimia 22 ya uwezo uliosimikwa. Mahitaji ya nondo nchini kwa mwaka ni tani 295,000, hivyo uzalishaji huo wa ndani hutosheleza asillimia 80 ya mahitaji yote ambapo asillimia 20 inayobaki huagizwa kutoka nje ya nchi. Aidha, viwanda hivyo vinaajiri jumla ya wafanyakazi 23,150, kati ya hao wafanyakazi 3,588 ni ajira ya moja kwa moja na wafanyakazi 20,000 wa ajira za muda.

**43. Mheshimiwa Spika;** Katika kundi la viwanda vya chuma, vipo viwanda vya mabomba ya chuma. Mabomba ya aina hiyo hutumika kwa shughuli mbalimbali za usambazaji maji na kama malighafi katika viwanda vya ujenzi na ufundi. Tanzania ina viwanda vya kutegeneza mabomba ya chuma vipatavyo saba (7) vyenye uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 223,200 kwa mwaka. Uzalishaji halisi ni tani 99,100 sawa na asilimia 44 ya uwezo uliosimikwa. Aidha, kuna viwanda viwili vikubwa vinavyozalisha mabati kuanzia hatua ya awali (*intergrated*) ambavyo ni ALAF na MMI Steel vyenye uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 158,000 kwa mwaka wakati uzalishaji halisi ni tani 58,189 kwa mwaka, sawa na asilimia 37 ya uwezo uliosimikwa. Kiwanda cha ALAF pia kimefungua tawi lake jijini Dodoma kina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 17,280 kwa mwaka, hivi sasa kinazalisha wastani wa tani 5,760 kwa mwaka, kwa mabati aina ya migongo mipana. Tawi hilo lipo kwenye mpango wa kuzalisha mabati ya kawaida

(corrugated iron sheets) ambapo mashine hizo zitaanza kufungwa mwishoni mwa mwezi Mei, 2019.

**44. Mheshimiwa Spika;** Hali ya uzalishaji wa bidhaa za chuma kuwa chini ya uwezo umetokana na sababu mbalimbali ikiwemo kupanda kwa bei ya malighafi na kuadimika kwa chuma chakavu nchini. Uzalishaji wa chuma chakavu nchini unakadirwa kuwa ni tani 10,000 ambazo hukusanywa na kurejelezwa katika viwanda vya hapa nchini. Hali hiyo imesababisha bei ya chuma chakavu kuongezeka. Hiyo inaonesha umuhimu wa kuanza kuzalisha chuma ghafi kwa kutumia madini ya chuma cha Liganga ili kutosheleza mahitaji ya chuma ghafi nchini kikiwepo chuma safi (bILLETS) na kuondokana na utegemezi wa kuingiza chuma toka nje. Kutokana na sababu hiyo, Wizara inafanya kila jitihada kuhakikisha maandalizi ya msingi kuwezesha utekelezaji wa Mradi wa Mchuchuma na Liganga ambayo yalishaanza yanakamilika.

### **Kusitisha Matumizi ya Mifuko ya Plastiki**

**45. Mheshimiwa Spika;** Utakumbuka kuwa tarehe 9 Aprili, 2019, Serikali ilitoa tamko la kusitisha matumizi, uzalishaji na usambazaji wa mifuko ya plastiki nchini ifikapo tarehe 31 Mei, 2019. Wizara yangu imeendelea kushawishi viwanda 15 vinavyozalisha mifuko mbadala kwa sasa nchini viongeze uzalishaji sambamba na kukaribisha wawekezaji wapya kuwekeza kwenye utengenezaji wa mifuko mbadala ambayo ni rafiki wa mazingira na haina madhara ya kiafya kwa binadamu na wanyama. Mifuko hiyo inaweza kutengenezwa kutokana na malighafi zinazotokana na kilimo kama vile Pamba, Mkonge, na Ukili. Malighafi hizi zinaweza kutengeneza mifuko ya karatasi, vikapu, mifuko ya katani na mifuko ya vitambaa. Matumizi ya bidhaa hizi yatachochea maendeleo endelevu ya kilimo na kutoa ajira nyingi kwa watanzania. Pia itapunguza matumizi ya fedha za kigeni ambazo zilikuwa zinatumika kuagiza malighafi za kutengeneza mifuko ya plastiki. Aidha, kiwanda cha kutengeneza karatasi cha *Mufindi Paper Mill Ltd* kilichopo Iringa kimeagizwa kitengeneze karatasi za kutosha kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la ndani.

### **3.2 SEKTA YA VIWANDA VIDOGO NA BIASHARA NDOGO**

#### **Mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndodo ya 2003**

**46. Mheshimiwa Spika:** Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndodo ya mwaka 2003, ndiyo mwongozo wa usimamizi na uendelezaji wa shughuli za Viwanda Vidogo na Biashara Ndodo na za Kati nchini. Mabadiliko ya kiuchumi, teknolojia na kijamii yanayotokea nchini na duniani kwa ujumla, ikiwemo ongezeko la shughuli za ujasiriamali, kukua kwa Sekta ya Madini na Sanaa na kupanuka kwa matumizi ya teknolojia ya habari, yamepanua wigo wa fursa za uwekezaji katika sekta hii na hivyo kuhitaji kurejewa kwa sera. Wizara immeendelea kurejea Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndodo ya mwaka 2003, ili iweze kuendana na mahitaji ya sasa ya sekta nchini. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019, Wizara kwa kushirkiana na wadau mbalimbali wa maendeleo imeweza kufanya na kukamilisha tafiti za kina katika maeneo saba kati ya kumi yaliyoainishwa baada ya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya mwaka 2003, kuwa ni muhimu na yanahitaji utafiti wa kina ili kuweza kubaini maeneo yenye changamoto zinazohitaji utatuzi wa kisera. Maeneo hayo ni Mfumo wa Kisheria na Kanuni (Legal and Regulatory Framework); Mfumo wa Upatikanaji wa Mitaji kwa Wajasiriamali (Access to Finance); Mfumo wa Uratibu wa Sekta (SME Sector Coordination); Upatikanaji wa Masoko(AccesstoMarkets); na Maendeleo ya Jasiriamali (Enterprise Development). Aidha, tafiti za kina zimekamilika katika maeneo mtambuka (Cross Cutting Issues) hususani ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Pia, maeneo ya Sekta mpya hususan Madini na Gesi na Sanaa (Emerging sectors and Creative Industries); Kwa sasa, Wizara inaendelea na maandalizi ya maeneo yaliyobaki kufanyiwa tafiti za kina ambayo ni Uendelezaji Viwanda Vijiji (Rural Industrialization); Huduma za Kuendeleza Biashara (Business Development Services); na Teknolojia na Ubunifu (Technology and Innovation). Baada ya tafiti hizo kukamilika, Sera iliyoreshwa itakamilishwa na inatarijiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2019/2020.

## **Maeneo na Majengo ya Uwekezaji wa Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo**

**47. Mheshimiwa Spika;** Wizara inatambua changamoto kubwa inayowakabili wajasiriamali ya upatikanaji wa maeneo rasmi ya kufanyia shughuli zao za viwanda na biashara ndogo na za kat. Changamoto hiyo, ambayo ni moja ya vichochoeo vikubwa vyta sekta isiyo rasmi, huikosesha Serikali mapato mengi na ni chanzo kikubwa cha uchafuzi wa mazingira ya sehemu za makazi na maeneo ya wazi. Hivyo, ili kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara katika kipindi cha mwaka 2018/2019, imeendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI kuhamasisha utengaji wa maeneo kwa ajili ya shughuli za viwanda vidogo na biashara ndogo kwa ngazi ya mikoa na wilaya. Aidha, Wizara imeweza kutembelea na kkusanya takwimu za maeneo yaliyotengwa katika mikoa ya Mbeya, Morogoro, Rukwa, na Mara. Kwa mujibu wa takwimu hizo, Mkoa wa Mbeya umetenga jumla ya ekari 464.17, Mkoa wa Morogoro ekari 16,022, Mkoa wa Rukwa ekari 1,154.48 na Mkoa wa Mara umetenga jumla ya ekari 10,054.67. Aidha, Mwongozo wa Kusimamia Ujenzi na Maendeleo ya Viwanda kwa Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa umekuwa nyenzo mahususi katika kuzisaidia mamlaka hizi wakati wa utengaji wa maeneo yatakayojengwa viwanda na masoko. Majengo haya yanatumika na wajasiriamali kuzalishia bidhaa zao. Mfumo wa kuwaweka wajasiriamali katika majengo haya, kunawarahishia kupata mikopo kutoka katika vyombo vyta fedha kwa kutumia mashine zilizo katika majengo haya kama dhamana.

## **Fursa za Masoko kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati**

**48. Mheshimiwa Spika;** Wizara imeendelea na juhudzi za kutafuta fursa za masoko ya wajasiriamali ndani na nje ya nchi. Kupitia majadiliano ya kupanua masoko ya Jumuia za nchi za Kusini mwa Afrika na ile ya Afrika Mashariki, wajasiriamali wameendelea kufaidika na masoko hayo. Kupitia taasisi za TANTRADE na SIDO, Wizara imekuwa ikiendesha maonesho ya biashara kwa wajasiriamali wadogo

ili wapate fursa za kuonesha bidhaa zao na kupata masoko. Wizara na SIDO walishirikiana na Mkoa wa Simiyu, walifanya Maonesho ya Kitaifa ya SIDO kwa wajasiriamali wadogo na wa katika yaliyofanyika Mkoa wa Simiyu tarehe 23 – 28 Oktoba, 2018 na kufunguliwa rasmi na Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 23 Oktoba, 2018. Maonesho hayo yalishirikisha wajasiriamali 700. Aidha, Maonesho ya SIDO ya Kikanda yaliyofanyika katika Mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Tanga yalishirikisha wajasiriamali 1,949 kutoka mikoa yote ya Tanzania na walifanya mauzo yenye thamani ya Shilingi 387,686,000 na kupata oda zenye thamani ya Shilingi 901,756,200. Maonesho haya pia yalitoa fursa kwa washiriki wa nchi jirani za Rwanda, Burundi, Uganda na Kongo na wajasiriamali wetu walipata fursa ya kujifunza wenzao wanafanyakaje katika uzalishaji. Pia, maonesho hayo yanatoa fursa kwa watanzania kuona na kununua teknolojia za aina mbalimbali zinazotengenezwa na SIDO pamoja na wajasiriamali wengine. Vilevile, maonesho hayo yanawapa fursa wajasiriamali kushiriki mafunzo yanayotolewa na taasisi mbalimbali za ubora, kibenki na udhibiti yakilenga kuwapa weledi na mitaji katika kuboresha bidhaa wanazozizalisha. Kupitia maonesho hayo, jumla ya wajasiriamali 1,249 walielimishwa na taasisi za TBS, TFDA, GS1 na WMA ili waweze kusajili bidhaa zao.

### **Mfuko wa Maendeleo yaWajasiriamali (NEDF)**

**49. *Mheshimiwa Spika:*** Upatikanaji wa mitaji ni moja ya changamoto kubwa inayowakabili wajasiriamali hapa nchini. Katika kujaribu kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali ilianzisha Mfuko wa Maendeleo ya Wajasiriamali (National Entrepreneurship Development Fund - NEDF), mwaka 1994 ukiwa na mtaji wa Shilingi 5,051,000,000. Hadi kufikia Februari, 2019, mtaji wa mfuko umekua na kufikia Shilingi 7,844,454,656 sawa na ongezeko la asilimia 35.9. Ukuaji huo umetokana na usimamizi mzuri wa Wizara pamoja makusanyo ya riba ambayo hurudishwa kutunisha mfuko. Mfuko huu umeendelea kuwa na umuhimu wa kipekee kwa wajasiriamli hasa katika ajira na vipato. Tangu uanzishwe, mfuko huu umeweza kuzalisha ajira kwa watanzania 186,138 kutokana

na mikopo 91,584. Wananchi waliowezeshwa kuanzisha na kuendesha shughuli za kiuchumi wameweza kutatua changamoto za kiuchumi na kijamii kama vile kupata matibabu, kujenga nyumba za kuishi, kupata usafiri na kusomesha watoto. Aidha, mfuko huu umewawezesha wanawake wengi kushiriki katika shughuli za kiuchumi, ambapo tangu uanzishwe asilimia 52 ya wafaidika wa mfuko huu ni wanawake. Mfuko huu pia umekuwa ni chagizo kubwa kwa watanzania kushiriki katika ujenzi wa viwanda hasa vile vidogo sana. Katika mwaka 2018/2019, kwa kutumia fedha zinazozunguka kurudi kutoka kwa wakopaji, jumla ya mikopo 1,706 yenye thamani ya Shilingi bilioni 3.164 imetolewa kwa wajasirimali na kupatikana kwa ajira 3,691.

### **Kuhamasisha Viwanda na Biashara Ndogo**

**50. *Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia SIDO inahamasisha uanzishwaji viwanda kupitia mikakati ya Wilaya Moja Bidhaa Moja (ODOP), Kongano za Viwanda, Programu ya Kiatamizi, na kuhamasisha mtu mmoja mmoja kupitia mafunzo na ushauri. Katika mwaka 2018/2019, mikakati hii imewezesha uanzishwaji wa viwanda 607. Kati ya hivi viwanda 151 vimeanzishwa kupitia ODOP; viwanda 28 kupitia kongano; viwanda 20 kupitia kiatamizi na viwanda 408 kupitia huduma nyingine za shirika. Pia, Programu ya KAIZEN iliwezesha viwanda 23 kuongeza tija katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Manyara, Mara, Morogoro, Mwanza, na Tanga. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo imeweza kutoa huduma zinazolenga kuboresha uzalishaji katika minyororo ya thamani. Kwa Mfano, kwa kushirikiana na Serikali ya Canada, kupitia Asasi ya *Menonnnite Economic Development Associates (MEDA)* inatekeleza Mradi wa Kukuza Biashara Sawia- *Strengthening Small Business Value Chains (SSBVC)*, wenye lengo la kuwajengea uwezo wajasiriamali katika sekta za kilimo, uzalishaji viwandani, usafirishaji, ujenzi na madini unaotekelawa katika kanda tatu za Arusha (Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Singida na Tanga); Morogoro (Dodoma, Iringa, Mbeya, Morogoro, na Songwe); na Mtwara (Dar es Salaam, Lindi, Mtwara na Pwani). Hadi Aprili, 2019 Mradi huo ulikuwa umehudumia jumla ya wajasiriamali 6,336.

## Kuimarisha SIDO

**51. Mheshimiwa Spika;** Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) ni nyenzo muhimu katika juhudzi za Serikali za kuimarisha wajasiriamali nchini. Kufuatia mchango wake katika kujenga uwezo wa Watanzania kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kiuchumi, Serikali imeendelea kujengea uwezo SIDO katika maeneo ya taaluma, vitendea kazi na miundombinu ili iweze kutoa huduma zake kwa tija zaidi. Katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia SIDO iliendelea na ujenzi wa majengo ya viwanda 12 kwa ajili ya kuongeza maeneo ya kufanya kazi wajasiriamali katika Mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Manyara na Mtwara. Pia, iliendelea kujenga ofisi nne katika Mikoa mipya ya Geita, Katavi na Simiyu pamoja na Wilaya ya Chato ili kufikisha huduma za SIDO katika sehemu hizo. Majengo hayo yamekamilika na baadhi yameanza kutumiwa na wajasiriamali. Jengo la SIDO Mtwara limekamilika na kutumika ipasavyo katika kipindi cha *Operation Korosho* ambapo viwanda vidogo vinne (4) nya kubangua korosho vimeanzishwa kwenye jengo hilo ambapo jumla ya ajira 411 zimepatikana. Aidha, kutokana na mafanikio hayo, Serikali imeamua kuboresha Kituo cha Teknolojia cha Lindi kwa kuboresha teknolojia za uzalishaji wa mitambo kwa kununua mitambo mipya yenye thamani ya Shilingi Milioni 335. Ni matarajio ya Serikali kuwa mitambo hiyo itaweza kuzalisha teknolojia nzuri zaidi za ubanguaji na kuimarisha ubanguaji wa Korosho nchini. Katika kuendelea kuimarisha SIDO, Serikali pia imetoea kiasi cha Shilingi Milioni 600 kwa ajili ya kuimarisha Vituo nya Teknolojia nya Shinyanga na Kigoma ili viwe katika nafasi nzuri ya kutengeneza teknolojia za kuchakata zao la Chikichi pamoja na mazao mengine. Vilevile, Serikali imetoea Shilingi Bilioni moja (1) ili kuongeza majengo ya viwanda mikoa ya Mtwara, Kigoma na Ruvuma. Majengo haya yatatumika na wajasiriamali kuzalishia bidhaa zao. Mfumo wa kuwaweka wajasiriamali katika majengo haya, unawarahisishia kupata mikopo kutoka katika vyombo nya fedha kwa kutumia mashine zilizo katika majengo haya kama dhamana.

**52. Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha 2018/2019; Wizara kupitia SIDO imetambua, imezalisha na kusambaza teknolojia

mpya 40. Mashine na zana hizo ziliwezesha kuanzishwa na kuimariswa kwa shughuli za viwanda 143 vya uzalishaji nchini kote. Maeneo ambayo teknolojia hizo zimejikita zaidi ni ubanguaji wa Korosho na usindikaji wa Mihogo. Vilevile, teknolojia za usindikaji wa vyakula, upunguzaji wa matumizi ya miti na mazao yake kama nishati, ufungashaji wa vyakula vilivyoosindikwa, utengenezaji wa vifaa vya ujenzi hasa matofali, utengenezaji wa chokaa na chaki, ukamuaji mafuta ya kula kutokana na Michikichi, utengenezaji wa Sabuni na usindikaji Ngozi kwa kutumia njia za asili. Teknolojia hizo zimesaidia kuimarisha na kuongeza ubora wa bidhaa za wajasiriamali. Aidha, vituo hivyo vimeweza kuboresha mifumo ya uzalishaji katika viwanda vinavyosindika chai - Luponde, Kibena (Njombe), Itona (Mufindi Tea Company), *Wakulima Tea Company* (Tukuyu); Kahawa - *Mbozi Coffee Curing* (Mbozi), Mfumo wa kusaga na kusindika nafaka Njoleko (Njombe); na utengenezaji vipuri na urekebishaji mifumo ya uzalishaji katika viwanda vya *Silverlands (T) Co. Ltd, Farm Abri Ltd, Mkwawa Pure Drinking Water* na *ASAS Group* mkoani Iringa.

### **3.3 SEKTA YA BIASHARA**

#### **Muunganiko wa Uzalishaji Viwandani na Usambazaji wa Bidhaa Mbalimbali**

**53. *Mheshimiwa Spika***, Mifumo ya Uzalishaji na Usambazaji wa bidhaa inatofautiana kutegemeana na aina ya mazao katika sekta za Kilimo na bidhaa za viwandani kwa Sekta ya Viwanda. Katika Sekta ya Kilimo, mazao kutoka kwa mzalishaji kwenda kwa Muuzaji hupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi kwa mazao ya biashara kama vile Korosho, Pamba na Kahawa na kwa mzao ya chakula mkulima anaauza moja kwa moja kwa muuzaji wa jumla au reja reja akiwa ni mlaji au mtumiaji wa mwisho. Ni aghalabu, kwa msambazaji wa bidhaa za chakula kufanya shughuli za usambazaji wa bidhaa za ujenzi.

#### **Hali ya Biashara ya Ndani**

**54. *Mheshimiwa Spika***; Hali ya biashara inaendelea vyema japo bei ya baadhi ya bidhaa imeendelea kupanda. Hali hii,

inatokana na uhitaji mkubwa wa bidhaa husika katika soko. Kutokana na kukua kwa sekta ya ujenzi nchini, bei ya vifaa vyaa ujenzi zimeendelea kupanda mwaka 2018/2019. Mathalan, bei ya nondo ya milimita 16 imepanda kutoka wastani wa Shilingi 32,500 kwa mwaka 2017/2018 na kufikia wastani wa Shilingi 37,579 kwa mwaka 2018/2019, ikiwa ni ongezeko la asilimia 15.6. Vilevile, katika kipindi hicho, bei ya nondo ya milimita 12 imeongezeka kutoka wastani wa Shilingi 16,842 hadi kufikia wastani wa Shilingi 20,453 ikiwa ni ongezeko la asilimia 21.4; na bei ya nondo ya milimita 10 imepanda kutoka wastani wa Shilingi 13,289 na kufikia wastani wa Shilingi 14,997 ikiwa ni ongezeko la asilimia 12.9. Bei ya nondo ya milimita 8 imepanda kutoka wastani wa Shilingi 9,892 na kufikia wastani wa Shilingi 12,086 ikiwa ni ongezeko la asilimia 22.

**55. Mheshimiwa Spika;** Vilevile, wastani wa bei ya bati geji 32 madukani imepanda kutoka Shilingi 13,456 mwaka 2017/2018 na kufikia Shilingi 14,520 mwaka 2019, ikiwa ni ongezeko la asilimia 7.9. Vilevile, katika kipindi hicho, bati ya geji 30 imepanda kutoka Shilingi 17,632 hadi kufikia Shilingi 18,385, sawa na ongezeko la asilimia 4.3 na bei ya bati geji 28 imepanda kutoka Shilingi 23,230 na kufikia Shilingi 24,359 ambalo ni ongezeko la asilimia 4.9. Aidha, hadi kufikia Desemba, 2018, wastani wa bei ya rejareja ya saruji kwa mfuko wa kilo 50 ilipanda na kufikia Shilingi 15,895 ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 14,759 mwaka 2017/2018 ikiwa ni ongezeko la asilimia 8.

**56. Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka 2018/2019, bei ya mazao makuu ya chakula hususan Mahindi, Maherage na Mcchele zimeshuka kwa viwango tofauti ikilinganishwa na msimu wa 2017/2018. Kwa mfano, wastani wa bei ya jumla ya mahindi kwa gunia la kilo 100 ilipungua kutoka Shilingi 52,445 msimu wa 2017/2018 hadi kufikia Shilingi 43,483 msimu wa 2018/2019, ikiwa ni upungufu wa asilimia 17. Bei ya jumla ya maharage kwa gunia la kilo 100 ilishuka kutoka Shilingi 172,564 mwaka 2017/2018 hadi kufikia Shilingi 159,394 mwaka 2018/2019, ikiwa ni upungufu wa asilimia 7.6. Aidha, bei ya jumla ya mchele kwa gunia la kilo 100 ilipungua kutoka

wastani wa Shilingi 184,089 msimu wa 2017/2018 hadi Shilingi 154,107 msimu wa 2018/2019 ikiwa ni upungufu wa asilimia 16.3. Kushuka kwa bei kulisabishwa na kuongezeka kwa mavuno.

### **Biashara za Bidhaa Kutoka Nje ya Nchi**

**57. *Mheshimiwa Spika***; Kwa ujumla, katika kipindi kati ya mwaka 2017 na 2018, Tanzania imeendelea kuwa na urari chanya katika mauzo ya bidhaa zake ambapo imeuza zaidi kuliko kununua kwenye nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki - EAC (asilimia 10.63), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika - SADC (asilimia 29.84) na Umoja wa Afrika - AU (asilimia 5.63).

**58. *Mheshimiwa Spika***; Mwaka 2018, mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) yalikuwa Dola za Marekani milioni 447.5 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 349.6 zilizopatikana mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 21.88. Ongezeko hilo limetokana na mauzo ya bidhaa za Chai, Mahindi, Ngano, Alizeti, Mchele, bidhaa za Karatasi, Mabati, Vigae, Vyandarua, Kemikali (methyl bromide), Saruji na Mafuta ya Kupaka. Kwa upande mwingine, Tanzania iliagiza bidhaa kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 302.93 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 220.4 kwa mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 27.24.

**59. *Mheshimiwa Spika***; Kwa upande wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), mauzo ya bidhaa za Tanzania yalikuwa Dola za Marekani Milioni 999.34 mwaka 2018 ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 877.8 kwa mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 12.16. Ongezeko hilo limetokana na mauzo ya bidhaa za Madini, Pamba, Chai, Kahawa, Vigae, Vyandarua, Kemikali (methyl bromide), *petroleum coke*, Saruji, Sabuni na Mafuta ya Kupaka. Kwa upande mwingine, Tanzania iliagiza bidhaa kutoka Jumuiya ya SADC zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 604.32 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 600.64 kwa mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 0.61.

**60. Mheshimiwa Spika;** Kwa upande wa Umoja wa Afrika (AU), mauzo ya bidhaa za Tanzania yalikuwa Dola za Marekani Milioni 1,485.05 mwaka 2018 ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 1,419.84 kwa mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 4.39. Ongezeko hilo limetokana na mauzo ya bidhaa za Madini, Pamba, Chai, Kahawa, Mahindi, Ngano, Alizeti, Mchele, bidhaa za Karatasi, Mabati, Vigae, Vyandarua, Kemikali (methyl bromide), Saruji na Mafuta ya Kupaka. Kwa upande mwingine, Tanzania ilagiza bidhaa kutoka Umoja wa Africa zenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 989.01 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani Milioni 895.88 kwa mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 9.42.

- *Tanzania na China*

**61. Mheshimiwa Spika;** Mwaka 2018, mauzo ya bidhaa za Tanzania yaliongezeka kwa Dola za Marekani milioni 1.98 kwenda China, kutoka Dola za Kimarekani milioni 142.3 mwaka 2017 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 144.28, sawa na ongezeko la asilimia 1.37. Ongezeko hilo linatokana na Tanzania kuuza zaidi ufuta, tumbaku, pamba, *jute*, manila (coconut, abaca) na nguo. Kati ya mwaka 2017 na 2018, Tanzania imeagiza bidhaa toka China zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 356.68, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 20.12. Hivyo, kufanya urari hasi wa biashara wa asilimia 21.79 kwa bidhaa zilizouzwa na Tanzania kwenda China kati ya kipindi husika.

- *Tanzania na India*

**62. Mheshimiwa Spika;** Mwaka 2018 mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda India yalikuwa ni Dola za Marekani milioni 734.27 mwaka 2018 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 977.6 zilizouzwa mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 33.4. Pia, mwaka 2018 Tanzania imeagiza zaidi bidhaa toka India zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 1,218.07 ikilinganishwa na bidhaa za Dola za Marekani milioni 1,077.60 zilizoagizwa mwaka 2017, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 11.53.

• *Tanzania na Japani*

**63. Mheshimiwa Spika;** Kwa nchi ya Japani, mwaka 2018 mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Japan yalikuwa ni Dola za Marekani milioni 66.72 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 75.7 zilizouzwa mwaka 2017, ikiwa ni sawa na upungufu wa asilimia 13.47 ya mauzo. Pia, mwaka 2018 Tanzania imeendelea kuagiza zaidi bidhaa kutoka Japani zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 398.13 ikilinganishwa na bidhaa za Dola za Marekani milioni 365.2 zilizoagizwa mwaka 2017, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 8.27.

**64. Mheshimiwa Spika;** Pamoja na biashara ya nje kuendelea vizuri, kumekuwepo na changamoto ambazo Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania (JWT) imezibainisha na kuhitaji Serikali kuingilia kati kwa nia ya kuboresha mazingira ya biashara. Baadhi ya changamoto hizo ni utoaji wa huduma usioridhisha katika bandari, mawasiliano hafifu baina ya mamlaka za Tanzania na wafanyabiashara wa DRC, kuwepo kwa udanganyifu wa baadhi ya wafanyabiashara, mawakala na watumishi wa Serikali wasio waaminifu, kutokuwepo kwa uwazi wa Ushuru wa Forodha na tuhuma za kuwepo kwa vitendo vya rushwa kwa baadhi ya watumishi wasio waadilifu. Katika kushughulikia changamoto hizo, Serikali imeanzisha na kuimarisha Vituo vya Pamoja Mipakani (OSBP) ambavyo taasisi za umma zinazosimamia na kuratibu masuala ya biashara zinafanya kazi kwa ushirikiano katika kila eneo moja la mpakani kupitia kamati za pamoja mipakani (Joint Border Committees - JBC) zenye wajumbe kutoka sekta binafsi wakiwakilisha jumuiya ya wafanyabiashara.

**Ushirikiano wa Kibiashara na EAC, SADC, AfCFTA**

**65. Mheshimiwa Spika;** Ili kusimamia muendelezo wa majadiliano ya kupeana fursa za masoko ya upendeleo mionganoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Biashara, Viwanda, Fedha na Uwekezaji (Sectoral Committee of Trade, Industry, Finance and

Investment - SCTIFI) wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 12 - 16 Novemba 2018 jijini Arusha. Moja ya suala muhimu liliojadiliwa na kufanyiwa uamuzi na Mkutano huo ni kwa Tanzania kufanikiwa kuiondoa Kampuni ya Nguo ya A to Z ya jijini Arusha kwenye orodha ya makampuni yanayonufaika na uingizaji wa malighafi za uzalishaji wa bidhaa za nguo kwa kutumia msamaha wa kodi (duty remission). Hatua hiyo itaifanya Kampuni hiyo kuendelea kuagiza malighafi zake kwa kulipa kodi stahiki na hivyo kuzalisha na kuuza bidhaa zake kwenye soko la EAC bila kutozwa kodi baada ya kukidhi vigezo vya uasili wa bidhaa.

### **Uhusiano wa Kibashara Kati ya Tanzania na Nchi Nyingine**

**66. Mheshimiwa Spika;** Katika kuendeleza na kukuza fursa za bishara nje, Wizara ilishiriki Mkutano wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano (JPC) baina ya Tanzania na Uganda tarehe 21 – 23 Agosti, 2018, Kampala, Uganda. Kupitia mkutano huo, Mawaziri walipokea taarifa ya hali ya utekelezaji wa maagizo ya Wakuu wa Nchi kuhusu ufanyaji kazi masaa 24 kwenye mpaka wa Mutukula ili kukuza bishara baina ya nchi hizo mbili. Ili kutatua changamoto za kibashara zinazojitokeza ikiwemo masuala ya vikwazo vya kibashara visivyo vya kiushuru, mkutano uliagiza kufanyike mkutano wa Mawaziri wa Biashara wa pande zote mbili kwa lengo la kuimarishe ushirikiano wa kibashara. Aidha, katika Mkutano huo, Mawaziri wa Tanzania na Uganda walisaini Hati za Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) katika Sekta za Ujenzi, Miundombinu, Nishati pamoja na Utumishi na Utawala Bora.

**67. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarishe uhusiano na kutekeleza uamuzi wa Mkutano wa 20 wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu Tanzania na Kenya kukutana kutatua changamoto za kibashara, nchi hizo zilifanya Mkutano wa 4 wa Pamoja tarehe 23-27 Aprili 2019 mjini Arusha. Kupitia Mkutano huo, Mawaziri waliweza kutatua baadhi ya vikwazo ambavyo vimekuwa kero kubwa hususan kwa wafanyabiashara nchini. Utatuzi huo ni pamoja na Kenya kukubali kuingiza bidhaa za Tanzania katika mfumo wa pamoja wa forodha unaotumia mtandao (Single Customs

Territory-SCT) ili kurahisisha utoaji wa mizigo pamoja na bidhaa za ngano kuruhusiwa kutumia utaratibu wa kuitisha mizigo kwa pamoja (bulk clearance) badala ya utaratibu wa awali wa mizigo mmoja mmoja (single clearance). Vilevile, Kenya iliahidi kupatia ufumbuzi haraka wa mizigo wa saruji iliyokuwa ikienda Pemba kutokea Iran kuititia bandari ya Mombasa ambao ulikuwa umekwama kwa zaidi ya mwaka mmoja.

### **Mikataba ya Kimataifa Kuhusu Biashara**

**68. Mheshimiwa Spika;** Wizara imeendelea na hatua za kujipanga katika kutimiza matakwa ya utekelezaji wa Mkataba wa Uwezeshaji Biashara wa Shirika la Biashara la Dunia (World trade Organization-WTO). Mkataba wa Uwezeshaji Biashara (Trade Facilitation Agreement) unaweka mfumo wa kisheria, muongozo na msukumo wa kimataifa kwa nchi wanachama wa WTO kwenye kutatua changamoto za ufanyaji biashara. Aidha, Mkataba huo pia unaweka utaratibu wa pamoja katika kushughulikia masuala ya uwezeshaji biashara mionganini mwa nchi wanachama wa WTO. Mkataba huo ulianza kutumika rasmi tarehe 22 Februari, 2017 baada ya kuridhiwa na nchi wanachama 112 kati ya wanachama 164 wa WTO. Aidha, hadi kufikia tarehe 27 Februari, 2019 nchi wanachama 141 tayari zimeridhia Mkataba huo. Hii ina maana nchi wanachama 23 ikiwemo Tanzania hazijaridhia Mkataba huo, ingawa taratibu za uridhiwaji za Mkataba huo nchini zimekwishaanza.

**69. Mheshimiwa Spika;** Katika kujipanga vyema na utekelezaji wa Mkataba huo, Wizara imeendelea kuratibu vikao vya Kamati ya Kitaifa ya Uwezeshaji Biashara. Kamati hiyo ilikutana katika mukutano wake wa kawaida tarehe 26- 29 Juni, 2018 Dar es Salaam. Mukutano huo ulifanyika kwa ajili ya maandalizi ya Mpango Kazi wa Kitaifa ambao utasaidia katika utekelezaji wa masuala ya uwezeshaji biashara nchini ikiwa ni pamoja na uingizaji wa masuala ya uwezeshaji biashara katika mipango na mikakati ya muda mfupi na mrefu ya Serikali. Rasimu ya Mpango Kazi huo itawasilishwa Serikalini mara itakapokamilika na kuridhiwa na wadau ifikapo mwezi Juni, 2019.

## **Uondoshaji wa Vikwazo vyat Ushuru na Visivyo vyat Ushuru (NTBs)**

**70. Mheshimiwa Spika;** Katika mukutano wa 20 wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (20th East African Community-EAC Heads of State Summit) uliofanyika tarehe 1 Februari, 2019, jijini Arusha, moja ya suala muhimu ambalo Viongozi hao walielekeza ni kuondoa Vikwazo vyat Biashara Visivyo vyat Ushuru (Non-Tariff Barriers – NTBs). Tayari vikwazo 45 kati ya 62 vimetatuliwa na 17 vinaendelea kutatuliwa. Aidha, mukutano ulielekeza nchi za Tanzania na Kenya kuhakikisha wanapata ufumbuzi wa NTBs mbili ambazo zinatakiwa kupatiwa muafaka kwenye ngazi ya Mawaziri. NTBs hizo zinahusu malalamiko ya Kenya kwenye sharti la Tanzania kutoza ushuru mkubwa katika sigara inayouzwa nchini ambayo uzalishaji wake haujatumia tumbaku ya Tanzania kwa kiwango cha asilimia 70 hadi 75 na Tanzania kuendelea kutoza kodi kwa bidhaa za Kenya zilizotengenezwa kwa kutumia sukari ya viwandani.

## **Mradi wa SADC Trade Related Facility (TRF)**

**71. Mheshimiwa Spika;** Tanzania ni moja ya nchi wanachama wa SADC zinazonufaika na Mradi wa *Trade Related Facility (TRF)*, unafadhiliwa na Umoja wa Ulaya kuitia Sekretarieti ya SADC Kwa kiasi cha Euro Milioni 1.4. Mradi huo unalenga kusaidia nchi wanachama wa SADC kutekeleza Itifaki ya Biashara ya Jumuiya hiyo (SADC Trade Protocol). Kwa upande wa Tanzania Mradi umejikita katika uendelezaji wa mnyororo wa thamani kwa zao la Alizeti; uwezesajhi biashara; na utafiti katika biashara ya huduma. Mradi wa TRF utafikia ukomo mwezi Septemba, 2019. Hadi sasa Mradi huo umeiwezesha TBS kununua mashine maalum yenye uwezo wakupima mafuta ya kula, ununuzi wa vifaa vyat maabara (pest and diseases diagnostic equipments) kwa ajili ya Wizara ya Kilimo; ununuzi wa vitendea kazi; na kuwezesha sekta binafsi kutafuta masoko ya mafuta ya alizeti kwenye nchi za SADC.

## **Mradi wa MARK UP**

**72. Mheshimiwa Spika;** Tanzania ni moja ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zitakazonufaika na Mradi wa *EU-EAC*

*Market Access Upgrade Programme (MARKUP).* Mradi huo unaafadhiliwa na Umoja wa Ulaya ili kusaidia nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kutekeleza vyema matakwa ya Mkataba na Itifaki za Jumuiya. Mradi huo una fursa (windows) mbili ambazo ni: fursa kwa ajili ya utekelezaji wa masuala ya kikanda ambayo yatakekelezwa na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; na fursa kwa ajili ya kila nchi mwanachama. Kupitia mradi huu Tanzania itanufaika na kuboresha mazao ya Kahawa, Chai, Viungo na Embe Mafuta (parachichi) na kuweza kuyafikia masoko ya Jumuia ya Ulaya.

### **Mapitio ya Sera ya Taifa ya Biashara**

**73. *Mheshimiwa Spika;*** Wizara inafanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Biashara (2003) ili kuendana na mahitaji ya ujenzi wa uchumi wa viwanda. Mapitio hayo pia yanazingatia mabadililkombalimbalyakiuchuminablasharayaliyojiteze kikanda (regional) na kimataifa (multilateral) kupitia utekelezaji wa Itifaki mbalimbali. Vilevile, zimekuwepo juhudzi za kupanua wigo zaidi wa kibashara kikanda na katika bara la Afrika. Juhudi hizo zinalenga kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Utatu litakalojumuisha kanda za EAC, SADC na COMESA (Tripartite FTA); na Eneo Huru la Biashara Afrika (African Continental Free Trade Area (AfCFTA). Sera hiyo inatarajiwaa kukamilika mwaka 2019/2020.

### **Usajili wa Makampuni, Majina ya Biashara, Alama za Biashara na Huduma, Leseni za Viwanda, Leseni za Biashara na Hatimiliki za ubunifu**

**74. *Mheshimiwa Spika;*** Mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao (Online Registration System - ORS) unaopatikana kupitia tovuti ya [www.brela.go.tz](http://www.brela.go.tz) unalenga kuwezesha kutoa huduma kwa njia ya mtandao ili kumfikia mteja popote alipo. Aidha, Mfumo huo unalenga kupunguza muda na gharama za usajili, kuiwezesha Serikali na wadau wengine kupata taarifa za usajili kwa haraka na kuweka kumbukumbu na taarifa sahihi katika mfumo ili kuwezesha mipango ya maendeleo. Vile vile, Mfumo unawezesha kuunganishwa na mifumo ya Taasisi nyingine za Serikali ili kuwezesha kupatikana kwa huduma

kwa njia ya kielektroniki mahali pamoja (Electronic One Stop Shop). Mfumo huo tayari umeunganishwa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kwa ajili ya utambuzi wa uhakika wa wamiliki na wakurugenzi wa Kampuni husika, TRA kwa ajili ya Namba za Utambulisho wa Mlipa Kodi (ambapo namba ya cheti cha Kampuni ni sawa na TIN), GePG kwa ajili ya kukusanya maduhuli ya Serikali, na TCRA kwa ajili ya kutambua maeneo.

**75. *Mheshimiwa Spika*:** Tangu Mfumo huo uanze kutumika hapo mwezi Februari, 2018 hadi Aprili, 2019 unafanya kazi vizuri na umeweza kusajili makampuni 6,918; Majina ya Biashara 11,382; Alama za Biashara na Huduma 4,117; Kutoa Hataza 28 na Leseni za Viwanda 166. Aidha, barua za kuomba taarifa 18,838 na taarifa za majalada zilizohuishwa 4,257 zilishughulikiwa.

#### **Mfumo wa National Business Portal (NBP)**

**76. *Mheshimiwa Spika*:** Mfumo wa Dirisha la Taifa la Biashara (National Business Portal) ulianzishwa pamoja na mambo mengine kutoa Leseni za Biashara kundi A na B kwa njia ya mtandao kwa wafanyabiashara popote walipo nchini ili kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini. Mfumo huo huwezesha kupunguza muda na gharama za kufuata leseni katika ofisi za BRELA au katika ofisi za Halmashauri, kupata taarifa za usajili kwa haraka kwa Serikali na wadau wengine, na kuweka kumbukumbu za Leseni za Biashara na taarifa sahihi katika mfumo.

**77. *Mheshimiwa Spika*:** Mfumo huo umekamilika na umefanyiwa majoribio na wataalam wa BRELA na TAMISEMI Makao Makuu baada ya kuunganishwa na Mfumo wa GePG na Mfumo wa TAMISEMI wa kukusanya maduhuli. Mafunzo kwa watumiaji (Maafisa Biashara na wataalmu wa TEHAMA) yametolewa katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani na yatafanyika katika ngazi za Mikoa na Halmashauri zote nchini. Mfumo huo utaanza kutumika rasmi pindi marekebisho machache yaliyotolewa na Maafisa Biashara na TEHAMA ikiwemo kuwepo kwa vifaa vya TEHAMA katika ofisi za Maafisa Biashara wa Halmashauri zote nchini yatakapokamilika.

## **Utekelezaji wa Mfumo Rafiki wa Ufanyaji wa Biashara Nchini**

**78. *Mheshimiwa Spika*:** Wizara imeendelea na jitihada za kurahisisha mazingira ya kufanya biashara nchini kupitia uratibu wa mikutano mbalimbali ambayo imekuwa ikizikutanisha Wizara za kisekta, Taasisi za Serikali pamoja na vyama vya wafanyabiashara ili kuainisha na kujadiliana namna bora ya kuondoa vikwazo mbalimbali vya biashara ikiwemo kodi. Kupitia mikutano hiyo, hadi kufikia Januari, 2019, tozo 1,010 zilizo katika Sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuuvi zimefutwa na tozo 4 zimepunguzwa. Tarehe 7 na 8 Novemba, 2018, Wizara iliratibu mikutano miwili na Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania na kujadili changamoto mbalimbali zinazoikabili jumuiya hiyo na kuzitafutia ufumbuzi. Wizara na Taasisi ziliweza kujibu hoja na malalamiko yaliyoelekezwa kwao na Jumuiya hiyo ya wafanyabiashara. Baadhi ya hoja zilizojitokeza ni pamoja na taratibu na kanuni zinazotumika bandarini, TRA, matumizi ya *Electronic Fiscal Device - EFD*, Mamlaka za Uthibiti, Mamlaka za Utoaji Leseni pamoja na ukosefu wa maeneo ya kufanya biashara. Kutokana na vikao hivyo, Wizara na Taasisi zote zimetakiwa kutoa taarifa kuhusu namna zinavyoshughulikia malalamiko ya wafanyabiashara kila mwezi ili kuwezesha Serikali kuchukua hatua mapema na kuepuka taasisi hizo kuwa kikwazo cha kufanya biashara nchini.

**79. *Mheshimiwa Spika*:** Wizara imeendelea na jukumu la kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini, kwa kuondoa mwingiliano wa majukumu katika taasisi za umma na kurahisisha utaratibu wa kupata vibali na leseni za biashara ili kupunguza urasimu na gharama za uanzishaji na uendeshaji wa biashara. Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilianda kitabu (blue print) kinachoainisha shughuli na majukumu mbalimbali ambayo yanatakiwa kutekelezwa. Rasimu ya Mpango kazi wa Utekelezaji (Action Plan) wa *Blue Print* umekamilika na utekelezaji utaanza mwezi Julai, 2019. Aidha, baadhi ya mapendekezo ya *Blue Print* yasiyohitaji maamuzi ya Serikali yamefanyiwa kazi bila kusubiri mpango kazi. Baadhi ya mapendekezo hayo ni pamoja na kuweka mifumo ya kielektroniki katika usajili wa majina ya biashara,

uandikishwaji wa makampuni, kusajili alama za biashara, hatazo na leseni za viwanda.

### **Kusimamisha kwa Muda Utekelezaji wa Kanuni za Sheria ya Vipimo Kwenye Biashara ya Viazi Mviringo**

**80. *Mheshimiwa Spika***; Katika kutambua changamoto zinazowakabili wafanyabiashra wa viazi mviringo hususan kukosekana kwa vifungashio vinavyotumika kusafirishia kutoka maeneo ya uzalishaji kwenda sokoni, Serikali imeamua kusitisha kwa muda matumizi ya sheria ya vipimo inayotaka kutumia vifungashio. Sheria ilikuwa ikiwataka wazalishaji kutumia vifungashio maalum ambayyo kwa bahati mbaya upatikanaji wake una matatizo.

#### **3.4 SEKTA YA MASOKO**

##### **Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ulivyosaidia Kipato cha Wakulima na Changamoto zake**

**81. *Mheshimiwa Spika***; Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ni utaratibu wa biashara unaowezesha bidhaa kuhifadhiwa ghalani na stakabadhi kutolewa kwa mwenye mali inayothibitisha umiliki wake, thamani, aina, idadi na ubora (daraja). Stakabadhi ya Ghala ni hati inayoweza kutumika kama dhamana kumwezesha mmiliki kupata mkopo kutoka taasisi za fedha. Hivyo, Mfumo umeweza benki za biashara kushiriki katika ununuzi na uuzaji wa mazao kwa kuwa urejeshaji wa mikopo ni wa uhakika. Manufaa yaliyopatikana kuitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ni pamoja na kuimarika kwa usimamizi wa ubora, hifadhi bora ya mazao na kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa wakulima na hivyo kuwapa fursa kuuza wakati wa bei nzuri. Manufaa mengine ni ongezeko la bei ya mkulima kutokeana na ushindani katika soko na ongezeko la ujenzi wa ghala za kuhifadhia mazao.

**82. *Mheshimiwa Spika***; Katika msimu wa 2018, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mfumo katika mazao ya Korosho ikiwemo kusajili maghala ya kuhifadhi korosho na waendesha maghala waliosimamia kupokea na kuhifadhi korosho katika maghala yaliyosajiliwa. Pia, Mfumo ultumika

katika mazao ya mpunga na mahindi. Aidha, matumizi ya Mfumo katika mazao mengine ikiwemo ufuta unategemea kuanzishwa katika msimu ujao.

**83. *Mheshimiwa Spika***; Pamoja na mafanikio ya Mfumo huo, kumekuwa na changamoto kwa viwanda nya ndani hususan katika kupata malighafi kwa bei shindani kwa mazao yanayopatikana kuititia Mfumo huo. Katika kushughulikia changamoto hiyo, Serikali inaandaa utaratibu mahsusii utakaowezesha viwanda nya ndani kupata malighafi kwa uhakika ili viweze kuwa shindani katika soko.

### **Biashara na Masoko ya Mipakani**

**84. *Mheshimiwa Spika***; Tanzania ina jumla ya njia 48 za kuitisha bidhaa katika mipaka na nchi jirani za Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda, DRC Congo, Zambia, Malawi na Msumbiji. Katika kuchochaea biashara rasmi, Serikali inahamasisha na kuanzisha ujenzi wa masoko ya mipakani ili kukuza biashara na kusaidia kuboresha hali za maisha ya wakazi wa maeneo hayo. Mikoa iliyotenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa masoko ni Kagera (Mtukula, Murongo, Kabanga na Rusumo), Mara (Sirari na Shirati), Mtwara (Kilambo na Mtambaswala), Ruvuma (Mbamba Bay na Mkenda), Kigoma (Kibiri na Manyovu), Rukwa (Kirando, Kipuli, Kasanga na Kasesya), Mbeya (Tunduma na Kasumulu) na mikoa mingine ni Tanga (Horohoro), Kilimanjaro (Tarakea) na Arusha (Namanga). Ili kuwezesha wafanyabiashara, magari na bidhaa kukaguliwa mara moja wakati wa kuingia au kutoka katika mpaka kwa gharama na muda mfupi, Serikali kwa kushirikiana na nchi jirani imeanzisha Vituo nya Pamoja nya Mipakani (One Stop Border Post-OSBP) ambapo Taasisi za udhibiti zikiwemo TRA na TBS hukagua bidhaa toka nchi za jirani. Utaratibu huu umeongeza ufanisi hususan kutumia muda mfupi kukamilisha ukaguzi na biashara kuendelea.

**85. *Mheshimiwa Spika***; Mpaka sasa vituo tisa (9) vimeanzishwa katika mipaka baina ya Tanzania na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, pamoja na nchi ya Zambia. Vituo hivyo ni Holili/Taveta (Tanzania na Kenya), Sirari/Isebania (Tanzania na Kenya), Namanga/ Namanga (Tanzania na

Kenya), Kabanga/Kobero (Tanzania na Burundi), Rusumo/Rusumo (Tanzania na Rwanda), Mtukula/Mtukula (Tanzania na Uganda), Horohoro / Lungalunga, (Tanzania na Kenya), Tunduma/Nakonde (Tanzania na Zambia) na Kasumulu/Songwe (Tanzania/ Malawi). Hali ya biashara mipakani inaendelea vizuri ambapo Serikali imeendelea kutumia Itifaki za umoja wa forodha (Custom Union Protocol) na Itifaki ya Soko huru la Pamoja (Common Market Protocol) kurahisisha biashara kati ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwa upande wa mipaka ya nchi na nchi wanachama wa SADC kama Zambia, Malawi na Msumbiji biashara inasimamiwa kupitia Itifaki ya biashara ya nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika (SADC Trade Protocol).

**86. *Mheshimiwa Spika***; Wizara kupitia TanTrade kwa kushirikiana na Shirika la Biashara la Kimataifa(ITC), iliratibu mradi wa kujenga na kuimarisha uwezo wa wanawake wanaofanya biashara isiyorasi (informal cross border trade) katika Wilaya ziliopo kwenye Mipaka ya Tanzania na Nchi jirani. Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2019 jumla ya vikundi tisa (9) vya Wafanyabiashara Wanawake wadogo na wa kati viliundwa, Wafanyabiashara Wanawake 292 Mpakani wamerasimisha biashara zao katika Halmashauri za Wilaya Nane (8), ambazo ni Buhigwe, Kasulu, Ngara, Misenyi, Tarime, Longido, Rombo na Mkinga zilishiriki. Aidha, wameweza kuunganishwa na fursa za masoko ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo zimekidhi matakwa ya hati ya uasili wa bidhaa (Rules of Origin).

**87. *Mheshimiwa Spika***; Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa utaratibu wa kurahisisha ufanyaji biashara mipakani kwa wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo ambapo mfanyakibashara mdogo mwenye bidhaa zisizozidi thamani ya Dola za Marekani 2,000 hazihitajiki kutumia cheti cha uasili wa bidhaa na badala yake anatumia utaratibu rahisi ujulikano kama *Simplified Trade Regime*. Utaratibu huo unatumika kwa mipaka rasmi yote kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na mpaka wa Tanzania na Zambia (Tunduma/Nakonde).

### **Umuhimu wa Maonesho ya Biashara ya Ndani na Nje**

**88. Mheshimiwa Spika;** Maonesho ya biashara ya ndani na nje ya nchi yameendelea kuwa nyenzo muhimu ya ukuzaji biashara, inayochochea maendeleo ya viwanda kwa kufungua fursa za masoko ya ndani na nje na kuvutia uwekezaji. Aidha, Maonesho hukutanisha Wauzaji na Wanunuzi wa bidhaa au huduma pamoja na kuwezesha kubadilisha na taarifa za biashara na huduma ikiwemo kuingia katika miadi ya kibiashara na bidhaa. Jukwaa hili huwawezesha Wazalishaji na Wafanyabiashara kupata mwanya wa kupokea maoni moja kwa moja kutoka kwa watumiaji wa bidhaa au huduma na hivyo hupata mawazo mapya; kuwezesha ubunifu, kubadilishana uzoefu, kuendeleza bidhaa, kuongeza ubora na hatimaye kuwezesha bidhaa za Tanzania kuwa na ushindani katika soko la Ndani, Kikanda na Kimataifa.

**89. Mheshimiwa Spika;** Kutokana na umuhimu wa Maonesho katika kukuza biashara, Wizara kuititia TanTrade imeendelea kuratibu Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam ambayo Mwaka huu yatatimiza miaka 43. Maonesho haya yameendelea kuvutia Washiriki wengi kutoka ndani na nje ya nchi ambapo mwaka 2018, Maonesho ya 42 yalishirikisha nchi 33. Vilevile, Wizara kuititia TanTrade imeendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika Maonesho ya dunia EXPO pamoja na kuandaa ushiriki katika Maonesho katika nchi jirani za Kenya, Rwanda, Uganda, Burundi, Swaziland, Msumbiji, Afrika Kusini na China.

### **Kufanya Tafiti za Mazao**

**90. Mheshimiwa Spika;** Wizara kuititia TanTrade hufanya tafiti za bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini ili kubaini changamoto na fursa za bidhaa na huduma hizo kwa lengo la kuziendeleza na kuzitafutia masoko ya ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia mwaka 2018, TanTrade imefanya tafiti za mazao 13 katika Mikoa 19 nchini zikijumuisha mahindi, mpunga, ufuta, mbaazi, kakao, alizeti, mwani, muhogo, sanaa za mikono, viungo, matunda na mbogamboga, ngozi na bidhaa za ngozi, bidhaa za nguo, asali na michikichi. Aidha, TanTrade inashirikiana kwa karibu na Wizara ya Mambo ya Nje na

Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Balozi za Tanzania nje ya nchi na Balozi za Nchi rafiki zilizopo nchini ili kupata taarifa zaidi za kiutafiti na masoko ya mazao na bidhaa za Tanzania.

### **Kutafuta Masoko ya Bidhaa za Viwanda**

**91. Mheshimiwa Spika:** Wizara kuptitia TanTrade inaendelea kuratibu na kusimamia Maonesho maalumu yanayolenga kutangaza bidhaa na fursa mbalimbali zilizopo katika Sekta ya Viwanda. Maonesho hayo, huwakutanisha wazalishaji wa malighafi za viwanda, wenyewe viwanda na wanunuzi mbalimbali wa bidhaa za viwandani ili kuweza kutengeneza mitandao ya kibashara. Aidha, wadau wa Sekta ya Viwanda na Taasisi za Serikali hupata fursa ya kujadili changamoto mbalimbali na kuzitafutia ufumbuzi. Pamoja na jitihada hizo, TanTrade imefanya tathmini ya mahitaji ya viwanda vinavyotumia malighafi za mazao ya kilimo ili kuunganisha vikundi vya wazalishaji na viwanda hivyo.

### **Umuhimu wa Sera ya Taifa ya Ubora**

**92. Mheshimiwa Spika:** Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaandaa Sera ya Taifa ya Ubora inayolenga kusimamia masuala yote ya ubora nchini sambamba na kulinda afya ya mlaji, wanyama, mimea na mazingira kwa ujumla. Pia, Sera hii itarajiwa kuwa muongozo wa mtangamano wa Miundombinu ya Taifa ya Ubora ambayo ni *Metrology, Standardization, Accreditation, Conformity Assessment* na *Market Surveillance*. Mtangamano huo unakusudiwa kuondoa muingiliano baina ya taasisi zinazojihusisha na masuala ya ubora. Aidha, Sera ya Taifa ya Ubora itatoa muongozo katika makubaliano ya Shirika la Dunia la Biashara (WTO) hasa vikwazo vya kiufundi vya biashara (TBT) na matumizi ya vikwazo vya kulinda afya ya mimea na wanyama (SPS). Hadi sasa nchi kadhaa barani Afrika zimeshaandaa Sera ya ubora ikiwa ni pamoja na Namibia, Nigeria na Rwanda.

### **Vituo Maalum vya Kuuzia Mazao**

**93. Mheshimiwa Spika:** Serikali inaendelea kuhamasisha ujenzi wa Vituo maalum vya ununuzi wa Mazao (*buying centers*)

vyenye kutengewa nafasi ya maghala kuweza kuhifadhi mazao. Kufuatia marekebisho ya Sheria ya Vipimo, Wizara imewasilisha Ofisi ya Rais (TAMISEMI) mapendekezo ya kutungwa kwa sheria ndogo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zitakazowaongoza wakulima na wafanyabiashara kufungasha mazao kwa mujibu wa sheria ya vipimo na kanuni zake. Ili kurahisisha usimamizi wa matumizi ya vipimo rasmi katika ununuzi wa mazao, Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaainisha vituo maalum (Buying centres) katika vitongoji nchi nzima na kwa mazao yote na hivyo hakuna mfanyabiashara atakayeruhusiwa kununua, kusafirisha na kuza mazao ambayo yamefungashwa kinyume na Sheria ya Vipimo. Kupitia Bunge lako tukufu, niwaombe Waheshimiwa Wabunge kuwahimiza wakulima kutumia vituo na kutokubali kurubuniwa kuza mazao yakiwa shambani.

### **Marekebisho ya Sheria za TBS, WMA, FCC na FCT**

**94. *Mheshimiwa Spika;*** Sheria ya Viwango Na 2/2009 na Sheria ya Vipimo Sura 340 zimefanyiwa mapitio na kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mwezi Januari, 2019 ili kuwezesha marekebisho kwa njia ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Miscellaneous Amendments). Aidha, Sheria ya Ushindani Sura 285 pia imefanyiwa mapitio na tayari Waraka wa Baraza la Waziri umeandaliwa kwa hatua zinazofuata

### **Itifaki ya Marrakesh**

**95. *Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ni moja ya nchi mwanachama iliyoridhia *Convention* ya Shirika la Miliki Ubunifu Duniani (World Intellectual Property Organization - WIPO) mwaka 1983 ilioanza kutumika mwaka 1979. Tarehe 27 Juni, 2013, Tanzania ilishiriki katika mkutano wa WIPO uliofanyika mjini Marrakesh – Morocco ambao ulipitisha Itifaki inayowezesha kupata na kuzalisha kazi kwa watu wasiona, uoni hafifu, ulemavu unaofanya mtu kushindwa kusoma kwa njia rahisi wa mwaka 2013 (*The Marrakesh Treaty to Facilitate Access to Published Works for Persons who are Blind, Visually Impaired or Otherwise Print Disabled (Mvt) 2013*). Itifaki hiyo imeanza kutekelezwa tarehe 30 Septemba, 2016 baada ya

masharti ya kuanza kutimia kwa maana ya idadi ya nchi wanachama kutimia.

**96. Mheshimiwa Spika;** Tanzania haikuweza kuweka sahihi kwa kipindi hicho ili kuweza kujipa muda kupata maoni kutoka kwa wadau. Mwaka 2018/2020, Wizara imeandaa waraka ili kupata ridhaa ya serikali na Bunge kwa Tanzania kujiunga na Itifaki hiyo. Itifaki hiyo inatoa fursa ya upendeleo na upekee kwenye sheria za Hakimiliki ili ziruhusu uzalishaji, usambazaji na kuwezesha upatikanaji wa kazi zilizochapishwa kuwa katika mfumo rafiki kwa walengwa walijotajwa hapo juu.

### **3.5 MASUALA MTAMBUKA**

**Kuhamia Dodoma, Ajira Mpya, Kujenga Uwezo Kupandisha Vyeo na OPRAS**

**97. Mheshimiwa Spika;** Wizara imekamilisha uhamisho wa watumishi wake sabini (70) wa awamu ya mwisho kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma. Pia hadi kufikia mwezi Machi, 2019, Wizara imefanikiwa kuajiri watumishi wapatao sita wa kada mbalimbali. Aidha, Wizara imepokea watumishi wanne wa kada mbalimbali waliohamia ambao wameongeza tija na ufanisi katika utendaji kazi wa kila siku.

**98. Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka 2018/2019, Wizara imefanikiwa kuapeleka katika mafunzo ya muda mrefu watumishi wake wapatao 17 pamoja na watumishi tisa katika mafunzo ya muda mfupi. Watumishi hao wanashiriki katika mafunzo hayo katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Watumishi wapatao 174 wako katika mpango wa kupandishwa vyeo pindi taratibu zitakapokamilika. Kwa mwaka 2018/2019, jumlayawatumishisitawamethibitishwa katika vyeo vyao baada ya kuthibitika kuwa wameweza kumudu majukumu ya vyeo vyao vipya katika kipindi chao cha majaribio.

**99. Mheshimiwa Spika;** Wizara imesimamia utekelezaji wa zoezi hilo ambapo jumla ya watumishi 184 wamejaza fomu za Kupima Utendaji Kazi kwa Watumishi kwa Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi (MWAMTUKE). Hata

hivyo, watumishi wapatao 24 hawakujaza fomu hizo kwani wako katika mafunzo ya muda mrefu

### **Mapambano Dhidi ya Rushwa**

**100. Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha mwaka 2018/2019, Wizara imefanikiwa kuandaa mpango kazi wa kutekeleza Mkakati wa Tatu wa Taifa wa Kupambana na Kudhibiti Rushwa. Pia, Wizara imeanza kuhuisha Mkataba wa Huduma kwa Mteja uliopo ili kuongeza ufanisi katika utoaji huduma bora kwa umma na wadau. Aidha, katika mwaka 2018/2019, Wizara haikupokea taarifa yoyote kuhusu vitendo wala viashiria vya rushwa katika utoaji wa huduma kutoka kwa wateja wake wa ndani na wa nje. Hii ni matokeo ya Wizara kupitia vikao vya Menejimenti na vikao kazi vya watumishi kutoa maelekezo na elimu ya Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya kiutumishi.

### **Mazingira**

**101. Mheshimiwa Spika;** Wizara imeendelea kutoa elimu juu ya athari za mazingira kwa wenyewe viwanda na wafanyakiasa sambamba na kuwashauri kutumia teknolojia rafiki (cleaner production technologies) kwa mazingira.

### **Mapambano Dhidi ya UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza**

**102. Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka 2018/2019, Wizara imeweza kutoa huduma bora kwa watumishi watatu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI waliojiweka wazi kwa mujibu wa Mwongozo wa Serikali. Huduma hizo ni pamoja na utoaji wa fedha kwa ajili ya lishe na usafiri kila mwezi pamoja na mafuta maalum ya ngozi kwa mtumishi mmoja mwenye ulemavu wa ngozi.

**103. Mheshimiwa Spika;** Kwa kushirikiana na wadau wa kupambana na UKIMWI, Virusi vya UKIMWI(VVU) na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) TACAIDS pamoja na

Jiji la Dodoma chini ya ufadhili wa ILO, Wizara ilifanikiwa kutekeleza zoezi la upimaji kwa watumishi wake wapatao 127 kwa lengo la kuangalia afya za watumishi na kubaini kiwango cha maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU). Kabla na baada ya upimaji, watumishi walipewa ushauri nasaha na elimu kuhusu namna bora ya kulinda na kutunza afya zao hali itakayowawezesha kuendelea kutekeleza majukumu yao ya kila siku wakiwa na afya njema. Pia, Wizara imekamilisha uteuzi wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) ambayo itafanya kazi ya kuratibu na kushauri Menejimenti ya Wizara namna nzuri ya kushughulikia masuala ya UKIMWI na MSY mahala pa kazi.

### **3.6           Ukaguzi wa Ndani, Ununuzi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha**

**104. *Mheshimiwa Spika***; Katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kulingana na sheria, miongozo na kanuni zilizowekwa. Katika kuhakikisha kuwa kunakuwa na matumizi sahihi ya rasilimali za Serikali, Wizara imefanya ukaguzi wa fedha, miradi ya maendeleo, rasilimali watu na ununuzi ili kuhakikisha kwamba sheria, kanuni na taratibu zinafuatwa na hatimaye kuiwezesha Wizara kupata Hati Safi ya Ukaguzi. Aidha, Kamati ya ukaguzi ya Wizara ilifanya vi kao viwilli ili kupitia taarifa za Hesabu pamoja na ukaguzi na kutoa ushauri unaostahili kwa Afisa Masuhuli

**105. *Mheshimiwa Spika***, Wizara imehakikisha inafanya matumizi kulingana na Kanuni, Taratibu na Sheria za fedha za Serikali. Matumizi yote yalifanyika kulingana na mpangilio wa Bajeti ya Wizara (objective, targets and activities). Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, Wizara imeendelea kuimarisha Kitengo cha Fedha na Uhasibu ili kiweze kuhakikisha taratibu zote za fedha zinafuatwa na malipo yanafanyika kulingana na vipaumbele vilivyowekwa kwenye Bajeti ya Wizara. Aidha, wahasibu wameendelea kujengewa uwezo kwa kupelekwa kwenye mafunzo ili kupanua taaluma yao na kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

**106. *Mheshimiwa Spika***; Kutokana na usimamizi huo mahiri wa Taratibu na Sheria za fedha, Wizara imeweza kupata hati

safi (unqualified opinion) kwa hesabu za mwaka wa fedha 2017/18 kwa Fungu 44 na Fungu 60.

**107. Mheshimiwa Spika;** Wizara imeendelea kusimamia shughuli mbalimbali za ununuzi kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi Na.7 ya mwaka 2011 (iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2016) na kanuni zake za mwaka 2013, GN 446. Katika mwaka 2018/2019, Wizara ilianda Mpango wa Ununuzi na kusimamia utekelezaji wake. Pia ilianda taarifa za ununuzi za kila mwezi na kila robo ya mwaka na kuwasilishwa kwa Taasisi ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA). Aidha, Wizara ilihakiki mali zake na kufanikisha uhuishaji wa Daftari la Mali za Wizara kwa mujibu wa Sheria ya Fedha Na. 6 ya Mwaka 2001 na Kanuni zake, GN.132 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2004.

### **3.7              Huduma ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)**

**108. Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kusimamia matumizi bora na sahihi ya miundombinu ya TEHAMA katika kutoa huduma kwa wateja wa ndani na nje. Miundombinu ya TEHAMA imeboreshwa na mafunzo mbalimbali yametolewa kwa watumishi kuhusu matumizi bora na sahihi ya miundombinu na rasilimali za TEHAMA. Aidha, Tovuti ya Wizara imehuishwa ili kuwapatia wananchi taarifa sahihi na kwa wakati na kuwawezesha kutoa na kupata mrejesho wa maoni au malalamiko juu ya huduma zinazotolewa na Wizara. Wizara pia imeongeza wigo wa kutoa taarifa kwa wananchi kwa kufungua akaunti katika mitandao ya kijamii, ili kuhakikisha Sera na Kauli Mbiu ya Tanzania ya viwanda inafika kwa kila mwananchi.

### **3.8              Huduma za Sheria**

**109. Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikaliilisimamianakuutiliamashaurimbalimbaliambayo Wizara na Taasisi zake zimeshitaki au kushitakiwa. Aidha, Wizara imefanya kazi marekebisho ya Kanuni mbalimbali

ikiwemo *The Weight and Measures (Metrological Control of Electricity and Natural Gas (Amendment) Regulations 2018; The Copyright (Licensing of Reproduction and Rental Rights (Amendments) Regulations, 2018; The Fair Competition Commission Procedure (Amendments) Rules 2019; The Copyright and Neighbouring Rights (Copyrighted Works - Communication to the Public (Amendments) Regulations, 2019; na Agricultural Mechanisation and Rural Technology (Amendment) Regulation 2018.*

**110. Mheshimiwa Spika;** Wizara imefanya kazi Mikataba mbalimbali ikiwemo Mkataba wa COSOTA na KONIPOR Norway ambao sasa umewasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa hatua zaidi. Pia, Wizara imefanya upekuzi wa Alama za Viwango vya Biashara chini ya Sheria ya Viwango ili kumlinda mlaji na mtumiaji wa bidhaa mbalimbali Tanzania. Vilevile, ulifanyika upekuzi wa wakaguzi wa TBS na kuwatangaza katika Gazeti la Serikali 2018 ili kuimarisha utendaji wa TBS.

### **3.9 Mawasiliano Serikalini**

**111. Mheshimiwa Spika;** Wizara katika mwaka 2018/2019 iliedelea kuandaa taarifa kwa umma kuhusiana na Sekta ya Viwanda na Biashara. Pia, imeendelea kutoa taarifa kwa umma kuhusiana na utekelezaji wa majukumu ya kisekta zikiwemo taarifa za masoko na masuala ya utendaji ya Wizara. Aidha, Wizara inaendelea na maandalizi ya kutengeneza Makala ya Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano katika Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko.

## **4.0 MWELEKEO NA VIPAUMBELE VYA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA KWA MWAKA 2019/2020**

### **4.1 MWELEKEO WA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA**

**Kuimarisha Sekta Binafsi Kama Injini ya Kujenga Uchumi wa Viwanda**

**112. Mheshimiwa Spika;** Ujenzi wa uchumi wa viwanda ikiwa ndiyo ajenda kuu ya Serikali ya Awamu ya Tano inatambua

umuhimu wa kufungamanisha sekta za uchumi kwa kushirikisha sekta binafsi na za umma. Mtazamo na mwelekeo mkuu utaendelea kuweka mbele nafasi ya sekta binafsi kuwa injini ya uchumi na Serikali kuendelea kuweka mazingira rafiki na wezeshi ili kuhakikisha wadau wote wanatoa mchango unaohitajika katika ujenzi za uchumi wa Taifa letu.

**113. *Mheshimiwa Spika***; Pamoja na kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji katika viwanda na biashara, utekelezaji wa *Blue Print* unaangaliwa kuwa sehemu kubwa ya tiba ya changamoto ambazo zinawatatiza sekta binafsi. Hivyo, ni mategemeo ya Serikali kuona kuwa sekta binafsi inachukua nafasi yake na kuchangamkia fursa zilizopo kuzalisha na kutoa huduma ikiwa ni hatua muhimu ya kutambua jitihada zilizofanywa na Serikali katika kutatua matatizo wanayokabiliana nayo.

**114. *Mheshimiwa Spika***; Katikakuendeleakujengauchumi wa viwanda ni mtazamo na dhamira ya Serikali kuwa sekta binafsi, kwa kutumia vivutio na maboresho yanayofanywa itajielekeza zaidi katika kujenga viwanda vinavyoongeza thamani mazao yanayozalishwa nchini ili kuondokana na uuzaaji wa malighafi nje ya nchi na hivyo kuwa soko la kwanza la uhakika kwa wazalishaji wa mazao nchini. Aidha, sekta binafsi inategemewa kujenga viwanda vinavyotoa ajira kwa wingi na vile vinavyozalisha bidhaa zinazotumiwa na Watanzania walio wengi ambavyo vitachangia katika kukuza soko la ndani na hivyo kuwa dirisha la mwendelezo wa soko la nje. Vilevile, Serikali itahakikisha inashirikiana na sekta binafsi katika kuendelea kuwezesha upatikanaji wa maeneo ya uwekezaji yenye miundombinu ili kuvutia wawekezaji zaidi.

**115. *Mheshimiwa Spika***; Aidha, jitihada zinafanywa za kuimarisha Taasisi za Kuendeleza Uwekezaji, Taasisi za Utafiti, Maendeleo ya Teknolojia na Mafunzo na Taasisi za Ushindani na Udhibiti wa Ubora wa Bidhaa na Huduma. Na ili kuchagiza zaidi maendeleo ya ujenzi wa uchumi unaonufaisha wadau wote, matumizi ya mifumo rasmi katika mnyororo wa thamani kama vile matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika manunuzi, vituo maalum vya mauzo, n.k lazima uimarishe

na kutumika kwa kiwango cha juu. Katika kufanya hivyo, chachu ya ulinzi wa viwanda na mlaji utakuwa kichocheo muhimu katika biashara nchini.

**116. *Mheshimiwa Spika***; Ni dhahiri kuwa, utekelezaji kwa ushirikishaji, ujumuishaji na uunganishaji wa jitihada hizo ni ishara ya wazi ya kutii na kuthamini umahiri wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 – 2020, Dira ya Taifa 2025 na Maagizo ya viongozi wa Serikali na hususan Mheshimiwa Rais wetu. Kwa misingi hiyo, msukumo wa kuendeleza viwanda vidogo sana, vidogo, vyatiki na vikubwa umejengwa vyema na unahitaji kuchangamkiwa na wazalendo wote ili kila mmoja awe sehemu ya ujenzi wa uchumi wa viwanda na hivyo kutoa mchango unaohitajika katika kujenga Taifa lenye furaha na maendeleo.

#### **Utekelezaji wa Mfumo Rafiki wa Uwekezaji na Ufanyaji wa Biashara Nchini**

**117. *Mheshimiwa Spika***; Kwa kutambua umuhimu wa kuweka mazingira rafiki kwa biashara na uwekezaji, Wizara katika mwaka 2019/2020 itaanza kutekeleza baadhi ya vipengele vyatiki Blue Print baada ya Mpango kazi wa utekelezaji kukamilika.

#### **Kuimarisha Taasisi za Kusajili, Kuratibu na Kuendeleza Uwekezaji, Utafiti, Maendeleo ya Teknolojia, Ushindani, Udhhibitii wa Ubora wa Bidhaa na Huduma, Kuimarisha Usimamizi wa Masoko, Vituo vyatiki Mauzo ya Bidhaa, Matumizi ya Soko la Bidhaa**

**118. *Mheshimiwa Spika***; Katika kuboresha mazingira ya biashara na kuongeza ushindani wa kibashara na kuhakikisha ubora wa bidhaa na huduma hudhibitiwa, Serikali imekamilisha na sasa inaendelea kuboresha mifumo ya usajili wa Kampuni na majina ya biashara na kuhakikisha leseni za biashara za daraja A zinazotolewa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na daraja B zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) kuitia mfumo wa

kielectroniki. Kufuatia kukamilika kwa mfumo wa Dirisha la Taifa la Biashara (National Business Portal) ambao ndio unaotoa leseni za biashara, Wakala imeanza kutoa mafunzo kwa maafisa biashara na wa TEHAMA wa Halmashauri zote nchini. Mafunzo hayo yatafanyika kwa Maafisa Biashara na Maafisa TEHAMA wa Mkoa na Wilaya zote nchini.

**119. *Mheshimiwa Spika***; Serikali pia itaendelea kufanya kaguzi za bidhaa zilizofungashwa kwenye maeneo ya Mipaka ya Holili, Namanga, Mutukula, Sirari, Kasumulo, Horohoro na Tunduma. Aidha, ukaguzi hizi pia zitahusisha Bandari za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na Kigoma. Vilevile, kaguzi za bidhaa zilizofungashwa kwenye maeneo ya viwandani ambazo ni pamoja na bidhaa za vyakula, vilainishi, saruji, rangi, mitumba, maziwa, mabati, nondo na vinywaji baridi zitaendelea kufanyiwa kwa mujibu wa Sheria.

**120. *Mheshimiwa Spika***; Shirika la Viwango Tanzania (TBS) litaendelea kuandaa viwango muhimu katika kilimo, chakula, uhandisi na viwango vya vifungashio mbalimbali na pia litaendelea kusimamia viwango vya kitaifa kwa kutumia mifumo iliyopo ya kuhakiki ubora (Certification Schemes). Aidha, Shirika litaendelea kutoa leseni za nembo ya ubora ya TBS kwa wajasiriamali wadogo wanaozalisha bidhaa mbalimbali zinazotokana na mazao na bidhaa za kilimo, mifugo na misitu na bidhaa kutoka sekta zingine za uchumi. Vilevile, Shirika litaendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali (SMEs) na wadau mbalimbali katika dhana nzima ya kuzingatia mifumo ya ubora ili kuzalisha bidhaa zenyne ubora. Mafunzo na semina hizo yatatolewa kwa wajasiriamali wadogo pamoja na wadau mbalimbali katika mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara.

**121. *Mheshimiwa Spika***; Serikali itaratibu ushirikiano wa Taasisi za udhibiti ambazo ni Shirika la TBS, Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS), TRA, GCLA, EWURA, SUMATRA, TFDA, FCC, NEMC, NIT, TPA na Jeshi la Polisi, katika kusimamia ubora wa bidhaa hasa zinazotoka nje kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa lengo la kuhakiki na kuthibitisha ubora ili kulinda viwanda vya ndani.

**122. *Mheshimiwa Spika***; Serikali itaendelea kufanya uchunguzi katika makubaliano yanayofifisha ushindani (Anti-Competitive Agreements). Katika eneo hilo, uchunguzi utafanyika katika sekta zote zitakazoonesha kuwa na makubaliano yanayofifisha ushindani ambazo ni pamoja na Sekta ya Michezo (mpira wa miguu) kuhusu haki za kutangaza mechi za mpira wa miguu (Sports Broadcasting Rights), Sekta ya Mawasiliano kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano nchini (TCRA), na Sekta ya Biashara na Kilimo kama Sekta Ndogo ya Tumbaku ambayo imeonesha kuwa na matumizi mabaya ya nguvu ya soko.

#### **4.2           VIPAUMBELE VYA MWAKA 2019/2020**

**123. *Mheshimiwa Spika***; Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2019/2020 ni:

- i) Kuendeleza miradi ya kimkakati;
- ii) Uendelezaji na urasimishaji wa viwanda na biashara ndogo na za kat;
- iii) Uongezajji thamani mazao ya kilimo na malighafi nyingine na kuunganisha na masoko;
- iv) Kutekeleza mfumo wa udhibiti wa ufanyaji biashara nchini (Blue Print);
- v) Kuimarisha utafiti na teknolojia kwenye sekta za viwanda na biashara;
- vi) Kuimarisha udhibiti na ushindani katika soko kwa ajili ya kuivilinda viwanda vya ndani na kukuza biashara;
- vii) Kuendeleza biashara;
- viii) Uendelezaji wa maeneo maalum ya kuendeleza viwanda;
- ix) Kuendeleza majadiliano ya biashara (SADC, EAC, AfCFTA); na

x) Ujenzi wa Ofisi ya Wizara katika Mji wa Serikali (Ihumwa – Dodoma).

## **5.0 MALENGO YA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA KWA MWAKA 2019/2020**

### **5.1 MALENGO YA WIZARA**

#### **5.1.1 SEKTA YA VIWANDA**

**124. *Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2019/2020, Sekta ya Viwanda itatekeleza malengo yafuatayo:

- (i) Kufanya tathmini ya hali halisi ya uzalishaji na mahitaji ya bidhaa viwandani katika viwanda vya sukari; korosho; mafuta ya kula; chuma; ngozi; nguo na mavazi; na dawa za binadamu.
- (ii) Kufuatilia na kusimamia Miradi ya Kimkakati kama vile Liganga na Mchuchuma n.k;
- (iii) Kuhamasisha uwekezaji wa Sekta Binafsi katika maeneo maalum ya EPZ/SEZ;
- (iv) Kufanya tathmini ya Utekelezaji wa Mikakati ya Pamba hadi Mavazi, Alizeti na Ngozi;
- (v) Kusimamia mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda (SIDP 1996-2020);
- (vi) Kuhamasisha uendelezaji wa Sekta Ndogo ya Mafuta ya Mawese;
- (vii) Kukamilisha maandalizi ya Sheria ya Biashara ya Chuma Chakavu na Kanuni zake; na
- (viii) Kueneza dhana ya KAIZEN nchini.

### **5.1.2 SEKTA YA VIWANDA VIDOGO NA BIASHARA NDOGO**

**125. Mheshimiwa Spika;** Katika Sekta ya Viwanda Vidogo, mwaka 2019/2020, Wizara itatekeleza malengo yafuatayo:-

- i) Kukamilisha mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ya mwaka 2003;
- ii) Kuendelea kuhamasisha Serikali za Mitaa kutenga na kuendeleza maeneo kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vidogo na biashara ndogo;
- iii) Kuendelea kusimamia na kuongeza mtaji wa Mfuko wa Wafanyabiashara Wananchi (National Entrepreneurship Development Fund - NEDF);
- iv) Kuendelea kuhamasisha ubunifu na matumizi ya teknolojia na viatamizi; na
- v) Kuendelea kuhamasisha Wajasiriamali kuchangamkia masoko ya ndani na nje ya nchi.

### **5.1.3 SEKTA YA BIASHARA**

**126. Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Sekta ya Biashara itatekeleza malengo yafuatayo:-

- i) Kuendeleza majadiliano ya kibiashara kati ya Nchi na Nchi (Bilateral), Kikanda (Regional) na Kimataifa (Multilateral) kwa ajili ya kupanua fursa za masoko na uwekezaji ili kuvutia uwekezaji nchini;
- ii) Kuendeleza majadiliano ya biashara kwenye nchi za China, Urusi, Mauritius, Uturuki, Misri, Israel, DRC Congo, Sudani ya Kusini, Vietnam na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na kuingia nazo makubaliano ya biashara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi;
- iii) Kuendelea na majadiliano ya kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara kwa Nchi za Afrika (Continental Free Trade Area – ACFTA);

- iv) Kukamilisha majadiliano ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Utatu linalojumuisha Kanda za COMESA, EAC na SADC;
- v) Kukamilisha majadiliano ya biashara ya huduma kwa sekta sita za kipaumbele katika nchi wanachama wa SADC;
- vi) Kutekeleza Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye masuala ya biashara ya bidhaa na huduma;
- vii) Kuratibu na kushiriki kwenye majadiliano ya biashara ya kimataifa katika mashirika yaliyo chini ya Umoja wa Mataifa na mengineyo ikiwemo WTO, UNCTAD, CFC na ITC;
- viii) Kuhamasisha Jumuiya ya Wafanyabiashara kuhusu fursa za masoko ya upendeleo yatokanayo na majadiliano ya Nchi na Nchi, Kikanda na Kimataifa;
- ix) Kukamilisha mapitio ya Sheria ya *Anti-dumping and Countervailing Measures*;
- x) Kutekeleza Mkataba wa Shirikala Biashara Duniani (WTO) unaohusu uwezeshaji wa Biashara;
- xi) Kuendelea na mapitio ya Sera ya Taifa ya Biashara 2003;
- xii) Kuimarisha kamati za kitaifa za kusimamia urahisishaji wa biashara nchini ambazo ni:
  - a. Kamati ya kusimamia Uondoaji wa Vikwazo vya Kibishara visivyokuu vya kiushuru (NTBs);
  - b. Kamati ya Urahisishaji Biashara (National Trade Facilitation Committee);
  - c. Kamati ya usimamizi wa masuala ya Afya za Binadamu, Wanyama na Mimea (National SPS Committee); na
  - d. Kamati ya Vikwazo vya Biashara vya Kiufundi (National TBT Committee); na

xiii) Kuandaa miradi na program mbalimbali kwa ajili ya kujenga uwezo kwa wataalam na Sekta Binafsi katika majadiliano ya kikanda na kimataifa.

#### **5.1.4 SEKTA YA MASOKO**

**127. Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Sekta ya Masoko itatekeleza malengo yafuatayo:

- i) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini;
- ii) Kuwaunganisha wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara na masoko ya ndani na nje ya nchi;
- iii) Kuendelea kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala;
- iv) Kutafiti na kutafuta masoko mapya nje ya nchi hususan katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), China, Mashariki ya Kati, Mashariki ya mbali, Ulaya, na nchi nyingine;
- v) Kuhamasisha matumizi ya vituo maalum vya kuuzia mazao;
- vi) Kuhamasisha na kurahisisha biashara mipakani;
- vii) Kuhamasisha na kuwezesha wananchi kutangaza bidhaa na huduma za Tanzania;
- viii) Kuimarisha Mfumo wa Ukusanyaji wa Taarifa za Masoko;
- ix) Kuandaa na kupitia Sera, Sheria na Kanuni za mbalimbali zikiwemo:
  - a) Kukamilisha Sera na Mkakati wa Miliki Bunifu;
  - b) Kukamilisha marekebisheso ya Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009 na Kanuni zake;
  - c) Kukamilisha Marekebisheso ya Sheria ya Haki Miliki na Haki Shiriki ya Mwaka 1999;

- d) Kukamilisha taratibu za kuridhia Itifaki ya *Marrakhesh*;
- e) Kuandaa Mkakati wa Kukuza Mauzo Nje;
- f) Kuandaa Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji (National Consumer Protection Policy); na
- g) Kuandaa Sera ya Ubora ya Taifa (National Quality Policy).

#### **5.1.5 RASILIMALI WATU**

**128. *Mheshimiwa Spika*:** Katika mwaka 2019/2020, Wizara kuititia Idara ya Utawala na Rasilimali watu itatekeleza yafuatayo:-

##### **a) Maendeleo ya Rasilimali Watu**

- i) Kuajiri watumishi 41 wa kada na ngazi mbalimbali kwa lengo la kuwezesha Idara na Vitengo kupata rasilimali watu wa kutosha na kutekeleza majukumu yao ipasavyo;
- ii) Kupandisha vyeo watumishi 147 wa kada mbalimbali;
- iii) Kupeleka watumishi mbalimbali katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi ya nyanja mbalimbali kwa lengo la kuwajengea uwezo, kuongeza ufanisi;
- iv) Kuandaa watumishi wanaotarajia kustaafu na kukidhi mahitaji ya kimundo;
- v) Kutekeleza Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi – Mwamtuka (OPRAS) kuititia yafuatayo:-
  - Kutoa mafunzo kwa watumishi wapya watakaoajiriwa namna ya ujazaji wa fomu za OPRAS;
  - Kuhakikisha kuwa Watumishi wote wanasaaini mikataba yao ya kazi kwa wakati;
  - Kufanya mapitio ya nusu mwaka; na

- Kufanya tathmini ya utendaji kazi wa Watumishi kwa mwaka mzima kwa wakati
- vi) Kuratibu na kusimamia masuala yote ya uendeshaji wa shughuli za Wizara;
- vii) Kutoa huduma stahiki kwa viongozi na watumishi wa Wizara kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo katika Utumishi wa Umma;
- viii) Kuandaa Programu mbalimbali za michezo kama vile mabonanza na kushiriki katika mashindano ya SHIMIWI kwa lengo la kujenga afya za watumishi, kuongeza ushirikiano na kufahamiana; na
- ix) Kuhakikisha watumishi watakaohitimisha ajira zao wanalipwa mafao kwa wakati.

***b) Masuala Mtambuka***

***(i) Rushwa***

Kuweka mikakati mbalimbali na kutoa mafunzo juu ya Sheria Kanuni na Taratibu kuhusu uzingatiaji wa maadili, uwajibikaji na utoaji huduma bora katika utumishi wa umma na kuhakikisha zinafuatwa na watumishi wote. Kuendelea kukusanya na kupokea malalamiko na kero kutoka kwa wateja wa ndani na nje ya ofisi kwa lengo la kuzitatu;

***(ii) Ukimwi na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza***

Wizara itaendelea na jitihada kuwashudumia watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na waliojiweka wazi. Kuendesha Semina kwa watumishi kuhamasisha na kuelimisha kuhusu wa masuala ya UKIMWI pamoja na upimaji afya wa hiarili kudhibiti UKIMWI na magonjwa sugu yasiyoambukizwa mahala pa kazi.

***(iii) Masuala ya Jinsia***

Kuratibu masuala ya kijinsia na kuyahuisha kwenye sera, mipango, mikakati na program za Wizara pamoja na Taasisi zake.

## **5.2 MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA**

### **5.2.1 TAASISI ZA KUENDELEZA UWEKEZAJI**

*a) Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kuzalisha Bidhaa za Kuza Nje (EPZA)*

**129.** *Mheshimiwa Spika;* Katika mwaka 2019/2020, Wizara kuititia Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uzalishaji wa Bidhaa kwa Mauzo Nje ya Nchi (EPZA) itatekeleza yafuatayo:

*a) Mini Tiger Plan 2020 – Bagamoyo SEZ na Benjamin Mkapa SEZ*

i) Kukamilisha majadiliano na Mwekezaji (CMPorts na SGRF) na kuandaa nyaraka za kisheria kwa ajili ya mradi wa Bagamoyo SEZ;

ii) Kuanza hatua za awali za kuendeleza eneo lilitolipiwa fidia: Kufanya upembuzi yakinifu (Feasibility Study), kuandaa mpango kabambe wa uendelezaji (Masterplan), Survey na kufanya usanifu wa miundombinu ya ndani (Design of onsite Infrastructure);

iii) Kuweka mipaka na kukamilisha taratibu zote za umilikishaji ardhi katika eneo la mradi wa Bagamoyo SEZ;

iv) Kuendeleza miundombinu ya ndani ya mradi awamu ya kwanza eneo lilitolipiwa fidia Bagamoyo SEZ;

v) Kusimamia maendelezo ya miundombinu ya Mradi wa *Bagamoyo Technological Park*;

vi) Kusimamia maendelezo ya Mradi wa Bagamoyo SEZ kwa kuziwezesha kamati maalum zinazosimamia mradi huo;

vii) Kutengeneza na kukarabati mifumo yote ya uhifadhi na upitishaji wa maji yaitayo katika eneo la uwekezaji la Benjamin Mkapa;

viii) Kutengeneza upya ukuta ulioanguka unaozunguka eneo lote la Benjamin Mkapa SEZ;

- ix) Kuweka kamera za ulinzi pamoja na mfumo wa kisasa wa ulinzi kuzunguka eneo lote Benjamin Mkapa SEZ; na
- x) Kushiriki katika huduma za kijamii (Corporate Social Responsibilities) kwenye maeneo yaliyozunguka miradi ya Bagamoyo SEZ na Benjamin Mkapa SEZ.

***b) EPZ Development: Kurasini Special Economic Zone***

- i) Kukamilisha malipo ya fidia kwa wakazi watatu (3) ambao nyumba zao hazikuthaminiwa awali baada ya kurukwa na Mthamini Mkuu wa Serikali wakati wa zoezi la Uthamini;
- ii) Kukamilisha taratibu zote za umilikishaji ardhi katika eneo la Mradi wa Bagamoyo SEZ; na
- iii) Kuanza hatua za awali za kuendeleza *Kurasini Special Economic Zone*- Kufanya upembuzi yakinifu (Feasibility Study), *Strategic Environmental Assessment (SEA)*, kuandaa Mpango Kabambe (Masterplan) wa Kuendeleza Eneo hilo, Survey na kufanya usanifu wa miundombinu ya ndani (Design of onsite Infrastructure).

***c) INSTITUTION SUPPORT: Kuendeleza Maeneo ya SEZ***

- i) Kuendelea kufanya tafiti na ufuatilaji wa kutathmini utendaji wa Mamlaka ya EPZ katika kufikia malengo yake (Research, Monitoring and Evaluation);
- ii) Kukamilisha ulipaji wa fidia kwa maeneo ya uwekezajiya Tanga, Ruvuma, Dodoma na Manyoni;
- iii) Kufanya *feasibility study* na *masterplan* kwa ajili ya maeneo ya uwekezaji ya Tanga, Kigamboni, Manyara, Ruvuma na Bunda;
- iv) Kufanya *cadastral survey* kwa ajili ya maeneo ya uwekezaji ya Manyara, Ruvuma na Bunda;
- v) Kusimamia masuala yote ya kisheria katika uendelezaji wa maeneo ya SEZ;

- vi) Kusimamia maendelezo ya miradi ya SEZ; na
- vii) Kukamilisha taratibu za umilikishwaji wa maeneo ya SEZ.

**b) Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC)**

**130. *Mheshimiwa Spika***; Katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

- i) Kuhimiza utekelezaji wa Mradi-Unganishi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma cha Liganga;
- ii) Kuanzisha miradi mipya ya kuzalisha makaa ya mawe ili kutosheleza soko la ndani na nje ya nchi;
- iii) Kuendeleza mradi wa kuzalisha Magadi soda wa Engaruka;
- iv) Kuendeleza mradi wa ufufuaji wa Kiwanda cha Matairi Arusha;
- v) Kuendeleza mradi wa kujenga miundombinu katika eneo la viwanda la TAMCO Kibaha;
- vi) Kukamilisha ujenzi wa Kiwanda cha Kuunganisha Matrekt ya URSUS na kuanza uunganishaji wa matrektakatika kiwanda kipyta;
- vii) Kuendeleza viwanda vya kuongeza thamani za mazao; na
- viii) Kuendeleza maeneo ya viwanda ya Kange na KMTC yaliyopo mkoani Tanga na Kilimanjaro mtawalia.

**c) Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO)**

**131. *Mheshimiwa Spika***; Katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

- i) Kuendeleza Mitaa ya Viwanda ya SIDO katika mikoa ya Iringa, Kagera, Katavi, Shinyanga, Kigoma, Lindi, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Pwani, Ruvuma, Tabora, Njombe, Dodoma na Kilimanjaro;
- ii) Kutengeneza Mfumo Unganishi wa Shughuli za TEHAMA za Shirika;
- iii) Kuimarisha Vituo vya Uendelezaji Teknolojia (TDCs) vilivyopo Kigoma, Iringa, Lindi na Kilimanjaro sambamba na kuboresha vituo vya mafunzo;
- iv) Kuwezesha bidhaa za viwanda vidogo na vya kati kuyafikia masoko ya ndani na nje;
- v) Kubuni teknolojia zitakazoweza kusaidia uanzishwaji wa viwanda nchini, chini ya Mkakati wa Bidhaa Moja Wilaya Moja (ODOP); na
- vi) Kuimarisha uendeshaji wa Mfuko wa NEDF ili uweze kuwafikia wananchi wengi zaidi.

#### ***5.2.2 TAASISI ZA UTAFITI, MAENDELEO YA TEKNOLOJIA NA MAFUNZO***

##### **a) Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO)**

**132. *Mheshimiwa Spika***; Katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO) itatekeleza yafuatayo:

- i) Kuendelea kutoa huduma za kitaalam viwandani zenyelengo la kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora bila kuchafua mazingira pia zinazolenga matumizi bora ya nishati;
- ii) Kuanzisha na kuhakiki maabara ya makaa ya mawe, mafuta na gesi zitakazokuwa na viwango vya kimataifa na kuweza kutoa huduma bora kwa wazalishaji viwandani pamoja na kuwa msaada kwa miradi ya Mchuchuma na Liganga;

- iii) Kuendelea na mchakato wa kufanya utafiti na kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali wa Sekta ya Ngozi jinsi ya kupunguza uharibifu wa mazingira kwa kuhifadhi na kurejesha taka za ngozi ili kutengeneza bidhaa kama *Leather boards*;
- iv) Kuendelea na kukamilisha mchakato wa kuhakiki (Accreditation) na kuboresha maabara ya chakula na mazingira ili ziweze kufikia viwango vya kimataifa na kuweza kutoa huduma bora kwa wazalishaji viwandani;
- v) Kuanzisha na kuhakiki (Accreditation) maabara ya vipimo vya chuma kigumu (Iron and Steel metallurgy laboratory);
- vi) Kuendelea kutekeleza miradi mbalimbali yenyе lengo la kuleta teknolojia mpya za uzalishaji;
- vii) Kuendelea kukamilisha mchakato wa kurejea Sheria ya Bunge Na. 5 ya mwaka 1979 ilioanzisha TIRDO;na
- viii) Kukamilisha Jengo la Utawala (Complete and furnish TIRDO administration block for Industrial Clinic, ICT and Information Centre).

**b) Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo (TEMDO)**

**133. *Mheshimiwa Spika***; Katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO) itatekeleza yafuatayo:

- i) Kuendelea na uboreshaji wa karakana na ofisi ya usanifu pamoja na miundombinu ya Taasisi kwa ujumla;
- ii) Kujenga uwezo wa wafanyakazi wa Taasisi kwa kuwapatia mafunzo na kufanya mapitio ya sheria ilioanzisha TEMDO na kutengeneza kanuni zake;
- iii) Kubuni na kuendeleza chasili cha mtambo wa kukausha mazao ya kilimo ili kuongeza thamani;

- iv) Kubuni na kuendeleza utengenezaji wa mtambo wa kuweka baridi (cold room) ili kuhifadhi bidhaa mbalimbali kama vile mboga mboga, matunda, mazao ya mifugo, bidhaa za hotelini, machinjio n.k;
- v) Kuendeleza chasili cha mtambo mdogo wa kutengeneza brikwiti kutokana na vumbi la makaa ya mawe;
- vi) Kuhawilisha teknolojia na kuhamasisha utengenezaji kibiasara wa mitambo iliyobuniwa na Taasisi ukiwemo mtambo wa kusindika mafuta ya kula yatokanayo na mbegu za alizeti;
- vii) Kujitangaza ili kujenga uelewa kwa umma kuhusu shughuli zinazofanywa na Taasisi ya TEMDO kwa kushiriki kwenye maonesho angalau manne ya teknolojia/biashara (kama vile DITF, Nane nane, Maonesho ya kanda ya SIDO, n.k) na kuwasaidia wajasiriamali wa kiatamizi cha teknolojia; na
- viii) Kuanzisha na kuwezesha mpango wa kusambaza viwanda nchini kwa utaratibu wa kiwanda kimoja kila wilaya (One District One Factory - ODOF) angalau kwa wilaya ishirini.

**c) Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC)**  
**134. Mheshimiwa Spika:** Katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC) itatekeleza yafuatayo:

- i) Kuendelea kufanya utafiti wa mahitaji ya teknolojia zinazohitajika vijijini (Technology Need Assessment) pamoja na kubuni/kutengeneza mashine za kilimo kulingana na mahitaji hayo;
- ii) Kuhamasisha na kutengeneza mashine za kilimo na teknolojia nyingine zinazohitajika vijijini kufanyika nchini Tanzania;
- iii) Kuendelea na Majaribio na Ukaruzi wa zana za kilimo na teknolojia za vijijini ili kuhakiki ubora wa zana hizo kwa manufaa ya wadau;

- iv) Kujenga uwezo wa Rasilimali Watu kwenye Kada ya Utafiti na Wafanyakazi wengine wasio watafiti;
- v) Kuendelea kusimamia masuala yanayohusu mazingira kwa kuhamasisha teknolojia zinazobuniwa na CAMARTEC; na
- vi) Kuimarisha miundombinu ya utafiti ya Kituo kwa kununua vifaa vya ili kuweza kufanya utafiti kwa ufanisi zaidi.

#### **5.2.3 TAASISI ZA USHINDANI NA UDHIBITI WA UBORA WA BIDHAA NA HUDUMA**

##### **a) Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA)**

**135. Mheshimiwa Spika:** Katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA) itatekeleza yafuatayo:

- i) Kuongeza makusanyo ya mirabaha kutoka kwa watumiaji wa kazi za sanaa ya muziki na kugawa kwa wasanii;
- ii) Kutoa elimu kwa wananchi na wadau wa sanaa kuhusiana na mambo ya Hakimiliki na Hakishiriki;
- iii) Kufanya ukaguzi wa kazi zinazolindwa na Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki (anti piracy raids);
- iv) Kushughulikia migogoro na kesi za Hakimiliki na Hakishiriki; na
- v) Kuandaa mfumo wa kieletroniki ili kurahisisha zoezi la usajili wanachama (wasanii) na kazi zao.

##### **b) Bodi ya Leseni za Maghala (WRRB)**

**136. Mheshimiwa Spika:** Katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

- i) Kuainisha na kufanya ukaguzi kwa ghala zitakazosajiliwa na kupewa leseni chini ya Mfumo wa Stakabdh za Ghala;

- ii) Kushirikiana na taasisi za fedha kuwawezesha wakulima wa vijijini kupata huduma za kifedha kwa urahisi;
- iii) Kuandaa au kuboresha miongozo ya mazao yatakayotumia Mfumo wa Stakabadhi kwa kushirikiana na taasisi zenyenye mamlaka;
- iv) Kutoa elimu ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa wadau mbalimbali ili waweze kuutumia kwa manufaa ya Taifa;
- v) Kupanua Mfumo wa Stakabadhi katika mazao ya nafaka, Mbegu za mafuta na mazao mengine; na
- vi) Kushiriki katika Maonesho ya Sabasaba na Nanenane kwa lengo la kupeleka elimu ya Mfumo wa Stakabadhi kwa wadau na kupata uzoefu kutoka kwa Taasisi zingine.

**c) Baraza la Ushindani (FCT)**

**137. *Mheshimiwa Spika***; Katika mwaka 2019/2020, Wizara kuititia Baraza la Ushindani (FCT) itatekeleza yafuatayo:

- i) Kusikiliza na kutoa maamuzi ya kesi za rufaa zinazotokana na mchakato wa udhibiti na ushindani wa kibashara nchini;
- ii) Kuendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi wa Baraza na wajumbe wa Baraza kwa lengo la kuwaongezaa uwezo; na
- iii) Kuendelea kutoa elimu kwa umma juu ya kazi za Baraza, umuhimu katika uchumi pamoja na namna ya kuwasilisha rufaa katika Baraza.

**d) Tume ya Ushindani (FCC)**

**138. *Mheshimiwa Spika***; Katika mwaka 2019/2020, Wizara kuititia Tume ya Ushindani (FCC) itatekeleza yafuatayo:

- i) Kukamilisha uchunguzi na kufanya maamuzi kwenye mashauri na kufanya utetezi wa maamuzi yake yatakayoflikishwa katika Baraza la Ushindani, Mahakama Kuu ya Tanzania na Mahakama ya Rufani kwa mwaka 2019/2020;
- ii) Kufanya tafiti tatu (3) katika sekta mbalimbali zenyenye lengo la kubaini mienendo inayokinzana na Sheria ya Ushindani;
- iii) Kutoa elimu na ushawishi juu ya uelewa wa Sheria ya Ushindani katika soko kwa;
- iv) Kufanya uchunguzi wa malalamiko ya walaji juu ya vitendo hadaifu vya wafanyabiashara nchi nzima na kuyatatua;
- v) Kuelimisha umma juu ya haki na wajibu wa mlaji kupitia semina na vipindi vya vyombo vya habari kwa nchi nzima;
- vi) Kuongeza mapambano dhidi ya bidhaa bandia na pia kuhakikisha kiwango cha bidhaa hizo kinapungua katika soko;
- vii) Kuboresha vitendea kazi kwa kununua samani za ofisi na kompyuta na
- viii) kuimarisha mifumo ya kielektroniki ndani ya Tume;
- ix) Kuongeza wafanyakazi mpaka kufikia 90 ukilinganisha na idadi ya sasa ya Wafanyakazi 60; na
- x) Kuimarisha ofisi ya Kanda ya Kati Dodoma na kufungua ofisi ya kanda katika mkoa wa Tanga.

**e) Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)**

**139. *Mheshimiwa Spika***; Katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) itatekeleza yafuatayo:

- i) Kuendelea kuboresha mifumo ya utoaji huduma kwa kutumia njia za mtandao ORS (Online Registrations System)

na NBP (National Business Portal) ili kutoa huduma bora popote mhitaji huduma alipo na kwa wakati;

ii) Kuendelea kusogeza huduma karibu na wananchi kwa kushirikiana na Ofisi za Maafisa Biashara wote katika ngazi za Mikoa na Wilaya;

iii) Kukamilisha kutoa mapendelezo ya mapitio ya sheria zote zinazosimamiwa na Wakala;

iv) Kuendelea kutoa elimu na uhamasishaji wa usajili na urasimishaji wa biashara kwa wananchi katika ngazi za mikoani na wilayani kwa kushirikiana na Maafisa Biashara kote nchini; na

v) Kuendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi pamoja na mafunzo kwa watumishi kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi kwa wateja.

**f) Wakala wa Vipimo (WMA)**

**140. *Mheshimiwa Spika***; Katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo (WMA) itatekeleza yafuatayo:

i) Kusimamia, kuhakiki na kukagua vipimo vyote vitumikavyo na viingiavyo nchini kwa lengo la kumlinda mlaji;

ii) Kuendelea na ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa kwenye maeneo ya Mipakani, Bandarini, na Viwandani kwa lengo la kuhakiki usahihi wa kiasi/ Idadi iliyotamkwa (decrealed quantity);

iii) Kununua vitendea kazi yakiwemo magari Matano na Vitendea kazi vytaalam;

iv) Kuongeza idadi ya watumishi 153 (Maafisa Vipimo 100, Madereva 50 na Wachumi 3);

v) Kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya vipimo; na

vi) Kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Wakala wa Vipimo Mkoani Dodoma na kujenga Ofisi za Mikoa ya Simiyu na Katavi.

**g) Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji (NCAC)**

**141. *Mheshimiwa Spika***; Katika kipindi cha mwaka 2019/2020, Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji litatekeleza yafuatayo:

- i) Kuendelea na mchakato wa kufanya marekebisho ya Sheria ya Ushindani ili iweze kuruhusu ajira ya Afisa Mtekelezaji Mkuu wa Baraza la Taifa la Mtetezi wa Mlaji;
- ii) Kukamilisha hadidu za rejea (ToR) za Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji; na
- iii) Kuandaa na kukamilisha Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji.

**h) Shirika la Viwango la Taifa (TBS)**

**142. *Mheshimiwa Spika***; Katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) itatekeleza yafuatayo:

- i) Kutayarisha viwango 450 vya kitaifa katika sekta ndogo ndogo, ambavyo kati ya hivyo 210 ni vya uhandisi (Engineering) na 240 ni vya usindikaji (Process Technology);
- ii) Kutoa leseni ya ubora kwa bidhaa 320 kutoka katika sekta mbalimbali zikiwemo bidhaa za wajasiriamali wadogo (SMEs);
- iii) Kukagua ubora wa bidhaa 38,000 zitokazo nchi za nje kabla ya kuingia nchini (Pre-Shipment Verification of Conformity to Standards- PVoC (CoCs);
- iv) Kufanya ukaguzi wa ubora na kutoa leseni za ukaguzi 41,000 za magari yaliyotumika (used motor vehicles) yanayoingizwa nchini;

- v) Kutoa mafunzo na semina 34 kuhusu viwango na udhibiti wa ubora (Quality Assurance Training) kwa wadau mbalimbali;
- vi) Kupima sampuli 23,000 za bidhaa mbalimbali;
- vii) Kufanya ugezi kwa vifaa/mashine mbalimbali vipatavyo 7,500, na
- viii) Kuanza ujenzi wa Viwango House Dodoma.

**i) Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)**

**143. Mheshimiwa Spika:** Katika mwaka 2019/2020, Wizara kuititia Chuo Cha Elimu ya Biashara (CBE) itatekeleza yafuatayo:

- i) Ujezi wa Kampasi ya Mbeya;
- ii) Kuboresha mifumo ya Tehama ili kuongeza ufanisi wa kazi;
- iii) Kuendeleza rasilimali watu (*Human Resources Development*);
- iv) Kuvutia wawekezaji kutoka sekta binafsi ili kuwekeza katika ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya kitaaluma na kibiasara;
- v) Kuimarishe Maktaba ya Chuo pamoja na Mifumo yake ya TEHAMA;
- vi) Kuimarishe Mikakati ya kimasoko; na
- vii) Kuboresha na kuimarishe shughuli za ujasiriamali ikiwa ni pamoja na kuboresha huduma za ushauri wa kitaalamu.

**j) Mamlaka ya Biashara Tanzania (TANTRADE)**

**144. Mheshimiwa Spika:** Katika mwaka 2019/2020, Wizara kuititia Mamlaka ya Biashara Tanzania (TANTRADE) itatekeleza yafuatayo:

- i) Kufanya utafiti wa masoko ya nje ambapo bidhaa za Tanzania zina fursa;
- ii) Kuimarisha utoaji wa Taarifa za Biashara na Intelijensia ya Biashara;
- iii) Kutangaza Bidhaa na Huduma Zinazosalishwa Nchini katika Masoko Nje na kuongeza ushiriki wa Tanzania katika biashara ya nje;
- iv) Kuimarisha Sekta Ndogo ya Biashara (SMEs) ili kuongeza Ushindani;
- v) Kuanzisha Vituo vya Biashara (Market Centers) ili kutangamanisha biashara ya ndani;
- vi) Kuratibu na kudhibiti uendeshaji wa maonesho ya kimataifa nchini;
- vii) Kuendeleza Miundombinu ya Biashara na Maonesho;
- viii) Kuimarisha na kuendeleza Biashara Zanzibar; na
- ix) Kuimarisha na kuongeza uwezo wa TanTrade kutekeleza Majukumu yake.

## **6.0           MAKADIRIO YA MAPATO NA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2019/2020**

### **6.1 Mapato ya Serikali**

**145. *Mheshimiwa Spika***; Katika mwaka 2019/2020, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 14,300,000** kutokana na uuzaaji wa nyaraka za zabuni na makusanyo mengine. Kati ya hizo, Shilingi **5,300,000** zitakusanya katika Fungu 44 na **Shilingi 9,000,000** zitakusanya katika Fungu 60.

### **6.2 Maombi ya Fedha**

**146. *Mheshimiwa Spika***; Kwa mwaka 2019/2020, Wizara ya Viwanda na Biashara inaombakutengewa jumla ya **Shilingi**

**100,384,738,648.** Kati ya hizo, **Shilingi 48,884,738,648** ni za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 51,500,000,000** ni za Matumizi ya Maendeleo. Aidha, katika Bajeti hiyo, **Shilingi 79,149,452,000** ni za Fungu 44 na **Shilingi 21,235,286,648** ni za Fungu 60.

## 7.0 SHUKRANI

**147. Mheshimiwa Spika;** Azma ya ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini ni maamuzi makini ya Serikali ya Awamu ya Tano ambayo yamejengwa katika misingi na busara za kuleta mageuzi makubwa ya maendeleo ya watu. Lengo ni kuwa na Tanzania inayoshamiri na yenye watu wenye afya na furaha tele na nchi yao. Jukumu hilo ni zito lakini manufaa yake ndiyo yanayozidi kutusukuma kuthubutu bila kuchoka kusimamia azma hiyo. Ni dhahiri kuwa matokeo hayo yanahitaji jitihada shirikishi na endelevu za kila mdau na hasa kila Mtanzania mzalendo. Kutokana na jitihada hizo, mchango wa sekta hiyo hauna budi kuendelea kuwa kichocheo kwa sekta nydingine kuchagiza matokeo chanya katika uchumi wetu. Hivyo, hatuna budi kuwashukuru wadau wote kwa kutuunga mkono katika kuendeleza juhudhi hizo. Kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru washirika wetu wa maendeleo, zikiwemo nchi rafiki ambazo ni Austria, Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Sweden, Uholanzi, Uingereza, Ujeruman na Usvisi. Aidha, tunayashukuru Mashirika ya Kimataifa ikiwa ni pamoja na: ARIPO, Benki ya Dunia, CFC, DANIDA, DFID, EU, FAO, IFAD, JICA, Jumuiya ya Madola, KOICA, SIDA, Taasisi za Umoja wa Mataifa (UNCTAD, UNDP, UNIDO, UNWOMEN), USAID, WIPO, TMEA, SADC na WTO. Vilevile, nashukuru taasisi zote, Sekta binafsi, taasisi zisizo za kiserikali (CBOs & FBOs) kwa kuwa sehemu muhimu ya injini ya ujenzi wa uchumi wetu. Matumaini yangu kuwa ushirikiano wa wadau hao pamoja na wadau wa ndani utaendeleza ari ya ushirikiano na hivyo kuchochea kwa mwendelezo katika maendeleo ya nchi na Taifa letu kwa ujumla.

**148. Mheshimiwa Spika;** Naomba nihitimishe kwa kuwashukuru tena Watanzania wote na wapenda nchi yetu

kwa jitihada na ushirikiano tunaopata katika kutekeleza azma ya ujenzi wa uchumi wa viwanda. Ni matumaini yangu kuwa jitihada hizo zitatutoa hapa tulipo na kutufikisha katika kilele cha mafanikio. Niwaombe wananchi wote kuendeleza jitihada hizo kwani matokeo yake yana manufaa makubwa kwetu na hasa kwa vizazi vijavyo.

## 8.0 MWISHO

**149. *Mheshimiwa Spika***; Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara yenyeye anuani ifuatayo: [www.mit.go.tz](http://www.mit.go.tz).

## 9.0 MAOMBI RASMI YA FEDHA

**150. *Mheshimiwa Spika***; Naomba Bunge lako liidhinishe makadirio ya Wizara ya Viwanda na Biashara ya kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 14,300,000** na matumizi ya jumla ya **Shilingi 100,384,738,648** kwa mwaka 2019/2020.

**151. *Mheshimiwa Spika***; Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Hoja imeungwa mkono.

Sasa nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira ili aweze kuwasilisha hoja yake, Mheshimiwa Kanali Masoud, karibu.

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa wa Kamati ya Kudumu Viwanda, Biashara na Mazingira naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara; Fungu 44 - Viwanda na Fungu 60 - Biashara kwa mwaka fedha 2018/2019 na Maoni ya Kamati kuhusu

Makaridio ya Mapato na Matumizi kwa Fungu 44 na Fungu 60 kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyenzi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujalia uhai kuweza kufikia siku ya leo ambayo tumkutana kwa ajili ya kujadili bajeti ya Wizara Viwanda na Biashara. Kwa kuzingatia umuhimu wa yaliyomo kwenye taarifa hii pamoja na kutoa maoni, naomba taarifa yote kama ilivyosemeka katika kitabu cha Kamati iingie katika kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Kanuni ya 99(9) na 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda Fungu 44 na Fungu 60 kwa Mwaka 2018/2019 na maoni ya kamati kuhusu Makadirio na Matumizi, Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa kwa Fungu 44 - Viwanda na Fungu 60 - Biashara kwa mwaka fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inaelekeza Kamati za Kisikta kufanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa lengo la kubaini ufanisi wa miradi hiyo. Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilitekeleza jukumu hilo ambapo ilitembelea miradi ya maendeleo iliyotekeliza chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara na kujionea hali halisi ya utekelezaji na wa miradi hiyo na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa taarifa utekelezaji wa bajeti ya Serikali ya mwaka 2018/2019 na Makadirio na Mapato na Matumizi 2019/2020 kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ikisomwa pamoja na kifungu cha 6(1) na 7(1)(a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha taarifa hii kwa lengo la kuelezea namna Kamati yangu ilivyotekeliza

majukumu yake kwa kuzingatia masharti ya kanuni 98(1) na (2). Sambamba na hilo, nalenga kuliomba Bunge lako Tukufu kuidhinisha maombi ya fedha kwa ajili ya Wizara ya Viwanda na Biashara Fungu 44 na Fungu 60 kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, taarifa hii itaainisha mapendekezo kuhusu masuala kadhaa ambayo Kamati inaamini ni muhimu yakifanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji Wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2018/2019. Mnamo mwezi wa Mei, 2018 Bunge lako tukufu liliidhinisha bajeti kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka fedha 2018/2019 kutokana na kuidhinisha kwa fedha hizo, Kamati ilitaka kujiridhisha kama dhamira ya Bunge lako la kuidhinisha bajeti hii limetimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya uchambuzi wa taarifa mbalimbali zilizowasilishwa na Wizara mbele ya Kamati na kufanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Lengo kuu la kutumia njia hiyo ilikuwa ni kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa malengo ya Wizara, ukusanyaji wa mapato na upatikanaji wa fedha ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya maduhuli; katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ya Viwanda na Biashara ilipanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 20,006,300,000. Shilingi bilioni 5.3 kwa Fungu 44 na shilingi bilioni 20,001,000,000 kwa Fungu 60. Kutokana na ada ya leseni, nyaraka na zabuni na faini ya kukiuka Sheria za Leseni za Biashara. Hadi kufikia Februari 2019, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi bilioni 8.99, kiasi hiki ni sawa na asilimia 44.94 ya lengo la makusanyo kwa mwaka wa Fedha 2018/2019. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, kiasi cha fedha kilichokusanywa ni pungufu kwa asilimia 55.06 ya makadirio yaliyowekwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Aidha, kutokana na muda mchache uliobaki ambao ni robo mwaka ya mwisho wa mwaka wa fedha unaoishia, matumaini na kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 11.02 ni hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaisisitiza Serikali kuwa ipange malengo ya makusanyo yanayoendana na uwezo wake halisi wa kukusanya na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Viwanda na Biashara ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 143.3 kwa ajili ya mafungu mawili yaani Fungu 40 na Fungu 60. Fedha hizo zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zote za Wizara hiyo. Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia Machi, 2019 ambayo ni robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 34.8 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na taasisi zote zilizoko chini ya Mafungu yote mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi hiki ni sawa na asilimia 24.28 tu ya fedha zote zilizotengwa katika bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kati ya fedha zilizopokelewa shilingi bilioni 28.32 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida kiasi hicho ni sawa na asilimia 65.4 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Mafungu yote mawili ya Fungu 44 na Fungu 60 na shilingi bilioni 6.47 tu ndio zilizopokelewa. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 6.48 tu ya fedha zilizoidhinishwa kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uchambuzi wa kina wa taarifa za utekelezaji wa majukumu ya bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Kamati ilibaini mambo mbalimbali kama inavyoonekana katika taarifa ya Kamati. Mtazamo wa Kamati kuhusu jambo hili ni kwamba mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha kwa Wizara ya Viwanda si wa kuridhisha, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha fedha zinazoidhinishwa na Bunge zinapelekwa tena kwa wakati ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kwa mujibu wa kanuni

ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilifanya ziara kutembelea baadhi ya miradi ya maendeleo kwa lengo lakujionea hali halisi na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wake. Kamati ilitembelea mradi namba 62.60, mradi huu unahusisha kuziwezesha taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara kutekeleza majukumu yake. Chini ya mradi huu, Kamati ilitembelea na kukagua:-

- (a) Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijiini (*CARMATEC*);
- (b) Shirika la Uhandisi Wanaosanifu Mitambo Tanzania (*TEMDO*); na
- (c) Mradi wa kuboresha miundombinu ya Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya mradi hiyo ni kama inavyoonekana katika taarifa ya kamati na kutokana na ufinyu wa muda naomba nisii some.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilipata fursa ya kutembelea na kukagua shughuli za Kiwanda cha *Tanzania Breweries* na Kiwanda cha Serengeti *Breweries* kwa lengo la kujionea namna vinavyoendesha shughuli zao pamoja na kubaini mafanikio na changamoto wanazokabiliana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda viliviyotembelewa vinajihuisha na utengenezaji na usambazaji wa vinywaji vikali kama vile bia na pombe kali. Viwanda hivi viliripoti juu ya changamoto kuu tatu wanazokabiliana nazo katika uendeshaji wa shughuli zao moja, tozo ya kodi ya kielektroniki; pili, changamoto ya kupata ardhi; na tatu, gharama kubwa za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati; wakati wa kupitia na kuchambua taarifa za utekelezaji wa iliyokuwa Wizara ya Viwanda na Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Kamati ilitoa

ushauri kwenye maeneo kumi na saba. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati. Hata hivyo kuna maeneo matatu ambayo Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wake na inaendelea kuisisitiza Serikali kuongeza juhudzi za utekelezaji wa maagizo hayo. Maeneo hayo ni kama yalivyooonekana katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mpango na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020; wakati wa kuchambua makadirio na mapato ya matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara, Kamati ilipitia maelezo ya Waziri kuhusu malengo waliyojipangia kuyatekeleza mwaka wa fedha 2019/2020. Lengo lilikuwa ni kufuatilia tija inayoweza kupatikana kutokana na malengo yaliyopangwa kutekelezwa kwa fedha zilizoombwa katika Fungu 44 na Fungu 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya Wizara ya Viwanda na Biashara mwaka 2019/2020, yamejitosheleza na utekelezaji wake unatarajia kuboresha hali ya biashara nchini na kukuza uchumi wa nchi. Ili malengo haya yatekelezwe kikamilifu Serikali inapaswa kuhakikisha fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara zinapelekwa Wizarani tena kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa makadirio na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020; katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara imetengewa jumla ya shilingi bilioni 100.38 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shughuli za maendeleo kwa mafungu yote mawili. Kati ya fedha hizo zinazoombwa shilingi bilioni 48.88 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 51.5 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa kina juu ya fedha hizi kama inavyoonekana katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati kuhusiana na mpango wa bajeti umebaini mambo yafuatayo:-

Moja, kiasi hicho cha bajeti kilichotengwa kwa ajili ya Mafungu mawili ni pungufu kwa asilimia 29.9 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ya mwaka wa Fedha unaoishia yaani 2018/2019.

Pili, upungufu wa bajeti wa Wizara ya Viwanda na Biashara unaathari kubwa kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo ambayo imepungua kwa asilimia 48.51 ukilinganishwa na Bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019. Kushuka kwa bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kunaashiria kukwama kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/20. Aidha, hali hii inaleta mashaka katika utekelezaji wa kipaumbele cha Taifa cha kuwa na uchumi wa kati kupitia viwanda ifikapo 2020/2025. Kwa kuwa miradi hii ni miradi ya kichocheo kwa sekta hii ya viwanda, Kamati inashauri Serikali kuongeza bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara ili kuongeza ufanisi katika miradi husika kwa lengo la kupata matokeo yenyе tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati; baada ya kufanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo na kuchambua utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2018/2019, pamoja na kuchambua mapendekezo na mapato kwa mwaka wa fedha 2019/2020 wa Wizara hii, Kamati imekuwa na maoni na ushauri kadhaa kwa Serikali.

Ni matumaini ya Kamati kuwa maoni na ushauri huu utafanyiwa kazi kwa lengo la kuboresha shughuli za sekta ya viwanda nchini. Mradi wa Liganga ni mionganini mwa miradi ya kimkakati ulioanzishwa kwa lengo la kujenga kiwanda cha kufua chuma. Utekelezaji wa mradi huu umechukua muda mrefu takriban miaka nane bado haujaanza. Kamati ilijulishwa na Wizara juu ya tathmini waliyofanya katika bidhaa ya chuma na kubaini kuwa vinakumbana na changamoto ya upatikanji wa malighafi.

KWA KUWA Liganga inakadiriwa kuwa na chuma kingi ambacho kinakadiriwa kuchimbwa kwa zaidi ya miaka 100 bila kuisha;

NA KWA KUWA Serikali bado ipo katika hatua za kutafakari namna ya kutekeleza mradi huo;

HIVYO BASI Kamati inashauri Serikali kutenga walau asilimia 25 za malighafi ya chuma ya Liganga na kuiiza kwenye viwanda vinavyozalisha bidhaa ya chuma. Hatua hii itawasaidia wazalishaji wa bidhaa za chuma kupata malighafi kwa urahisi. Pia itaisaidia Serikali kupata fedha ambazo zinaweza kutumika katika hatua za awali ikiwa ni pamoja na kulipa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Mchuchuma unahuishisha uzalishaji wa umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Mchuchuma. Changamoto ya mradi huu ni kuwa utaenda kuzalisha umeme ambao utakuwa wa gharama ya juu, umekadiriwa kuuzwa *unit* moja kwa senti 10 hadi 12 ya dola za Kimarekani wakati *regulations* za *EWURA* zinaeleza umeme wa makaa ya mawe usiuzwe zaidi ya senti nane dola za Kimarekani.

KWA KUWA Serikali yetu imeshajipanga kutekeleza miradi mikubwa ya uzalishaji umeme ambapo utakuwa na gharama nafuu;

NA KWA KUWA bidhaa ya makaa ya mawe imeonekana kuwa na soko la kutosha ambapo viwanda vingi hususan vya saruji vimeduwa vimehitaji kutokana na mahitaji yao yanakuwa makubwa yakiingizwa nchini kutoka nchi za mbalimbali;

HIVYO BASI, Kamati inashauri Serikali kuachana na mkakati uliopo wa kuzalisha umeme kwa mradi wa Mchuchuma badala yake makaa ya Mchuchuma yauzwe kwenye viwanda vinavyotumia aina hiyo ya nishati katika uzalishaji wake. Hatua hii itaisaidia kupunguza uingizaji wa makaa ya mawe kutoka nje na vilevile itapunguza gharama za uzalishaji na hatimaye watapunguza bei ya bidhaa. Kamati inashauri pia hatua hii iende sambamba na ujenzi wa miundombinu ya uhakika ambayo itasaidia kufikika kwa urahisi eneo la mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa mradi wa Bagamoyo. Mradi huu pamoja na mambo mengine ulilenga kuboresha Mji wa Bagamoyo na kufungua fursa ya kiuchumi ikiwepo wawekezaji wa viwanda ambavyo vitatoa ajira kwa kiasi kikubwa. Kamati inashauri Serikali kutafakari tena maamuzi yaliyofanyika ya kusitisha utekelezaji wa mradi huu kwa kuwa kuna baadhi ya hatua za utekelezaji zimekwishafanyika, ikiwepo kulipa fidia kwa baadhi ya wananchi walio takiwa kuhama kwenye eneo la mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vilivyobinafsishwa; uchumi mkubwa wa nchi umehodhiwa katika eneo la viwanda vilivyobinafsishwa ambapo mapato ya nchi pamoja na ajira vinaendelea kupotea. Kwa mara kadhaa Kamati imekuwa ikifuatilia utekelezaji wa jukumu hilo, lakini imekuwa ikikosa maelezo yanayo jitoshaleza. Kukosekana kwa maelezo ya kutosha kumepeleka Kamati kuamini kuwa bado hakuna mpango mkakati madhubuti wa Serikali katika kutekeleza jukumu la kufufua viwanda vilivyobinafsishwa. Kamati inashauri Serikali kuandaa mpango mkakati, Madhubuti na ikiwezekana iundwe tume maalum ambayo itasimamia kwa ukaribu na umakini eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Maendeleo wa Wajasiriamali; madhumuni ya kuanzishwa kwa Mfuko wa *NEDF* ni kuweza kuwasaidia wajasiriamali kupata mitaji itakayowawezesha kuanzisha na kukuza biashara. Chanzo kikuu cha mapato ya Mfuko huu ni ruzuku kutoka Serikalini na riba zitokanazo na mikopo inayotolewa na Mfuko, lakini kwa miaka saba mfululizo, Serikali imekuwa haipeleki kiasi kinachoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Mfuko huu. Jambo hilo linapelekeea mtaji wa Mfuko huo kkuwa kwa kiasi kidogo sana hali ambayo inapelekeea kuendelea ku wahudumia wahitaji wachache.

Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kiasi kinachotengwa kwa ajili ya Mfuko huo kinapelekwa tena kwa wakati ili kuwezesha Mfuko huo kuongeza mtaji wake na kuongeza idadi ya wanufaika kwa huduma ya Mfuko huo. Kamati inashauri Serikali kuangalia namna ya kuupatia Mfuko

huo mtaji wa kutosha ili kuweza kuuondoa katika utegemezi wa ruzuku ya kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo wa Uratibu wa Kodi za Kieletroniki. Kamati ilikutana na malalamiko ya wawekezaji wengi wenye viwanda juu ya gharama inayoambatana na mfumo wa kodi wa kieletroniki. Gharama hizo ni kubwa na zinaenda kuongeza gharama za uzalishaji. Kwa mfano juisi inayotengenezwa na Bahresa inalipa kodi ya *TRA* shilingi tatu, lakinitalipa gharama ya *ETS* ya shilingi tisa. Maelezo ambayo yanamaanisha kwamba tutatumia shilingi tisa kukusanya shilingi tatu jambo ambalo haliko sawa kabisa. Gharama hizi zitakuwa na madhara katika vipengele viwili ambavyo moja, itaongeza gharama za uzalishaji ambazo zitaenda kutolewa katika *running cost* hivyo kupunguza mapato ya *TRA*. Pili, itaongeza gharama za bidhaa ambazo itaenda kubewa na mlaji pia itapelekea kuzitoa bidhaa zetu katika ushindani wa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inakubaliana na nia nzuri ya Serikali ya kuanzisha mfumo wa *ETS* kwa kuwa mfumo utaleta uwazi na kuondoa wafanyabiashara wasio waaminifu wanaodanganya mahesabu ya kodi. Hata hivyo, Kamati inaendelea kushauri Serikali kukaa chini na viwanda vivilvyotumika kama mfano, kampuni iliyotumika kuandaa mfumo wa *ETS (SIPCA)* na kufanya mazungumzo juu ya changamoto zilizobainika kuambatana na mfumo kisha kuzitatua kabla haujaanza kutumika rasmi kwa wadau wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati imeshuhudia mashine za mfumo huu na kubaini kuwa teknolojia iliyotumika si kubwa wala si ngeni sana na inaweza kuzalishwa hapa nchini badala ya kutumia mshauri kutoka nje kama inavyofanyika hivi sasa. Kamati inashauri Serikali baada ya kufanya majadiliano na bei na *SIPCA* na ikitokea wameshindwa kukubaliana na kurekebisha changamoto zilizopo ikiwa ni pamoja na kupunguza bei ni vyema Serikali ikaamua kuwatumia wataalam wetu wa ndani, *TTCL*, kuandaa mfumo mwingine ambao utakuwa na bei nafuu na wa manufaa kwa pande zote yaani Serikali walaji na

wenye viwanda. Hatua hii ifanyike kabla ya mfumo huu kwenda kutumika katika viwanda vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wingi wa taasisi za udhibiti; Kamati pia ilipokea malalamiko juu ya uwepo wa wa mamlaka nyingi za udhibiti tena zinazofanya kazi kwa pamoja, jambo linalopeleka kuonekana ni kero kwa wafanyabiashara na wenye viwanda. Kwa kuwa Wizara ya Viwnada na Biashara ndio Wizara mama katika usimamizi wa Sekta ya Viwanda na Biashara na kwa kuwa mamlaka hizo pamoja na kuwa katika Wizara tofauti lakini bado zinasimamia Sekta ya Viwanda na Biashara. Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali kuzifanya taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuwa ndio waratibu wakuu wa Sekta ya Viwanda na Biashara na kuwa taarifa zote za sekta hiyo pindi inapotokea mamlaka taasisi zote zinazofanya kazi zinazoshabihiana na taasisi za udhibiti zilizopo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara ziombwe kwa Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano *TFDA* atumie taarifa za *TBS* kutoa kibali na Mkemia Mkuu atumie taarifa za *TBS* kujua aina ya ubora wa bidhaa inayoingia bandarini. Hatua hiyo itapunguza gharama kwa wafanyabiashara na wenye viwanda, pia itaondoa kero za kukaguliwa zaidi ya mara moja. Aidha, hatua hii iende sambamba na kuziboresha taasisi zilizopo nchini chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kuzipatia wafanyakazi wenye taaluma stahiki na kuboresha mishahara yao, kuwapatia vitendea kazi na kuwawezesha kupata mafunzo ya mara kwa mara kwa ajili ya kuhuisha utaalam wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifuutilia utekelezaji wa majukumu ya taasisi za tafiti zilizopo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara ikiwemo taasisi ya *TEMDO*, *CARMATEC* na *TIRDO* na kubaini kuwa majukumu ya taasisi hizi yanashabihiana. Kamati inashauri Serikali kuangalia namna ya kufanya marejeo ya sheria ya uundaji wa taasisi hizo na kuangalia namna ya kuziunganisha na kuziweka chini ya uongozi mmoja na zikiwa zinaendelea kutekeleza majukumu

ya asili yaliyopangwa. Hatua hii itasaidia kupunguza ghamama za uendeshaji na kuleta ufanisi kwani wanaweza kushirikiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa za ngozi; katika kufuatilia utekelezaji wa malengo ya kazi ya Wizara ya mwaka 2018/2019, Kamati iliarifiwa kuwa Wizara ya Viwanda na Biashara ilifanya tathmini ya sekta ya ngozi na bidhaa za ngozi nchini. Kwa kuwa tathmini hiyo imeainisha uwezo wa viwanda vya ndani na kubainisha mahitaji halisi ya viwanda hivyo na kiasi kinachosalia. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kutumia matokeo ya tathmini hii kufanya mazungumzo katika Jumuia ya Afrika Mashariki yatakayosaidia kuondoa kizuizi kilichowekwa juu ya uuzaji wa malighafi ya ngozi nje ya jumuia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ishawishi uwekwe utaratibu ambao viwanda vya ndani watapewa kipaumbele cha kupata malighafi kwanza na kisha kiasi kinachosalia waweze kuuza nje ya nchi. Tanzania ni nchi iliyobarikiwa na idadi kubwa ya mifugo Afrika na ngozi ni kati ya bidhaa zinazokuwa zikiongozwa kwa kuuzwa sana nje ya nchi na kuingiza fedha nydingi za kigeni. Hivyo ni vyema kuitumia fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya sera za maendeleo endelevu ya viwanda; sera hiyo iliandaliwa kipindi ambacho nchi haikuwa na mipango ya ujenzi wa viwanda iliyopo sasa, hivyo kuifanya isijitosheleze. Kamati inatambua kuwa Serikali ipo katika mapitio ya sera hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha sera inayokwenda kuandaliwa itoe nguvu kwa Wizara ya Viwanda na Biashara kusimamia masuala ya viwanda na yale masuala mtambuka yanayohusika moja kwa moja katika huduma za ujenzi wa viwanda. Sera hiyo iwe na kauli juu ya upatikanaji wa huduma zote ambazo zinahusika katika ujenzi wa viwanda, mfano, upatikanaji wa vibali vya uwekezaji, upatikanaji wa ardhi ya uwekezaji, upatikanaji wa vibali vya kufanya kazi nchini, upatikanaji wa huduma za maji, umeme na usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Sukari; sekta hii imegubikwa na malalamiko juu ya viwango vya sukari vinavyoingia nchini, ukillingamnisha na mahitaji halisi ya nchi. Kamati inaishauri Serikali kuweka umakini mkubwa wakati wa kutoa vibali vya kuingiza sukari nchini na kuwa vibali hivyo vitolewe baada ya Serikali kufanya tathmini na kubaini upungufu wa sukari uliopo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mafuta ya kula; mahitaji ya bidhaa ya mafuta ya kula nchini ni tani laki saba na uzalishaji wa bidhaa hiyo hapa nchini ni tani laki mbili na elfu kumi. Takwimu hizi zinadhahirisha kuwa ili kukidhi mahitaji ya soko ni lazima tofauti iliyopo iruhusiwe kuingizwa kutoka nje. Changamoto ni kwamba viwanda vya mafuta ya kula nchini vinavyoingiza mafuta kutoka nje ya nchi vimekumbana na changamoto ya mgongano wa maamuzi baina ya mamlaka za udhibiti juu ya vipimo vinavyobainisha hali ya mafuta yaliyoingizwa jambo linalopelekea ucheleweshaji wa kutoa mafuta haya bandarini na kuongeza gharama za *storage*. Kwa sasa bandarini kuna mzigo wa mafuta tani 1,500 ambaao umekaa kwa zaidi ya miezi saba na hali hiyo inatokana na mgongano wa maamuzi uliopo. Kamati inaishauri Serikali kusimamia kwa karibu mamlaka hizi kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa maslahi mapana ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya kufanya biashara nchini. Kuimarika kwa mazingira ya biashara nchini ni moja ya chachu ya kukua kwa sekta ya viwanda na biashara. Tumeendelea kushuhudia kushuka kwa nafasi za Tanzania katika orodha ya nchi zenye mazingira mazuri ya kufanya biashara, jambo ambalo kwa kiasi kikubwa limechangiwa na changamoto mbalimbali ambazo zimeendelea kulalamikiwa na wafanyabiashara nchini. Changamoto hizo ni pamoja na malimbikizo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*). (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Sheria za *VAT* yaani *VAT refund* ni kuwa fedha hizo zilipaswa kurudishwa ndani ya miezi mitatu, lakini kumekuwa na ucheleweshaji

ambao umepelekea malimbikizo makubwa. Kwa mwaka 2017/2018, madai yalikuwa ni shilingi bilioni 32 na kwa sasa yameongezeka kufikia bilioni 45 na hayajawahi kulipwa ndani ya miaka mitatu. Malimbikizo haya yanaathiri mitaji ya wafanyabiashara walio wengi. Kamati inatambua mchakato wa uhakiki uliokuwa unaendelea kufanyika lakini inashauri kukamilika kwa mchakato huo na kuanza kurudisha fedha hizo kwa wahusika ili waweze kujiendesha bila kuendelea kukopa katika mabenki na kuendelea kuomba *overdraft* ambazo zinaendelea kuwaongeza ghamama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kucheleta kurejeshwa kwa Ushuru wa Forodha wa asilimia 15. Mfumo huu wa Ushuru wa Forodha ulianzishwa kwa lengo la kuwasimamia waingizaji wa sukari wa viwandani, kuhakikisha wanaingiza nchini sukari kwa kuzingatia mahitaji halisi ya kiwanda. Namna uliviyopangwa kuendesha ni kwa kutoa asilimia 15 ya *import duty* na fedha hizi zitarudishwa mara itakapowasilishwa taarifa ya matumizi ya sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua nia njema ya Serikali ya kuanzisha mfumo huu lakini utekelezaji wake umekuwa na changamoto ambapo kwa mfululizo wa miaka minne tangu umeanzishwa Serikali imeshindwa kurejesha fedha hizi kwa wahusika, jambo lililopelekea kiasi cha mitaji ya wazalishaji kushikiliwa na Serikali na kuwapunguzia mitaji yao. Kwa kuwa Serikali inajipanga kuanzisha Mfumo wa Kodi wa Elektroniki (*EIS*) na kwa kuwa utekelezaji wa mfumo wa u Ushuru wa Forodha asilimia 15 umeonekana kufeli, hivyo basi Kamati inashauri Serikali kuachana na mfumo wa Ushuru wa Forodha wa asilimia 15 kwa kutumia Mfumo wa Kodi za Kielektroniki ambao utaleta matokeo sawa na yale ya asilimia 15. Sambamba na hilo, Serikali ifanye jitihada za makusudi kuhakikisha fedha zinazodaiwa chini ya Ushuru wa Forodha asilimia 15 zinarejeshwa kwa wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mapokeo mazuri katika utekelezaji wa ujenzi wa Tanzania ya Viwanda, ambapo Watanzania pamoja na wawekezaji kutoka nje ya

nchi wamewekeza na kuzalisha bidhaa mbalimbali lakini wamekuwa wakikabiliwa na changamoto za ushindani usio wa haki sokoni unaotokana na bidhaa zinazoingizwa kutoka nje kuuzwa kwa bei nafuu. Mfano, viwanda nya chuma, mabomba, mabati vilivyopo nchini vinatosheleza mahitaji ya soko la ndani na ziada kupatikana lakini bado nchi inaruhusu kuingizwa kwa bidhaa hizo ambazo baadhi yake hazina viwango. Hali hiyo inapelekea kuharibu soko la viwanda vyetu nya ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya kuivilinda viwanda vyetu nya ndani na jambo hilo lianze kwa kuzipatia *HS Code* ya tofauti kwenye bidhaa zinazozalishwa nchini ili kuwezesha kuzitofautisha na zinazotoka nje. Baada ya kuzitofautisha, kipangwe kiasi kikubwa cha kodi kwa bidhaa zinazoingizwa nchini. Hatua hii itawezesha viwanda vyetu nya ndani kushindana katika soko. Hatua hii lianze hasa kwa bidhaa ambazo viwanda vyake vina uwezo wa kuzalisha na kutosheleza mahitaji ya soko la ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa miradi yote mikubwa inayoteklezwa na Serikali ni vyema ikatumia vifaa vinavyopatika nchini. Sambamba na hilo, kwa ile miradi ya ufadhili tuangalie namna ya kuvipatia viwanda nya ndani msamaha wa kodi (*exemption*) ili viweze kushindana na viwanda nya nje katika kupata tenda za kusambaza vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upangaji wa kodi. Kamati inaishauri Serikali kuwa makini na kupanga viwango nya kodi kulingana na viwango nya kodi duniani hususan ndani ya Jumuiya ya Kikanda. Hatua hiyo inasaidia kuendana na kodi ya washirika wetu lakini pia itatuwezesha kushindana katika masoko na kuntuondolea hali ya kuwa soko la bidhaa za wenzetu kwani bidhaa zetu za ndani zitakuwa na bei sawa na zile zinazoingizwa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuelekea Tanzania ya Viwanda tunahitaji teknolojia mpya inayoendana bila ya kuleta wataalam watakaoturithisha teknolojia hii hatuwezi

kufanikiwa. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha vibali nya kazi haviwi vikwazo tena kwa kupata teknolojia na ujuzi wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) linafanya kazi nzuri lakini limezidiwa na uwezo wa mahitaji ya sasa ya soko la Tanzania. Kwa sasa wahitaji wa huduma za *TBS* wameongezeka lakini Shirika lina uwezo uleule wa awali jambo linalopelekea kuhudumia sampuli nyingi kwa wakati mmoja na kuchelewesha matokeo ya vipimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ucheleweshaji huu umekuwa kero hususan kwa watumiaji wa bandari ambapo mizigo yao hulazimika kukaa muda mrefu bandarini hivyo kuwaongeza gharama (*storage*). Kamati inashauri Serikali kuongeza uwezo wa *TBS* na kuwaongeza watumishi na kuboresha maslahi yao, jambo litakalowaondolea tamaa ya kufanya chochote nje ya utaratibu. Sambamba na hilo Serikali ihakikishe inasimamia ujenzi wa *Test House* ya *TBS* kuhakikisha inakamilika, jambo hili litaongeza ufanisi wa Shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Tanzania ya Viwanda umepokelewa vizuri sana ambapo kuna viwanda vingi vidogo, nya kati na vikubwa vimeanzishwa. Viwanda hivyo vina uwezo wa kuzalisha bidhaa zenyе ubora unaohitajika lakini kumekuwa na kasumba ya Watanzania pamoja na Mamlaka za Serikali kutumia bidhaa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, tuna Kiwanda cha Bora ambacho ni mionganoni mwa viwanda vilivyobinafsishwa na kinafanya kazi nzuri sana ya kuzalisha viatu mbalimbali kuanzia kandambili na buti. Miaka miwili iliyopita Kiwanda cha Bora kilipewa changamoto na Mheshimiwa Rais ya kuzalisha viatu nya Jeshi na kikafaulu kwenye jambo hilo na kuzalisha viatu nya Jeshi vizuri vinavyokidhi viwango. Jambo la kushangaza, mwaka wa pili sasa Jeshi halijawahi kuchukua viatu Bora, pamoja na kuwa Bora ilishiriki katika tenda ya jeshi na wana bidhaa zinazokidhi viwango na za bei ya chini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Makamu Mwenyezekiti, naomba uhitimishe.

**MHE. KANALI (MST.) MASOUD ALI KHAMISI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyezekiti, Kamati inashauri Serikali kuzielekeza Mamlaka zote za Serikali wakati wa kufanya manunuzi kuhakikisha wanatafuta bidhaa hizo kwanzo nchini na pindi zinapokosekana ndiyo ziagizwe nchi za nje. Kamati pia inawahamasisha Waheshimiwa Wabunge kuonesha uzalendo wa kutumia bidhaa zetu za Kitanzania na inawaomba kuwashawishi wapiga kura wetu kuwa Tanzania ya Viwanda inawezekana tutumie vyatkwetu.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, hitimisho, naomba nikushukuru sana wewe, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyevitl wote wa Bunge kwa kuendesha Bunge hili Tukufu kwa umahiri mkubwa. Vilevile, naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kutupatia maelekezo mazuri ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, naomba nitumie fursa hii kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuitekeleza azma ya kujenga Tanzania ya Viwanda kwa vitendo. Kamati inaunga mkono juhud zake na itaendelea kutoa ushirikiano ili azma hiyo itimie. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyezekiti, kwa namna ya kipekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kushiriki kikamilifu wakati wa kupitia na kuchambua na hatimaye kupitisha maoni kuhusu bajeti ya Wizara hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka kwenye kitabu chetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyezekiti, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Joseph Kakunda, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Eng. Stella

Martin Manyanya, Makatibu Wakuu pamoja na Wataalam wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa jinsi walivyoshirikiana na Kamati katika kujibu hoja za Wajumbe wa Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na kufafanua kwa kina kuhusu Makadirio na Mapato ya Matumizi ya mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bwana Athumani Hussein; Mkurugenzi Msaidizi, Sehemu ya Fedha na Uchumi, Bwana Michael Chikokoto; Makatibu wa Kamati Bi. Zainab Mkamba, Bi. Mwajuma Ramadhani pamoja na Msaidizi Bi. Paulina Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 40 na Fungu 60 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kiasi cha Sh.100,384,738,648 ambapo shilingi bilioni 48.88 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 51.05 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofj*)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA,  
BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA  
MAJUKUMU YA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA,  
FUNGU 44-VIWANDA NA FUNGU 60-BIASHARA KWA MWAKA  
2018/2019 NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA  
MAPATO NA MATUMIZI FUNGU 44 NA FUNGU 60 YA MWAKA  
WA FEDHA 2019/2020**

---

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na 117 (11) ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016,

naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara, **Fungu 44-Viwanda na Fungu 60-Biashara** kwa Mwaka wa Fedha **2018/2019** na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa **Fungu 44-Viwanda na Fungu 60-Biashara** kwa Mwaka wa Fedha **2019/2020**.

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 98(1), ya Kanuni za kudumu za Bunge inazielekeza Kamati za Kisekta kufanya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa lengo la kubaini ufanisi wa miradi hiyo. Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilitekeleza jukumu hilo ambapo ilitembelea Miradi ya Maendeleo inayotekelawa chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara na kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo na kuishauri Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati za kisekta ikiwepo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, zimefanya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Katika kutekeleza jukumu la Uchambuzi wa Bajeti ya Serikali Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira imezingatia kifungu cha 6(1) na 7(1)(a) vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha Taarifa hii kwa lengo la kueleza namna Kamati yangu ilivyotekeliza majukumu yake kwa kuzingatia masharti ya Kanunu ya 98 (1) na (2), sambamba na hilo nalenga kuliomba Bunge lako tukufu kuidhinisha maombi ya Fedha kwa ajili ya Wizara ya Viwanda na Biashara , **Fungu 44-Viwanda na Fungu 60-Biashara** kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Aidha, taarifa hii itaainisha mapendekezo kuhusu masuala kadhaa ambayo Kamati inaamini ni muhimu yakafanyiwa kazi.

**2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA MPANGO WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 NA MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019.**

**2.1 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, mnamo mwezi Mei, 2018, Bunge lako Tukufu liliidhinisha Bajeti kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Kutokana na kuidhinishwa kwa fedha hizo, Kamati ilitaka kujiridhisha kama dhamira ya Bunge lako ya kuidhinisha bajeti hii limetimia. Ambapo kamati ilifanya uchambuzi wa taarifa mbalimbali zilizowasilishwa na Wizara mbele ya Kamati na kufanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo. Lengo kuu la kutumia njia hizo lilikuwa ni kujiridhisha kuhusu Utekelezaji wa malengo ya Wizara, Ukusanyaji wa mapato na Upatikanaji wa fedha ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa na Bunge.

**2.1.1 Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Viwanda na Biashara (**Fungu 44 & 60**) ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi **20,006,300,000** (yani Shilingi **5,300,000.00** kwa **Fungu 44** na Shilingi **20,001,000,000.00** kwa **Fungu 60**) kutokana na ada za leseni, nyaraka za zabuni na faini ya kukiuka Sheria ya Leseni ya Biashara. Hadi kufikia February, 2019 Wizara lilikuwa imekusanya jumla ya Shilingi **8,990,341,969.04**, kiasi hiki ni sawa na asilimia **44.94** ya lengo la makusanyo ya mwaka wa fedha 2018/2019.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba kiasi cha fedha kilichokusanywa ni pungufu kwa asilimia **55.06** ya makadirio waliyoweka kwa mwaka wa fedha 2018/2020. Aidha, kutokana na muda mchache uliobaki ambaao ni robo mwaka ya mwisho ya mwaka wa fedha unaoishia, matumaini ya kukusanya kiasi cha shillingi **11,015,958,031** ni hafifu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaisisitiza Serikali kuwa, ipange malengo ya makusanyo yanayoendana na uwezo wake halisi wa kukusanya na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.

### **2.1.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha **2018/2019**, Wizara ya Viwanda na Biashara ilitengewa jumla ya shilingi **143,334,153,648** kwa ajili ya mafungu mawili yani Fungu **44** na Fungu **60**. Fedha hizo zilitegwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zote za Wizara hiyo. Mgawanyo wa fedha hizo ulikuwa kama ifuatavyo:-

#### **i) FUNGU 44**

Fungu **44** Viwanda lilitengewa kiasi cha shilingi **117,287,008,000**. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi **93,024,525,000** zillikuwa kwa ajilli ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kiasi cha shilingi **24,262,483,000** zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

#### **ii) FUNGU 60**

Fungu **60** Biashara lilitengewa Shilingi **26,047,145,648**. Kati ya fedha hizo kiasi cha Shilingi **7,000,000,000** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na kiasi cha Shilingi **19,047,145,648** kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

### **➤ Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia Machi, 2019 ambayo ni robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Shillingi **34,799,351,984.24** kwa ajili ya Matumizi ya Wizara na taasisi zote zilizopo chini yake kwa Mafungu yote mawili (**Fungu 44 na 60**). Kiasi hiki ni sawa na asilimia **24.28** tu ya fedha zote zilizotengwa katika Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kati ya fedha zilizopokelewa Shilingi **28,322,130,670.24** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kiasi hicho ni sawa na asilimia **65.4** ya Shilingi **43,309,628,648.00** ambazo ni fedha ilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mafungu yote mawili (**Fungu 44 & 60**).

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo hadi kufikia mwezi Machi, 2019 ni shilingi **6,477,221,314** tu ndio zilikuwa zimepokelewa, kiasi hiki ni sawa na asilimia **6.48** tu ya shilingi **100,024,525,000** ambayo ndio fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka fedha **2018/2019**, Kamati ilibaini kwamba:-

- i) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina umeendelea kushuka kwa miaka mitatu mfululizo, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 zilitoka asilimia **42.37**, mwaka 2017/2018 zilitoka asilimia **30.64** na mwaka 2018/2019 zimetoka **24.28**;
- ii) Upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kutoka Hazina sio wa kuridhisha, ni asilimia **6.48** tu ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ndio zilikuwa zimepokelewa hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka. Kiasi kilichopokelewa ni pungufu kwa asilimia **93.52** na kwa kipindi kilichobaki cha robo mwaka ni vigumu kupatikana kwa kiasi chote kilichosalia;
- iii) Ukiacha suala ya kupelekwa fedha kidogo kwa mwaka wa fedha unaoishia, vilevile upatikanaji wa fedha hizo umeendelea kupungua mwaka hadi mwaka, ambapo kwa miaka mitatu mfululizo hadi kufikia kipindi cha robo ya tatu ya mwisho wa mwaka wa fedha mtiririko wa upatikanaji wa fedha ulikuwa kama ifuatavyo; mwaka wa fedha 2016/2017 zilipokelewa asilimia **18.9**, mwaka 2017/2018 zilipokelewa asilimia **9.97** na mwaka 2018/2019 zimepokelewa asilimia **6.47** tu ya fedha zilizoidhinishwa; na
- iv) Fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida zinatolewa kwa wakati ukilinganisha na utoaji wa fedha za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, mtazamo wa Kamati kuhusu jambo hili ni kwamba mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha kwa

Wizara ya Viwanda na Biashara unaashiria kukwama kwa utekelezaji wa baadhi ya majukumu yaliyopangwa na Wizara kwa mwaka huu wa fedha. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha fedha zinazoidhinishwa na Bunge zinapelekwa tena kwa wakati ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yote yaliyokusudiwa.

### **2.1.3 Utekelezaji wa Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifuatilia utekelezaji wa malengo yaliyopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa lengo la kujiridhisha na utekelezaji wake. Wizara ilibainisha hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa malengo hayo. Kamati ilipongeza hatua hizo, hata hivyo iliendeleo kuisisitiza Serikali kuongeza kasi katika maeneo yafuatayo: -

- i) Kukamilisha tathimini ya hali halisi ya uzalishaji wa viwandani pamoja na mahitaji ya bidhaa za viwandani. Kamati inasisitiza kuzingatia Sekta ambazo mara kwa mara zimekuwa zikikumbana na changamoto kama Sekta ya Sukari na Sekta ya Mafuta ya Kupikia.
- ii) Kukamilisha mapitio ya Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya Mwaka 1996-2020. Sera hii ni ya muda mrefu na wakati inaanizishwa hatukuwa na mipango ya ujenzi/usimamizi wa viwanda ambayo ipo sasa. Hivyo basi ni vyema Serikali ikakamilisha mapitio yake na kuiboresha kuhakikisha inaendana na mazingira ya sasa ya Viwanda na biashara.
- iii) Kuhakikisha huduma za usajili wa biashara na makampuni zinazofanyika kupitia mitandao ya kompyuta (online registration) zinakuwa na mfumo rahisi kiasi cha kuweza kutumiwa na mtu mwenye elimu yejote. Sambamba na hilo tupunguze urasimu katika masharti ya nyaraka za kuambatisha.
- iv) Kuendelea kuziboresha taasisi za utafiti ambazo zipo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa lengo la kuziwezesha kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa.

## **2.2 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

### **2.2.1 Mapitio ya Taarifa za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Februari, 2016 katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilifanya ziara ya kutembelea baadhi ya miradi iliyo tengewa fedha na inatekelezwa na Wizara hii.

Kamati ilifanya ziara ya kutembelea baadhi ya miradi ya maendeleo kwa lengo kujionea hali halisi na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wake. Kamati ilitembelea **Mradi Namba 6260 – *Institutional Support* (Fungu 44)**, Mradi huu unahuishisha kuziwezesha Taasisi zilizopo Chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara kutekeleza majukumu yake. Chini ya Mradi huu Kamati ilitembelea na kukagua; -

Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini - (CAMARTEC);

a) Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO); na

b) Mradi wa kuboresha Miundombinu ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS);

Maelezo ya Miradi hiyo ni kama yafuatavyo; -

#### **a) Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini - (CAMARTEC) (Mradi Namba 6260, Fungu 44)**

Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini - (CAMARTEC) ni moja ya taasisi inayosimamiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 CAMARTEC kupitia **Mradi Namba 6260 - *Institution Support*** iliidhinishiwa Shilingi **3,000,000,000.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Fedha hizo zillenga kuendeleza utafiti wa teknolojia, kukuza wazalishaji wa ndani wanaojihusisha na zana za kilimo, kuhakiki ubora wa zana za kilimo, kuimarisha miundombinu ya utafiti wa zana za kilimo, kusambaza zana za kilimo kwa wakulima zilizofanyiwa utafiti na kushughulikia masuala yanayohusu tafiti katika kutunza mazingira.

➤ **Hali ya Mradi wakati wa Ziara ya Kamati**

Hali ya Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini - CAMARTEC si ya kuridhisha ambapo karakana zake zimejaa mitambo chakavu na teknolojia zinazotumika ni duni, jambo linalopelekea kuzalisha zana duni na za gharama ya juu ukilinganisha na hali halisi ya soko kwa sasa. Aidha, kwa takribani miaka mitatu mfululizo kituo hakijapokea ruzuku kutoka Serikalini na hivyo kimekuwa kikitekeleza majukumu yake katika mazingira magumu. Pia, kituo kimekuwa kikikabiliana na changamoto mbalimbali kama vile; Upungufu wa watumishi wenye taaluma za uhandisi, watafiti na mafundi sanifu wakati kada hizo ndio uhai wa kituo na majukumu ya kituo hayataweza kutekelezwa pasipokuwa na wataalamu wa kutosha wa kada tajwa hapo juu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kutembelea na kukagua utekelezaji wa Shughuli za Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini - (CAMARTEC), Kamati ilikuwa na maoni na ushauri ufuataao; -

i) Teknolojia inabadilika kila siku hivyo basi shughuli za ubunifu, usanifu na utafiti zinahitaji mafunzo ya mara kwa mara ili kuhuisha taaluma hizo. Mafunzo hayo yataiwezesha taasisi hii kushindana katika soko la dunia, ni vyema Serikali ihakikishe inaziwezesha taasisi zote zinazojihusisha na utafiti wa teknolojia kupata fursa za mara kwa mara kwenda kujifunza kwa nchi zilizoendelea;

ii) Chanzo kikuu cha mapato katika kituo hiki ni ruzuku kutoka Serikalini, lakini mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini si wakuridhisha, jambo linalopelekea uzalishaji wa kituo kuwa mdogo ukilinganisha na ukubwa na umuhimu wa taasisi hiyo. Kamati inashauri Serikali kupeleka fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge, hatua hii itakiwezesha kituo hicho kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi hivyo kupelekea kuweza kuhimili kwenye soko la ushindani. Pia, Kamati inakishauri kituo kujiongeze kwa kuamua kuijendesha kibishara Zaidi. kwa Mfano kituo kinaweza kuamua kubuni zana ndogo ndogo nyingi na kuziwa, hatua hii itawaongezea kipato na kupunguza utegemezi wa fedha kutoka Serikalini;

- iii) Mazingira ya eneo la CARMATEC si yakuridhisha kwa upande wa mpangilio (set up) wa kituo hicho na kukosekana kwa safety gear kwa wafanyakazi, wateja na wanaotembelea kituo. Kamati inaishauri Wizara kutekeleza program ya KAIZEN katika kituo hiki kwa lengo la kuboresha mazingira ya kazi lakini pia itasaidia kulinda usalama wa wadau wote wa kituo;
- iv) Bidhaa inapoingia sokoni inatakiwa kuwa na ubora ambaو utaweza kushindana na bidhaa nyingine. Ili kufanikisha hilo kituo kinapaswa kuboresha njia za upatikanaji wa malighafi (vipuli, vyuma na mabati) za kuzalishia mashine wanazozitengeneza. Hatua hiyo itawasaidia kuzalisha bidhaa bora na imara. Ushauri huu wa kamati unatokana na ukweli kwamba, malighafi zinazotumika kwa sasa zinanunuliwa mahala popote tu na nyingi hazina ubora stahiki hivyo kipelekea zana za kituo kuwa duni na kushindwa kushindana katika soko;
- v) Dhana ya kuanzisha kituo hiki iliwalenga watanzania wa hali ya chini kwa kuzalisha zana za kilimo na teknolojia vijijiini, lakini zana zinazotengenezwa na kituo zimekuwa na gharama ya juu, Kamati inaishauri Wizara kutenga bajeti ya kutosha ambayo itawawezesha kutosheleza asilimia kubwa ya gharama za uzalishaji jambo litakalowawezesha kuuza bidhaa zao kwa gharama nafuu na kuwanufaisha watu wa hali zote;
- vi) Dhana ya kituo ni kuwasaidia wakulima vijijiini, lakini shughuli za kilimo zinahusisha mnyororo mrefu mpaka kumfikia mlaji sokoni. Ili kuwa na mnyororo wa thamani ya mazao ambaو unalinda ubora wa mazao, Kamati inaishauri Serikali kuititia CAMARTEC kujipanga kuzalisha zana/mashine ambazo zitamsaidia mkulima kuanzia hatua ya kuandaa shamba hadi kufika kwa mlaji;
- vii) Nafasi nyingi katika taasisi zinakaimiwa na baadhi ya wafanyakazi wa taasisi hiyo. Hali hiyo inapelekea kupoteza ari ya kazi na kutokuwa na uwezo wa kufanya maamuzi. Hivyo

serikali ifanye juhudzi za kujaza nafasi hizo za kiutendaji ili kuboresha taasisi hiyo;

**b) Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO); (Mradi Namba 6260, Fungu 44)**

Kama ilivyo kwa CAMARTEC, Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania - TEMDO pia linapata ruzuku kutoka serikalini kupitia **Mradi namba 6260 - Institution Support**, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 Shirika limetengewa jumla ya Shilingi **4,000,000,000.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kiasi kilichotengwa kwa ajili ya Shirika la Uhadisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania - TEMDO kililenga Kujenga miundombinu ya kiatamizi cha teknolojia na biashara pamoja kuwajengea uwezo wajasiriamali wa katni na wadogo; Kupitia upya sheria iliyoanzisha kituo; kubuni na kuendeleza chasilli cha mtambo wa kukausha mazao ya kilimo, kubuni na kutengeneza chasilli cha mtambo mdogo wa kusindika chai; Kubuni na kuendeleza utengenezaji wa mtambo wa kuhifadhi baridi (cold room) ambao utasaidia kuhifadhi bidhaa mbalimbali. Pamoja na hilo shirika Kuendeleza na kuhamasisha utumiaji wa technolojia za utengenezaji na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali kama vile marumaru, kwa mfano Vigae kwa kutumia malighafi zinazopatikana nchini.

➤ **Hali ya Mradi wakati wa ziara ya Kamati**

Wakati wa Ziara ya Kamati tarehe 16 Machi, 2019 katika kituo hicho, Kamati ilikuta kazi mbalimbali zikiendelea ikiwemo ufungaji (*installation*) wa mashine mpya za kisasa ndani ya karakana hiyo ya shirika na majoribio ya mashine hizo. Shughuli zote zilizokwua likiendelea katika eneo la shirika zilitkelezwa kwa kutumia fedha ya Maendeleo ya Mwaka wa Fedha **2017/2018** ambapo shirika litumia jumla ya Shilingi **1,582,240,655.00** ambazo zilihusisha shilingi **1,263,435,000.00** ruzuku kutoka Serikalini na shilingi **318,805,655.00** makusanyo ya Shirika kwa mwaka 2017/2018.

Kwa Mwaka wa Fedha **2018/2019** mpaka kufikia tarehe 16 Machi, 2019, shirika hilo halikuwa limepokea kiasi chochote kutoka Serikalini kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo. Hadi kufikia tarehe tajwa hapo juu, shirika lilikuwa limepokea fedha za mishahara tu.

Sambamba na hili, Shirika linakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ni upungufu wa fedha za kufanya utafiti jambo linalopelekea Shirika kushindwa kufanya utafiti kwa uwezo wake wote; ukosefu wa fedha za matumizi mengineyo (OC) hali inayopelekea Shirika kushindwa kumudu shughuli zake zilizokuwa zimekusudiwa kutekelezwa; upungufu wa wafanyakazi wenye taaluma ya kada ya uhandisi na usanifu; na uhaba wa rasilimali fedha hivyo kupelekea kushindwa kusambaza mashine na mitambo iliyozalishwa na Shirika kwa kiwango kilichotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya ziara ya Kamati katika Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO), ilikuwa na maoni na ushauri ufuatao; -

- i) Hali ya karakana ya Shirika inaridhisha walau kwa kiasi kidogo, kwa kuwa bajeti yake ya Mwaka wa Fedha **2017/2018** ilipokelewa kwa asilimia **57.9**. Fedha hiyo iliwezesha kununua baadhi ya mashine mpya ambazo zitaongeza ufanisi wa shirika kwa kiasi kikubwa. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Shirika inapelekwa na kwa wakati, ili kuendelea kuboresha na kuliwezesha shirika hilo kutekeleza dhamira ya kuanzishwa kwake;
- ii) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwenda kwa taasisi za utafiti sio wa kuridhisha, zimekuwa zikitolewa kwa kusua sua sana. Vilevile kuna baadhi ya miaka zimekuwahaziendi kabisa, jambo linalokwamisha utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo. Kamati inaishauri Serikali kama inaona utaratibu wa kutoa mwaka hadi mwaka ni mgumu ni bora ikajipanga kuzipatia taasisi hizi mitaji ili ziweze kuijendesha bila kusubiri ruzuku;
- iii) Kama ilivyo kwa taasisi nyingine zote za utafiti duniani, wafanyakazi wa TEMDO wanatakiwa kupatiwa mafunzo ya mara kwa mara ili waweze kuendana na mabadiliko ya teknolojia. Hivyo Serikali ijitahidi kuiwezesha TEMDO kwenda kujifunza kwa nchi zilizoendelea kiteknolojia.

iv) Nafasi nyingi za uongozi katika shirika zinakaimiwa, hali ambayo imedumu kwa muda mrefu, hivyo basi Kamati inaisisitiza Serikali kuchukua hatua ya kujaza nafasi hizo za uongozi.

v) Taasisi itoe elimu na kujitangaza kwa wananchi kuhusu kazi wanazozifanya. Hatua hiyo itaongeza uelewa kwa jamii juu ya shughuli wanazozifanya na hatimaye kukuza soko na mauzo ya shirika.

**c) Mradi wa kuboresha Miundombinu ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) (Mradi Namba 6260, Fungu 44)**

Kamati ilipata fursa ya kutembelea Mradi wa kuboresha Miundombinu ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS). Mradi huu unatekelezwa chini ya **Mradi Namba 6260 - *Institutional Support*** na unatekelezwa kwa kutumia fedha za ndani za Shirika pamoja na ruzuku kutoka Serikalini. Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, TBS kuititia mradi huu ilitenga shilingi **2,000,000,000.00** kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa maabara ya kisasa kwa ajili ya Shirika. Mradi huu unahusisha ujenzi wa *Test House* ambayo itakuwa njengo la ghorofa nane ambalo ndani yake inatarajiwa kujengwa maabara za kisasa zitakazo endana na mahitaji ya shirika.

➤ **Hali ya Mradi wakati wa ziara ya Kamati**

Wakati wa Ziara ya Kamati tarehe 20 Machi, 2019, Kamati ilikuta ujenzi ukiendelea na hatua za awali za ujenzi wa jengo hilo zilikuwa zimekamilika, hivyo hatua za umalizaji (finishing) zilikuwa zikiendelea.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi ulikadiriwa kutekelezwa ndani ya wiki 69 yaani kuanzia Januari, 2018 hadi Aprili, 2019, lakini kwa hatua iliyokuwa imefikiwa wakati wa ziara ya Kamati ilidhihirisha kuwa mradi huo hauwezi kukamilika ndani ya muda uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu gharama za Mradi, imekadiriwa kutumika shilingi **19,325,304,165.00** na kwa hatua za awali za

ujenzi ambazo kamati ilizikuta wakati wa ziara yake, ujenzi ulikuwa umekwishatumia shilingi **6,727,643,213.00**.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unapaswa kutekelezwa kwa kutumia fedha za ndani za shirika pamoja na ruzuku kutoka Serikalini, lakini hadi kufikia tarehe 20 Machi, 2019 Shirika halikuwa limepokea kiasi chochote kutoka Serikalini kwa ajili ya kutekeleza mradi huo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilijulishwa juu ya changamoto wanazokabiliana nazo TBS katika utendaji wao. Baadhi ya changamoto zinazowakabili ni upungufu wa rasilimali watu, mishahara midogo kwa watumishi wa shirika jambo linalopelekea kushuka kwa morali, Upungufu wa vifaa vya maabara kwa ajili ya kufanya vipimo mbalimbali jambo linalopelekea baadhi ya maabara za shirika kutopata cheti cha umahiri, Utayari wa umma kuhusu umuhimu wa viwango katika kulinda afya na usalama wa walaji ni mdogo na Uingizaji wa bidhaa zisizo na viwango kuititia njia za panya jambo linalopelekea lawama kurudi kwa TBS pale bidhaa hizo zinapokutwa sokoni, kuwa Shirika halitimizi majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji ya Mradi wa kuboresha Miundombinu ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS), kutembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huo, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa gharama iliyokadiriwa katika utekelezaji wa ujenzi wa jengo hilo ni kubwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilihoji kwa lengo la kupatiwa ufanuzi juu ya gharama hizo, majibu ya TBS yalikuwa gharama hizo zipo sahihi na zinatokana na kuwa jengo linalojengwa ni jengo maalumu na linatofauti na majengo mengine.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haijaridhishwa na majibu yaliyotolewa na TBS, hivyo Kamati inaitaka Wizara ya Viwanda na Biashara kufanya uchunguzi maalumu katika Mradi huo na kuiwasilishwa kwa Kamati ili kubaini uhalsia wa gharama

za mradi huo. Kamati inaitaka Wizara kufanya haraka uchunguzi huo ili kuzuia upotevu wa fedha Zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, mradi huu unatarajiwa kuipatia TBS uwezo wa kuhudumia sampuli nyingi na kwa haraka na kuiwezesha kuendana na mahitaji. Kamati inaishauri Serikali kuwaongezea uwezo watumishi wa TBS kwa kuwawezesha kupata mafunzo yatakayowasaidia kuandaa viwango/vipimo vipyta ambavyo kwa sasa TBS haina uwezo wa kuvikagua na imekuwa ikiwaelekeza wadau kwenda kupima bidhaa zao nje ya nchi. Mfano ni bidhaa za *electronics* hususani simu na televisheni.

Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kupeleka fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya mradi huu ili mradi uweze kukamilika kwa wakati na kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa.

**d) Ziara ya Kamati katika Kiwanda cha Tanzania Breweries Limited (TBL) na Kiwanda Serengeti Breweries Limited (SBL)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilipata fursa ya kutembelea na kukagua shughuli za Kiwanda cha Tanzania Breweries Limited (TBL) na Kiwanda cha Serengeti Breweries Limited (SBL) kwa lengo la kujiona namna wanavyoendesha shughuli zao, pamoja na kubaini mafanikio na changangamoto wanazokabiliana nazo.

**Mheshimiwa Spika**, Viwanda hivi vinajihuisha na utengenezaji na usambazaji wa vinywaji vikali kama vile bia na pombe kali. Katika uendeshaji wa shughuli zao wanakabiliana na changamoto zifutazo; -

**i) Tozo ya Kodi ya Kielektroniki – Electronic Tax Stamp (ETS)**

**Mheshimiwa Spika**, ETS ni mfumo wa uratibu wa ukusanyaji kodi ambao unahusisha mtambo maalumu uliouniganishwa na mashine za uzalishaji kwa ajili ya kuhesabu idadi ya bidhaa zilizozalishwa. Mfumo huu umelengwa kuleta uwazi wa kila kinachozalishwa kiwandani kionekane katika hesabu za

kiwanda tayari kwa kulipiwa kodi. Changamoto ya mfumo huu ni kuwa hakuna na wataalamu (on-site personnel) wa kurekebisha mitambo mara inapotokea hitlafu; Upya na ugeni wa kutumia mfumo huo, hivyo kupelekea kuhitaji (servicing) mara kwa mara ambapo hupelekea kusababisha ucheleweshaji (down time); kuongezeka kwa gharama za uzalishaji katika viwanda hivyo zinazosababishwa na gharama ya mfumo wa ETS; na mabadiliko ya gharama ambazo zilipangwa kutumika awali, mfano Tanzania Cigarate Company waliambambiwa kuwa watalipa Dolla za Kimarekani 10/1000 ETS stamps lakini baada ya kuanza mfumo wanatakiwa kulipa Dolla za Kimarekani 20/1000 stamps.

Kamati inaishauri Serikali kukaa na wamiliki wa viwanda ambavyo vilitumiwa kama mfano kuanza kuutumia mfumo huu na kujadiliana juu ya changamoto tajwa kwa lengo la kuboresha kabla mfumo huu haujaanza kutumiwa na viwanda vyote nchini.

**ii) Changamoto ya kupata Ardhi ya Uwekezaji**

**Mheshimiwa Spika**, TBL imeomba eneo ambalo lilikuwa ni eneo la kiwanda cha KILTEX- Arusha ambacho kilishakufa. TBL imelenga kutumia eneo hilo kwa ajili ya kupanua uwekezaji wa kiwanda hicho na imekwisha andika na kuwasilisha maombi ya kupata eneo hilo lakini kuna urasimu/ mvutano unaoendelea. Kamati inaona kuwa kuna umuhimu TBL kupewa eneo hilo kwa kuwa hakuna shughuli zozote za uzalishaji zinazoendelea katika eneo husika, vilevile ni eneo ambalo limepakana na kiwanda hivyo itakuwa rahisi kwa TBL kuendeleza uwekezaji wa kiwanda hicho.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa SBL kuna mgogoro wa eneo kati ya SBL na TRC, mgogoro huo unatokana na madai ya TRC kwamba sehemu ya eneo la SBL ni eneo la TRC hivyo kupelekea kuwawekea alama za kuvunja ili waweze kuchukua eneo lao. Kwa kuwa SBL ilipewa nyaraka zote za kuwamilikishwa eneo hilo, na kwa kuwa SBL imeshafanya uwekezaji mkubwa katika eneo hilo, hivyo Serikali itafute namna ya kusuluhisha mgogoro huu bila ya kuathiri uwekezaji

uliofanywa na SBL. Pia, Serikali iielekeze TRL wakubali kutumia eneo jingine walilopewa na Halmashauri kwa kuwa wao bado hawajaanza kufanya uwekezaji wowote.

**iii) Gharama kubwa za Maji**

**Mheshimiwa Spika**, Kiwanda cha SBL kimechimba visima viwili kwa ajili ya matumizi ya uzalishaji katika Kiwanda hicho, kutokana na sheria mpya inayotaka kulipia matumizi ya maji ya visima kiwanda kinalipa shilingi 10 kwa lita moja ya maji, hivyo kupelekea gharama kubwa kwenye utumiaji wa maji ya kisima ukizingatia wana matumizi makubwa ya maji kwa kuwa sehemu kubwa ya utengenezaji wa bidhaa zao unahusisha maji. Kamati inaipongeza Serikali kwa kufuta tozo ya matumizi ya maji ya visima kwa visima vya majumbani. Kutokana na hatua hiyo Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya gharama hizo kwa upande wa viwandani, ukizingatia kuwa Serikali yetu haljawa na uwezo wa kutosha wa kuvihudumia viwanda hivyo.

**3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI  
KUHUSU BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa iliyokuwa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji (ambayo sasa imegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Uwekezaji) kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Kamati ilioa ushauri kwenye maeneo Kumi na Saba (17). Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati, hata hivyo kuna maeneo ambayo Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wake na inaendelea kuisisitiza Serikali kuongeza juhudii ya utekelezaji wa maagizo hayo, maeneo hayo ni pamoja na:-

- i) Serikali kuendelea kuchukua hatua kwa wawekezaji ambaa bado hawajaitikia wito wa Serikali wa Kufufua viwanda vilivyobinafsishiwa. Sambamba na hilo Serikali iangalie namna ya kuunda Tume Maalumu itakayofuatilia eneo la viwanda vilivyobinafsishiwa kwa lengo la kufuatilia kwa ukaribu na kujua ukweli wa eneo hili.

- ii) Jitihada za Makusudi ziendelee kuchukuliwa katika kuendelea kuboredha mazingira ya Uwekezaji nchini ili kuvutia wawekezaji wengi.
- iii) Serikali kuendelea na juhudzi za kuziwesha taasisi zake za utafiti ikiwemo CAMARTEC, SIDO, TIRDO na TEMDO ili ziweze kubuni zana mbalimbali za kilimo ambazo zitasaidia na kumrahisishia mkulima kuendeleza shughuli zake kwa urahisi ukizingatia Kilimo ndio shughuli kuu ya watanzania walio wengi.

- 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020
- 4.1 Uchambuzi wa Mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020

#### 4.1.1 Uchambuzi wa malengo/mpango

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara, Kamati ilipitia maelezo ya Waziri kuhusu malengo waliyojipangia kuyatekeleza kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Lengo lilikuwa ni kufatilia tija inayoweza kupatikana kutokana na malengo yaliyopangwa kutekelezwa kwa fedha zinazoombwa katika **Fungu 44 na 60**. Aidha, Kamati illingenisha utekelezaji wa malengo ya Mwaka wa Fedha **2018/2019** na malengo yaliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha **2019/2020** na katika ulinganisho huo kamati ilibaini yafuatayo:-

Malengo haya yalikuwa yanaendana na hati idhini Serikali ilioainisha majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara;

- i) Malengo ya Mwaka wa Fedha 2019/2020 yalikuwa yakifanana na malengo ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambayo yalikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji;

**Mheshimiwa Spika**, malengo ya Wizara ya Viwanda na Biashara ya Mwaka 2019/2020 yamejitosheleza na kuwa utekelezaji wake unatarajiwa kuboresha hali ya biashara nchini na kukuza Uchumi wa Nchi. Ili malengo haya

yatekelezwe kikamilifu Serikali inapaswa kuhakikisha fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara zinapelekwa wizarani tena kwa wakati.

#### **4.1.2 Makisio ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ya Viwanda na Biashara imepanga kukusanya shilingi milioni **6,300,000** kutokana na uuzaji wa nyaraka za zabuni. Ambapo kati ya fedha hizo shilingi **5,300,000** zitakusanya kwa **Fungu 44** viwanda na shilingi **1,000,000** zitakusanya kutoka **Fungu 60** Biashara, uchambuzi wa Kamati ulibaini mambo yafuatayo; -

**Mheshimiwa Spika**, Kiasi kilichopangwa kukusanya na Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kimepungua kwa kiasi kikubwa ukililinganisha na mpango wa makusanya ya Mwaka wa fedha 2018/2019. Maelezo ya Wizara ya kuhusu kuporomoka kwa kiwango cha makusanyo ni kuwa chanzo kikubwa cha makusanyo ya Wizara kilikuwa uuzaji wa Leseni za Biashara na Faini zitokanazo na leseni za Biashara ambavyo kwa sasa vimehamia TRA. Hivyo Wizara imebakiwa na uuzaji wa Nyaraka za Zabuni ambayo mapato yake ni madogo. Kamati iliishauri Wizara kuweka mikakati mahususi ya kutafuta vyanzo vingine/vipyta vya mapato ili waweze kuongeza makusanya.

#### **4.1.3 Mpango wa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara imetengewa jumla ya Shilingi **100,384,738,648** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shughuli za maendeleo kwa mafungu yote mawili **Fungu 44 na 60**. Kati ya fedha zinazoombwu shilingi **48,884,738,648** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **51,500,000,000** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

##### **i) FUNGU 44 -VIWANDA**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Viwanda na Biashara **Fungu 44** – Viwanda

limetengewa jumla ya shilingi **79,149,452,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Wizara yanayoangukia ndani ya **Fungu 44**. Katika fedha hizo shilingi **27,649,452,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida na shilingi **51,500,000,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya **Fungu 44** ni sawa na asilimia **78.8** ya fedha zote zinazombwa na Wizara ya Viwanda na Biashara, ambapo asilimia **34.9** ya Bajeti ya **Fungu 44** ambayo ni shilingi **27,649,452,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida na inahusisha shilingi **22,530,079,000.00** ya mishahara ya watumishi na shilingi **5,119373,000.00** ya matumizi mengineyo (OC). Kiasi kilichosalia ambacho ni shilingi **51,500,000,000.00** sawa na asilimia **65.1** ya fedha zinazombwa kwa ajili ya **Fungu 44** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**ii) FUNGU 60- BIASHARA**

**Mheshimiwa Spika**, **Fungu 60** - Biashara inaombewa Shilingi **21,235,286,648** ambazo ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo Shilingi **7,000,000,000** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo na Shilingi **19,765,196,000.00** kwa ajili ya mishahara.

**Mheshimiwa Spika**, kiasi kilichotengwa kwa ajili ya **Fungu 60** kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ni pungufu kwa asilimia **18.47** ya fedha zilizotengwa kwa fungu hili katika Mwaka wa Fedha unaoishia yani 2018/2019. Aidha, chini ya Fungu hili haijatengwa fedha yoyote kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutokana na ufinyu wa ukomo wa bajeti kwa fungu hili. Hivyo kupelekea Mradi uliokuwa chini ya **Fungu 60** wa ASDP II kuhamishiwa na kutekelezwa chini ya Idara ya Sera na Mipango chini ya **Fungu 44**.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati kuhusiana na Mpango wa bajeti umebaini mambo yafuatayo:-

i) Kiasi hicho cha bajeti kilichotengwa kwa ajili ya mafungu yote mawili ni pungufu kwa asilimia **29.9** ukilinganisha na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ya Mwaka wa Fedha unaoishia yani 2018/2019;

ii) Upungufu wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara unaathari kubwa kwa upande wa fedha za Miradi ya Maendeleo ambayo imepungua kwa asilimia **48.51** ukilinganisha na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019;

**Mheshimiwa Spika**, kushuka kwa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kunaashiria kukwama kwa utekelezaji wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Aidha, hali hii inaleta mashaka katika utekelezaji wa kipaumbele cha taifa cha kuwa na Uchumi wa Kati kwa kupitia Viwanda ifikapo 2025 kwa kuwa miradi hii ni miradi ya kichocheo kwa Sekta hii ya Viwanda. Kamati inaishauri serikali kuongeza bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara, ili kuongeza ufanisi katika miradi husika kwa lengo la kupata matokeo yenye tija.

## **5.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kufanya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2018/2019, pamoja na kuchambua mapendekezo ya Mapato kwa Mwaka wa fedha 2019/2020 ya Wizara hii, Kamati imekuwa na Maoni na Ushauri kadhaa kwa Serikali. Ni matumaini ya Kamati kuwa maoni na ushauri huu utafanyiwa kazi kwa lengo la kuboresha shughuli za Sekta za Viwanda na Viashara nchini.

### **i) Utekelezaji wa Mradi ya Liganga**

**Mheshiwa Spika**, mradi wa Liganga ni mionganini mwa miradi ya kimkakati na ulianzishwa kwa lengo la kujenga kiwanda cha kufua chuma. Utekelezaji wa mradi huu umechukua muda mrefu takribani miaka nane (8) bado haujaanza. Kamati ilijulishwa na Wizara juu ya tathimini walioifanya katika bidhaa za chuma na kubaini kuwa vinakumbana na changamoto ya upatikanaji wa malighafi.

**Mheshimiwa Spika, kwa kuwa** Liganga inakadiriwa kuwa na chuma kingi ambacho kinakadiriwa kuchimbwa kwa zaidi

ya miaka mia (100) bila ya kuisha. **Na Kwa kuwa** Serikali bado ipo katika hatua za kutafakari namna ya kuutekeleza mradi huo. **Hivyo basi** Kamati inaishauri Serikali kutenga walau asilimia ishirini na tano (25) za malighafi ya chuma cha Liganga na kuuza kwa wenyewe viwanda vinavyozalisha bidhaa ya chuma. Hatua hiyo itawasaidia wazalishaji wa bidhaa za chuma kupata malighafi kwa urahisi, lakini pia itaisaidia Serikali kupata fedha ambazo zinazoweza kutumika katika hatua za awali ikiwa ni pamoja na kulipa fidia.

## **ii) Utekelezaji wa Mradi wa Mchuchuma**

**Mheshimiwa Spika**, mradi wa Mchuchuma unahuishisha uzalishaji wa umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya mchuchuma. Changamoto ya mradi huu ni kuwa ustaenda kuzalisha umeme ambao utakuwa ni wa gharama ya juu na umekadiriwa kuuza uniti moja kwa senti 10-12 ya dolla ya Kimarekani wakati *Regulation* za EWURA zinaekeleza umeme wa Makaa ya Mawe usiuzwe zaidi ya senti 8 Dolla ya Kimarekani.

**Mheshimiwa Spika, kwa kuwa** Serikali yetu imeshajipanga kutekeleza miradi mikubwa ya uzalishaji umeme ambao utakuwa wa gharama nafuu. **Na kwa kuwa**, bidhaa ya makaa ya mawe imeonekana kuwa na soko la kutosha ambapo viwanda vingi hususani vya saruji vimekuwa vinahitaji na kutokana na mahitaji yao kuwa makubwa yamekuwa yakiingizwa nchini kutoka nchi mbalimbali. **Hivyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kuachana na mkakati uliopo wa kuzalisha umeme katika Mradi wa Mchuchuma, badala yake makaa ya Mchuchuma yauzwe kwenye viwanda vinavyotumia aina hiyo ya nishati katika uzalishaji wake. Hatua hiyo itasaidia kupunguza uingizaji wa makaa ya mawe kutoka nje na vilevile itawapunguzia gharama za uzalishaji na hatimaye watapunguza bei ya bidhaa zao.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri pia hatua hii iende sambamba na ujenzi wa miundombinu ya uhakika ambayo itasaidia kufikika kwa urahisi eneo la mradi.

**iii) Utekelezaji wa Mradi wa Bagamoyo SEZ**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu pamoja na mambo mengine ulilenga kuboresha mji wa bagamoyo kwa kufungua fursa za kiuchumi ikiwepo uwekezaji wa viwanda ambavyo vitatoa ajira kwa kiasi kikubwa. Kamati inaishauri Serikali kutafakari tena maamuzi yaliyofanyika ya kusitisha utekelezaji wa mradi huu kwa kuwa kuna baadhi ya hatua za utekelezaji zimekwisha fanyika ikiwepo kulipa fidia kwa baadhi ya wananchi waliotakiwa kuhama kwenye eneo la mradi.

**iv) Viwanda vilivyobinafsishwa**

**Mheshimiwa Spika**, uchumi mkubwa wa nchi umehodhiwa katika eneo la viwanda vilivyobinafsishwa ambapo mapato ya nchi pamoja na ajira vimeendelea kupotea. Kwa mara kadhaa Kamati imekuwa ikifuatilia utekelezaji wa jukumu hilo lakini imekuwa ikikosa maelezo yanayo jitiosheleza. Kukosekana kwa maelezo ya kutosha kumepelekea Kamati kuamini kuwa bado hakuna mpango/mkakati madhubuti wa Serikali katika kutekeleza jukumu la kufufua viwanda vilivyobinafsishwa. Kamati inaishauri Serikali kuandaa mpango/mkakati madhubuti na ikiwezekana iundwe Tume Maalumu ambayo itasimamia kwa ukaribu na umakini eneo hili.

**v) Uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali**

**Mheshimiwa Spika**, madhumuni ya kuanzishwa kwa Mfuko wa NEDF ni kuweza kuwasaidia wajasiriamali kupata mitaji itakayowawezesha kuanzisha na kukuza biashara zao. Chanzo kikuu cha mapato ya mfuko huo ni ruzuku kutoka Serikalini na riba zitokanazo na mikopo inayotolewa na mfuko. Lakini kwa miaka Saba (7) mfululizo Serikali imekuwa haipaleki kiasi kinachoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya mfuko huo, jambo linalopelekea mtaji wa mfuko huo kukua kwa kiasi kidogo sana hali ambayo inapelekea kuendelea kuwashudumia wahitaji wachache. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kiasi kinachotengwa kwa ajili ya mfuko huo kinapelekwa tena kwa wakati ili kuwezesha mfuko huo

kuongeza mtaji wake na kuongeza idadi ya wanufaika wa huduma ya mfuko huo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia inaishauri Serikali kuangalia namna ya kuupatia mfuko huo mtaji wa kutosha ili kuweza kuuondoa katika utegemezi wa ruzuku za kila mwaka.

**vi) Mfumo wa Uratibu wa kodi wa kielektroniki (Electronic Tax System - ETS)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na malalamiko ya wawekezaji wenye viwanda juu ya gharama iliyoambatana na Mfumo wa Kodi wa Kielektroniki, gharama hizo ni kubwa na zinaenda kuongeza gharama za uzalishaji. Mfano juisi ya kijoti inayotengenezwa na Bakharesa inalipa kodi TRA shilingi 3 lakini italipa gharama ya ETS shilingi 9, maelezo haya yanamaanisha kwamba tutatumia shilingi 9 kukusanya shilingi 3 jambo ambalo haliko sawa kabisa. Gharama hizi zitakuwa na madhara katika vipengele viwili ambavyo ni:-

- Itaongeza gharama za uzalishaji ambazo zitaenda kutolewa katika *running cost* hivyo kupunguza mapato ya TRA; na
- Pia, itaongeza gharama za bidhaa ambayo inaenda kubebwa na mlaji lakini pia itapelekea kuzitoa bidhaa zetu katika ushindani sokoni.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubaliana na nia nzuri ya Serikali ya kuanzisha mfumo wa ETS kwa kuwa mfumo utaleta uwazi na kuondoa wafanyabishara wasio waaminifu wanaodanganya mahesabu ya kodi. Lakini Kamati inaendelea kuishauri Serikali kukaa chini na viwanda vilivyotumika kama mfano, Kampuni iliyotumika kuandaa mfumo wa ETS (SIPCA) na kufanya mazungumzo juu ya changamoto zilizobainika kuambatana na mfumo kisha kuzitatua kabla haujaanza kutumika rasmi na wadau wote.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, Kamati imeshuhudia mashine za mfumo huu na kubaini kuwa teknolojia iliyotumika si kubwa/

ngeni sana na inaweza kuzalishwa hapa nchini badala ya kutumia mshauri kutoka nje kama inavyofanyika sasa. Kamati inaishauri Serikali baada ya kufanya majadiliano ya bei na SIPCA na ikitokea wameshindwa kukubaliana kurekebisha changamoto zilizopo ikiwa ni pamoja na kupunguza bei, ni vema Serikali ikaamua kuwatumia wataalamu wetu wa ndani (TTCL) kuandaa mfumo mwengine ambao utakua wa bei nafuu na wa manufaa kwa pande zote yaani Serikali, walaji na wenye viwanda. Hatua hii ifanyike kabla ya mfumo huu kwenda kutumika kwa viwanda vyote.

#### **vii) Wingi wa Taasisi za Udhibiti**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilipokea malalamiko juu ya uwepo wa mamlaka nyangi za udhibiti tena zisizofanya kazi kwa pamoja, jambo linalopelekea kuonekana ni kero kwa wafanyabiashara na wenye viwanda. **Kwa kuwa**, Wizara ya Viwanda na Biashara ndio wizara mama katika usimamizi wa Sekta za Viwanda na Biashara. **Na kwa kuwa**, Mamlaka hizo pamoja na kuwa katika wizara tofauti lakini bado zinasimamia Sekta ya Viwanda na Biashara. **Hivyo basi** Kamati inaishauri Serikali kuzifanya taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuwa ndio waratibu wakuu wa Sekta ya Viwanda na Biashara na kuwa taarifa zote za Sekta hiyo, pindi zitakapohitajika na mamlaka taasisi zote zinazofanyakazi zinazoshabihiana na taasisi za udhibiti zilizopo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara ziombwe kwa Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mfano TFDA atumie taarifa za TBS kutoa kibali na Mkemia Mkuu atumie taarifa za TBS kujua aina na ubora wa bidhaa inayoingia bandarini. Hatua hiyo itapunguza ghamrama kwa wafanyabiashara na wenye viwanda, pia itaondoa kero ya kukaguliwa zaidi ya mara moja. Aidha, hatua hii iende sambamba na kuziboresha taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kuzipatia wafanyakazi wenyetaaluma stahiki na kuboresha mishahara yao; kuwapatia vitendea kazi; na kuwawezesha kupata mafunzo ya mara kwa mara kwa ajili ya kuhuisha utaalamu wao.

viii) Muingiliano wa Majukumu ya Taasisi za Utafiti zilizopo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifuatilia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi za Utafiti zilizopo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara ikiwepo Taasisi ya TEMDO, CAMARTEC, na TIRDO na kubaini kuwa majukumu ya taasisi hizi yanashabihiyana. Kamati inaishauri Serikali kuangalia namna ya kufanya marejeo ya Sheria za uundaji wa taasisi hizo na kuangalia namna ya kuziunganisha na kuziweka chini ya uongozi mmoja na zikiwa zinaendelea kutekeleza majukumu ya asili waliyopangiwa. Hatua hii itasaidia kupunguza gharama za uendeshaji na kuleta ufanisi kwani wataweza kushirikiana.

ix) Bidhaa ya Ngozi

**Mheshimiwa Spika**, katika kufuatilia utekelezaji wa malengo/ kazi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Kamati iliarifiwa kuwa Wizara ya Viwanda na Biashara ilifanya tathimini ya Sekta ya Ngozi na Bidhaa za ngozi nchini. **Kwa kuwa** tathimini hiyo imeainisha uwezo wa viwanda vya ndani na kubainisha mahitaji halisi ya viwanda hivyo na kiasi kinachosalia. **Hivyo basi** Kamati inaishauri Serikali kutumia matokeo tathimini hiyo kufanya mazungumzo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki yatakayosaidia kuondoa kizuizi kilichowekwa juu ya uuza ji wa malighafi ya ngozi nje ya Jumuiya. Serikali ishawishi uwekwe utaratibu ambao viwanda vya ndani vitapewa kipaumbele cha kupata malighafi kwanza na kisha kiasi kilichosalia kiweze kuuzwa nje ya nchi. Tanzania ni nchi iliyobarikiwa na idadi kubwa ya mifugo Afrika na ngozi ni kati ya bidhaa zilizokuwa zikiongozwa kwa kuuzwa sana nje ya nchi na kuiingizia nchi fedha nydingi za kigeni, hivyo ni vema tukaitumia fursa hii vizuri.

x) Uzamani wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya Mwaka 1996-2020

**Mheshimiwa Spika**, Sera hiyo iliandaliwa kipindi ambacho Nchi haikuwa na mipango ya ujenzi wa viwanda iliyopo sasa hivi hivyo kuifanya isijitosheleze, Kamati inatambua kuwa

Serikali ipo katika mapitio ya Sera hiyo. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha Sera inayokwenda kuandaliwa itoe nguvu kwa Wizara ya Viwanda na Biashara kusimamia masuala ya viwanda na yale masuala mtambuka yanayohusika moja kwa moja katika kuhudumia ujenzi wa Viwanda. Sera hiyo iwe na kauli juu ya upatikanaji wa huduma zote ambazo zinahusika katika ujenzi wa viwanda. Mfano upatikanaji wa vibali vya uwekezaji, upatikanaji wa ardhi ya uwekezaji, upatikanaji wa vibali vya kufanyakazi nchini, upatikanaji wa huduma za maji, umeme na usafiri (barabara na reli).

#### **xii) Sekta ya Sukari**

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Sukari imegubikwa na malalamiko juu ya viwango vya sukari inayoingia nchini ukilinganisha na mahitaji halisi ya nchi. Kamati inaishauri Serikali kuweka umakini mkubwa wakati wa kutoa vibali vya kuingiza sukari nchini na kuwa vibali hivyo vitolewe baada ya Serikali kufanya tathimini na kubaini upungufu wa sukari uliopo (*Gap Sugar*).

#### **xii) Sekta ya Mafuta ya Kula**

**Mheshimiwa Spika**, mahitaji ya bidhaa ya mafuta kula nchini ni tani 700,000 na uzalishaji wa bidhaa hii hapa nchini ni tani 210,000. Takwimu hizi zinadhihirisha kuwa ili kukidhi mahitaji ya soko ni lazima tofauti iliyopo iruhusiwe kuingia kutoka nje ya nchi. Changamoto ni kwamba viwanda vya mafuta ya kula nchini vinavyoingiza mafuta kutoka nje ya nchi vimekumbana na changamoto ya mgongano wa maamuzi baina ya mamlaka za udhibiti juu ya vipimo vinavyobainisha aina ya mafuta yaliyoingizwa jambo linalopelekea ucheleweshaji wa kutoa mafuta haya bandarini na kuongeza għarama ya *storage*. Kwa sasa Bandarini kuna mzigo wa mafuta wa tani 1500 ambaο umekaa bandarini kwa zaidi ya miezi saba (7) na hali hiyo inatokana na mgongano wa maamuzi uliopo. Kamati inaishauri Serikali kuzisimamia kwa ukaribu mamlaka hizi kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa maslahi mapana ya nchi.

xiii) Mazingira ya kufanyabisahra Nchini

**Mheshimiwa Spika**, kuimarika kwa mazingira ya kufanya biashara nchini ni moja ya chachu ya kukua kwa sekta ya Vivanda na Biashara. Tumeendelea kushuhudia kushuka kwa nafasi ya Tanzania katika orodha ya nchi zenyé mazingira mazuri ya kufanya biashara. Jambo ambalo kwa kiasi kikubwa limechangiwa na changamoto mbalimbali ambazo zimeendelea kulalamikiwa na wafanyabisahara nchini. Changamoto hizo ni pamoja na; -

- a) **Malimbikizo ya Kodi ya Ongezeko la thamani (VAT refund) ambayo hayajarejeshwa kwa wahusika,**

**Mheshimiwa Spika**, taratibu za sheria ya VAT refund ni kuwa fedha hizo zilipashwa kurudishwa ndani ya miezi mitatu lakini kumekuwa na ucheleweshaji ambao umepelekea malimbikizo kuwa makubwa (mwaka wa fedha 2017/18 madai yalikuwa shilingi... na yalilipwa shilingi.... na kwa sasa 2018/2019 yameongezeka na kufikia shilingi bilioni 45), malimbikizo haya yanaathiri mitaji ya wafanyabiashara walio wengi. Kamati inatambua mchakato wa uhakiki uliokuwa unaendelea kufanyika lakini Kamati inashauri kukamilisha mchakato huo na kuanza kurudisha fedha hizo kwa wahusika ili waweze kujiendesha bila kuendelea kukopa katika mabenki au kuendelea kuomba *over draft* ambazo zinaenda kuwaongeza gharama.

- b) **Kuchelewa kurejeshwa kwa Ushuru wa Forodha 15% (refundable import duty 15%) katika Sukari ya Viwandani.**

**Mheshimiwa Spika**, mfumo huu wa ushuru forodha ulianzishwa kwa lengo la kuwasimamia waingizaji wa Sukari ya Viwandani kuhakikisha wanaingiza nchini Sukari kwa kuzingatia mahitaji halisi ya kiwanda, namna uliyopangwa kuendeshwa ni kuwa utatoa 15% ya *import duty* na fedha hizi zitarudishwa mara zinapowasilishwa taarifa ya matumizi ya sukari hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua nia njema ya Serikali ya kuanzisha mfumo huu lakini utekelezaji wake umekuwa

changamoto ambapo kwa mfululizo miaka minne tangia umeanzishwa Serikali imeshindwa kurejesha fedha hizi kwa wahusika jambo lililopelekea kiasi cha mitaji ya wazalishaji yetu kushikiliwa na Serikali na kuwapunguzia mitaji yao. **Kwa kuwa** Serikali inajipanga kuanzisha mfumo wa kodi wa kielektroniki - *ETS*, **na kwa kuwa** utekelezaji wa mfumo wa ushuru wa forodha wa 15% umeonekana kufeli, **hivyo basi** Kamati inaishauri Serikali kuachana na mfumo wa forodha wa 15%, kwa kuwa mfumo wa kodi za kielektroniki utaleta matokeo sawa na yale ya 15%. Sambamba na hilo Serikali ifanye jitihada za makusudi kuhakikisha fedha zinazodaiwa chini ya ushuru wa forodha 15% zinarejeshwa kwa wahusika.

c) **Uingizwaji holela wa Bidhaa ambazo pia zinazalisha hapa nchini,**

**Mheshimiwa Spika**, kuna mapokeo mazuri katika kutekeleza Ujenzi wa Tanzania ya Viwanda ambapo watananza pamoa na wawekezaji kutoka nje ya nchi wamewekeza na kuzalisha bidhaa mbalimbali. Lakini wamekuwa wakikabiliwa na changamoto ya ushindani usio wa haki sokoni unatokana na kwa bidhaa zinazoingia kutoka nje kuuzwa kwa bei nafuu. Mfano viwanda vya chuma, mabomba, mabati vilivyopo nchini vinatosheleza mahitaji ya soko la ndani na ziada inapatikana, lakini bado nchi inaruhusu kuingizwa kwa bidhaa hizo ambazo baadhi ya bidhaa hizo hazina viwango, hali hiyo inapelekeea kuharibu soko la viwanda vyetu vya ndani.

**Mheshimiwa Spika**, kuna haja ya kuvilinda viwanda vyetu vya ndani na jambo hilo lianze kwa kuzipatia *H.S code* ya tofauti kwenye bidhaa zinazosalishwa nchini ili kuweza kuzitofautisha na zinazotoka nje. Baada ya kuzitofautisha kipagwe kiasi kikubwa cha kodi kwa bidhaa zinazoingia nchini hatua hii itaviwezesha viwanda vya ndani ya nchi kushindana katika soko. Hatua hii ianze hasa kwa bidhaa ambazo viwanda vyake vinauwezo wa kuzalisha na kutosheleza mahitaji ya soko la ndani.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia inaishauri Serikali kuhakikisha kwa miradi yote mikubwa inayotekelzwa na Serikali ni vema

ikatumia vifaa vinavyopatikana nchini, sambamba na hilo kwa ile miradi ya ufadhili nchi tuangalie namna ya kuvipatia viwanda vya ndani msamaha wa kodi (*exemption*) ili viweze kushindana na viwanda vya nje katika kupata tenda ya kusambaza (supply) vifaa.

**d) Upangaji wa viwango vya Kodi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuwa makini wakati wa kupanga viwango vya kodi kwa kulinganisha na viwango vya kodi duniani hususani ndani ya Jumuiya za Kikanda ambazo Tanzania ni wanachama. Hatua hiyo itasaidia kuendana na kodi za washirika wetu lakini pia itatuwezesha kushindana katika masoko na kutuondolea hali ya kuwa soko la bidhaa za wenzetu kwani bidhaa zetu za ndani zitakuwa na bei sawa na zile zinazoletwa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, mfano mmoja wapo wa bidhaa ambazo zimeshindwa kushindana katika soko, kutokana na masuala ya kodi ni vyandarua vya kujikinga kutokana na mbu waenezao malaria vinavyozalishwa na Kiwanda cha A To Z Textile Mills LTD. Bidhaa hiyo imepata ithibati ya Shirika la Afya Duniani (WHO) lakini inashindwa kushindana katika soko la ndani. Hali hiyo inatokana na vyandarua vinavyotoka nje ya nchi havitzwi kodi wakati kiwanda hicho kinalipa VAT kwenye malighafi za kutengenezea bidhaa hiyo ya chandarua hivyo kuongeza gharama ya uzalishaji na kupelekea bei ya vyandarua kuwa kubwa ukilinganisha na bei ya vyandarua vinavyotoka nje. Kamati inaishauri Serikali kukipatia Kiwanda hicho ushindani wa haki kwa kukiondolea VAT katika malighafi zinazotumika kutengenezea vyandarua vya kujikinga na mbu waenezao malaria. Vilevile hatua hiyo itasaidia kuokoa ajira za watu zaidi ya elfu tatu (**3000**) walioajiriwa katika kiwanda hicho katika idara ya vyandarua, kwa sababu kipindi hiki kutokana na changamoto ya soko iliyopo sasa idara hiyo ipo katika hati hati ya kufungwa na wafanyakazi hao kupoteza ajira zao.

**e) Kuchelewa taratibu za kupata vibali vya kufanya kazi nchini**

**Mheshimiwa Spika**, katika sekta ya Viwanda kuna badhi ya kada ambazo Tanzania bado hatuna wataalamu wa kutosha

kuzihudumia, jambo hili linapelekea wenyeviwanda kuamua kutafuta wataalamu hao nje ya nchi. Kamati inatambua kuwa kuna utaratibu wa kupata vibali vya kuingia nchini, lakini kuna changamoto kubwa hapa vibali hivi vinachukua muda mrefu (zaidi ya miezi mitatu) na muda wowote vibali hivi vinaweza kufutwa jambo linaloshusha ari ya wawekezaji na hao wataalamu wenyewe.

**Mheshimiwa Spika**, kuelekea Tanzania ya Viwanda tunahitaji teknolojia mpya na iliyօendelea (*modernized technology*), bila kuleta wataalamu watakao turithisha teknolojia hizi hatuwezi fanikiwa. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha vibali vya kazi haviwi kikwazo tena cha kupata teknolojia na ujuzi kutoka nje

**f) Kuchelewa kwa vibali vya shirika la Viwango Tanzania**

**Mheshimiwa Spika**, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linafanya kazi nzuri lakini limezidiwa uwezo mahitaji ya sasa ya soko la Tanzania. Kwa sasa wahitaji wa huduma za TBS wameongezeka lakini Shirika lina uwezo ule ule wa awali jambo linalopelea kuhudumia sampuli nyingi kwa wakati mmoja na kuchelewesha matokeo ya vipimo.

**Mheshimiwa Spika**, ucheleweshaji huu umekuwa kero hususani kwa watumiaji wa bandari ambapo mizigo yao hulazimika kukaa muda mrefu Bandarini hivyo kuwaongezea gharama (*storage cost*). Kamati inaishauri Serikali kuiongezea uwezo TBS kwa kuwaongezea watumishi na kuboresha maslahi yao jambo litakalowaondolea tamaa ya kufanya chochote nje ya utaratibu. Sambamba na hilo Serikali ihakikishe inasimamia ujenzi wa Test House ya TBS kuhakikisha inakamilika, jambo hili litaongeza ufanisi wa Shirika.

**g) Hali ya kutokuwa na uzalendo wa kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini,**

**Mheshimiwa Spika**, Ujenzi wa Tanzania ya Viwanda umepokelewa vizuri sana ambapo kuna viwanda vingi vidogo, vya kati na vikubwa vimeanzishwa. Viwanda hivyo vina uwezo wa kuzalisha bidhaa zenye ubora unaohitajika lakini kumekuwa na kasumba ya watanzania pamoja na

Mamlaka za Serikali kutumia bidhaa kutoka nje ya nchi. Mfano tuna kiwanda cha Bora ambacho ni miongoni mwa viwanda vilivyobinafishwa na kinafanya kazi nzuri sana ya kuzalisha viatu mbalimbali kuanzia kandambili, *sandals, safe boots na boots* za kijeshi.

**Mheshimiwa Spika**, miaka miwili iliyopita kiwanda cha Bora kilipewa changamoto (challenged) na Mheshimiwa Rais ya kuzalisha viatu nya jeshi na kilifaulu kwenye jambo hilo na kuzalisha viatu nya jeshi vizuri na vinavyokidhi viwango. Jambo la kushangaza ni mwaka wa pili sasa Jeshi la Taifa halijawahi kuchukua viatu nya Bora pamoja na kuwa Bora ilishiriki katika tenda za Jeshi zikiwa na bidhaa zinazokidhi viwango na za bei ya chini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuzielekeza Mamlaka zote za Serikali wakati wa kufanya manunuzi kuhakikisha wanatafuta bidhaa hizo nchini kwanza na pindi zinapokosekana ndio ziagizwe nje ya nchi.

*Kamati pia inawahamasisha Waheshimiwa Wabunge kuonyesha uzalendo kwa kutumia bidhaa zetu za kitanzania na inawaomba kuwashawishi wapigakura wetu kuwa Tanzania ya Viwanda inawezekana na tutumie vyakwetu.*

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, naomba nikushukuru sana wewe, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na wenyeviti wote wa Bunge kwa kuendesha Bunge lako tukufu kwa umahiri mkubwa. Vilevile naomba nikushukuru kwa kutupatia maelekezo mbalimbali ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kutoa pongezi nyingi kwa **Mheshimiwa John Pombe Mgufuli**, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutekelza azma ya kujenga Tanzania ya Viwanda kwa vitendo. Kamati inaungamkono juhudhi zake na itaendelea kutoa ushirikiano ili azma hiyo itimie.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kushiriki kikamilifu wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni kuhusu Bajeti ya Wizara hii mbele ya Bunge lako tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini na kwa ruhusa yako naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge (Hansard).

	<b>Mwenyekiti</b>
i) Mhe. Suleiman Ahmed Sadiq,	M/Mwenyekiti
ii) Mhe. Kanal (Mst.) Masoud Ali Khamis, Mb	Mjumbe
iii) Mhe. David Cecil Mwambe, Mb	Mjumbe
iv) Mhe. Gimbi Dotto Masaba, Mb	Mjumbe
v) Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb	Mjumbe
vi) Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma, Mb	Mjumbe
vii) Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb	Mjumbe
viii) Mhe. Munira Mustafa Khatibu, Mb	Mjumbe
ix) Mhe. Musa Rashid Ntimizi, Mb	Mjumbe
x) Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb	Mjumbe
xi) Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb	Mjumbe
xii) Mhe. Kmamis Ali Vuai, Mb	Mjumbe
xiii) Mhe. Zainabu Mndolwa Amiri, Mb	Mjumbe
xiv) Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb	Mjumbe
xv) Mhe. Sylvestry F. Koka, Mb	Mjumbe
xvi) Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb	Mjumbe
xvii) Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb	Mjumbe
xviii) Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb	Mjumbe
xix) Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb	Mjumbe
xx) Mhe. Jafar Sanya Jussa, Mb	Mjumbe
xxi) Mhe. Machano Othman Said, Mb	Mjumbe
xxii) Mhe. Kalanga Julius Laizer, Mb	Mjumbe
xxiii) Mhe. Saed Kubenea, Mb	Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Joseph George Kakunda (Mb), Naibu Waziri wake Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya (Mb), Makatibu Wakuu, pamoja na wataalamu wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa jinsi walivyoshirikiana na kamati katika kujibu hoja za Wajumbe wa Kamati, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha **2018/2019**,

na kufafanua kwa kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha **2019/2020**.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Athumani Hussein, Mkurugenzi msaidizi Sehemu ya Fedha na Uchumi Bw. Michael Chikokoto, makatibu wa Kamati Bi. Zainab Mkamba na Bi Mwajuma Ramadhani pamoja na Msaidizi wa Kamati Bi. Paulina Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu **44** na **60**, kwa Mwaka wa Fedha **2019/2020** kiasi cha shilingi **100,384,738,648** ambapo shilingi **48,884,738,648** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **51,500,000,000** ni kwa ajili matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Suleiman Ahmad Sadiq, (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA**

13 Mei, 2019

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kuwasilisha taarifa ya Kamati. Sasa nimkaribishe Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ili awasilishe maoni ya Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia uhai, afya njema na kunipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu mapitio

ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa malengo ya wizara kwa kipindi cha mwaka 2018/2019. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ya Biashara, Fungu Namba 44 na Fungu Namba 60 ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi 20,006,300,000 na hadi kufikia mwezi Februari, 2019 Wizara ilikuwa imeshakusanya jumla ya Shilingi 8,990,341,969.04 sawa na 44.94% ya lengo tarajija. Aidha, sababu iliyopelekea kushuka kufikia malengo husika kwa Wizara ni makadirio makubwa yaliyokuwa yamewekwa Wizarani hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Randama ya Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2019/2020, katika ukurasa wa 177 inaonesha kwamba Serikali hii ya Hapa Kazi Tu, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 inatarajia kukusanya Shilingi 4,000,000 tu kutoka Fungu Namba 44, zikihusisha uuzaji wa nyaraka za zabuni na marejesho ya mishahara endapo mtumishi ataacha kazi na Shilingi 1,000,000 kutoka Fungu Namba 60, ambazo zinatarajiwa kutokana na makusanyo na mishahara endapo mtumishi ataacha kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno mengine, Wizara hii katika mwaka wa fedha 2019/2020 matarajio ya maduhuli kwa Wizara hii ni Shilingi 5,000,000 tu kwa Fungu Namba 44 na Fungu Namba 60. Huu ni mwendelezo wa kukosa umakini kwa Serikali hii, inawezekanaje tukawa na Wizara ambayo inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 111,473,056,927 wakati Wizara hiyo ikitarajia kukusanya maduhuli ya Shilingi 5,000,000 kwa mwaka mzima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo na matarajio ya Wizara hii umeshuka tofauti na Sh. 20,001,300,000. kama Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara kutoa maelezo kwa nini mapato ya Serikali yanatarajiwa kushuka kwa Shilingi 20,001,300,000 ikiwa ni tofauti kutoka shilingi 20,006,300,000 kwa mwaka wa fedha

2018/2019 hadi kufikia Shilingi 5,000,000 kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nyakati tofauti, Serikali ya Awamu ya Tano imejinasibu kwamba imedhamiria kujenga uchumi wa viwanda ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Hata hivyo, inaelekea kwamba kauli za Serikali ni maneno tu, kwa vile hayaendani na uhalisia, uchumi wa viwanda hauwezi kujengwa kwa maneno matupu bila vitendo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya Serikali inayojinasibu kujenga Tanzania ya uchumi wa Viwanda inashindwa kutoa fedha za maendeleo kwa miradi mbalimbali iliyo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara na kusababisha miradi mingi illyokuwa imepangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kushindwa kutekelezeka na hivyo kuathiri maisha ya Watanzania ambao pamoja na mambo mengine wanatarajiwa kupata ajira kutoka katika miradi hiyo. Hii ndiyo maana halisi ya madai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba bajeti ya Serikali ni bajeti hewa yenye lengo la kuwalaghai Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi iliyotarajiwa kutekelezwa kwa bajeti hiyo hewa, ambayo kwa vyovypote vile itakuwa imeathirika na vitendo cha Serikali kutotekeliza Bajeti yake, ni pamoja na Mradi wa Makaa ya Mawe ya Mchuchuma. Sasa hivi tunafahamu kwamba makaa ya mawe ya Mchuchuma kuna miradi miwili pale, tunataka Serikali ije hapa na kutueleza wazi, wanakwenda kufanya kazi ya kuchimba chuma au *vanadium*, tunataka tusikie ili wananchi waweze kufahamu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliwashukuru wahisani mbalimbali ambao walikuwa wakichangia na kushirikiana na Serikali, baadhi ya wahisani waliotajwa kwenye hotuba ya Waziri 2018/2019 ni pamoja na Benki ya Dunia, JICA, KOICA, GIZ, Serikali ya Uswisi, Taasisi za Umoja wa Mataifa ambazo ni UNIDO, UNDP, UNCTAD, UNWOMEN, ILO, EIF, EU, TMEA na

*USAID.* Wakati hawa ni wahisani wetu kama Taifa, kuna jambo la kushtusha na kushangaza hasa katika Serikali hii ukurasa wa 24 wa randama unaonesha kwamba wahisani hawakutoa hata senti tano. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kuwaambia Watanzania ni jambo gani limetokea kati ya wafadhili wa Serikali kwa sababu haiwezekani wafadhili ambao wamekuwa wakisaidia ghafla na wote kwa pamoja washindwe kutoa fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali kwa ajili ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali ya Chama cha Mapinduzi ikijinasibu kwamba ujenzi wa uchumi wa viwanda lilikuwa ni chaguo mahsus na azma ya viongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano, azma hiyo ni lazima ipimwe katika utekelezaji wa shughuli za Serikali ili Watanzania na dunia nzima waone kama kweli mwenendo huu wa Serikali utafikisha Tanzania katika uchumi wa kati unaotajwa na viwanda itakapofikia mwaka 2025. Mashaka haya yanatokana na hali mbaya ya utekelezwaji wa miradi ya maendeleo kwa Wizara ambayo ndiyo uti wa mgongo kufikia azma tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la upungufu wa fedha za bajeti Wizara ya Viwanda na Biashara. Takwimu za Wizara zinaonesha kushuka kwa bajeti iliyotengwa kwa Wizara hii ili kugharamia miradi ya maendeleo. Mathalani, mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ilitengewa jumla ya Shilingi 97,500,000,000 fedha kutoka ndani na nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara imetengewa jumla ya Shilingi 51,500,000,000 kwa shughuli za miradi ya maendeleo, fedha ambazo ni pungufu kwa zaidi ya Shilingi 46,000,000,000. Je, kwa mwenendo huu sekta ya maendeleo ya viwanda nchini inatekelezeka? Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kuliambia Bunge lako Tukufu na Watanzania sababu za Serikali kushindwa kutoa fedha za maendeleo kama zilivyoidhinishwa na Bunge lako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Namba 60 kwa mwaka wa fedha unaomalizika zilitengewa jumla ya Shilingi

7,000,000,000. Fedha za maendeleo wakati mwaka wa fedha 2019/2020 Fungu hili halijatengewa hata senti moja kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaomba ufanuzi kutoka Serikalini kuhusu miradi ambayo haikukamiliika katika Fungu Namba 60 kutokana na kutopatikana kwa fedha katika mwaka wa fedha 2018/2019 itatekelezwa kwa fedha zifi ikiwa Serikali haijatenga fedha yoyote kwa ajili ya miradi hiyo au iliambie Bunge hili kwamba miradi hiyo haitatekelezwa tena na liwe wazi mbele ya wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachia mbali na Mpango wa Serikali wa Miaka Mitano ambao unazungumzia kidogo uchumi wa viwanda, Waziri wa Viwanda na Biashara hajawahi kusikika hata siku moja kwenye Bunge lako tukufu wala kuleta mpango wa ujenzi wa viwanda na namna uzalishwaji wa masoko utakavyofanyika. Aidha, yapo maelekezo yaliyotolewa kwa Wakuu wa Mikoa kuhusisha kuwa kila Mkoa utajenga viwanda 100 kwa mwaka mmoja. Haijaleezwa ni viwanda vya namna gani vinaenda kujengwa kwa tafiti zifi za masoko ya bidhaa zitakazozalishwa viwandani huko. Taarifa ya Jarida la *The Economist Intelligence Unit* ya tarehe 17 Januari, 2018 inaonesha kuwa pamoja na Serikali kueleza kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kuwa itajikita kwenye uchumi wa viwanda na kutengeneza ajira, ongezeko la kodi na kubadilisha kwa ghafla kwa mifumo ya usimamizi wa biashara inayofanywa na Serikali yameathiri ukuaji wa uchumi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufungamanisha kilimo na maendeleo ya viwanda (*Agro Economy*). Katika bajeti ya Serikali 2018/2019, imeainisha sekta ya kilimo kama kipaumbele cha Serikali lakini haijaonesha ni kwa namna gani hasa inalenga kufanya Mapinduzi ya Kilimo (*Agrarian Revolution*) ili kuweza kusisimua na sekta ya viwanda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa hotuba ya Mpango ya Waziri inaonesha kuwa katika Pato la Taifa kilimo kilichangia asilimia 30.1 mwaka wa fedha 2017 huku sekta hiyo ikichangia utoaji wa ajira kwa asilimia 66 lakini ukuaji

wake ni wa wastani wa asilimia 3.7. Katika kujuliza sekta hiyo ambayo inatoa ajira asilimia 66 inachangia mapato ya kodi kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuangalia unyeti wa sekta hii katika kuifanya kuwa nchi ya kipato cha kati na uchumi wa viwanda ni lazima sekta ya kilimo iwe ndiyo *engine* ya kutupeleka huko. Hivyo basi, pamoja na mambo mengine Kambi Rasmi ya Upinzani inalenga kuondoa kodi zote kwenye uwekezaji katika sekta ya kilimo (kilimo, uvuvi pamoja na mifugo). Hii ni pamoja na kuondoa kodi kwenye uingizaji wa mashine mbalimbali zinazoingia katika mnyororo wa uongezaji wa thamani za kilimo, mifugo na uvuvi, viwanda vinavyotengeneza na kukarabati mashine na zana nyngine za kilimo kama vile matrekta, pampu za umwagiliaji, mashine za uvunaji, viwanda vya kutengeneza madawa, mbolea, mbegu na vifungashio na zana za uvuvi kama vile mitumbwi, nyavu na zana nyngine za uvuaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Shirika la Fedha Duniani ya Januari 2018 kuhusu mapitio ya saba ya Mwongozo wa Sera ya Viwanda Tanzania imeeleza pamoja na mambo mengine, pamoja na pato la taifa kuonekana kukua mazingira ya biashara nchini sio rafiki kwa uwekezaji maendeleo ya biashara. Kutokana na hali hiyo sasa, inaonekana dhahiri kuwa shughuli za kiuchumi ni dhaifu na hivyo kupelekea kushindwa kuzalisha ajira na kupunguza umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kueleza kuwa pamoja na taarifa za biashara nyngi kufungwa, ambayo tulieleza kwa kirefu wakati uliopita, Waziri wa Fedha alijibu kwa idadi ya biashara mpya zilizofunguliwa na kueleza kwa *propaganda* kuwa zilizofungwa zilikuwa zinahusishwa na ukwepajji kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufungwa kwa biashara nchini siyo jambo la kushangilia kwa sababu ni dhahiri kuwa wafanyabiashara hao walikuwa wanalipa na hivyo

kuongezeka kwa makusanyo. *IMF* wameeleza kuwa makusanyo ya kodi yameshuka tofauti na jinsi ilivyokuwa inategemewa na hivyo kupelekea utekelezaji wa bajeti ya Serikali kuwa dhaifu. Kwa kutumia nafasi hii pia tuwape pole wafanyabiashara wa Mtwara zaidi ya 100 ambao jana nao wamefunga biashara zao na kurudisha leseni *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufika mwezi Septemba mwaka 2017 mikopo isiyolipika katika mabenki ya biashara iliongezeka kutoka asilimia 9.1 hadi 12.5. Hii ilipelekea mabenki nchini kupata hasara kubwa jambo ambalo halijawahi kutokea toka mwaka 2007. Pamoja na juhudzi za Benki Kuu kupunguza kima cha chini cha fedha zinazohitajika kifidiwa na kuhifadhiwa na Benki za Biashara nchini pamoja na kushusha kiwango cha riba, bado sekta hiyo inafanya vibaya na hivyo kuathiri mazingira ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haiwezi kukusanya kodi ya kutosha kama mazingira ya biashara na sekta za kodi ziko hovyo. Aidha, Serikali haitapiga hatua kama maamuzi ya namna ya kuboresha biashara yatafanywa Serikali Kuu bila hata kuzingatia uhalisia wa mazingira ya kibiashara. Ikumbukwe kuwa Serikali imejinasibu kupunguza matumizi ya kawaida kwa ajili ya kubana matumizi. Jambo hili ni jema hasa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo pia malalamiko ya wazabuni ambao walikuwa na madeni na Serikali kwa sababu ya huduma au bidhaa ambazo walihudumia katika taasisi mbalimbali za Serikali ambao hawajalipwa na bado wanasema wanafanya uhakiki madeni wa hayo kama ni halisi. Wahanga wa uhakiki huu ni wafanyabiashara ambapo pamoja na kushindwa kufanya biashara kwa sababu za madeni, hata madeni hayo yakilipwa bado hayalipwi kulingana na bei ya soko au kuangalia na thamani ya shilingi yetu ambayo bado imekuwa inasuasua. Tunataka Serikali iseme wazi, ni lini watamaliza kufanya uhakiki ili kuweza kuwalipa wafanyabiashara wanaoidai Serikali kwa sababu nao wanadaiwa na Benki ama vingenevyo Serikali itoe

maelekezo kusimamisha pia na riba kwenye mabenki hayo ikiwemo pamoja na wafanyabiashara wa korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu uwekezaji wa miundombinu na ushirikishwaji hafifu wa Sekta Binafsi. Serikali inafanya uwekezaji mkubwa kwenye reli ya *Standard Gauge Railway (SGR)*, mradi wa umeme wa *Stiegler's Gorge*, bomba la mafuta kutoka Hoima mpakani mwa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara kadhaa Mheshimiwa Rais Dkt. John Magufuli anasikika akisema kuwa miradi hiyo inagharamiwa na fedha za ndani za walipa kodi na wakati mwingine Waziri wa Fedha ananukuliwa akisema kuwa miradi hiyo inagharamiwa na fedha za mikopo mbalimbali. Hata hivyo, kutokuwa wazi kuhusu gharama za miradi mikubwa na muda wa kukamilisha miradi hiyo kunazua sintofahamu kuhusu uwezekano wa kumaliza miradi hiyo mikubwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kuwa kama Serikali haitashirikisha Sekta Binafsi kupitia ubia (*PPP*) wachambuzi wa uchumi wameshauri kuwa deni la Taifa litaendelea kukua na kuwa mzigo kwa walipa kodi wa nchi hii. Aidha, ikumbukwe kuwa Serikali imekua ikikopa sana ndani na hivyo kutengeneza ushindani wa wawekezaji wa ndani ambao pia wanatumia mikopo kuendeleza biashara zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi ndiyo utachochaea mazingira ya biashara na mzunguko wa fedha nchini, bali pia itaipunguzia Serikali mzigo wa kuwekeza kwenye kila mradi mkubwa, jambo ambalo linasababisha ugumu katika kupata mikopo yenye masharti nafuu kutoka nje na kuepuka Serikali kukopa sana ndani kugharamia miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu athari za kiuchumi kutokana na kusitishwa Mradi wa Ukanda Maalumu wa Kiuchumi wa Bagamoyo (*Bagamoyo SEZ*). Serikali imetangaza kusisitiza mradi mkubwa wa Ukanda Maalumu wa kiuchumi wa Bagamayo...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, subiri kidogo. Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Jenista.

### KUHUSU UTARATIBU

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sana ya msomaji anayeendelea kusoma kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani anakwenda kuanza eneo ambalo kabla hajaendelea ninaomba nilitolee utaratibu kwa mujibu wa Kanuni ya 67(1) na Kanuni ya 64(1) kifungu cha (a), Kanuni ya 63(4), Kanuni ya 58(8); na ninamwomba atakapofika kifungu chake cha 54 mpaka cha 71, kwa heshima ya kiti chako ninaomba maneno hayo yaondolewe na yasisomwe ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazo hoja za msingi ninapoweka jambo hili mbele ya meza yako. Nitasema maeneo machache ya kuashiria ni kwa nini ninataka vifungu hivyo viondolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja ambayo anataka kuendelea nayo kwa sasa anapofika kifungu cha 54, msomaji anataka kuliarifu Bunge kwenye mradi amba anataka kuusema sasa kwamba anazo taarifa kwamba Taasisi za Kimataifa zimeingia katika vita kusaidia nchi zenyen guvu duniani, kwa mfano, Benki ya Dunia na Taasisi nyingine za namna hiyo na anataka...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa naomba tutulie, tusikilize kuhusu utaratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda na utaratibu wa Kikanuni. Kanuni ya

63(4) inanitaka ninapotaka kuthibitisha uongo wa msemaji, lazima mimi nieleze ni kwa nini ninathibitisha kinachosemwa ni uongo. Kwa hiyo, ninakwenda kwa mujibu wa kanuni; na ninaomba sana wenzetu upande wa pili tunapowasikiliza na wao wawe wana tabia ya kusikiliza na hiyo pia ni kwa mujibu wa kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kweli, mimi ni Mjumbe wa Baraza la Mawaziri na jana Waziri mwenye dhamana ya miundombinu amelieza jambo hili vizuri. Siyo kweli kwamba Benki ya Dunia imetushawishi tukatae mradi wa Bagamoyo eti kwa sababu Benki ya Dunia inaikopesha nchi yetu katika kutekeleza miradi mbalimbali na hivyo Benki ya Dunia na Taasisi nydingine za Kimataifa zimeshawishi Serikali yetu na tumeingia mkenge kwa ushawishi wa taasisi hizo za Kimataifa na kufuta mradi wa Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kweli na kama msemaji anao ushahidi wa Taasisi hizo tena azitaje zilizotushawishi ikiwemo Benki ya Dunia. Asipotaka kuyaondoa maeneo niliyoyasema, anatakia aje kulithibitisha Bunge lako kwamba ana uhakika wa jambo hilo analosema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa Kambi ya Upinzani anatuambia kwamba anazo taarifa kwamba mradi huu umeingiliwa na utashi wa kisasa na anasema kwamba ni kwa sababu mradi huu ulianzishwa na Serikali ya Awamu ya Nne na anasema kwa kuonesha kuwa Rais aliyepitisha mradi huo anatoka Mkoa wa Pwani na hivyo imesababisha mradi huo kwenda Bagamoyo na ni kwamba alijipendelea na anasema anazo taarifa; vikao vya Baraza la Mawaziri vya mwanzo, utawala wa Awamu ya Tano vilifuta mradi huo kwa sababu hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Msemaji, mimi ni Mjumbe wa Baraza la Mawaziri, hatujafuta mradi huo eti kwa sababu ulianzishwa na Rais aliyetoka kwa sababu ya kujipendelea na kupeleka mradi huo Bagamoyo alikotokea. Nitaomba taarifa hizo alikozitoa kwamba kwenye vikao vya Baraza la Mawaziri tulizungumza mambo hayo, alithibitishie

Bunge hili na aje atuambie kama kweli Serikali hii illifanya hayo maamuzi kwa sababu mradi huu umepelekwa na Rais aliyepita kule nyumbani kwake na hivyo ni suala la upendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, anaendelea kusema tu, huko kote nimekwambia lazima tuondoe. Kwamba...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tutulizane amalizie. Mheshimiwa Jenista, maliza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa namheshimu sana *Chief Whip* wa upande wa pili na hivyo, nami naomba nipewe heshima yangu kama *Chief Whip* wa Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge na hilo ni jambo la heshima tu. Kwenye kifungu cha 69 ni lazima nitii Kanuni ya 63(4). Anaendelea kusema kwamba mradi huu unasababisha kupoteza heshima yetu ya Kimataifa na kupoteza marafiki wetu wa nchi ya China na Oman. Maneno haya ni ya fitina na kutuharibia mahusiano ya kidiplomasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunazo taarifa hapa na Wabunge ni mashahidi, urafiki wetu na nchi hizi ni mkubwa na mahusiano yetu ni makubwa kweli kweli. Ni hivi juzi tu kwa mfano, Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwinyi, Serikali ya China imeingia mkataba wa kujenga chuo kikubwa kabisa cha ulinzi katika Taifa letu. Kwenye eneo hilo bado wanasesma kwamba sisi tuna hofu ya mambo ya ulinzi na usalama. Siyo kweli, maneno hayo ni uchonganishi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna watalii zaidi ya 10,000 na tumewapokea kama 300 na kitu kutoka China, ni mahusiano mazuri ya kidiplomasia ambayo tumeendelea kuwa nayo na mikataba mingine mingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa, ninaamini kabisa nia njema ya Kambi ya Upinzani kutukumbusha kwamba pamoja na yote yanayojiri, mradi huu ni mradi wa msingi na ni mradi wa kimkakati, lakini maneno yaliyotumiwa ninaomba nirudie kutoka kifungu cha 54 mpaka cha 71, hayana nia njema ya kutujenga bali ni kutuchonganisha na kutufitinisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa heshima kubwa maneno hayo yaondolewe ama Kambi ya Upinzani msomaji anayesema awe tayari kuja kuthibitisha moja baada ya lingine kwa kuzingatia taratibu na kanuni za Bunge. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Haya. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa *Chief Whip*, Mheshimiwa Jenista ametoa Kuhusu Utaratibu kwa mujibu wa kanuni ya 67(1), 64(1) a, 63(4) na 58 ambazo zote zinakwenda sambamba katika kutaka kutoa taarifa zilizo sahihi ndani ya Bunge. Kwa hiyo, kutokana na kwamba yeye ni Mjumbe wa Baraza la Mawaziri na amelithibitishia Bunge hili kwamba kuanzia kifungu cha 54 hadi 71 vinaashiria uchochezi na siyo vinaashiria uchochezi wa Kitaifa tu hadi wa Kimataifa, kwa hiyo, naagiza vifungu hivyo vyote uvifute na uendelee na vifungu vingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Cecil Mwambe, naomba uendelee kifungu cha 73, masuala ya Sera ya Kodi na Urasimu yanavyoathiri biashara nchini.

**MHE. CECIL D. MWAMBE - K.n.y. MSEMADI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kwanza nimshukuru *Chief Whip* kwa kutukumbusha kanuni, lakini ninaamini amefanya pia kazi ya kusoma. Kwa hiyo, ile sehemu ambayo nilitakiwa niifanye, mimi nasoma, naomba unielekeze niende ukurasa gani? (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, endelea. Hayo yameshapita. Naomba uendelee na Kifungu cha 73 ukurasa wa 27.

**MHE. CECIL D. MWAMBE - K.n.y. MSEMADI WA KAMBI  
YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA VIWANDA NA  
BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu masuala la Sera ya Kodi na Urasimu unaoathiri biashara nchini. Mpango wa maendeleo wa miaka mitano unazungumzia na kuonesha ahadi ya Serikali kujenga mazingira mazuri kwa ajili ya ukuaji wa sekta binafsi nchini. Kinachotokea kwa sasa ni Serikali kutaka kumkamua ng'ombe maziwa ambaye hamjampeleka kwenye malisho yenyе majani ambayo yatamfanya ng'ombe huyo kuzalisha maziwa ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ndivyo Serikali inavyofanya kwa wafanyabishara nchini, ambapo Serikali inawahimiza kulipa kodi ya maendeleo, jambo ambalo ni jema, lakini haijaweka mazingira mazuri kwa ajili ya ukuaji wa biashara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya Benki ya Dunia kuhusu urahisi wa kufanya biashara duniani, Tanzania imekuwa nchi ya 137 kati ya nchi 190 duniani na moja ya changamoto zilizotajwa ni pamoja na masuala ya kodi ambazo siyo rafiki, kufanya biashara mpakani na ugumu katika uanzishaji wa biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila wakati Serikali hii inapokosolewa Kiongozi Mkuu wa Nchi amekuwa akinukuliwa akisema kuwa wanautoa ukosoaji huo na wanaupokea na wanatumwa na mabeberu jambo ambalo linaonyesha kuwa bado tunao viongozi ambao wanafikiria kijamaa kuliko kufikiria katika nyanja za utandawazi na kukua kwa sekta binafsi. Ni lazima Serikali ijue kuwa haiwezi kuirudisha nchi kwenye Ujamaa kama inavyozungumza lugha za kijamaa. Kama Taifa, tulishatoka kwenye zama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutofumbia macho upungufu huu uliopo wa

mazingira ya kufanya biashara. Ni vyema kama wanahitaji makusanyo mazuri ya kodi watatue changamoto zinazowakumba wafanyabiashara kuliko kujikita zaidi kwenye ukusanyaji wa kodi bila kuweka mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara kufanya biashara nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ieleweke kuwa zipo pia changamoto za kimazingira ambazo kama nchi tutakumbana nazo katika kile ambacho Serikali hii inakiita uchumi wa viwanda. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa Serikali hii inacheza ngoma ambayo hajafanyiwa utafiti wa kutosha na kuhusu uanzishwaji na uendeshaji wa viwanda nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu uhitaji wa maboresho katika Shirika la Huduma ya Viwanda Vidogo (*SIDO*). Majukumu ya shirika hili ni pamoja na uendelezaji wa teknolojia, kutoa mafunzo na huduma za ugani, kusimamia masuala ya masoko na habari na huduma za fedha. Katika uendelezaji wa teknolojia, *SIDO* ina upungufu mkubwa kwa sababu ilitegemewa kuzalisha mashine mbalimbali kuitia vituo vyao vya kuzalisha mashine (karakana) lakini mpaka sasa ni Mikoa saba tu yenye vituo vya kuzalishia mashine ambayo ni Iringa, Mbeya, Kigoma, Lindi, Arusha, Shinyanga na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uwezo wa karakana hizo, mashine zake siyo za kisasa na zinahitaji kuboreshwa. Mikoa iliyobaki inategemea wajasiriamali wanaozalisha mashine hizo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa *SIDO* inakuwa na karakana katika mikoa iliyosalia ili kuwa mfano kwa wajasiriamali wengine nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu changamoto za Sekta ya Viwanda Nchini Tanzania, Serikali kushindwa kurejesha malipo ya VAT na VAT Refund. Wazalishaji wengi hivi sasa wanapata changamoto za mitaji inayotokana na malimbikizo ya VAT inayolipwa Serikali. Ikumbukwe kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Mapato,

Ongezeko la Thamani (*Value Added Tax Act, 2014*), viwanda vinavyosafirisha bidhaa na kununua malighafi kutoka nje ya nchi vinapaswa kulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*), kodi ambayo inapaswa kurejeshwa kwa walipaji ndani ya kipindi cha miezi mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kusikitisha na kukatisha tamaa kwa wafanyabiashara hawa, malimbikizo ya fedha hizo zilizolipwa hazijarejeshwa kwa zaidi ya miaka mitatu sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara viwandani sasa wanadai kurejeshewa zaidi ya shilingi bilioni 45 kutoka kwa Serikali kwa zaidi ya miaka mitatu. Kitendo cha Serikali kushindwa kurejesha fedha hizo kwa wafanyabiashara kinasababisha ongezeko la gherama katika uzalishaji wa bidhaa viwandani na hivyo kuathiri ufanisi na kuathiri uchumi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo hicho kinaathiri sana na kuwakatisha tamaa wazalishaji wa bidhaa zinazozalishwa viwandani kwenda nje ya nchi kwa kuwa mzalishaji anapaswa kulipa fedha nydingine, wakati kwa zaidi ya miaka mitatu amekuwa akilipa lakini Serikali imeshindwa kurejesha fedha hizo kama sheria inavyotaka; na mwisho kitendo cha Serikali kushindwa kurejesha malimbikizo ya *VAT* kinaathiri upatikanaji wa pesa za kigeni. Pia tuikumbushe Serikali kwamba pesa hizi ni za wafanyabiashara na siyo mapato kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwanusuru wafanyabiashara wa viwanda ambao asilimia kubwa walikopa fedha hizo kutoka kwenye taasisi mbalimbali za kifedha zenyetibya kubwa na ili kupunguza gherama za uzalishaji na kuongeza ufanisi wa viwanda, kuhamaisha bidhaa zilizozalishwa hapa nchini kusafirishwa nje ya nchi, masoko na kuliingizia Taifa fedha nydingi za kigeni; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kuliambia Bunge lako Tukufu ni lini itawalipa wazalishaji wenye viwanda madai yao

ya malimbikizo yanayokadiriwa kuzidi shilingi bilioni 45 ili uchumi wa viwanda uonekane kwa vitendo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu kodi kubwa inayotozwa kwenye Ushuru wa Forodha, asilimia 15, sukari ya viwandani. Kuna changamoto nyingine dhidi ya malighafi inayotumika viwandani kutengeneza vinywaji, vyakula na katika viwanda vya kifamasia. Hata hivyo, sukari ya viwandani, siyo Tanzania wala nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinazozalisha malighafi hii. Ikumbukwe kwamba chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki sukari hii hutozwa ushuru wa asilimia 10. Tanzania ni nchi pekee mionganoni mwa nchi za Afrika Mashariki ambayo hutoza asilimia 15 ambayo inapaswa kurejeshwa kwa walipaji (*additional or refundable import duty of 15%*) na hivyo kufanya jumla ya ushuru unaolipwa kuwa asilimia 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia njema ya kudhibiti wafanyabiashara wenye nia ya kuuza malighafi hiyo katika soko la ndani, lakini ukweli ni kwamba ongezeko hilo halizuii chochote kwa kuwa mfanyabiashara anaweza kuingiza akalipa ushuru unaotakiwa na akaiuza katika soko la ndani kwa faida, lakini kwa wazalishaji wa viwandani ambao wanaingiza sukari viwandani kama malighafi za kuzalisha bidhaa, mfumo huu ni mzigo kwao na kuongeza gharama za uzalishaji ndiyo kuongeza taratibu za kiutawala zisizo na ulazima wowote kwa Serikali. Pia tunaikumbusha Serikali kwamba ushuru huu nao siyo mapato ya Serikali, ni pesa za wafanyabiashara, zirudishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hoja hizo lipo tatizo la muda mrefu la kutorejeshwa kwa ushuru huo, kutoka Mamlaka za Mapato (*TRA*), hadi sasa kwa mujibu wa taarifa walizonazo na wamiliki wa viwanda Tanzania *Confederation of Tanzania Industries*, ambazo kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeziona, uagizwaji wa sukari ya viwandani wanadai marejesho ya zaidi ya bilioni 35 kutoka *Tanzania Revenue Authority*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato nchini kwa kushindwa kuwarejeshea waagizaji wa sukari ya viwandani shilingi billioni 35, wamewasababishia hasara ya zaidi ya bilioni 3.5 ambazo wamelazimika kuzilipa kwenye taasisi za fedha yakiwemo mabenki ya biashara kutokana na ucheleweshwaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Changamoto za Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) na malighafi za viwandani nchini! Mfumo wa sasa mpya wa stempu za kielektroniki (*ETS*) ambao ulikusudia kuongeza mapato ya Serikali umeshindwa kutimiza azma hiyo na hauna budi sasa kuondolewa, kama ambavyo hata kamati imeshauri. Taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani inazo, zinaonesha kwamba stempu moja ina gharama ya shilingi nane, lakini Serikali haipati mapato kutokana na fedha hiyo. Taarifa zinadai kwamba kazi ya mwenye tenda ya kutengeneza stempu ni kutoa taarifa kwa Serikali juu ya kiasi cha bidhaa kilichozaishwa na ukiangalia mfumo wa utendaji kazi unagundua kwamba kampuni ya *SIPA* ndiye mnufaikaji kuliko Serikali na hata mapato ya Serikali yameshuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutafakari upya mfumo huu na kuliambia Bunge hili ni mapato kiasi gani Serikali ilikuwa ikipata kutoka katika Makampuni ya Sigara (*TCC*) na Kampuni ya Bia (*TBL*) na makampuni ya vinywaji baridi ikiwemo *Cocacola* Kwanza na mengine, kabla ya mfumo wa *ETS* na kiasi cha mapato ambacho pia inapata baada ya kuanzisha mfumo huo. Pia Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kufuatilia na kuja kueleza hapa wazi kwamba mkandarasi huyo anayezalisha *stamps* hizo alipatikanaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria mpya ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) ya mwaka 2014 iliyoanza kutumika Julai, 2015 iliondoa vyandarua vya kuzuia malaria kutoka jedwali la *ZERO KODI (ZERO RATE)* na kuviweka kwenye jedwali la msamaha wa kodi. Utaratibu huu unavifanya vyandarua vinavyozalishwa nchini kuwa na bei ghali kuliko vyandarua vinavyoingizwa nchini (*imported*) ambavyo havitozwi ushuru

wala kodi. Kwa sheria hii mzalishaji wa ndani ya Tanzania hawezি kurejeshewa malipo ya kodi ya VAT (*import tax*) aliyolipa wakati wa kuagiza malighafi na pia katika mchakato mzima wa kuzalisha umeme na usafirishaji. Kwa vile chandaria hakitozwi VAT malipo hayo ya 18% hubaki kama gharama kwa mzalishaji kwa vyandarua vyote vitakavyotumika nchini ambapo lazima gharama hii iingizwe kwenye bei na hatimaye kutomudu ushindani dhidi ya vyandarua kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ucheweshwaji wa vibali nya kufanya kazi nchini. Mchakato wa kupata vibali nya kufanya kazi nchini kwa waajiriwa kwenye sekta mbalimbali bado ni changamoto kubwa pamoja na matamko mbalimbali ambayo yamekuwa yakinolewa na Idara ya Kazi. Wafanyakazi wanaoajiriwa katika viwanda na maeneo mengine wanalazimika kutumia hadi mlezi mitatu katika kutafuta vibali nya kufanya kazi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kufanya hivyo, hali hii pia inayakumba makampuni ambayo yamesajili chini ya Kituo cha Uwekezaji Nchini (*Tanzania Investment Centre*) na ambayo yanaombewa vibali nya ajira katika kuhakikisha inarahisha mchakato wa kuomba vibali nya ajira nchini kufanya kwa njia ya mtandao yaani *online*, ili kuondoa ukiritimba uliopo na kuharakisha mchakato mzima wa maombi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Taktamu, hadi kufikia mwezi machi, 2018 Tanzania ilikuwa na jumla ya viwanda 53,876 kwa mgawanyo wa viwanda vikubwa 251, viwanda nya kati 173 na viwanda vidogo vikiwa ni 6,957, viwanda vidogo sana vikiwa ni 46,495. Tunachotaka sasa kufahamu, Kambi Rasmi ya Upinzani ijue mchango wa viwanda hivyo tunavyovitaja na uhalsia wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa viwanda Tanzania unategemea kilimo imara na hapa naomba Waheshimiwa Wabunge tusikilizane. Maamuzi ya kutouza Korosho nje ya nchi yameisababisha hasara Serikali zaidi ya

triliuni 1. 8. Wakati Serikali ikifanya hivyo, Serikali hiyo hiyo, mapema mwaka huu, kuitia Bodi ya Nafaka Mchanganyiko (*CPB*) iliingia makubalianao na Kampuni ya *Indo Power* ya Kenya kwa ajili ya ununuzi wa korosho tani 100,000 kwa bei ya Dola za Marekani 180 milioni sawa na TZS 418 bilioni. Hatua ilijili baada ya mipango, mikakati na melekezo ya Serikali kuhusu zao la korosho kushindwa kutekelezeka na kusababisha hasara kubwa kwa wakulima wa zao la korosho ambalo ni zao wanadolitegemea kama zao la biashara. Hata hivyo, miezi minne baadaye Serikali imevunja mkataba na kampuni hiyo kwa kile kinachoelezwa kuwa ni kampuni hiyo kushindwa kutekeleza mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba huo ambao Serikali iliingia, ulisainiwa mbele ya Mawaziri wa Katiba na Sheria, Waziri wa Kilimo, Waziri wa Viwanda na Biashara, lakini pla tunaamini vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vina jukumu katika mikataba hii mikubwa ya kitaifa, taarifa za kwamba kampuni hii imeshindwa kutekeleza vifungu vya kimkataba zinatia ukakasi kwa kuwa ilikuwa ni wajibu wa Serikali hii kwa kutumia vyombo vyake kufanya uchunguzi wa kampuni hiyo, haiingii akili kwamba, Taifa lenye vyombo vya usalama wa Taifa walishindwa kujua uwezo wa kampuni husika. Ni kwa bahati mbaya sana waliotekeleza jambo hili wakiwemo Mawaziri husika wako ofisini utadhani hakuna kilichotokea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na udhaifu huo, matamko na maelekezo ya Serikali kuhusu biashara ya zao la korosho imesababisha hasara kubwa kwa wakulima na Taifa kwa sababu ambazo zingeweza kuepukwa kutohana na sakata hili la zao la kibiashara. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawataka wahusika wote wajitafakari kama wanatosha kuendelea kushika nyadhifa walizonazo ama wanapaswa kupisha ofisi hizo za umma kuongozwa na watu wengine, kwa kuwa maamuzi ya Chama cha Mapinduzi yamelisababishia Taifa hasara ya Dola za kimarekani millioni 500 sawa na Tanzania *Shillings 1.18 trillion* kutohana na maamuzi mabovu ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaitaka Serikali ije hapa na itueleze, ni gharama kiasi gani ambacho Serikali ilitumia kukusanya zao hili la kibashara la korosho kutoka kwa wakulima na kuzipeleka kwenye maghala ya Serikali. Mwisho kabisa pia Serikali itueleze, baada ya gharama zote zilizotumiwa na Serikali, je, Serikali inategemea kuza korosho kwa bei gani na kama wamepata mnunuzi mwingine kwa sababu karibu msimu mwingine wa korosho unaanza tena. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie kifungu hiki, nia ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ni kutaka Mawaziri wote waliohusika na sakata hili la kuliingizia hasara Taifa wajiuuzulu mara moja ili waweze kumsaidia Rais katika kutekeleza wajibu huu mgumu na kuwasaidia wakulima wa korosho na tulishuhudia jana Mkuu wa Mkoa wa Lindi akiwaomba radhi wakulima wa korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo uhusiano wa moja kwa moja kati ya kilimo na uchumi wa viwanda na kwa muktadha huo huo upo uhusiano wa karibu kati ya uchumi wa Viwanda na *ASDP II*. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuhakikisha inaboresha kwanza kilimo na kujielekeza katika viwanda ambavyo vitaongeza thamani katika mazao ya mifugo kama vile nyama, maziwa, ngozi, damu, kwato, pembe na hata kusindika mazao yanayotokana na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero za wafanyabiashara Tanzania kutokana na marejesho kutoka Mamlaka za Mapato Tanzania. Wafanyabiashara mbalimbali hapa nchini wanakumbana na adha kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kipindi kirefu sasa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe, naomba uhitimishe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, naomba nirudie maneno yangu, ambayo

nimeyasema hapo mwanzoni, tunawataka Mawaziri wote waliohusika kulitia hasara Taifa letu wajiuzulu mara moja ili kulisaidia Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na taarifa yangu iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. (*Makof*)

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI  
BUNGENI KATIKA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA,  
MHESHIMIWA ANTONY CALIST KOMU (MB), AKIWASILISHA  
MAPITIO YA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA  
2018/2019 PAMOJA MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI  
KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA,  
KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za  
Bunge, Toleo la Januari, 2016*

---

**A. UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika**, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunijalia uhai, afya njema na kunipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako tukufu ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**2. Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Viwanda na Biashara imeundwa kwa Tangazo la Serikali Na. 144 la tarehe 22 Aprili, 2016 ikiwa na dhamana yenye kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera, maendeleo ya viwanda, biashara na Masoko. Aidha mionganini mwa majukumu ya Wizara hii kama yalivyoainishwa katika Tangazo hilo ni pamoja na kuandaa, kuratibu na kupitia sera na mikakati ya sekta ya viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo, kubuni na kuandaa programu za kuendeleza sekta za

viwanda, biashara, uwekezaji, masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo na taasisi zinazowezesha maendeleo ya viwanda na biashara.

**3. Mheshimiwa Spika**, Wizara hii pia inasimamia mashirika matano ambayo ni Shirika la Maendeleo la Taifa (National Development Corporation – NDC), Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Small Industries Development Organization - SIDO), Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (Tanzania Industrial Research Development Organization - TIRDO), Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania - TEMDO na Shirika la Viwango Tanzania - TBS. Wizara ina kituo cha kuendeleza Teknolojia, biashara na uwekezaji kinacho julikana kama Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijiini, Wakala za Vipimo na Usajili wa Biashara na Leseni, Mamlaka za Kuzalisha Bidhaa na Kuza Nje yaani Export Processing Zone Authority na Maendeleo ya Biashara Tanzania yaani Tanzania Trade Development Authority - TANTRADE. Mabaraza ya Ushindani (Fair Competition Tribunal) na Baraza la Utetezi wa Haki za Mlaji. Hotuba yangu inajielekeza kuangazia ufanisi wa kiutendaji kwa Wizara hii kwa kuzingatia majukumu kama yalivyo idhinishwa na hati idhini ya Serikali. Kwa maana hiyo hotuba yetu inaangazia utendaji wa Wizara hii kwa mujibu wa hati idhini hiyo.

**B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA  
KWA KIPINDI CHA MWAKA 2018/2019**

**4. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara ya Viwanda na Biashara, Fungu 44 & 60 ilipanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni Ishirini, Milioni Sita na Laki Tatu (**20,006,300,000**) na hadi kufikia mwezi Februari, 2019 Wizara ilikuwa imeshakusanya jumla ya shilingi bilioni Name, Milioni Mia Tisa na Tisini, Laki Tatu Arobaini na Moja Elfu Mia Tisa Sitini na Tisa na Senti Nne (**8,990,341,969.04**) sawa na 44.94% ya lengo tarajiwa. Aidha sababu iliyopelekea kushindwa kufikia malengo husika kwa Wizara ni makadirio makubwa yaliyokuwa yamewekwa na Wizara hii.

**5. Mheshimiwa Spika**, Randama ya Bajeti ya Mapato na Matumizi ya fedha za kawaida na za Miradi ya Maendeleo

kwa mwaka 2019/2020, inaonesha katika ukurasa wa 177; kwamba, Serikali hii ya hapa kazi tu,kwa mwaka wa fedha 2019/2020 inatarajia kukusanya Shilingi Milioni Nne, (**4,000,000**) kutoka Fungu 44, zikihusisha uuzaaji wa nyaraka za zabuni na marejesho ya mishahara endapo mtumishi ataacha kazi; na Shilingi Milioni Moja (**1,000,000**) kutoka fungu 60, ambazo zinatarajija kutokana na marejesho ya mishahara endapo mtumishi ataacha kazi. Kwa maneno mengine Wizara hii katika mwaka wa fedha 2019/2020 matarajio ya Maduhuli kwa Wizara hii ni shilingi Milioni Tano (5,000,000)kwa Fungu 44 na Fungu 60. Huu ni mwendelezo wa kukosa umakini kwa Serikali hii, inawezekanaje tukawa na Wizara ambayo inaomba kuidhinishiwa jumla ya Bilioni Mia Moja Kumi na Moja, Milioni Mia Nne Sabini na Tatu, Hamsini na Sita Elfu, Mia Tisa Ishirini na Saba (111,473,056,927) wakati Wizara hiyo ikitarajia kukusanya Maduhuli ya Milioni Tano kwa Mwaka?

**6. Mheshimiwa Spika**, Ushahidi mwingine kwamba Serikali ya Chama Cha Mapinduzi haiwezi tena kuongoza Nchi yetu, unaonekana katika utekelezaji wa bajeti inayopitishwa na Bunge lako Tukufu. Mathalani, Matarajio ya kukusanya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2019/2020 yameshuka kutoka Shilingi bilioni ishirini, Milioni Sita na Laki Tatu (**20,006,300,000**)kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia shilingi Milioni Tano (5,000,000) kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Uwezo na Matarajio ya Wizara hii umeshukwa kwa tofauti ya Shilingi Billioni Ishirini, Milioni Moja na Laki Tatu. (**20,001,300,000.00**). Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara kutoa maelezo kwa nini mapato ya serikali yanatarajija kushuka kwa Shilingi Bilioni Ishirini, Milioni Moja na Laki Tatu (20,001,300,000.00) ikiwa ni tofauti kutoka Shilingi Bilioni Ishirini, Milioni Sita na Laki Tatu(20,006,300,000) kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia Shilingi Milioni Tano (5,000,000) kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**C. KUSHINDWA KUTOLEWA KWA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO**

**7. Mheshimiwa Spika**, Kwa nyakati tofauti serikali ya awamu ya tano imejinasibu kwamba imedhamiria kujenga uchumi

wa viwanda ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Hata hivyo inaelekea kwamba kauli za serikali ni maneno tu, kwa vile hayaendani na uhalisia, uchumi wa viwanda hauwezi kujengwa kwa maneno matupu bila vitendo.

**8. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Randama, uk. 21 Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Fungu 44 & Fungu 60 ilitengewa jumla ya shilingi Bilioni Mia Moja, Milioni Ishirini na Nne, Mia Tano Ishirini na Tano Elfu (100,024,525,000) kwa matumizi ya maendeleo sawa na 70% ya bajeti yote ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni Tisini na Milioni Mia Tano (**90,500,000,000.00**) zilikuwa ni fedha za ndani na Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tano Ishirini na Nne, Laki Tano na Ishirini na Tano Elfu (**2,524,525,000.00**) zilikuwa ni fedha za maendeleo kutoka nje. Hata hivyo, kiasi kilichotengwa ilikuwa ni propaganda tu, na kilikuwa hakina uhalisia wowote kwa kuwa Serikali haikuwa na uwezo huo isipokuwa kulaghai umma wa watanzania. Takwimu za Randama zinaonesha kwamba hadi kufikia mwezi Machi, 2019 kati ya Shilingi Bilioni Tisini na Milioni Mia Tano (**90,500,000,000.00**) zilizokuwa zimetengwakwa matumizi ya maendeleo, Wizara ilikuwa imepokea Shilingi bilioni Sita, Mia Nne Sabini na Saba Milioni Mia Mbili ishirini na Moja elfu, Mia Tatu kumi na Nne(**6,477,221,314**) sawa na 6.5% ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo, kutoka ndani kwa Fungu 44, wakati fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo kutoka Fungu 60, zilikuwa ni Shilingi Bilioni saba (7,000,000,000.00) na hadi kufikia mwezi Machi, 2019 Hazina ilikuwa imetoa shilingi 0.00 sawa na 0% ya fedha za maendeleo kwa Fungu 60.

**9. Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya Serikali inayojinasibu kujenga Tanzania ya uchumi wa Viwanda kushindwa kutoa fedha za maendeleo kwa miradi mbalimbali ilio chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, kumesababisha miradi mingi iliyokuwa imepangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kushindwa kutekelezeka na hivyo kuathiri maisha ya watanzania ambao pamoja na mambo mengine walitarajiwa kupata ajira kutoka katika miradi hiyo. Hii ndiyo

maana halisi ya madai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba Bajeti ya Serikali ni Bajeti hewa yenyе lengo la kuwalaghai watanzania. Miradi iliyotarajiwa kutekelezwa kwa bajeti hiyo hewa, ambayo kwa vyovyote vile itakuwa imeathirika na vitendo cha Serikali kutotekeleza Bajeti yake, ni pamoja na Miradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na Liganga, Special Economic Zone za Bagamoyo, Benjamini Mkapa, EPZ Development, Kurasini SEZ,EPZ katika mikoa ya Kigoma Tanga, Manyara, Mara, Ruvuma, Kiwanda cha Matairia Arusha, Leather Value Addition-Dodoma Cluster na Lake Natron/Engaruka ni mionganoni mwa miradi ambayo watanzania waliaminishwa kwamba ni vipaumbele vilivyozingatiwa katika matumizi ya Maendeleo na Serikali ikaishia kutoa fedha 7.16% tu kwa ajili ya miradi hii.

**10. Mheshimiwa Spika**, Wakati wa kuwasilisha Hotuba yake kwa mwaka wa fedha 2018/2019 aliyekuwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, kama ilivyokuwa kwa kipindi hicho kabla ya kufanyiwa marekebisho na waziri husika kutumbuliwa, Serikali iliwashukuru wahisani mbalimbali ambao walikuwa wakichangia na kushirikiana na Serikali, baadhi ya wahisani waliotajwa katika ukurusa 4, aya ya 12 wa Hotuba ya Waziri ya 2018/2019 ni pamoja na Benki ya Dunia, JICA, KOICA, GIZ, Serikali ya Uswisi, Taasisi za Umoja wa Mataifa ambazo ni UNIDO, UNDP, UNCTAD, UNWOMEN, ILO, EIF, EU, TMEA na USAID. Wakati hawa ni wahisani wetu kama Taifa, kuna jambo la kushitusha na kushangaza hasa katika taarifa ya serikali uk 24 wa randama unaoonesha kwamba wahisani hawakutoa hata senti tano. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kuwaambia watanzania ni jambo gani limetokea kati ya wafadhili na serikali kwa sababu haiwezekani wafadhili ambao wamekuwa wakisaidia ghafla na wote kwa pamoja washindwe kutoa fedha yoyote.

**11. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ilitengewa jumla ya shilingi bilioni Mia Moja Arobaini na Tatu, Mia Tatu Thelathini na Nne Milioni, Mia Moja Hamsini na Tatu Elfu, Mia sita Arobaini na Nane (**143,334,153,648.00**) kwa matumizi ya kawaida ya Wizara na fedha za Miradi ya

Maendeleo na mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara inaomba jumla ya shilingi Bilioni Mia Moja, Milioni Mia Tatu Themanini na Nne, Laki Saba Thelathini na Nane, Mia Sita arobaini na Nane (**100,384,738,648.00**) kwa Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kwa takwimu hizi za Wizara, Fedha hizi ni pungufu kwa shilingi bilioni Arobaini na Mbili, Milioni Mia Tisa Arobaini na Tisa, Laki Nne na Kumi na Tano Elfu (**42,949,415,000.00**). Kutokana na upungufu huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili na watanzania kwa ujumla kauli mbiu ya Tanzania ya Viwanda itatimiaje wakati serikali inapunguza bajeti kila mwaka na ikubaliane na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba Tanzania ya Viwanda inawezekana CCM ikiondoka Madarakani!

**12. Mheshimiwa Spika**, Wakati serikali ya Chama Cha Mapinduzi ikijinasibu kwamba Ujenzi wa uchumi wa viwanda liliikuwa ni chaguo mahsus na azma ya viongozi wa serikali ya awamu ya tano, azma hiyo ni lazima ipimwe katika utekelezaji wa shughuli za serikali ili watanzania na Dunia nzima waone kama kweli kwa mwenendo huu wa serikali ya CCM utalifikisha Taifa katika uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda itakapofikia mwaka 2025. Mashaka haya yanatokana na hali mbaya ya utekelezwaji wa miradi ya maendeleo kwa Wizara ambayo ndiyo uti wa mgongo wa kufikia azma tajwa hapo juu.

**D. UPUNGUFU WA FEDHA ZA BAJETI KWA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA.**

**13. Mheshimiwa Spika**, takwimu za Wizara zinaonesha kushuka kwa bajeti inayotengwa kwa Wizara hii ili kugharamia miradi ya maendeleo, Mathalani kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ilitengewa jumla ya Shilingi Bilioni Tisini na Saba na Millioni Mia Tano (**97,500,000,000.00**) fedha kutoka ndani na nje kwa ajili ya Miradi ya maendeleo, Mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara imetengewa jumla ya Shilingi Bilioni Hamsini na Moja na Millioni Mia Tano (**51,500,000,000.00**) kwa shughuli ya miradi ya maendeleo, fedha ambazo ni pungufu kwa shilingi Bilioni Arobaini na Sita (**46,000,000,000.00**) kwa hali hii Sekta ya Maendeleo ya Viwanda nchini inatekelezeka? Kwa Kambi

Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka serikali kuliambia Bunge lako Tukufu na watanzania sababu za serikali kushindwa kutoa fedha za maendeleo kama zilivyoidhinishwa.

**14. Mheshimiwa Spika**, Fungu 60 kwa mwaka wa fedha unaomalizika ilitengewa jumla ya shilingi bilioni saba (7,000,000,000.00) Fedha za maendeleo wakati mwaka wa fedha 2019/2020 fungu hili halijatengewa hata senti moja kwa ajili ya shughuli za maendeleo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaomba ufanuzi kutoka serikalini kuhusu miradi ambayo haikukamilka katika fungu 60 kutokana na kutopatikana kwa fedha katika mwaka wa fedha 2018/2019 zitatekelezwa kwa fedha zipe ikiwa serikali hajatenga fedha yoyote kwa ajili ya maendeleo katika fungu hili.

**15. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2018/2019 Wizara illoba na kutengewa jumla ya Shilingi Billioni Mia Moja Kumi na Saba, Milioni Mia Mbili Themanini na Saba na Elfu Nane (**117,287,008,000.00**) kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Miradi ya Maendeleo wakati kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi Billioni Mia Moja Kumi na Moja, Milioni Mia Nne Sabini na Tatu, Hamsini na Sita Elfu, Mia Tisa Ishirini na Saba (**111,473,056,927**) kwa Matumizi ya kawaida na Miradi ya Maendeleo katika mafungu yote mawili, yaani Fungu 44 & Fungu 60. Takwimu hizi zinathibitisha namna ambavyo Bajeti hii ya Viwanda na Biashara imeshuka kwa Billioni Tano, Milioni Mia Nane na Kumi na Tatu, Iaki Tisa hamsini na Moja Elfu, na Sabini na Tatu (**5,813,951,073.00**) Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaomba kupatiwa ufanuzi wa muujiza utakaotumika kulifikisha Taifa katika uchumi wa viwanda katika mazingira ambayo bajeti ya Wizara ambayo inahusika na kubeba kauli mbiu ya uchumi wa nchi inakosa bajeti inayojitosheleza!

**16. Mheshimiwa Spika**, Upungufu wa bajeti umeendelea hadi kwenye fedha za miradi ya maendeleo. Mathalani kwa Fungu 44 & 60 kwa mwaka 2018/2019 ilikuwa ni shilingi bilioni Mia Moja, Milioni Ishirini na Nne, Laki Tano Ishirini na Tano Elfu (**100,024,525,000**) sawa na 70% ya bajeti yote ya Wizara wakati kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020 Wizara inaomba

kuidhinishiwa jumla ya bilioni Hamsini na Moja na Milioni Mia Tano (51,500,000,000). Fedha hizi ni sawa na 46% ya bajeti yote ya Wizara na hivyo kufanya fedha za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kuwa kupungufu ya fedha za maendeleo ya mwaka 2018/2019 kwa 24%.

#### E. PROPAGANDA ZA SERIKALI NA UHALISIA WA VIWANDA NA MASOKO NCHINI

**17. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya awamu ya tano imekua ikijinasibu mara kwa mara kuwa inajenga uchumi wa viwanda na imekua ikitoa takwimu mbalimbali zikonesha idadi ya viwanda vinavyoanzishwa nchini na kuwa kama nchi tunaendelea vizuri kiviwanda.

**18. Mheshimiwa Spika**, ukiachia mbali mpango wa serikali wa miaka mitano ambao umezungumzia kidogo uchumi wa viwanda, Waziri wa Viwanda na Biashara hajawahi kuwasilisha kwenye Bunge lako tukufu mpango wa ujenzi wa viwanda na namna uzalishaji na masoko ya bidhaa utakavyofanyika. Aidha yapo maelekezo yaliyotolewa kwa Wakuu wa Mikoa kuhakikisha kuwa kila Mkoa unajenga viwanda mia moja kwa mwaka.

**19. Mheshimiwa Spika**, hajaelezwa ni viwanda vya namna gani vinaenda kujengwa na kwa tafiti zipi za masoko ya bidhaa zitakazozalishwa na viwanda husika. Taarifa ya jarida la *The Economist Intelligence Unit* ya tarehe 17 Januari, 2018 inaonesha kuwa pamoja na serikali kueleza kwenye mpango wa maendeleo wa miaka mitano kuwa itajikita kwenye uchumi wa viwanda na kutengeneza ajira ongezeko la kodi na kubadilika kwa ghafla kwa mifumo ya usimamizi wa biashara inayofanywa na serikali yameathiri ukuaji wa biashara nchini<sup>1</sup>.

**20. Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto wanazopitia wafanyabiashara za kodi na maelekezo ya

---

<sup>1</sup> Economist Intelligence Unit report, generated on 17<sup>th</sup> January, 2018 uk.

kiutawala na mifumo ya usimamizi wa biashara nchini taarifa za kiuwekezaji zinaonyesha kuwa uwekezaji nchini utapungua kwa kiasi kikubwa pamoja na uwepo wa mipango ya serikali.

**21. Mheshimiwa Spika**, katika hali kama hii ni wazi kuwa serikali kuendelea kujinasibu na uchumi wa viwanda ni kauli za majukwaani pekee kuliko hali halisi ya mazingira ya biashara nchini. Ni wazi kuwa huwezi kujenga uchumi wa viwanda bila kuwa na uhakika wa soko, na kama huna uhakika wa soko na hakuna uwekezaji wenye tija unaofanyika ni wazi pia kuwa serikali haiwezi kukusanya kodi.

**22. Mheshimiwa Spika**, aidha zipo takwimu tofauti tofauti ambazo zimetolewa kuhusu idadi ya viwanda viliivyojengwa nchini. Rais anapohutubia wananchi kwenye shughuli zake za uzinduzi wa miradi mbalimbali amekuwa akitoa takwimu za idadi ya viwanda viliivyojengwa na vinavyotegemewa kujenga, aidha wakati mjadala wa mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Kambi Rasmi ya Upinzani ilihoji juu ya utofauti ya takwimu za idadi ya viwanda vinavyojengwa nchini tofauti na idadi ambao raia anawatangazia wananchi.

**23. Mheshimiwa Spika**, utofauti wa takwimu za idadi ya viwanda umeonyeshwa katika hotuba ya Waziri wa Fedha na takwimu ambazo amezitoa Waziri wa Viwanda na Biashara katika Randama ya Wizara. Kama serikali ni moja na Rais ni mmoja, mbona kunakuwa na tofauti ya idadi ya viwanda? Takwimu mnazotoa tofauti tofauti kwa umma na propaganda za idadi ya viwanda mnamfurahisha nani? Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Waziri kutoa taarifa Bungeni ya aina viwanda na uwezo wake wa uzalishaji pamoja na takwimu sahihi kwa sababu tukiendelea kudanganyana hivi, kama Taifa hatuendi popote.

**F. KUFUNGAMANISHA KILIMO NA MAENDELEO YA VIWANDA (AGRO ECONOMY)**

**24. Mheshimiwa Spika**, Katika bajeti ya serikali 2018/2019 imeainisha sekta ya kilimo kama kipaumbele cha serikali lakini

haijaonyesha ni kwa namna gani hasa inalenga kufanya Mapinduzi ya Kilimo (Agrarian Revolution) ili kuweza kusisimua na sekta ya viwanda.

**25. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa hotuba ya Mpango ya Waziri inaonesha kuwa mchango katika sekta za kiuchumi katika Pato la Taifa kilimo kilichangia asilimia 30.1 mwaka 2017 huku Sekta hiyo inachangia utoaji wa ajira kwa asilimia 66, lakini ukuaji wake ni wa wastani wa asilimia 3.7. Katika kuijuliza sekta hiyo ambayo inatoa ajira asilimia 66 inachangia mapato ya kodi kiasi gani?

**26. Mheshimiwa Spika**, ukweli ni kwamba mapato ya kodi kutokana na sekta hiyo ya kilimo ni kidogo sana. Kwa bahati mbaya sana katika hotuba ya Mpango wa Maendeleo uk. 38 aya ya 54 sekta ambazo zinaimarishwa ili kufangamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu, sekta ya kilimo haipo.

**27. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuangalia unyeti wa sekta hii katika kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati na uchumi wa viwanda ni lazima sekta ya kilimo iwe ndiyo engine ya kutupeleka huko. Hivyo basi, pamoja na mambo mengine Kambi Rasmi ya Upinzani italenga kuondoa kodi zote kwenye uwekezaji katika sekta ya kilimo(kilimo,uvuvi na mifugo).

**28. Mheshimiwa Spika**, hii ni pamoja na kuondoa kodi kwenye uingizaji wa mashine mbalimbali zinazoingia katika mnyororo wa uongezaji thamani wa bidhaa za kilimo, mifugo na uvuvi, viwanda vinavyotengeneza na kukarabati mashine na zana nyingine za kilimo kama vile matrekta, pampu za umwagiliaji, mashine za uvunaji, viwanda vya kutengeneza madawa, mbolea, mbegu na vifungashio, zana za uvuvi kama vile mitumbwi, nyavi, na zana nyingine za uvuaji. Katika mifugo itahakikisha kodi za mifugo zinaondolewa, na kodi za viwanda vinavyotengeneza madawa na chanjo mbalimbali za mifugo, pamoja na kupunguza kodi katika viwanda vya kuongeza thamani za mazao.

**G. HALI MBAYA YA MAZINGIRA YA KUFANYA BIASHARA  
TANZANIA**

**29.** Taarifa ya Shirika la Fedha Duniani ya Januari 2018 kuhusu mapitio ya saba ya Mwongozo wa Sera ya Tanzania<sup>2</sup> imeeleza pamoja na mambo mengine pamoja na pato la taifa kuonekana kukua mazingira ya biashara nchini sio rafiki kwa uwekezaji maendeleo ya biashara.

**30. Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali hiyo ya sasa inaonekana dhahiri kuwa shughuli za kiuchumi ni dhaifu na hivyo kupelekea kushindwa kuzalisha ajira na kupunguza umasikini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kueleza kuwa pamoja na taarifa ya biashara nyingi kufungwa ambayo tulieleza kwa kirefu mwaka uliopita, Waziri wa Fedha alijibu kwa idadi ya biashara mpya zilizofunguliwa na kueleza kwa propaganda kuwa biashara zilizofungwa zilikuwa zinahusishwa na ukwepajji kodi.

**31. Mheshimiwa Spika**, kufungwa kwa biashara nchini sio jambo la kushangilia kwa sababu ni dhahiri kuwa wafanyabiashara hao walikuwa wanalipa, na hivyo kuongezeka kwa makusanyo. IMF wanaeleza kuwa makusanyo ya kodi yameshuka tofauti na jinsi ilivyokuwa inategemewa na hivyo kupelekea utekelezaji wa bajeti ya serikali kuwa dhaifu.

**32. Mheshimiwa Spika**, aidha kumekuwa na ongezeko kubwa la mikopo isiyolipika katika mabenki jambo ambalo linaathiri pia mazingira ya ufanyaji biashara kwa sababu kutokana na madhaifu yaliyopo katika mfumo wa sasa kodi na maelekezo ya kiutawala yasioangalia maslahi ya wafanyabiashara, wafanyabiashara wameshindwa kulipa mikopo kwenye mabenki ya ndani.

**33. Mheshimiwa Spika**, kufikia mwezi Septemba mwaka 2017 mikopo isiyolipika katika mabenki ya biashara iliongezeka

---

<sup>2</sup>IMF Country Report No. 18/11 The Seventh Review Under The Policy Support Instrument.

kutoka asilimia 9.1 hadi 12.5. Hali hii ilipelekeea mabenki nchini kupata hasara kubwa jambo ambalo halijawahi kuwepo toka mwaka 2007. Pamoja na juhudzi za Benki Kuu kupunguza kima cha chini cha fedha zinazohitajika kuhifadhiwa na Benki za Biashara nchini pamoja na kushusha kiwango cha riba bado sekta hiyo ilifanya vibaya na hivyo kuathiri mazingira ya biashara.

**34. Mheshimiwa Spika**, mauzo ya bidhaa kwenda nje ya nchi (export) yalionekana kushuka na pia makusanyo ya ushuru wa bidhaa nayo yalishuka kutokana na wananchi kupunguza matumizi ya bidhaa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuangalia kwa umakini hali ya uchumi wa nchi kuliko kuendelea kutoa kauli za kutongoza wananchi kuwa hali ni nzuri wakati katika takwimu hali inaonekana tofauti.

**35. Mheshimiwa Spika**, serikali haiwezi kukusanya kodi ya kutosha kama mazingira biashara na sera za kodi ziko hovyo. Aidha serikali haitapiga hatua kama maamuzi ya namna ya kuboresha biashara yanafanywa na serikali kuu bila hata kuzingatia uhalisia wa mazingira ya biashara. Ikumbukwe kuwa serikali imejinasibu kupunguza matumizi ya kawaida kwa ajili ya kubana matumizi, jambo hili ni jema hasa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.

**36. Mheshimiwa Spika**, kupunguza matumizi kwa sekta muhimu ambazo wafanya biashara walikuwa wanaingia mikataba ya kibiashara pamoja na zabuni za serikali usitegemee kukua kwa biashara nchini kwa sababu serikali ndiyo inayohitaji huduma na kupata huduma na bidhaa ni lazima ishirikishe sekta binafsi.

**37. Mheshimiwa Spika**, yapo pia malalamiko ya wazabuni ambaao walikuwa na madeni na serikali kwa sababu ya huduma au bidhaa ambazo walihudumia katika taasisi mbalimbali za serikali ambaao hawajalipwa na serikali inasema bado inahakiki madeni hayo kama ni halisi. Wahanga wa uhakiki huu ni wafanya biashara ambapo pamoja na kushindwa kuendelea kufanya biashara kwa sababu ya madeni, hata madeni hayo yakilipwa bado hayalipwi

kulingana na bei ya soko au kuangalia na thamani ya shilingi yetu ambao bado inasuasua.

**38. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inalitaka Bunge kuititia Kamati zake za kisekta zinazohusikana masuala ya uwekezaji na biashara nchini kuangalia hali hii ambayo si njema katika mustakabali wa Taifa letu na kuchukua hatua za dharura kuisimamia serikali ili kuepuka anguko la uchumi ambalo linakuja mbeleni.

**H. UWEKEZAJI WA MIUNDOMBINU NA USHIRIKISHWAJI  
HAFIFU WA SEKTA BINAFSI NCHINI**

**39. Mheshimiwa Spika**, Serikali inafanya uwekezaji kwenye reli ya *Standard Gauge Railway* (SGR), Mradi wa umeme wa Stiegler's Gorge, bomba la mafuta kutoka Hoima Uganda mpaka Tanga na mradi wa Bandari ya Bagamoyo ambao kwa sasa hauzungumziwi sana lakini hakuna mkakati wa wazi wa namna miradi hiyo inagharamiwa.

**40. Mheshimiwa Spika**, mara kadhaa Rais John Magufuli anasikika akisema kuwa miradi hiyo inagharamiwa na fedha za ndani za walipa kodi, na wakati mwingine Waziri wa Fedha ananukuliwa akisema kuwa miradi hiyo inagharamiwa na fedha za mikopo mbalimbali. Hata hivyo kutokuwa wazi kuhusu gherama za miradi mikubwa na muda wa kuimaliza kunazua sintofahamu kuhusu uwezekano wa kumaliza miradi hiyo mikubwa kwa wakati.

**41. Mheshimiwa Spika**, ukweli ni kuwa kama serikali haitashirikisha sekta binafsi kuititia ubia (PPP) wachambuzi wa uchumi wameshauri kuwa deni la taifa litaendelea kukua na kuwa mzigo kwa walipa kodi. Aidha ikumbukwe kuwa serikali imekua ikikopa sana ndani na hivyo kutengeneza ushindani na wawekezaji wa ndani ambao pia wanatumia mikopo kuendeleza biashara zao.

**42. Mheshimiwa Spika**, Ushirikishwaji wa sekta binafsi sio utachochea mazingira ya biashara na mzunguko wa fedha nchini bali pia itaipunguzia serikali mzigo wa kuwekeza

kwenye kila mradi mkubwa jambo ambalo linasababisha ugumu katika kupata mikopo yenyenye masharti nafuu kutoka nje na kuepuka serikali kukopa sana ndani kugharamia miradi hiyo.

**I. ATHARI ZA KIUCHUMI KUTOKANA NA KUSITISHWA KWA MRADI WA UKANDA MAALUMU WA KIUCHUMI WA BAGAMOYO (BAGAMOYO SEZ)**

**43. Mheshimiwa Spika**, Serikali imetangaza kusitisha mradi mkubwa wa Ukanda Maalumu wa kiuchumi wa Bagamayo na kwamba mradi huo wa thamani ya Dola za Marekani 10 sawa na TZS 23 Triliioni, sasa hautafanyika tena. Mradi huu mkubwa wa uwekezaji ambao thamani yake ni zaidi ya Bajeti ya Maendeleo ya Wizara nzima ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa miaka minne unafutwa bila kutolewa kwa sababu na kufanyika kwa mjadala wowote wa kina.

**44. Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulikuwa ni mradi wenye lengo la kuufanya mji wa kihistoria wa Bagamoyo kuwa kituo kikubwa cha usafirishaji mizigo (Main Logistic Hub) katika Bara zima la Afrika. Ni mradi ambao ni uwekezaji wa ubia katika wawekezaji kutoka China na Oman, ambao walikuwa tayari kuutekeleza kama eneo la ukanda maalumu wa Uchumi Bagamoyo (Special Economic Zone)

**45. Mheshimiwa Spika**, Ukanda Maalumu wa Uchumi Bagamoyo unahusisha miradi ya Ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo, ujenzi wa eneo la viwanda (industrial park) ambalo katika awamu ya kwanza litakuwa na viwanda 190 vitakavyozalisha ajira mpya za moja kwa moja 20,000 na awamu ya pili na tatu ikikamilika kutakuwa na viwanda 790 vitakavyozalisha ajira mpya 100,000. Mradi pia unahusisha ujenzi wa mji wa kisasa wa makazi unaoendana na mahitaji ya karne ya 21 ambao ulilenga kupunguza msongamano wa Jiji la Dar es Salaam kutokana na shughuli nyingi za uzalishaji kuvutia idadi kubwa ya watu kuhamia Bagamoyo kutoka Dar Es Salaam.

- 46. Mheshimiwa Spika**, mradi pia unahusisha Ujenzi wa kituo cha Usafirishaji ambacho kingeifanya Bagamoyo kuwa kitovu cha usafirishaji wa mizigo na hivyo kuiimarisha Tanzania kama njia kuu ya usafirishaji mizigo “transit route” inayotoka na kuingia kwenda nchi mbalimbali tunazopakana nazo. Aidha ni Logistic Park ililenga kuhudumia Meli kutoka Afrika kwenda Ulaya na Marekani.
- 47. Mheshimiwa Spika**, kama mradi huu ungekamilika pamoja na maeneo yake yote manne, hasa eneo la Logistic Hub jumla ya makontena milioni 20 zilitarajiwa kupitia Bagamoyo kwa mwaka na kuifanya kuwa bandari kubwa kuliko ile ya Rotterdam ya Uholanzi ambayo ndiyo kubwa kuliko zote Bara la Ulaya, kwa wale tunaoitakia mema Tanzania, tunaona ndani ya miaka 10 Bagamoyo ingekuwa Dubai ya Bara zima la Afrika.
- 48. Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Tanzania siyo kisiwa ni bora tuangalie baadhi ya nchi nyingie duniani ambazo zimefanikiwa katika uwekezaji wa maeneo kama haya, ikumbukwe kwamba wazo la mradi huu linafanana na wazo la Mradi wa Shenzhen – Special Economic Zone ambapo kampuni inayotaka kuwekeza Bagamoyo ilikuwa mojawapo ya Kampuni zilizowekeza huko. Ukanda Maalumu wa Uchumi wa Shenzhen ulikuwa mpango maalumu wa kuleta mabadiliko ya kiuchumi ya China chini ya kiongozi Deng Xiaoping. Ulikuwa mji wa majaribio ya sera za Kiuchumi ambazo zimeibadilisha nchi ya China na kuwa inavyoonekana sasa. Bagamoyo ilikuwa inajengwa kuwa Shenzhen ya Afrika kupitia mradi wa Bagamoyo Special Economic Zone ambayo wengi hupenda kuita Bagamoyo Port kwa makosa. Hivi kweli Serikali ya Tanzania na watawala wake wameona sasa kujengwa kwa mradi huu hakuna manufaa tena kwa ustawi la Uchumi wa Tanzania?
- 49. Mheshimiwa Spika**, kwa bahati mbaya sana wadau wengi wakati wanapajaribu kuzungumzia mradi huu hujikuta wakizungumzia bandari peke yake na kuacha maeneo mengine ya mradi huu, na hivyo kushindwa kufikiria manufaa mapana ya mradi huu ikiwa ni pamoja na ajira kutoka

maeneo mengine matatu ya mradi, hasa kipindi hiki ambacho vijana wengi wa Tanzania wanamaliza shule bila matumaini ya kupata ajira rasmi au hata kujajiri wenyewe.

**50. Mheshimiwa Spika**, Mradi huu mkubwa umekuwa gumzo sehemu mbalimbali ulimwenguni kutokana na ukubwa wake pamoja na athari zake kwa maslahi ya makundi mbalimbali ulimwenguni. Jambo moja muhimu sana kukumbukwa ni kuwa Biashara ni vita ya makundi yenye maslahi mbalimbali. Kauli ya Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kuwa nchi yetu ipo kwenye vita vy

**51. Mheshimiwa Spika**, Yapo Maslahi kutoka maeneo kadhaa ambaao ni washindani wetu kiuchumi pia, uamuzi wa Serikali ulipaswa kuangalia jambo hili kwa mapana, Kwa mfano; Kwa mataifa ya Ulaya Magharibi mradi huu ulikuwa tishio kwa hoja za kiushindani na ushawishi ndani ya ukanda wa Bahari ya Hindi ambaao unabashiriwa kuwa kitovu muhimu katika biashara ya kimataifa katika miaka michache ijayo. Wazungu waliuona mradi huo kuwa utaipa China nguvu kubwa zaidi ya kiuchumi. Ilikuwa ni muhimu sana kwa wao kuhakikisha mradi huu hautekelezwi kwa namna ye yeyote ile ili kuzuia nguvu ya China katika ukanda huu.

**52. Mheshimiwa Spika**, Kwa mataifa mengine ya Afrika, mfano kwa SADC nchi kama Afrika ya Kusini - mradi huu ulikuwa tishio kwa maslahi yao ya kiuchumi kwa kuwa ungepelekea ushindani mkubwa kwa Biashara ya Bandari ya Durban ambaao hivi sasa ndio kuna bandari pekee zenye uwezo wa kuhudumia meli kubwa kabisa za mizigo (4th generation ships). Inawezekana kabisa Afrika Kusini haikufanya kitu kuhujumu Mradi huu lakini kutofanyika kwake ni faida kubwa wa Durban kwani Bagamoyo ilikuwa inakwenda kuwa mshindani wake Mkuu. Hali ni hiyo hiyo kwa Angola ambayo inataka kujenga reli ya kuiunganisha DRC Kongo ili mizigo ya nchi hiyo ipitie bandari yao ya Luanda.

**53. Mheshimiwa Spika**, Kwa Afrika Mashariki, hasa Kenya, mradi wa Bagamoyo ulikuwa ni tishio kubwa kwa mradi wa

Bandari mpya wanayopanga kujenga huko Lamu, ambayo nayo itakuwa na uwezo wa kuhudumia meli kubwa (4th generation ships) na pia itakuwa na kitovu cha usafirishaji wa mafuta Barani Afrika. Siamini kuwa Kenya imefanya chochote kuhujumu mradi huu wa Bagamoyo SEZ, lakini maamuzi ya Tanzania kusitisha mradi huo yametoa ushindi wa bure bure kwa Kenya, kwani sasa Meli kubwa zitahudumiwa Lamu na kuipa Kenya nafasi kubwa sana katika biashara ya usafirishaji katika eneo la Afrika Mashariki na Kati (The Great Lakes Region).

#### **[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]**

**72. Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa miradi hii mitatu ungerahisisha sana utekelezaji wa miradi ambayo Serikali inafanya sasa. Mradi wa LNG ya Lindi ungeipa nchi mabilioni ya fedha za kigeni kutekeleza mradi wake pendwa wa Stiegler's Gorge kama ingekuwa kuna haja kuendelea nao. Mradi wa Mchuchuma na Liganga ungewezesha kuzalisha mataruma ya reli hapa hapa nchini kujengea reli ya SGR na kuokoa mabilioni ya fedha za kigeni tunayotumia kununulia mataruma nje ya nchi. Mradi wa Bagamoyo ungeleta mizigo yote ya Afrika hapa Tanzania na Reli mpya kupata biashara na hivyo kupata faida ya uwekezaji. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kutafakari upya maamuzi yake.

#### **J. MASUALA YA SERA YA KODI NA URASIMU YANAVYOATHIRI BIASHARA NCHINI**

**73. Mheshimiwa Spika**, Mpango wa maendeleo wa miaka mitano unazungumzia na kuonyesha ahadi ya serikali kujenga mazingira mazuri kwa ajili ya ukuaji wa sekta binafsi nchini. Kinachotokea kwa sasa ni serikali kutaka kumkamua ng'ombe maziwa ambaye hajampeleka kwenye malisho yenyе majani ambayo yatamfanya Ng'ombe huyo kuzalisha maziwa ya kutosha.

**74. Mheshimiwa Spika**, Hivi ndivyo serikali inavyofanya kwa wafanyabishara nchini, ambapo serikali inawahimiza kulipa

kodi ya maendeleo (jambo ambalo ni jema) lakini hajjaweka mazingira mazuri kwa ukuaji wa biashara hizo.

**75. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa ya Benki ya Dunia kuhusu urahisi wa kufanya biashara duniani, Tanzania imekuwa nchi ya 137 kati ya nchi 190 duniani na moja ya changamoto zilizotajwa ni pamoja masuala ya kodi ambazo sio rafiki, kufanya biashara mpakani na ugumu katika uanzishaji wa biashara.

**76. Mheshimiwa Spika**, kila wakati serikali hii inapokosolewa Kiongozi Mkuu wa nchi amenukuliwa akisema kuwa wanaotoa ukosoaji huo wanatumwa na mabeberu jambo ambalo linaonyesha kuwa bado tunao viongozi ambao wanafikiria kijamaa kuliko kufikiri katika Nyanja za utandawaza na kukua kwa sekta binafsi. Ni lazima serikali ijue kuwa haiwezi kuirudisha nchi kwenye Ujamaa kama walivoyzungumza lugha za kijamaa wakati kama Taifa tulishatoka kwenye zama hizo.

**77. Mheshimiwa Spika**, mazingira ya kuanzisha biashara nchini ni magumu, Waziri anaweza kuja na takwimu nzuri za namna Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni alivyosajili biashara kadhaa kwa mwaka huu wa fedha lakini ukweli ni kuwa mazingira ya kuanzisha biashara nchini ni magumu sana. Mathalani kuanzisha biashara ya kawaida unaweza ukatakiwa kupitia kwenye mamlaka na wakala zaidi ya tano na sehemu zote hizo kuna gharama ambazo lazima uzilipe kama mfanyabiashara kupata vibali au leseni.

**78. Mheshimiwa Spika**, hata utendaji wa Mamlaka ya Mapato (TRA) sio rafiki kwa wafanyabiashara. Hii ni kutokana na maafisa kuambatana na vyombo vyya ulinzi na usalama wakati wa ukusanyaji au ufuatiliaji wa kodi jambo ambalo linatia wafanyabiashara hofu na kuamua kufunga biashara zao.

**79. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kutofumbia macho mapungufu haya yaliyopo ya mazingira ya kufanya biashara. Ni vema kama wanahitaji

makusanyo mazuri ya kodi watatue changamoto zinazowakumba wafanyabiashara kuliko kujikita zaidi kwenye ukusanyaji wa kodi bila kuweka mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara kufanya biashara nchini.

#### **K. GHARAMA ZA KUANZISHA VIWANDA**

**80. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kuwa sio kazi rahisi kuanzisha kiwanda kama ambavyo serikali hii imekuwa ikipiga kelele hapa Bungeni na kwenye vyombo vya habari. Hasa ukizingatia kuwa kuanzisha viwanda vikumbwa ambavyo huzalisha mathalani kama magari viwanda hivyo vipyta hasa vya "fabrication industries" ni ghali si tu katika kuvianzisha bali hata kuviendesha.

**81. Mheshimiwa Spika**, pamoja na gharama kubwa za kuanisha na kuviendesha muda wa bidhaa zitakazozalishwa ili kuingia kwenye soko na kukubalika katika jamii ya watumiaji huwa mrefu sana.

**82. Mheshimiwa Spika**, serikali makini duniani kwa sasa huwa jambo la muhimu kwao ni kuanzisha viwanda vya uunganishaji (assembly plants), kama wenzetu wa Kenya walivyofanya au kama inavyofanyika kwa matrekt ya ARSUS yanayounganishiwa hapa Tanzania lakini kiwanda mama kipo nchi za nje.

**83. Mheshimiwa Spika**, kwa njia hii ni dhahiri tutakuwa tumeepuka gharama kubwa ya matumizi ya nishati umeme, gharama kubwa ya kutangaza bidhaa husika na hivyo bidhaa husika zitakuwa shindani katika soko la ndani na nje. Nchi nyingi za Mashariki ya Kati hutumia teknolojia ya kuunganisha bidhaa kama mbadala wa kuanzisha viwanda vipyta kuepuka changamoto ambazo tumeeleza.

**84. Mheshimiwa Spika**, ielewewe kuwa zipo pia changamoto za kimazingira ambazo kama nchi tutakumbana nazo katika kile ambacho serikali hii inakiita "uchumi wa viwanda". Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa serikali hii inacheza

ngoma ambayo hajafanyiwa utafiti wa kutosha kuhusu uanzishwaji na uendeshaji wa viwanda nchini.

**L. UHITAJI WA MABORESHO KATIKA SHIRIKA LA  
KUHUDUMIA VIWANDA VIDOGO (SMALL INDUSTRIES  
DEVELOPMENT ORGANIZATION- SIDO)**

**85. Mheshimiwa Spika**, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) lilianzishwa mnamo mwaka 1973 kwa mujibu wa Sheria namba 28. SIDO ina ofisi katika mikoa yote ya Tanzania Bara isipokuwa Tanzania Visiwani (Zanzibar), kwa sababu Wizara ya Viwanda na Biashara sio ya Muungano.

**86. Mheshimiwa Spika**, majukumu ya Shirika hili ni pamoja na uendelezaji teknolojia, kutoa mafunzo na huduma za ugani, kusimamia masuala ya masoko na habari pamoja na huduma za fedha.

**87. Mheshimiwa Spika**, Katika huduma ya uendelezaji teknolojia, SIDO ina mapungufu makubwa kwa sababu ilitegemewa SIDO kuzalisha mashine mbalimbali kuititia vituo vyao vya kuzalishia mashine (KARAKANA) lakini mpaka hivi sasa ni Mikoa saba tu yenye vituo vya kuzalishia mashine ambayo ni Iringa, Mbeya, Kigoma, Lindi, Arusha, Shinyanga na Kilimanjaro.

**88. Mheshimiwa Spika**, pamoja na uwepo wa Karakana hizo, mashine zake sio za kiasasa na zinahitaji kuboreshwa. Mikoa iliyobaki inategemea wajasiriamali wanaozalisha mashine. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuhakkisha kuwa SIDO inakuwa na Karakana katika Mikoa iliyoosalia ili kuwa mfano kwa Wajasiriamali wengine nchini.

**89. Mheshimiwa Spika**, mpaka sasa Karakana za SIDO zilizopo zinashughulikia Mkoa mzima na kukosa matawi wilayani, sasa katika kutoa huduma zenye tija kwa taifa kuna haja ya shirika kujipambanua hadi wilayani kuwe na ofisi ili kuwafikia wananchi kwa karibu zaidi kuliko ilivyo sasa. Mfano mtu yupo Mpwapwa anahitaji huduma ni lazima aje Dodoma Mjini ndipo apate huduma, labda itokee bahati kukiwa na

maonyesho Wilayani ndipo inakua rahisi kwa wananchi kupata huduma.

**90. Mheshimiwa Spika**, Katika huduma ya uendelezaji wa teknolojia, unakuta kuna taasisi nyingine ambazo zina ofisi mkoja mmoja au miwili tu nazo zinajihusisha katika uendelezaji wa teknolijia ambazo ni TEMDO, CARMATEC na TIRDO. Ili kuboresha zaidi hili shirika la kuhudumia viwanda ambalo lipo Mikoa yote ya Tanzania Bara, ni vema taasisi hizi zenyelengo sawa la uendelezaji teknolojia zingeunganishwa kama Shirika moja la kuhudumia viwanda kwa manufaa ya umma kwa kila Mkoa kupata huduma muhimu katika uendelezaji tekhnologia nchini.

**91. Mheshimiwa Spika**, kwa njia hii ni dhahiri tutakuwa tumeepuka gharama kubwa ya matumizi ya nishati umeme, gharama kubwa ya kutangaza bidhaa husika na hivyo bidhaa husika zitakuwa shindani katika soko la ndani na nje.

#### M. CHANGAMOTO ZA SEKTA YA VIWANDA NCHINI TANZANIA.

##### i. Serikali kushindwa kurejesha Malipo ya VAT (VAT Refund).

**92. Mheshimiwa Spika**, wazalishaji wengi hivi sasa wanapata changamoto ya mitaji inayotokana na malimbikizo ya VAT iliyolipwa kwa serikali. Ikumbukwe kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Mapato ya Ongezeko la Thamani yaani (The Value Added Tax Act, 2014) viwanda vinavyosafirisha bidhaa na kununua malighafi kutoka nje ya nchi, vinapaswa kulipa kodi ya ongezeko la thamani VAT, kodi ambayo inapaswa kurejeshwa kwa walipaji ndani ya kipindi cha miezi mitatu. Katika hali ya kusikitisha Na kukatisha tama Kwa wafanya biashara hawa, malikimbikizo ya fedha hizo zilizolipwa hayajalejeshwa kwa zaidi ya miaka mitatu sasa.

**93. Mheshimiwa Spika**, Wafanya biashara Viwandani sasa wanadai kurejeshewa zaidi ya Shilingi Bilioni 45 kutoka kwa serikali kwa zaidi ya miaka mitatu. Kitendo cha Serikali kushindwa kurejesha fedha hizo kwa wafanya biashara

kinasababisha ongezeko la gharama katika uzalishaji wa bidhaa viwandani na hivyo kuathiri ufanisi wa uzalishaji na kuathiri uchumi kwa ujumla, kitendo hicho pia kinaathiri na kukatisha tamaa usafirishwaji wa bidhaa zinazozalishwa viwandani kwenda nje ya nchi kwa kuwa msafirishaji atapaswa kulipa fedha nyingine wakati kwa zaidi ya miaka miatatu amekuwa akilipa lakini serikali imeshindwa kurejesha fedha hizo kama sheria inavyotamka na mwisho kitendo cha serikali kushindwa kurejesha malimbikizo ya VAT kinaathiri upatikanaji wa fedha za kigeni.

**94. Mheshimiwa Spika**, Ili kuwanusuru wafanya biashara wa viwandani ambao asilimia kubwa walikopa fedha hizo kutoka kwenye taasisi mbalimbali za kifedha zenyе riba kubwa na ili kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza ufanisi wa uzalishaji viwandani, kuhamasisha bidhaa zinazozalishwa hapa nchini kusafirishwa nje ya nchi kwenye masoko na kuliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni, Kambi Rasmii ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuliambia Bunge lako Tukufu ni lini itawalipa wazalishaji wenye viwanda madai yao ya malimbikizo yanayokadiriwa kuzidi Bilioni 45 ili uchumi wa viwanda uonekane kwa vitendo?

**ii. Kodi kubwa inayotozwa kwenye ushuru wa forodha 15%, sukari ya Viwanda.**

**95. Mheshimiwa Spika**, kuna changamoto nyingine dhidi ya malighafi inayotumika viwandani kutengeneza vinywaji, vyakula na katika viwanda vya kifamafasia. Hata hivyo sukari ya viwandani si Tanzania wala nchi za jumuiya ya Afrika Mashariki zinazozalisha malighafi hii. Ikumbukwe kwamba chini ya Jumuia ya Afrika Mashariki, Sukari hii hutozwa ushuru kwa 10%. Tanzania ni nchi pekee mionganoni mwa nchi za Afrika Mashariki ambazo hutoza nyongeza ya 15% ambayo inapaswa kurejeswa kwa walipaji (**additional refundable import duty of 15%**) na hivyo kufanya jumla ya ushuru unaolipwa kuwa 25%. Pamoja na nia njema ya kudhibiti wafanyabishara wenye nia ya kuza malighafi hiyo katika soko la ndani lakini ukweli ni kwamba, ongezeko hilo halizuijochchote kwa kuwa mfanyabiashara anaweza kuingiza,

akalipa ushuru unaotakiwa na akaiuza katika soko la ndani kwa faida. Lakini kwawazalishaji wa viwandani ambao wanaingiza sukari ya viwandani kama malighafi ya kuzalishia bidhaa, mfumo huu ni mzigo kwao kwa kuongeza gharama za uzalishaji na kuongeza taratibu za kiutawala zisizo na ulazima wowote.

**96. Mheshimiwa Spika**, pamoja na hoja hizo, lipo tatizo la muda mrefu la kutorejeshwa kwa ushuru huo kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), hadi sasa kwa mujibu wa taarifa za Umoja wa Wamiliki wa Viwanda Tanzania (**Confederation of Tanzania Industries**) ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeziona, waagizaji na sukari ya viwandani wanadai marejesho ya zaidi ya Billioni 35 kutoka Tanzania Revenue Authority.

**97. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Mamlaka ya mapato nchini kwa kushindwa kuwarejeshea waagizaji wa sukari ya viwandani shilingi Billioni 35, wamewasababishia hasara ya bilioni 3.5 ambazo wamelazimika kulipa kwenye taasisi za fedha yakiwemo mabenki ya biashara kutokana na ucheleweshwaji huo. Hali hiyo pia inaongeza gharama ya uzalishaji kwa wazalishaji wa Tanzania wakati washindani wenzao kutoka nchi za jumuia ya Afrika Mashariki wanaolipa ushuru wa 10% peke yake bila gharama nyininge wakipata faida kulingana na uzalishaji wa Tanzania na hivyo, gharama zinazosalishwa Tanzania zinakuwa na gharama kubwa kuliko bidha zinazofanana ambazo zimezalishwa katika nchi wanachama wa jumuia ya Afrika Mashariki.

**98. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kurejesha / kulipa malimbikizo ya wazalishaji hawa yanayotokana na nyongeza ya ushuru kwa 15% kwa mujibu wa sheria na kanuni kwa waingizaji wa sukari ya Viwandani, kiasi cha zaidi ya Billioni 35. Pamoja na hayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri serikali kuondoa nyongeza ya 15% ambayo ni ushuru unaorejeshwa kwa kuwa haiongezi mapato wala thamani kwa Serikali, na badala yake nyongeza hiyo ambayo inachelewa kurejeshwa inaleta athari kwenye mzunguko wa fedha za mitaji ya wafanyabiashara,

huku ikiongeza gharama za kufanya biashara na ni kikwazo cha ukuaji wa bishara za Viwanda. Serikali iondoe vikwazo hizi zisivo na ulazima wowote ili kujenga uchumi wa viwanda kwa vitendo kuliko maneno matupu.

**iii. Changamoto za sheria ya Kodi ya Ongezeko la thamani VAT namalighafi za Viwandani nchini!**

**99. Mheshimiwa Spika**, Mfumo wa mpya wa stempu za kielektroniki (ETS) ambao ulikusudia kuongeza mapato ya serikali umeshindwa kutimiza azma hiyo na hauna budi sasa kuondolewa. Taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani inazo zinaonesha kwamba stempu moja ina gharama ya shilingi nane, lakini Serikali haipati mapato kutokana na fedha hiyo. Taarifa zinadai kwamba kazi ya mwenye tenda ya kutengeza stempu ni kutoa taarifa kwa Serikali juu ya kiasi cha bidhaa kilichozalishwa, na ukilangalia mfumo wa utendaji kazi unagundua kwamba kampuni ya SIPA ndiye mnufaikaji kuliko Serikali na hata mapato ya Serikali yameshuka. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kutafakari upya mfumo huu na kuliambia Bunge hili ni mapato kiasi gani Serikali ilikuwa ikipata kutoka katika makampuni ya Sigara (TCC) na Kampuni ya Bia (TBL) kama mfano, kabla ya mfumo wa ETS na kiasi cha mapato ambacho serikali inapata baada ya kuanzisha mfumo wa ETS.

**100. Mheshimiwa Spika**, sheria mpya ya Ongezeko la Thamani yaani VAT ya mwaka 2014 iliyoanza kutumika Julai 01, 2015 iliondoa vyandarua vya kuzuia malaria kutoka jedwali la ZERO KODI (ZERO RATE) na kuviweka kwenye jedwali la msamaha wa kodi. Utaratibu huu Mheshimiwa Spika, unavifanya vyandarua vinavyozalishwa nchini kuwa na bei ghali kuliko vyandarua vinavyoingizwa nchini (imported) ambavyo havitozwi ushuru wala kodi. Kwa sheria hii mzalishaji wa ndani ya Tanzania hawezi kurejeshewa malipo ya kodi ya VAT (input tax) aliyolipa wakati wa kuagiza malighafi na pia katika mchakato mzima wa uzalishaji kama umeme na usafirishaji. Kwa vile chandarua hakitozwi VAT malipo hayo ya 18% hubaki kama gharama kwa mzalishaji kwa vyandarua vyote vitakavyotumika nchini ambapo lazima gharama hii iingizwe

kwenye bei na hatimaye kutomudu ushindani dhidi ya vyandarua kutoka nje ya nchi ambavyo havitozwi kodi yoyote.

**101. Mheshimiwa Spika**, kutokana na sheria hii ya VAT 2014 kuitaka TRA kukusanya kodi ya VAT kwa mzalishaji wa ndani wakati huo huo wakikusanya lakini wakikusanya kodi ZERO kwenye vyandarua kutoka nje ni kitendo kinachohamasisha uingizwaji wa vyandarua kutoka nje ya nchi na hivyo kuendeleza ajira za huko vinakotengenezwa badala ya hapa nchini. Aidha viwanda vya ndani vinadidimizwa kwa kutoweza kushindana katika soko na pia inalazimika wakati mwингine kutumia fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza vyandarua vya malaria kutoka nje pasipo ulazima na ambapo fedha hizo zingeweza kutumika katika shughuli nyingine za maendeleo nchini.

**102. Mheshimiwa Spika**, katika kuendeleza viwanda kwa ajili ya kilimo cha kisasa, vipo viwanda ambavyo vinatengeneza vyandarua kwa ajili ya kilimo biashara cha mbogamboga (horticulture). Hata hivyo, vyandarua hivi hutozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na hivyo kuvifanya kuwa ghali. Endapo greenhouse nzima inaagizwa toka nje hazina ushuru wa VAT lakini pale changarua chake kinapoisha, ili kuweka kingine kinachozalishwa hapa nchini ndipo hutozwa VAT pamoja na kwamba ni mojawapo ya pembejeo za kilimo. Mali ghafi zake ni pamoja na High Density Polyethylene (HDPE) HS 3901.20.00 na ULTRA – Violet (UV D- 770 – Calcium base filler MB) – HS 3206.19.00 – VAT

**103. Mheshimiwa Spika**, wakati katika kipindi hiki cha Awamu ya Tano, tatizo la ukosefu wa ajira limekuwa kubwa na serikali kwa kipindi hiki ikituasua kuajiri watanzania wanaohitimu katika fani mbalimbali, uchumi wa viwanda pamoja na mambo mengine ungetarajiwa kuzalisha ajira nyingi hapa nchini. Pamoja na ukweli huu lakini bado sera za serikali kama hii ya kutoza VAT kwenye vyandarua vyenye viatilifu siyo tu kuhatarisha ajira kwa watanzania lakini pia inaonesha ni kwa kiasi gani mikakati ya kutikomeza ugonjwa wa malaria hauwezi kufanikiwa kutokana na sera mbaya kama hizi.

**104. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza na kushauri Serikali kuondoa Kodi ya VAT kwenye malighafi zinazotumika kutengeneza vyandarua vya kuzuia mbu waenezao ugonjwa hatari wa malaria. Malighafi ambazo ni High Density Polyethylene (HDPE) Monofilament Grade – HDPE – HS.3901.20.00 na Colour Master Batch HS.3204.20.00 ziondolewe kodi na mbadala wake uwe ni kutoza kodi na ushuru kwenye vyandarua visivyoitiwa kiatilifu na kuvipatia HS Code tofauti na vile vyenye kiuatilifu ambayo hutumika kama vifaa tiba, ikumbukwe kwamba vyandarua vyote hutumia HS. 6304.91.10.

**iv. Utitiri wa Kodi kwenye viwanda vya mbao shindani wa kibiashara usiozingatia usawa.**

**105. Mheshimiwa Spika**, wafanyabiashara wa Tanzania sasa wanapitia katika mazingira ambayo siyo rafiki kiblashara. Ni kipindi ambacho kuna utitiri wa kodi, tozo na ada mbalimbali hali inayowalazimu baadhi ya wafanyabishara kufunga biashara zao kutokana na kushindwa kumudu gharama hizo.

**106. Mheshimiwa Spika**, kuonesha jinsi ambavyo utitiri huo wa kodi, tozo na ada zinavyoathiri biashara, nitatumia sekta ya viwanda vya samani za mbao kama mfano. Pamoja na kukua kwa sekta hii na kufikia katika kiwango cha kusafirishwa kwenda nje ya nchi, lakini biashara hii ya mazao ya mbao na misitu kwa ujumla inakutana na changamoto ya uwepo wa kodi nyingi, ushuru, tozo, ukiritimba kwenye taratibu za kupata vibali vya kusafirisha bidhaa za misitu kwenda nje ya nchi. Sekta hii tu inakumbana na kodi, tozo na ushuru kwa mfano, Mfanya biashara anatakiwa kulipa kodi na tozo zifuatazo ili kufanya biashara ya samani, Annual Export Permit Renew Fees, kutoka Tanzania Forest Agency, Annual Renewal fees for the certificate of Forest produce in the furniture category, Additional charges of on consignment below USD 299.00 and TZS 270,000.00 more on consignment above USD 300.00, Additional fees of TZS 500 to Ministry of Livestock on wood furniture that uses leather product, Business Licence Fees of TZS 300,000 BRELA, Export License of TZS 100,000.00 (BRELA) Municipal Levy of 0.3% on sale revenue (Local government)

Fire and Rescue Force fee of Tzs 400,000.00 na Ada ya OSHA kiasi cha TZS 350,000.00 na hivyo kufanya jumla ya gharama za kodi, tozo na ushuru kufikia jumla ya 9. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona haya siyo mazingira mazuri kwa ustawi wa biashara hapa nchini na KRUB inataka serikali kupunguza kodi na tozo hizi, pia kuja na mkakati ambao utawawezesha watanzania kufanya biashara katika mazingira mazuri kuliko hali ilivyo hivi sasa.

v. **Ongezeko la huduma za Bima viwandani.**

**107. Mheshimiwa Spika**, hivi karibuni serikali imefanya mabadiliko ya kanuni ambayo yalitangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 251 la tarehe 8 Juni, 2018 kanuni ambazo zimeleta malalamiko mionganoni mwa wadau wa biashara hususani wamiliki wa Viwanda hapa nchini hususani kuhusu ongezeko la bima kwenye sekta ya viwanda. Malalamiko yao makubwa yakiwa ni kutoshirikishwa kama wadau wakati wa kutengenezwa kwa kanuni hizo na hivyo kuwa na madhara makubwa ikiwa ni kuongezeka kwa gharama za kufanya biashara na kuathiri moja kwa moja ushindani wa kibishara kwa viwanda vyetu. Ili kuendana na kanuni hizi, Taarifa ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani tunayo ni kwamba, wamiliki wa viwanda sasa wanalazimika kulipia bima za kiwango cha chini ili kupunguza gharama za bima. Kutoka na changamoto hiyo, ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba, Serikali kuititia Mamlaka ya Udhhibit wa Bima (Tanzania Insurance Regulatory Authority – TIRA) ikae chini na wamiliki wa viwanda ili kuona namna ya kutatua changamoto zinazojitokeza kwenye kanuni hizi mpya, kwa maslahi mapana ya sekta binafsi nchini na Taifa kwa ujumla wake.

vi. **Ucheweshwaji wa vibali vya kufanya kazi nchini.**

**108. Mheshimiwa Spika**, mchakato wa kupata vibali vya kufanya kazi nchini kwa waajiriwa kwenye sekta mbalimbali bado ni changamoto kubwa pamoja na matamko mbalimbali ambayo yamekuwa yakitolewa na Idara ya Kazi. Wafanyakazi wanaaoajiriwa katika viwanda na maeneo

mengine wanalazimika kutumia hadi miezi mitatu wakitafuta vibali vya kufanya kazi nchini, na katika hali ya kufanya mchakato kuwa mrefu zaidi, waombaji wanatakiwa kuwasilisha maombi wao wenyewe hapa jijini Dodoma. Hali hii pia inayakumba makampuni ambayo yamesajili chini ya kituo cha uwekezaji nchini (Tanzania Investment Centre) na ambayo yanaruhusiwa kuwaombea vibali vya ajira watumishi wao. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuhakikisha inarahisha mchakato wa kuomba vibali vya ajira nchini kufanywa kwa njia ya mtandao yaani online, ili kuondoa ukiritimba uliopo na kuharakisha mchakato mzima wa maombi hayo.

**N. CHANGAMOTO ZA KIUTENDAJI KATIKA SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA(TBS)**

**109. Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Shirika la Viwango Nchini kudhibiti ubora, bado yapo malalamiko kutoka kwa wadau mbalimbali wakiwemo CTI kuhusu ucheleweshaji wa majibu ya vipimo vya sampuli za bidhaa zinazowasilishwa kwa ajili ya kuhakikiwa ubora. Hali hii inasababisha kuongezeka kwa gharama hasa katika mazingira ambayo yanahusishwa na uagizwaji wa malighafi kutoka nje ya nchi. Pamoja na changamoto hiyo pia upo ucheleweshwaji mkubwa wa vyeti vya ubora kutoka TBS ambapo hutolewa kwa kipindi cha zaidi ya mwezi mmoja. Inadaiwa pia TBS inamahusiano mabaya ya kimawasiliano mionganoni mwa wadau, kuna ucheleweshwaji mkubwa wa kujibu hoja mbalimbali kwa wadau kitendo kinachowafanya wadau kutumia muda mwangi na rasilimali fedha kufuatilia mrejesho wa hoja zao TBS. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kupitia TBS kuhakikisha kunakuwepo na uharaka wa huduma kwa wadau na kupunguza muda wa kushughulikia na kutoa huduma kwa kujali muda na hasara zinazowapata wadau wanaotumia shirika hilo.

**O. BAJETI HEWA ISIYOAKISI MAENDELEO YA VIWANDA:**

**110. Mheshimiwa Spika**, ni wazi kuwa Serikali ya awamu ya tano na zile zote zilizotangulia zinashindwa kuongoza mageuzi

ya viwanda nchini kutokana na kuendesha masuala nyeti ya Kitaifa bila kuzingatia nyakati husika na kukubali kujifunza kutoka wataalam mbalimbali ndani na nje ya nchi.

**111. Mheshimiwa Spika**, Dira ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati kiviwanda ifikapo mwaka 2025 haina uhalisia, sio kwa sababu ilichelewa kupangwa bali ni kwa sababu Serikali ya CCM haiwezi kuongoza kadiri ya dira inazojiwekea yenye. Ili Tanzania ifanikiwe kuwa ya uchumi wa kati kiviwanda ifikapo mwaka 2025 basi sharti sekta ya uzalishaji (manufacturing) ichangie wastani wa chini wa asilimia 40 katika pato la Taifa ifikapo 2025.

**112. Mheshimiwa Spika**, Leo hii takribani miaka 6 kabla ya mwaka 2025, sekta ya viwanda vya uzalishaji (manufacturing) inachangia asilimia 5.2 tu ya pato la Taifa kwa mujibu wa kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Miaka mitano (National Five Year Development Plan, 2016/17 – 2020/21).

**113. Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Serikali ya CCM imechoka kiuwezo, kiakili, kiutashi na kidhamira, hata kama Rais Magufuli akifanikiwa kukaa madarakani kwa miaka 8 ijayo mpaka kufikia mwaka 2025, yeye na Serikali yake yote hataweza kabisa kuigeuza Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati kiviwanda kwa sababu ili afanye hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inampa changamoto kuwa kila mwaka wa fedha ikiwamo mwaka huu wa 2019/2020, sekta ya uzalishaji (manufacturing) inapaswa kukua kwa asilimia 4.35 kila mwaka wa fedha mpaka ifikapo mwaka 2025 ili kufikia lengo la kuifanya ‘manufacturing’ ichangie asilimia 40 ya pato la Taifa na hatimaye Tanzania kuwa ya uchumi wa kati kiviwanda!

**114. Mheshimiwa Spika**, Ukisoma kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Miaka mitano (National Five Year Development Plan, 2016/17 – 2020/21) Serikali ilijipangia kutumia jumla ya Shilingi Trilioni 5.78 kwa ajili ya uwekezaji katika miradi mikubwa ya kimkakati kwenye sekta ya uzalishaji (manufacturing), wakati ahadi (commitment) ya Serikali pekee ikiwa ni billioni 659.

**115. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaposema hoja ya Tanzania ya viwanda ni hoja hewa, inamaanisha inachokisema. Kwa ‘facts’ ambazo tayari zinaainishwa katika nyaraka na takwimu mbalimbali Tanzania ya viwanda inawezekana pale tu, CCM itakapoondolewa madarakani.

**116. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulielezea Bunge lako tukufu na Watanzania kwa ujumla inapojigamba kuwa inajenga Tanzania ya viwanda, je Tanzania ya Viwanda itajengwa kwa bajeti ipi? Wakati bajeti yake ni asilimia 0.3 ya fedha zote walizotakiwa kupanga kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**117. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, hadi kufikia mwezi machi, 2018 Tanzania ilikuwa na jumla ya viwanda 53,876 kwa mgawanyo wa viwanda vikubwa 251, viwanda vyta kati 173 na viwanda vidogo vikiwa ni 6,957 na viwanda vidogo sana vikiwa ni 46,495. Aidha taarifa za serikali zinaonesha kwamba tangu awamu ya tano iingie madarakani jumla ya viwanda vipyta 3,306 vinasemekana vimejengwa. Rejea hotuba ya waziri wa viwanda na biashara katika mwaka wa fedha 2018/2019 uk 6 , hata hivyo karibia asilimia 96.5 ya viwanda vyote ambayo ni viwanda 53,876 ni viwanda vidogo vinavyoajiri wafanyakazi 1 hadi 9. Asilimia 3.5 vinatoa ajira kuanzia watu 10 na kuendelea. Takwimu hizi hazitoi matumaini makubwa ya kuingia katika uchumi wa viwanda Hivi viwanda vyta mtu mmoja mpaka kumi ni kujidanganya, ndio maana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana hujigamba kuwa navyo kwa ajili ya kuvigawa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka kufahamu viwanda vyote vilivyopo Tanzania vinachangia asilimia ngapi ya Pato la Taifa?

**P. UCHUMI WA VIWANDA TANZANIA UNATEGEMEA  
KILIMO IMARA:**

**a. Maamuzi ya kutouza Korosho nje ya Nchi yasababisha hasara Serikali zaidi ya Trion 1.18.**

**118. Mheshimiwa Spika**, Mapema mwezi Juni, 2018 serikali ilitangaza na kuzindua awamu ya pili ya mpango wa

kuendeleza sekta ya kilimo ambao unatekelezwa kwa miaka 10, pamoja na malengo mengine mkakati huo unakusudia kuongeza tija katika uzalishaji na kufanya kilimo kiwe cha biashara.

**119. Mheshimiwa Spika**, wakati Serikali ikifanya hivyo, Serikali hiyo hiyo, mapema mwaka huu, kupitia Bodi ya Nafaka Mchanganyiko (CPB) iliingia makubalianao na Kampuni ya Indo Power ya Kenya kwa ajili ya ununuzi wa tani 100,000 za korosho kwa bei ya Dola za Marekani 180.2 milioni sawa na TZS 418 bilioni. Hatua ilijili baada ya mipango, mikakati na melekezo ya serikali kuhusu zao la korosho kushindwa kutekelezeka na kusababisha hasara kubwa kwa wakulima wa zao la korosho ambao ni zao wanadolitegemea kama zao la biashara. Hata hivyo miezi minne baadaye serikali imevunja mkataba na kampuni hiyo kwa kile kinachoelezwa kuwa ni kampuni hiyo kushindwa kutekeleza mkataba huo.

**120. Mheshimiwa Spika**, Mkataba huo ambao serikali iliingia, ulisainiwa mbele ya Mawaziri wa Katiba na Sheria, Waziri wa Kilimo, Viwanda na Biashara, lakini pia tunaamini vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinajukumu katika mikataba hii ambayo Taifa linaingia. Taarifa za kwamba kampuni hii imeshindwa kutekeleza vifungu vya kimkataba zinatia ukakasi kwa kuwa ilikuwa ni wajibu wa serikali hii kwa kutumia vyombo vyake kufanya uchunguzi wa kampuni hiyo, haiingii akili Taifa kwamba vyombo vyetu vya usalama wa Taifa walishindwa kujua uwezo wa kampuni husika. Ni kwa bahati mbaya haya yanatokea na mawaziri waliohusika wako Ofisi utadhani hakuna kilichotokea. Pamoja na udhaifu huo, Matamko na maelekezo ya Serikali kuhusu biashara ya zao la korosho imesababisha hasara kubwa kwa wakulima na Taifa kwa sababu ambazo zingeweza kuepukwa. Kutokana na sakata hili la zao la kibiashara la korosho

i. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawataka wahusika wote wajitafakari kama wanatosha kuendelea kushika nyadhifa walizonazo ama wanapaswa kupisha Ofisi hizo za Umma kuongozwa na watu wengine, kwa kuwa maamuzi ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi yamelisababishia Taifa hasara ya

Dola za kimarekani Millioni 500 sawa na Tzs 1.18 Trioni kutokana na maamuzi mabovu ya serikali.

- ii. Ni gharama kiasi gani ambacho serikali ilitumia kukusanya zao hili la kibiaresha la korosho kutoka kwa wakulima na kuzipeleka kwenye maghala ya serikali.
- iii. Baada ya gharama zote zilizotumiwa na Serikali, je serikali inategemea kuuza korosho kwa bei gani?

b. **Mchango wa Sekta ya Kilimo katika Uchumi wa Viwanda.**

**121. Mheshimiwa Spika**, Tangu kuingia madarakani serikali ya Awamu ya Tano imekuwa ikijinasibu na kujigamba na kauli mbiu ya uchumi wa viwanda. Kwa mtazamo yakinifu zipo falda za kuwa na uchumi wa viwanda ikiwa ni pamoja na uwezekano wa kuongeza ajira, kuongezeka kwa mapato ya kodi na yasiyo na Kodi, fedha za kigeni, kukuza sekta nyingine zinazofungamana na viwanda kwa kuzipatia malighafi na bidaa nyingine, hivyo basi ni sahihi kwa kusema kwamba uchumi wa viwanda unategemea sana kilimo kwa kuwa sekta ya kilimo peke yake inachangia takribani 65% ya malighafi zote za viwandani.

**122. Mheshimiwa Spika**, Endapo Serikali hii ya Chama Cha Mapinduzi ingekuwa na dhamira ya kulifanya Taifa hili kufikia uchumi wa kati kwa msingi wa viwanda, tungetarajia kuona jitihada za kuimarisha viwanda vilivyopo ili kuifanya sekta hii kuongeza pato la Taifa na kuhakikisha angalau 40% ya ajira za Tanzania zinatokana na sekta ya viwanda na kushawishi sekta binafsi kuwekeza katika viwanda.

Aidha tungetegemea kuona bidhaa mbalimbali za kutoka katika viwanda vya Tanzania katika masoko ya upendeleo ya kikanda duniani ili kukuza uchumi na kuondoa umasikini uliopo, lakini mambo yanaonekana ni kinyume na matarajio kutokana kukosekana kwa utashi wa kisiasa.

**123. Mheshimiwa Spika**, upo uhusiano wa moja kwa moja kati ya kilimo na uchumi wa viwanda na kwa mukitadha huo

huo upo uhusiano wa karibu kati ya uchumi wa Viwanda na ASDP II kwa kuwa nchi kama Tanzania ni rahisi kuwa na uchumi wa viwanda unaotarajiwala malighafi katika kilimo kuliko sekta nyingine nahii inatokana na ukweli kwamba Tanzania ni nchi ya kilimo, japokuwa serikali ya ccm imeshindwa mara zote kuwasaidia wananchi kuboresha kilimo chao na kuwatafutia masoko ya mazao yao.

**124. Mheshimiwa Spika**, huenda dhana ya Serikali kuhusu Viwanda ni tofauti na dhana ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu dhana hiyo ya viwanda. Kwa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni azma ya uchumi wa viwanda Tanzania, ambayo pia imejadiliwa na kuandikwa na wanazuoni mbalimbali, tunafikiri kwamba vingekuwepo viwanda vyaa ina tatu, viwanda vinavyoweza kuajiri watu wengi, viwanda vinavyoweza kuzalisha bidhaa kwa walaji wengi na vile vitakavyozalisha ili kuuza nje ya nchi, tujulize sote hapa, miaka mine sasa ya Serikali ya awamu ya tano, Tanzania ya Viwanda imetengeneza ajira asilimia ngapi za wahitimu wetu katika fani mbalimbali, tunaingiza fedha za kigeni kiasi gani ukilinganisha na takwimu za miaka ya nyuma na tunasafirisha nje bidhaa kiasi gani kwa takwimu za sasa?

**125. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri serikali kuhakikisha inaboresha kwanza kilimo, na kujielekeza katika viwanda ambavyo vitaongeza thamani katika mazao ya mifugo kama vile nyama, maziwa, ngozi, damu, kwato, pembe na hata kusindika mazao yanayotokana na uvuvi. Kwa maneno mengine Mheshimiwa Spika, ili kutimiza azima ya Tanzania ya Viwanda ni lazima Serikali itenye na kupeleka angalau 10% ya bajeti yake katika sekta ya kilimo ili kuzalisha malighafi kwa wingi, ni aibu hadi sasa viwanda vyaa nguo hapa nchini kuagiza pamba kutoka nchini Ugnada kwa ajili ya matumizi ya viwanda vyaa Tanzania.

- Q.        KERO ZA WAFANYA BIASHARA TANZANIA**  
**a.        MANYANYASO KUTOKA MAMLAKA YA MAPATO  
                NCHINI TANZANIA**

**126.** Mhesmiwa Spika, wafanya biashara mbalimbali hapa nchini wanakumbana na adha kutoka Mamlaka ya Mapato

Nchini - TRA. Kwa kipindi kirefu sasa mamlaka ya mapato nchini TRA imeshindwa kubuni mkakati wa kukusanya kodi na badala yake wanatumia vibaya mamlaka katika kutekeleza majukumu yao na hali inayosababisha malalamiko ya kuwepo kwa vitendo vinavyoashairia rushwa.

**127. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Mapato nchini, TRA, kwa mkoa wa Dar Es Salaam kwa mfano wameanzisha utaratibu wa kuvizia wateja wanaotoka madukani kununua bidhaa huku wakiwa na risiti mikononi mwao, na mara wanapomuona mwananchi aliyetoka dukani, humwamuru kuonesha bidhaa alizonunua na sehemu alizonunulia. Yapo malalamiko ya kwamba, mara waoneshwapo duka husika, maafisa hao wa TRA hupanga bei zao dukani na kudai bidhaa iliyouzwa na kutolewa risiti imeuzwa chini ya kiwango na humtaka mwenye duka kufika TRA na au kuwasiliana na maafisa hao. Operation giyo iko maeneo ya kariakoo kuelekea jangwani ambako wananchiu hununua bidha na kusafirisha kwenda mikoani, kwa hali ya kawaida hoja kubwa ya TRA ingekuwa ni kudai risiti ya bidhaa zinazonunuliwa lakini malalamiko haya ya kupanga bei si majukumu ya TRA. Kufuatia malalamiko haya, Kambi Rasmi Bungeni inataka kauli ya serikali kuhusu vitendo hivyo vinavyofanywa na TRA dhidi ya wafanya biashara hawa.

**a. VITAMBULISHO VYA UJASIRIAMALI**

**128. Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Rais wakati akizungumza na maafisa kutoka Mamlaka ya Mapato Nchini - TRA, katika Ukumbi wa Mikutano wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alitumia mikutano huo, kulitangazia Taifa kuwepo kwa vitambulisho vya wafanyabishara ndogondogo ambavyo kwa maeleo yake mwenyewe alisema amevitengeneza ye. Maeleo na maelekezo ya Mheshimiwa Rais ni kwamba, vitambulisho hivyo, viliviyotengenezwa na Ikulu vinauzwa kwa gharama ya Tsh 20,000/- kwa mwaka na kwamba wafanyabiashara wasiolipia mapato Mamlaka ya Mapato Nchini (TRA) wanapaswa kuwa na vitambulisho hivyo.

**129. Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Rais alieleza ubora wa vitambulisho kutokana na teknolojia aliyotumia kutengeneza vitambulisho hivyo, huku akiwielezea kuwa ni mkombozi wa wajasiriamali ambao walikuwa kwa kipindi kirefu sasa wananyanyaswa na kubughudiwa.

**130. Mheshimiwa Spika**, kwa bahati mbaya sana, hotuba hiyo ya Mheshimiwa Rais ni kama ilitolewa bila kuangalia sana tatizo la msingi na nia kubwa ya Serikali hii ilikuwa ni kujipatia fedha kutoka kwa wafanyabiashara ndogo ndogo wajulikanao kama wajasiriamali. Hawa ni wafanyabiashara ambao Serikali yenye imeshindwa kuwatengenezea mazingira rafiki ya kujipatia mitaji na masoko ili waweze kulipa kodi za serikali kwa ufanisi. Kwa maneno mengine, ni kama Serikali inang'ang'ania kumkamua ng'ombe maziwa bila kumlisha majani, huku ikitarajia kupata maziwa.

**131. Mheshimiwa Spika**, wafanyabiashara ndogo ndogo ambao ni wajasiriamali, wamachinga, mama ntilie au mama lishe, wafanya biashara barabarani wanahitaji kujengewa mazingira mazuri na Serikali hii, wanahitaji mazingira ya kuwezeshwa kiuchumi, mikopo, maeneo ya kuuzia bidhaa zao kuliko kutozwa kodi bila kuwajengea uwezo wao wa ki biashara. Aidha, wafanya biashara hawa wananyanyaswa na wamekuwa wakinyanyaswa na serikali hii hii, kuititia kwa wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi, wamepata na wanapata shubiri na vipigo kutoka kwa mgambo kwa maelekezo ya viongozi wa serikali, sasa badala ya kuwatengenezea mazingira ya kufanya biashara serikali imejielekeza tu kutafuta fedha kutoka kwao.

**132. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka serikali kuiga sera mbadala kwa kuwa na uchumi wa soko jamii ambao unazingatia maendeleo na ustawi wa jamii. Katika mfumo huu msingi mkubwa wa uchumi wa soko jamii itakuwa soko huria liliojikita katika ushirikishwaji na mshikamano, ambapo jamii inatakiwa kusimama pamoja wakati wote na kushiriki katika masuala ya maendeleo. Katika mukitadha huu mfumo wa kodi lazima usaidiekeki ya Taifa

kutumika kwa manufaa ya watu wote chini wakiwemo wajasiliamali hawa tunaowauzia vitambulisho hivi.

- **Utaratibu mbaya wa kutoa vitambulisho vyatujasiriamali.**

**133. Mheshimiwa Spika,** Serikali, ilitangaza kwamba vitambulisho hivyo vinatolewa kwa wafanyabiashara wenye mitaji ya kuanzia milioni 4 kushuka chini lakini hakushuka chini, hii kwa tafsiri nyingine ni kwamba akina mama wanaouza nyanya wenye mitaji ya elfu tano, wauza miwa na karanga mitaani wanapaswa kuwa na vitambulisho hivyo ambayo gharama zake ni 20,000/- hali hii ikwa bahati mbaya hakuna kikomo, utaratibu huu umezua malalamiko miongoni mwa wananchi kwa kuwa wapo wengine ambao hata mitaji yao halisi haifiki kiasi hicho cha gharama ya kitambulisho, na ili kumudu gharama ya kitambulisho hicho inailazimu familia kuuza mbuzi au kuku ili kupata fedha hizo. Utaratibu huu na uamuvi huu unawaumiza watanzania ambao wanahitaji kujengewa mazingira bora ya biashara kuliko vitambulisho. Sambamba na hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji, ni kampuni gani ilipewa tenda ya kutengeneza vitambulisho vyatujasiriamali, Kampuni hiyo ilishindanishwa na makampuni yapi, tenda ilitangazwa lini na wapi? Na je kampuni iliyoshinda tenda ilishinda kwa thamani ya shilingi ngapi? Taarifa hizi ni muhimu kwa kuwa ukosefu wake unaleta sintofahamu na unathibitisha harufu ya rushwa katika mradi huu.

**134. Mheshimiwa Spika,** ukiacha, utaratibu wa kutoa tenda kwa kampuni za kutengeneza vitambulisho vyatujasiriamali kwa wafanya biashara ndogondogo pamoja na dhamira yake ambayo inaweza kuwa nzuri lakini jambo hilo halikufikirika kwa kina, bado Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona mchakato huu una madhaifu mengi yanayojitokeza katika utekelezwaji wa zoezi hilo huku likiachaka maswali mengi yasiyojibika.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kufahamu, vitambulisho vyatujasiriamali vinavyouzwa katika halmashauri mbalimbali kwa gharama zao, Halmashauri zetu zinanufaikaje

kiuchumi kutokana na mradi huo wa vitambulisho vinavyogawiwa kwa wafanyabiashara ndogondogo.

▪ **Kupotea mapato ya serikali**

**135. Mheshimiwa Spika,** Serikali inapoteza mapato mengi sasa kuliko kipindi cha nyuma kutokana na utaratibu huu mpya wa vitambulisho. Mjasiriamali ambaye alikuwa analipa ada/ushuru wa Tsh. 500 kwa siku kulingana na biashara yake, itamlazimu kwa mwezi, (ndani ya siku thelathini) kulipa jumla ya shilingi elfu kumi na tano, ukizidisha kwa miezi kumi na mbili ambazo ni mwaka mmoja , mwananchi huyu atalipa jumla ya shilingi laki moja na elfu themanini. Ukitoa elfu ishirini, ni dhahiri kwamba serikali inapoteza mapato ya shilingi laki moja na elfu sitini kwa mwaka kutoka kwa mjasiriamali mmoja kwa mwaka, tujiulize Taifa hili lina wafanyabiashara hizo ndogo ndogo wangapi na Taifa hili linapoteza mapato kiasi gani kwa maamuzi haya, ambayo kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni siyo sahihi.

**136. Mheshimiwa Spika,** sasa inashangaza kwamba serikali hii ya awamu ya tano iko mtaani kujishughulisha na uuzaaji wa vitambulisho vya wajasiriamali, viongozi wote wa Serikali ngazi za mikoa, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Maafisa Tawala wa Mikoa na Wilaya, pamoja na watendaji sasa wamegeuka wauza vitambulisho, hii ni aibu na kimsingi siyo wajibu wao, vitendo hivi vinadhihirisha kwamba, Serikalini sasa imefika mwisho wa kuibua vyanzo vya mapato na kwamba, viongozi wa ngazi wa Serikali wanashubiria maelekezo kutoka juu, kutokana na wao kushindwa kuwa wabunifu kwenye maeneo ya kazi.

**137. Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Cecil D. Mwambe (Mb)

**K.N.Y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI**

**BUNGENI**

**KATIKA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

14 Mei, 2019

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Cecil Mwambe. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza majadiliano yetu sasa na nitaanza na Mheshimiwa Riziki Lulida. Hayupo, tunaendelea na Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuwa mwongeaji kwa siku ya leo kwenye hii Wizara ya Viwanda na Biashara. Kwanza nataka niseme tu kwamba, humu ndani Wabunge tumeingia kila mtu ana fani yake, wako wakulima, wako wafugaji, wako Walimu, tuko wafanyakishaa, wako Wanasheria. Kwa hiyo, kila mtu anajua sekta yake vizuri, pamoja na kuwa wapo wengine wanajua kila sehemu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, Wizara ya Viwanda na Biashara, kama inavyoitwa, Waziri wa Wizara hii anachotakiwa ni kuhakikisha kwamba anatengeneza biashara inakwenda vizuri kwenye nchi yetu ya Tanzania, asiwe ni mmoja wa sehemu ya kubomoa biashara kwenye nchi hii. Kwa nini nasema hivyo? Inaonekana kabisa wazi Wizara hii ya Viwanda na Biashara hailelewi chochote kuhusu biashara kwenye hii nchi. Kabisa, hili ni suala la wazi, kwenye ukweli lazima tuseme ukweli, na ndiyo maana sasa hivi Rais wetu anapata tabu sana, kila anapokwenda anaelezea mambo, anakuwa yeye ndiye Waziri, yeye ndiye Rais. Kwa kweli, Rais mwishowe atapasuka kichwa, watu aliowaweka hawamsaidii! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwenye ukweli huwa sipindishi maneno, ukweli ni ukweli tu. Hivi, mimi nauliza Wizara ya Biashara, leo hii ukiangalia kodi kila Wizara inaanizisha kodi kuhakikisha kwamba inakomesha biashara au inakomoa biashara, kila Wizara. Leo hii ukienda kwenye Wizara ya Kazi, Vijana na Ajira, unakuta kuna *WCF*, hawa wanaambwa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, wao wana chaji zao kibao. Ukienda kuna *OSHA*, (*Usalama wa Mahala pa Kazi*), wao wana kodi zao nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mfano mmoja tu wa hawa *OSHA*, mimi nafanya biashara zote, ya mafuta nafanya na biashara zingine. Nitolee mfano kwenye biashara ya mafuta, wanachukua kodi kwa mwaka laki tano, *OSHA*. Mwaka huu wanataka milioni tatu na laki tano, kwenye kituo cha kijijini. Kituo cha mjini mpaka milioni sita, kwa mwaka, ada. Sasa imekuwa kila mtu anakusanya fedha na anaona sifa, kwamba akimkomesha, akimfungia mfanyabiashara, yeze anaona sifa! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niulize, hapo hapo kuna *WCF*, wako hivyo hivyo. Ukija Halmashauri kuna *service levy*, anachukua kwenye mauzo, siyo kwenye faida, kwenye mauzo, 0.3%. Sasa ukiangalia kwenye viduka vidogo, nendeni hapa Dodoma tu, viduka vyote vidogovidogo hivi, mtu anaanzisha kiduka chenyewe kina thamani ya milioni tatu, nne, anapigwa mpaka laki tatu, laki nne, hiyo *service levy*, halafu sasa Waziri wa Viwanda na Biashara yupo. Sasa yeze biashara yake ni ipi, ni kuua biashara au kukuza biashara? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo ukweli, nini biashara ambayo anaitetea, maana yake anatakiwa atetee wafanyabiashara wawe wengi, aingilie kila sehemu ambapo anaona wafanyabishara wanaonewa. Ndiyo maana ya biashara, lakini sasa kila mtu amekuwa sasa mchukua kodi, ukija vipimo, anakwenda dukani mtu wa vipimo, ameshapima ule mzani wa dukani, kagonga na *label* yake, kila kitu, kwenye duka dogodogo tu linauza mchele na nini, kesho anakuja tena, anasema mbona huu mzani wako unapunja, wakati yeze ndiye kagonga ule muhuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nijue, ndugu yangu, Mheshimiwa Kakunda, maana ya kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara maana yake lazima ahakikishe kwamba anakuza biashara, si kuua biashara. Kwa hiyo, inatakiwa kila sehemu ambako mfanyabiashara anaonewa, yeze aingilie, kutetea, lakini wamejielekeza sana kwenye viwanda, viwanda, viwanda, sawa, kuna kiwanda cha *General Tyre*, kilikuwa namba moja katika *East and Central*

*Africa* kwa ajili ya kutengeneza matairi bora. Wote hakuna mtu ambaye hajapenda *tyre la General Tyre*, mpaka leo hiki kiwanda kipyा hakifufuki! Kiwanda cha Serikali, leo hii tunashindwa na *firestone* ya Kenya, inaingiza mpato makubwa sana kwenye Serikali ya Kenya, lakini sisi *General Tyre*, tumeingia tu tunapiga siasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siyo Mbunge wa kushangilia, kwenye ukweli nitasema ukweli kutetea maslahi ya nchi yangu. *General tyre* ni muhimu, mimi siwezi kukaa hapa nasema tu haya tu Mheshimiwa Waziri, umeanzisha kiwanda fulani, umeanzisha kiwanda fulani wakati viwanda havipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *Yuasa, Yuasa* mpaka Uingereza walikuwa wanunuua betri za *Yuasa*, kiwanda cha Serikali, kimebinafishwa, mpaka leo, wameangalia kinafanya kazi gani! Kuna viwanda vingapi vilibinafishwa nchi hii, vinafanya kazi gani, watu wamevikalia tu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vimekaliwa tu, kwa hiyo, naomba...

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimweleze ndugu yangu, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, asimamie Wizara yake ya Viwanda na Biashara na hasa upande wa biashara, ahakikishe kwamba biashara anaisimamia katika Wizara zote....

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa muhimu.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Sasa wewe naona, ungekaa kwanza kidogo, unanichanganya.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shabiby naomba uendelee.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ahsante. Kwa hiyo, ninachoomba, kwamba hatua zichukuliwe, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara aangalie biashara, kila Wizara sasa hivi, wanasema *TRA* tu, *TRA* kweli inachukua kodi yake, lakini kuna kodi zingine kubwa kuliko za *TRA*, tozo zimekuwa nyingi sana sana kuliko hata hizo za *TRA*. Kwa hiyo, naomba sana waangalie sana na Waziri afanye vikao na wadau ili apate hayo matatizo, siyo kila siku tunamwona tu naangalia *tiles*, anaangalia mbolea, ajaribu kukaa na wadau wamwambie, wampe changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ahmed Shabiby. Tunaendelea na Mheshimiwa Hussein Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa kuchangia Wizara hii, jambo moja la kwanza kabisa kabla sijaanza kutoa mchango wangu, nataka niiombe Serikali, Wizara ya Fedha, waangalie huu Mwezi wa Ramadhan, kuna *request* kubwa za Taasisi mbalimbali za Kiislam ambazo zimeleta tende na vyakula kwa ajili ya kutoa sadaka kwa watu maskini ziweze kupata *request* ya *exemption* ambazo wameomba kutoka *Tanzania Revenue Authority*. Taasisi hizi ziko *regulated* chini ya BAKWATA na zimepeleka *requests* zake na wengi wanatoa katika maeneo ambayo watu wana umaskini mkubwa, *they cannot afford* kupata futari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita katika maeneo makubwa yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni suala la kufanya biashara; biashara yoyote duniani, ina mambo makubwa mawili na ninachomshukuru Mwenyezi Mungu, Rais Magufuli alivyoingia madarakani, aliweka *vision* yake *clear*, kwamba anataka kujenga nchi yenye uwezo wa kujitegemea ya

viwanda. Hii ndiyo *vision*, ni matarajio yangu mimi na wengine wote tuliomo humu na Watanzania, kwamba wanaomsaidia Mheshimiwa Rais kusaidia utekelezaji wa *vision* hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ina mambo mawili, moja kuna *software part of business* na upande mwingine ni *hardware part of business*. *Hardware part of business*, tunajenga barabara, tunajenga reli, tunanunua ndege, tunajenga miundombinu ya umeme, lakini hii *hardware part* ya biashara, isipokuwa *compatible* ya *software partya* biashara ambayo ni *regulation* na sheria, hii itakuwa ni *wastage* ya *resources*. Kama tutajenga reli, tutajenga barabara, tualeta umeme, vyote hivi vikakosa biashara ambayo itavifanya hivi vitu *viwe effective*, havitakuwa na maana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nitoe mifano michache, kwenye Kamati yetu ya Bajeti, walikuja watu wa *CTI*. *CTI* kwenye *presentation* yao, ambayo ninayo hapa na bahati nzuri Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara tulikuwa naye, wanazungumzia *existence of multiple Regulatory Authority leading to high costs of doing business*, kwa sababu biashara vilevile gharama ni jambo la msingi. Sasa anakwambia *an example for the food processing industry is registered by more than 15 authorities*, taasisi 15 zina-regulate food processing industry.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *pharmaceutical industry*, ili aanzishe biashara ya kiwanda kidogo cha *pharmaceutical industry* huyu mtu aliyejuka kufanya hii presentation ni mtu ambaye anataka kuweka kiwanda Mkoa wa Mwanza kwa ajili ya kutumia pamba iliyoko pale kutengeneza pamba kwa ajili ya mahospitali. Huyu mtu, anahitaji *regulatory authorities* zimepe jumla la ya leseni 26 ili aweze kuanzisha huu mradi. (*Makofî*)

**WABUNGE FULANI:** Duuh.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, a registered company kwa ajili ya ku-export hotculture

*products*, maua na bidhaa zingine za *hotculture*, anahitaji kupata jumla ya vibali 45 ili aweze ku-export biashara hii. (*Makofii*)

**WABUNGE FULANI:** Duuh.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kwa ajili ya kuzalisha maziwa ana tozo na kodi na leseni jumla 26 ili anzishe kiwanda hicho.

**WABUNGE FULANI:** Duuh.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwape mfano, kuna kiwanda kidogo kiko Nanenane hapa Dodoma, mwaka 2016 aliamua kuanzisha kiwanda chake cha *ku-process* asali ambacho kina uwezo wa *ku-process* tani 3 kwa siku. Februari 2016 na ninazo barua zake hapa, huyu mwananchi ameandikia *TFDA* ije ikague kiwanda chake iangalie mfumo wa uzalishaji na kumpa *approval* amejibowi Novemba 6, barua ya kwamba tutakuja kukagua. Mpaka amepata *certificate* ni Februari 2019.

**WABUNGE FULANI:** Duuh.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu ni mfanyabiashara mdogo, kachukua mkopo *Tanzania Investment Bank* wa shilingi milioni 200, benki sasa iko mlangoni kwake inataka kuli-recall mkopo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini sasa ushauri wangu? Ushauri wangu ni hivi, ile taarifa ya *IMF*iliyo-leak (*unofficial*), imetupa mambo mazuri mno na mimi nataka nishauri Serikali ipokeeni kwa sababu imetupa *two options*, imetuambia kama tunataka *ku-growkwenda 6%, 7%* kuna mambo manne ya kufanya. La kwanza *improve business environment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu *TFDA*, *OSHA*, taasisi zote hizi anzisheni *one building* wawekeni pale andikeni *business facilitation of whatever* ili mfanyabiashara akishachukua leseni yake ya usajili wa Kampuni *BRELA*, the

*second place* anayoenda anaenda kwenye *business facilitation building*. Akifika pale analipia taasisi zote na muweke chini pale *cage* kama za benki, iwe imeandikwa *NEMC, TFDA, TBS*, ndani ya jengo moja. Yule mfanyabiashara aki-launch application yake pale and the world is connected, akitoka anatoka na *document* zake anaenda kufanya biashara yake, hili ni jambo muhimu mno. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingne ambalo nataka niulize, *TBS* ana evaluate standardya bidhaa na vitu ambavyo tunazalisha. Kama mtu kapata certificate ya *TBS* anazalisha maziwa kwa nini tena akatafute certificate ya *TFDA*? Wawekeni hawa watu wote ndani ya one umbrella *TFDA* awe unit ndani ya *TBS* ili mtu akiingia afanye kila kitu mule, *OSHA* awe unit ndani ya *NEMC* may be ili tuangalie namna gani ya ku-harmonize mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe kaka yangu Waziri Kakunda, *blueprint* leta sheria. Kama kuna mahitaji ya mabadiliko ya sheria jamani mwaka wa fedha huu upo bado hatujamaliza, hata kama ni weekend moja tukae hapa tuwasaidieni kufanya haya mambo yawe rahisi katika kufanya biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano, hapa mkononi nina taarifa *leather sector*. Sijui kama Kanuni zinaruhusu ni vizuri sana kwenye Kamati ya Bajeti Waziri Jenista awe anakuja, hili ni ombi ili aone mambo yalivyo ndani ya Serikali. Yeye yuko pale kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya ku-coordinate Mawaziri na taasisi za Serikali inakuwa rahisi center of coordination ya shughuli za Serikali kutokea Ofisi ya Waziri Mkuu kuwepo, ni muhimu na nasema hii from my heart kwa sababu kuna mambo yanafanyaika unajiuliza are we one Government? Inasikitisha! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikupe mfano, usafirishaji wa ngozi wet blue, mwaka 2016 tulisafirisha ngozi wet blue pieces 1.2 million kwenda nje, leo tuna export wet blue pieces 200,000. Wet blue ni stage ya kwanza ya ku-process, ngozi kutoka raw kwenda wet blue ni stage ya

kwanza ambapo tumesafirisha *1.2 pieces* mwaka 2016 leo tume *export only 200,000 pieces*, hii hapa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajiuliza swali kama tunazalisha *pieces* milioni 3 kwa mwaka kama nchi hizi zinazobaki ambaz hatujasafirisha ziko wapi? Ukienda kuangalia *raw exported only* iliyokuwa *exported ni pieces* 400,000 kuna *pieces* zaidi ya 800,000 vimeondoka *under smuggling* na mnajua ni kwa nini? Ni kwa sababu ya *one thing*, tume *impose 10% export levy* ya *wet blue* ambayo *competitors* wetu wote kwenye *East Afrika* hawana kodi hiyo, tunayo sisi. Ni kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulienda Arusha tukasaini makubaliano ya Afrika Mashariki tukaingizwa mkenge halafu wao wenzetu hawatekelezi sheria hiyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, hapa tumesikia suala la Mchuchuma na Liganga, Waheshimiwa Wabunge hebu tujiulize swali, kwenye Mradi wa Mchuchuma na Liganga kuna Mradi wa Makaa ya Mawe, Mradi wa Chuma, Mradi wa Umeme na mradi wa kuchakata *product* zinazotokana na chuma, sasa wapi tumekwama? Ukitikiliza kabisa kutoka *NDC* mkwamo unatokana na umeme na chuma. Sasa nauliza kama miradi miwili ina matatizo, kwa nini tunazuia utekelezaji wa mradi wa makaa mawe? Kwa nini hii miradi yote minne tunaifunga pamoja ukifa mmoja *they entire project is dead.* (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tunaona kuna matatizo tunapeleka barabara Liganga na Mchuchuma, tunapeleka *line* kubwa ya umeme, *why are we spending that money*kupeleka kule kama nchi? Kwa nini tusipeleke kwenye madarasa au kwenye maeneo mengine? (*Makof!*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bashe, nilikuongezea dakika tatu.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Julius Kalanga atamalizia Mheshimiwa Shamsia.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea na maeneo mengine, naomba Waziri wakati anakuja kuhitimisha anipe maelezo kuhusu Mradi wa Magadi wa Engaruka. Wananchi wetu wametoa eneo la kubwa sana karibu eka 100,000 kwa ajili ya mradi huu na katika llani ya Chama cha Mapinduzi pamoja na Mpango wa Maendeleo wa 2015-2020 wamesema mradi huu ni wa kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma katika kitabu cha Waziri katika ukurasa wa 17 maneno ya Waziri anasema: "Mradi wa Uchimbaji Magadi Soda katika Bonde la Engaruka, Wilaya ya Monduli unahu ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha magadi soda tani milioni moja kwa mwaka kwa ajili ya matumizi ya viwanda hususan vya dawa, vioo na sabuni. Utafiti wa kina (techno-economic study) utakaojumuisha utafiti wa maji safi (detailed hydrological study), mazingira (ESIA), na upembuzi yakinifu (feasibility study) umeanza kufanyika".

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana ilikuwa ni bajeti ya Wizara ya Uchukuzi lakini hata kilometra moja ya lami kwenda kwenye Mradi wa Engaruka kilometra 70 kutoka Mto wa Mbu kwenye bajeti ya Serikali hakuna. Sasa mimi nataka niulize hivi ushirikiano wa Wizara za Serikali katika kutekeleza miradi ya maendeleo uko wapi? Kwa nini Wizara ya Biashara inazungumza ya kwake na Wizara ya Ujenzi inazungumza ya kwake. Unatekelezaji Mradi wa Engaruka bila miundombinu wenzeshi, maji lakini tunasema ni mradi wa kimkakati. Mmewazuia wananchi wetu wasiendeleze maeneo yao katika eneo lile hata fidia hamjalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Wizara ituambie barabara ya kutoka Mto wa Mbu kwenda Engaruka ili eneo lile liwe *accessible*, muweze kufika unaanza lini? Kama mradi huu mnashindwa kuutekeleza tuwaachie wananchi wetu waanze kufuga ng'ombe wao katika maeneo yale. Tumetoa maeneo yale kwa bei kutupwa Sh.200,000 kwa eka moja lakini mpaka leo hamjaanza. Leo hakuna hata mradi wa barabara katika eneo lile, halifikiki, ni mwekezaji gani ataenda kufanya *investment* Engaruka wakati barabara ya kufika tu haipo? Ni miujiza gani yule anayefanya utafiti kule kuchukua yale magadi anachukua *material* yake aje apeleke kwenye bandari ya Dar es Salaam asafirishe? *Let us be serious* katika miradi hii, kama mradi huu umefeli tuuache. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo niende katika eneo la ngozi. Amesema kaka yangu hapa kwamba katikati ya Bunge hill tuna watu tofauti tofauti, lakini sisi tunaotokana na jamii ya ufugaji maisha yetu ni ng'ombe, uchumi wetu ni ng'ombe, kuvaah wetu ni ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nitofautiane na baadhi watu. Mnasema mnazuia ngozi isiende nje kwa sababu ya kulinda viwanda vya ndani lakini uzalishaji wa ngozi ya ng'ombe kwa mwaka ni milioni 3,500,000 lakini viwanda vyetu vya ndani havichukui ngozi hata 200,000, kwa nini mnatengeneza gharama ya kulinda viwanda vya ndani kwa gharama zetu sisi wafugaji wa nchi hii? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wenye viwanda na vinavyofanya kazi ni karibu vinne tu nchi nzima, ukipeleka kuuza ngozi kwao wanunuua Sh.300 kwa *piece* mpaka Sh.1,200, lakini ye ye aki-*process* ile ngozi anakuuzia kwa Sh.100,000, haki iko wapi katika eneo hili? Kwa sababu ninyi mmeweka kodi katika usafirishaji wa ngozi nje na kwa sababu hakuna mahali pa kuuza wao wameamua kutokununuua kwa bei ya kawaida kwa sababu wanajua hakuna mahali pa kupeleka kwa sababu mmetuwekea kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana kulinda viwanda vya ndani lakini nataka Waziri aniambie unalinda

viwanda vipi ambavyo hauna? Unalinda kiwanda kipi cha ngozi ambacho kinawenza kuchukua ngozi 3,000,000 kutoka kwa wafugaji wa nchi hii? Kwa nini mnatengeneza gharama ambayo inatumiza sisi wafugaji? Tunataka Serikali iruhusu upelekaji wa ngozi nje mpaka viwanda vya ndani vitakavyotengemaa ili tuweze kupata mahali pa kuuza, sasa hivi hakuna mahali pa kuuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza hapa Mbunge mmoja kuhusu 10% ya *wet blue* lakini 80% ya ngozi ghafi zimewekwa ili kulinda viwanda vya ndani na viwanda vyenye vya ndani havipo. Tunaomba Serikali kwa unyenyekevu kabisa isivilinde viwanda vya ndani kwa gharama za wafugaji wakati ngozi tunazalisha sisi hatuna mahali pa kuuza kwa sababu viwanda vya ndani havinunui na mmezuia visiende nje kwa sababu mmeweka kodi kubwa. Ni muhimu kuliangalla jambo hilli ili kuwasaldia wafugaji wa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ukiangalia kama ambavyo wengine wasema tatizo hili la ngozi hata sera na usimamizi wa viwanda hivi haupo. Kwa mazingira kama haya lazima ngozi yetu ikose thamani. Sasa hivi wanasema soko limepatikana Nigeria kwa sababu wao wanakula ngozi lakini kama Serikali inaona kwamba soko hilo ni kubwa kwa nini *Isingewasaidia wafugaji kupata soko la uhakika kuliko* *discourage exportation* wakati ndani ya nchi hakuna uwezo wa ku-*accommodate* ngozi zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali itoe maelekezo kwenye taasisi zake kama Majeshi na Polisi, bidhaa zinazotengezwa na viwanda vyetu hasa viatu wanunue. Kuna kiwanda kinaitwa Bora wanasema wanazalisha viatu vizuri sana lakini bado Serikali katika Majeshi yetu ya Polisi na Jeshi la Kujenga Taifa tunaagiza viatu nje. Kama hatuwezi kuthamini cha kwetu unategemea nani anunue bidhaa za ndani kama sisi Serikali hatununui bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka kulinda viwanda vya ndani ni pamoja na kutafuta soko la ndani na Serikali kupitia Majeshi inaweza ikawa ni sehemu ya soko kwa viatu vinavyotengenezwa ndani ya nchi. Wenyewe hatununui, kwa nini tusifanye kama Waziri wa Nishati alivyoagiza kwamba trasfoma zote za TANELEC zinunuliwe kuliko kuagiza nje. Tukienda huko tutakuwa tumesaidia viwanda vyetu vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo tunaliona, tatizo kubwa ambalo viwanda vyetu linakumbana nal ni kodi kubwa katika bidhaa na mitambo ya kujenga viwanda vya ndani, vilevile kodi kubwa ya umeme. Mimi nilikuwa nafikiri katika maeneo ambako tuna viwanda vya ndani tuondoe kodi kwenye umeme ili viwande vile viweze kuzalisha na kuleta faida kwa taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.  
*(Makof)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunamalizia Mheshimiwa Shamsia.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia katika Wizara hii ya Wiwanda na Biashara. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya mzuri na leo hii nikaweza kusimama katika Bunge hili. Pia nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa Fulbright Prof. Ibrahimu Haruna Lipumba kwa kuchaguliwa na Wajumbe wa Mkutano Mkuu Taifa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi CUF. Nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Muftaha Abdalla Nachuma kwa kuchaguliwa na Wajumbe wa Mkutano Mkuu Taifa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi CUF. Vilevile nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Baraza Kuu la Uongozi wa Taifa kwa kumchagua Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya kuwa Naibu Mkuu wa Chama cha Wananchi CUF. *(Makof)*

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, atueleze hiyo anasoma ukurasa wa ngapi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, naomba ukae. Mhesimiwa Shamsia endelea.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anasoma ukurasa wa ngapi hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shamsia endelea.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, azma ya Serikali ni kuelekea Tanzania ya viwanda. Katika kuelekea Tanzania ya viwanda hatua ya kwanza ni kuondoa urasimu pale wanapokuja wawekezaji kwa kuapatia maeneo ya ujenzi haraka na mapema iwezekanavyo. Hata hivyo, Wizara ya Viwanda kumekuwa na urasimu na kodi kubwa hali inayopelekea baadhi ya wawekezaji kuhamia nchi jirani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ni Kiwanda cha Kubangulia Korosho cha Olam ambacho kilikuwa katika Mkoa wa Mtwara. Kiwanda kile kilifanya kazi vizuri sana na kuliweza kutoa ajira kwa wanachi wa Mkoa ule vijana na akina mama waliweza kuendesha maisha yao kupitia kiwanda hicho lakini mpaka sasa napozungumza kiwanda hicho hakipo kimehamia nchini Msumbiji. Je, Serikali haionti kuwa inakosa mapato na ajira kwa Watanzania? Nataka *commitment* ya Serikali hali hii ya kuhamahama wawekezaji katika nchi yetu itaisha lini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoimarisha viwanda nchini tunahitaji malighafi (*materials*) zinazozalishwa na wakulima wetu. Wakulima wakiwa na masoko ya uhakika wataweza kuongeza juhudzi za uzalishaji wa mazao ambayo ndiyo malighafi viwandani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee Shirika la Viwanda Vidogovidogo (*SIDO*). Tanzania tunalo Shirika la Viwanda Vidogovidogo (*SIDO*) lakini hatulitumii ipasavyo kwa sababu

*SIDO* wanabuni na kutengeza mashine na mitambo mbalimbali inayoweza kutumika katika kilimo, ujenzi, nishati, uchimbaji wa visima, lakini havitangazwi. Tumekuwa tukiona karakana nyingi za *SIDO* mitambo yake ni chakavu na haifanyi kazi kabisa matokeo yake wananchi na Serikali wanatumia fedha nyingi kununua mashine na mitambo mbalimbali kutoka China. Natoa wito kwa Serikali itumie teknolojia yetu mzuri ya *SIDO*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la wafanyabiashara wadogo wadogo. Ni ukweli kuwa akina mama wengi ndiyo wafanyabiashara ndogondogo na za kati, lakini nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuliona suala la vitambulisho kwa wajasiliamali wadogo wadogo. Pia niishauri Serikali akina mama lishe, wauza matunda, maandazi, samaki, wasamehewe au walipe kidogo kidogo kutockana na kipato chao kuwa kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shamsia kwa mchango mfupi na ushauri mzuri kwa Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa shughuli zetu kwa asubuhi hii umeishia hapo na wale ambao wameleta majina yao watakaofika mapema ndiyo nitawapa nafasi wachangie mwanzo na watakochelewa wanaweza kupata baadaye au kukosa kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi jioni.

(*Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni*)

(*Saa 10.00 jioni Bunge lilitrudia*)

**MWENYEKITI:** Haya, Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu. Tutaanza na Mheshimiwa Zainab Mndolwa, baadaye Mheshimiwa Mwanne Mchemba ajiandae.

**MHE. ZAINAB M. AMIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nami fursa hii ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema ili nami niweze kutoa mchango wangu katika hoja iliyokuwa mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa uchumi wa viwanda hautafikiwa ikiwa Serikali yenyewe ni kikwazo katika kufikia Tanzania ya viwanda. Nayasema haya kwa sababu mimi nipo katika Kamati ya Viwanda na Biashara, lakini kumekuwa na kusuasua kwa Hazina kupeleka fedha katika Wizara hii kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoishauri ni Serikali itenye fedha ya kutosha katika Wizara hii ili kuweza kufikia hiyo Tanzania ya viwanda. Tunaona takribani miaka mitatu mfululizo mpaka sasa hivi fedha inayotolewa ni kiwango cha chini sana na haikidhi. Licha ya kuwa ni kiwango cha chini, lakini pia haifiki kwa wakati. Kwa hiyo, naishauri Serikali, fedha ambayo inatengwa katika Bunge hili la bajeti ifike kwa wakati ili kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wale wamiliki wa viwanda ambavyo vinatumia sukari ya viwandani. Wamiliki wale wanadai fedha nyingi sana, kwa sababu waingizapo sukari hiyo huwa wanatozwa asilimia 15, lakini mpaka sasa hivi wafanya biashara hao wakubwa wanaidai Serikali shilingi bilioni 43. Hadi sasa hivi ni shilingi bilioni sita tu ambazo wamelipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoshangaa, wakati wanailipa ile asilimia 15 wale wafanyabiashara walikuwa wanailipa hela *cash* na ile fedha yao ni ya kuweka ili watakapomaliza kuitumia ile sukari watatoa taarifa yao na kurudishwa, lakini wanaporudishiwa wanarudishiwa kidogo kidogo. Sasa naiuliza Serikali, ni kwa nini, wakati wale wafanyabiashara wanailipa *cash* na hawalipi kidogo kidogo? Mpaka sasa hivi ni mwaka wa nne huu kumekuwa na kusuasua kwa ulipaji wa hiyo fedha. Naishauri Serikali, ili ifikie

Tanzania ya viwanda iwasaidie wananchi, iwasaidie hawa wafanyabiashara kulipa fedha hiyo kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusimdanganye Mheshimiwa Rais, Rais anataka Tanzania ifikie katika uchumi wa viwanda na ili kumsaidia, Wizara kama Wizara pamoja na Mheshimiwa Waziri ni kumpa ushirikiano. Wale wenye viwanda wanalamika mpaka sasa hivi fedha zao wanadai ni mwaka wa nne, wamendika barua nyingi na mpaka sasa hivi fedha zao hawajarudishiwa. Shilingi bilioni 43 mpaka sasa ni mwaka wa nne wamelipwa shilingi bilioni sita na hizo shilingi bilioni sita siyo kwa mfanyabiashara mmoja, kila mtu amelipwa kidogo kidogo. Mwingine shilingi bilioni moja, mwingine bilioni mbili. Kwa hiyo, Serikali yenyewe inakwamisha hii Tanzania kufikia uchumi wa viwanda. Naishauri Serikali iwalipe fedha zao kwa wakati kwa sababu ule ni mtaji wao na ni haki yao kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiyti, kingine ni kwamba viwanda vilibinafsishwa miaka ya 1990 na viwanda vile wakati vinabinafsishwa nia na madhumuni ni kuviendelea na kuweza kuwapatia ajira wananchi wetu na pia kupata pato la Taifa, lakini kuna wenye viwanda waliomilikishwa, wamechukua viwanda vile na kwenda kukopa fedha na kufanya miradi mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Kamati, tuliomba kuundwe Tume Maalum, kwa sababu, sisi kama Kamati tuliomba tutembelee vile viwanda kuangalia makaratsasi, kuwaambia kwamba viwanda vilivyobinafsishwa vingine vinafanya kazi vizuri, vingine vimefungwa, vingine vimeuza mitambo yao; lakini haitasaidia endapo sisi wenyewe kama Kamati hatutakwenda kwenye eneo husika na kujua hali halisi. Tumeomba kuvitembelea mpaka sasa hivi, hatujapata nafasi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, ili kufuatilia viwanda vilivyobinafsishwa na viweze kufanya kazi sawa sawa iundwe Tume Maalum ambayo itasaidia kufuatilia vile viwanda vyote vilivyobinafsishwa na kuviangalia kama kweli

vinafanya kazi kwa kususua na kama vingine havifanyi kazi kabisa ili wapewe wawekezaji wengine ambao wataweza kuviedeleza na kusababisha uzalishaji uwe mwingi na ajira ipatikane kwa wananchi wetu na pia kulipa kodi. Kwa sababu tunajua kuna maeneo mengi kuna viwanda ambavyo vilikuwa ninafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mwaka 1985 nilikuwa nasoma Shule ya Sekondari Morogoro, *Form One*; mwaka ule ukifika Morogoro viwanda vilikuwa vingi, unapata ajira mara moja, lakini ni vigumu sana kupata eneo la kuishi. Kulikuwa na viwanda vya *Canvas, Ceramic, Polyester, Moro Shoe*, vilikuwa vingi sana lakini viwanda vile vimekufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri, wakati Serikali inatafuta wawekezaji kwenda kukata mapori na kuanzisha viwanda vingine kwanza vifualiwe vile viwanda kwa sababu maeneo yapo, majengo yapo kinachotakiwa ni kubadilisha tu miundombinu iliyokuwepo pale na kiuweka ya kisasa ili kuweza kuleta uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni ulipishwaji wa kodi kwa wafanyabiashara kabla ya kuanza kufanya biashara. Tumewaona wafanyabiashara wengi ambao wanataka kuanzisha biashara zao hususan mijini kwenye maduka, kwanza ili wapate leseni ni lazima wakalipe mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, itoe muda maalum ambao utamsababisha yule mfanyabiashara anapotaka leseni, natolea mfano kwa Mkoa wa Dar es Salaam, ukitaka kufungua duka lako unakwenda pale Anatoglo (Mnazi mmoja) unataka leseni, hawakupati leseni wanakwambia kwanza nenda *summit tower* pale makutano ya Lumumba na Uhuru ili kuweza kupatiwa *tax clearance* na hiyo *tax clearance* huwezi kupewa mpaka utoe mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza, mimi biashara ndiyo nakwenda kufanya au mfanyabiashara anataka aanze biashara, unamkdiria mapato; hayo mapato ameuza kitu gani? Hii ndiyo inakwamisha wananchi. Inakwamisha

wafanyabiashara kushindwa kuendelea baada ya mwaka mmoja hufunga maduka yao na kuacha kwa sababu Serikali inatakiwa impe muda na kama imempa mashine ya *EFD* itatumia ile mashine kuweza kukadiria mapato na kuweza kumkadiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, mwananchi atakapofungua biashara kwanza apewe muda maalum angalau miezi mitatu ndipo aanze kulipa mapato, lakini kitendo kinachofanywa na Serikali sasa hivi kuititia *TRA* kuanza kumpa mtu makato kabla ya kufanya biashara, kusema kweli ni kitendo cha dhuluma na hiki hupelekeea wafanyabiashara wengi kufunga maduka yao hususan maeneo ya mijini ninayozungumzia ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia biashara zinazofanywa, wanaolipa kodi ni wachache. Kuna kaulimbiu ya Mheshimiwa Rais inasema "ukiiza toa risiti na ukinunua dai risiti", lakini sasa hivi ukifika Mkoa wa Dar es Salaam kuna wafanyabiashara. Hatuwakatai kwamba ni wafanyabiashara ndogo ndogo nao wana wajibu wa kufanya baishara, lakini wanauza mbele ya maduka ambayo wanalipa kodi. Wafanyabiashara wale hawalipi kodi yoyote kwa Serikali na ukiuliza unaambiwa ni wapigakura wetu. Tunaisaidia Serikali au tunaangamiza Taifa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni na madhumuni ni kupata kodi; na kama umempa kitambulisho cha shilingi 20,000/= basi tuwatafutie maeneo maalum. Kwa sababu *tendency* ya Mwfrika, *tendency* ya Mtanzania anaona biashara inayouzwa barabarani ni rahisi mno kulikoni ya madukani; na hii ndiyo maana inapelekeea wafanyabiashara wengi wanafunga maduka yao kwa sababu hata kama ukiiza wanaona barabarani ndiyo rahisi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawe mwenyewe ukipita maeneo ya Kariakoo utaona msongamano mkubwa kwenye barabara. Hata barabara ya Msimbazi ni vigumu kupita watu,

wafanyabiashara wamepanga biashara zao mpaka milangoni mwa maduka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishauri Serikali itenye maeneo maalum kwa wale wafanyabiashara wanaolipa kodi ili waweze kuwa na uwezo sasa wa kuuza na kuweza kulipa kodi na ikifikia mwisho wa mwaka wasiweze kufungiwa maduka yao. Wale wanaoambwa kwamba wao ni wapiga kura hawatakiwi kulipa kodi ni kitambulisho tu ambacho kinamwidhinisha afanye biashara, basi watengewe maeneo yao. Naishauri Serikali ifuatilie jambo hili ili kuweza kuwa na mapato zaidi katika nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naishauri Serikali itumie malighafi inayopatikana katika viwanda vyetu. Malighafi hiyo itasaidia kukuza kilimo chetu ambacho kitapelekea wananchi kupata kipato na kulima zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara ya Viwanda na Biashara, watendaji wengi wamekaimishwa. Naishauri Serikali sasa ijaze zile nafazi zilizokaimishwa ili wale Watendaji wawe na nafasi ya kuweza kutoa maamuzi yao katika kuendeleza Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zainab Mndolwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Mwanne Mcemba, baadaye Mheshimiwa Njalu Silanga na Mheshimiwa Riziki Lulida, wajiandae.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kwa siku hii ya leo nami niweze kuchangia Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nashukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kuamka leo salama na kunipa nafasi kama hii ya pekee kuweza kuchangia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na pungezi. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuleta Sera ya Viwanda nchini na kuisimamia yeye mwenyewe kikamilifu. Nampongeza sana kwa sababu siyo hilo tu ameyafanya Mheshimiwa Rais wetu, lakini ana mengi ameyafanya katika nchi hii kwa kutekeleza llani ya Uchaguzi ya mwaka 2015/2020. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Makamu wa Rais, anafanya kazi nzuri ya kumsaidia Mheshimiwa Rais, wamejipanga. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake, wanafanya kazi nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia. Nimeanza kwanza kwa pungezi, sasa nakwenda kwenye jukumu kubwa ambalo ninalo moyoni mwangu. Mheshimiwa Waziri naomba Mwenyekiti alipokee hili na alisikilize kwa makini. Nataka nizungumzie habari ya kiwanda cha Tabora cha Nyuzi (*TABOTEX*). Kiwanda hiki kimeanza muda mrefu, tangu mwaka 1978 kama sikosei au 1975. Baada ya kubinafsishwa, kiwanda hicho kimesuasua na mpaka leo hakifanyi kazi. Malighafi yote imeondolewa. Nilishamwomba hapa ndani Mheshimiwa Naibu Waziri twende mimi na yeye akaangalie hali halisi ilivyo kwa sababu hatuvezi kukubali kutafuta wawekezaji ambao ni wababaishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda hiki kilikuwa kinasaidia sana ajira kwa watu wa Mkoa wa Tabora, lakini mpaka sasa hakuna ajira, vijana wanahangaika, lakini mwekezaji hakuna chochote alichokifanya. Nilitegemea basi, kwamba angalau Mheshimiwa Waziri angeweza kuiweka mle *TABOTEX*. Nimeangalia ukurasa wa nane hamna kitu, nimeangalia ukurasa wa 20 hamna kitu, labda mimi sijui kusoma. Kama sijui kusoma leo Mheshimiwa Waziri ataniambia kwamba ameiweka wapi? Kiwanda cha Nyuzi ambacho ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda hiki historia yake ni kwamba kulikuwa na Mbunge anaitwa Marehemu Mzee Misigalo. Miaka ya nyuma ili kuweza kufanikisha alimwombwa

Baba wa Taifa kwamba kiwanda hiki kiwepo Tabora baada ya kuonekana kwamba hakuna kiwanda chochote ambacho kinawezekikawa kinatengeneza nyuzi kwa Kanda ile ambayo wanalima pamba. Kwa hiyo, akaitoa shilingi, nami leo naitoa kwako. Aliitoa Shilingi, Baba wa Taifa akampa hicho kiwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri mwaka uliofufuta anaomba kura, wakampa tena akatawala vipindi viwili. Aliviyotawala vipindi viwili, hakuna tena aliyejunja ile historia kwa sababu ya kile kiwanda. Sasa nami kwako Mheshimiwa Waziri shilingi hii nitaondoka nayo, naenda nayo Tabora mpaka wewe uje ujieleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni ujenzi wa Kiwanda cha Tumbaku. Ujenzi wa Kiwanda cha Tumbaku tulitegemea pia tungekiona humu kwenye kitabu hiki, hamna. Tumbaku inalimwa Tabora asilimia 60 na tuliomba kwamba kuwepo na kiwanda cha kutengeneza, kusindika Tumbaku Mkao wa Tabora lakini hakimo. Mheshimiwa Waziri ana ajenda gani? Ana ajenda gani wakati Tumbaku tunailima sisi wenyewe? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda hiki ghamara zake ni kubwa ambazo wanatoa tumbaku kupeleka Morogoro. Wakipeleka Morogoro, ghamara yote inakwenda kwa mkulima na wakulima wa tumbaku wanalima katika mazingira magumu, hawana afya nzuri kutokana na usumbufu wa zao la tumbaku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliweka mazingira mazuri ya suala zima la bei ya tumbaku, lakini nilitegemea sasa leo Waziri mhusika mwenye dhamana angeweza pia akaliongelea hili suala la kiwanda cha tumbaku kwa ajili ya Mkao wa Tabora na nchi nzima, kwa sababu Kanda ile yote Kigoma, wapi wanalima tumbaku, lakini hakuna kitu chochote alichowezekikawa kuandika. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie hili kwa upana, ni jinsi gani atakavyojipanga aliweke hili jambo la

kiwanda cha nyazi aweke pia na suala zima la kiwanda cha tumbaku. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la *SIDO*. *SIDO* ni mkombozi mkubwa sana, watu wanadharau; *SIDO* imeweza kulea wanawake, imewatoa wanawake na vijana kwenye ujasiriamali sasa wamekuwa wawekezaji wakubwa, lakini hakuna fedha yoyote ambayo inakwenda kwenye mikopo. Kwa hiyo, bado nina wasiwasi, tunawasaidiaje vijana na wanawake kwa kuidharau *SIDO*? *SIDO* ilitakiwa ipewe fedha nydingi ili waweze kukopesha wanawake na vijana na walemavu, watu wote ambao ni wajasiriamali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia vifungashio. *SIDO* imewaelimisha wananchi, wajasiriamali wote wamepita mafunzo ya *SIDO* na ndiyo maana wanajua maana ya vifungashio. Sasa hivi wanafnyakai nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Maonyesho ya Saba Saba. Wajasiriamali wanateuliwa wachache sana tena kwa kuitia vikao ambavyo havihuksiki na *SIDO*. *SIDO* wanaleta tu mwelekeo, wanatoa waraka, lakini nani anayeweza kudhibiti wajasiriamali ili waende kwenye Masoko ya Maonyesho ya Kimataifa na Maonyesho ya Saba Saba? Ni lazima *SIDO* iingize mkono wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili *SIDO* iweze kufanya kazi nzuri, mimi siafiki kutokuwapa pesa *SIDO*. *SIDO* hawapati fedha zozote. Kwa hiyo, hata mimi ningeweza kuishauri Serikali, kama kuna fedha nydingine zozote ambazo wanaona ni rahisi kuwafikia walengwa, wananchi ambao ni wa chini, lazima ipitie *SIDO*. Tangu imeanza *SIDO* haina mgogoro wowote wa kazi kubwa ambayo inafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, ukiisoma kwenye taarifa ya *SIDO*, urejeshaji wa mikopo ni tofauti na asilimia 10 ambayo inatolewa na Manispaa au Halmashauri. Wao wameweza kukusanya marejesho asilimia 91.5. Hata ukitaka kusoma lile jedwali lake liko ukurasa namba 16. Ni watu ambao wanawea wakasaidia nchi hii kuondokana na figisu

figisu ya mikopo midogo midogo kwa sababu mikopo yao ni ya riba nafuu. Kwa hiyo, nilikuwa nataka nizingatie hayo ambayo ni ya muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho mimi sikutaka kuchangia mengi. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, sitaki kuichafua Serikali yangu, lakini utakapokuja hapa unipe majibu ya mambo mawili; la kwanza Kiwanda cha Nyuzi, kwa nini wanaondoa vifaa wanapeleka Manonga? Vingi wamepeleka Manonga. Kwa hiyo, nataka majibu hayo, kwa sababu sasa hivi asilimia 100 ya wakulima wa pamba wanatoka Igunga. Kwa hiyo, bila hilo, sitaki kukosana, nimesharudia mara tatu, mara nne; nitakosana na wewe kwa ajili ya Kiwanda cha TABOTEX, nitakosana na wewe bila kupata majibu. Sitaki kujua kama unatoka Tabora au unatoka wapi! Mimi sitambui. (*Makofi*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mimi najua wewe ni Waziri, kwa hiyo, siitambui. Yeye ni Waziri lakini sitaki kujua huko nyuma kama anatoka Tabora. Mimi na wewe humu ndani ama kesho patakuwa hapatoshi. Nipate majibu mawili ya Kiwanda cha Nyuzi na Kiwanda cha Tumbaku, lini kitaanza mchakato? Hayo ndiyo ya kwangu ambayo nataka wewe Mheshimiwa Waziri sasa, nakuomba, nam-address yeye kwa sababu haijalishi kama anatoka wapi? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanne Mcchemba. Tunaendelea na Mheshimiwa Njalu Silanga, baadaye Mheshimiwa Riziki Lulida na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, wajiandae.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Wizara

hii ya Viwanda na Biashara. Naungana na Waheshimiwa wenzangu wote waliochangia katika Wizara hii. Nataka tu kufahamu, kuna mazao matano ya kimkakati, lakini kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri hapa nimetezama sijaona sehemu yoyote ile. Sasa ndiyo utakuta unapata mkanganyiko wa kujua anayesimamia hiyo biashara ni nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuelewa mwenye dhamana ya biashara na mikokotoo yote tunayohangaika nayo humu ndani, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana hii anaweza akawa na mchango mkubwa sana kuisaidia Serikali na kujua tumekusanya kiasi gani na changamoto zilizoko kwa wafanyabiashara ni kiasi gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunalo zao la Pamba, Kahawa, Tumbaku, Korosho na MBAAZI, lakini Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ambaye ndiye kabeba jukumu la kibashara na Waziri huyu anatakiwa afanye mazungumzo na wafanyabiashara kujua changamoto zao zote na kuzipeleka Serikalini ili zitatuliwe lakini tumekuwa na mkanganyiko mkubwa sana. Waziri wa Kilimo ndiye mwenye sera, lakini yule ni mzalishaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na malalamiko mengi, kila Bunge likikutana lazima wazungumze, lakini Waziri mwenye dhamana haonekani katika sekta nzima ya biashara. Kwa hiyo, ningeshauri Mheshimiwa Waziri aje atueleze, majukumu yake ni yapi? Labda ni Waziri wa Viwanda tu pekee bila biashara. Naamini kama ni Waziri wa Viwanda na Biashara anaweza akawa na mchango mkubwa na akasaidia nchi hii. Naye tu kwa uelewa wangu, Waziri wa Fedha anaweza akawa ndiyo Mhasibu wake, lakini yeye ndio anaweza akajua makadirio tunayoyakadiria haya tunaweza tukakusanya kodi zaidi kuliko mtu ye yeyote mwengine humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Waziri mwenye dhamana hajui biashara zinakwendaje hapa nchini, lakini kuna Wajumbe wenzangu wamezungumza vitu vingi. Kuna mambo yamezungumzwa ya *OSHA*, sijui *WFP* na kadhalika,

yote haya Mheshimiwa Waziri yanakulenga wewe ili uwasaide wafanyabiashara. Ili Serikali hii isiwe na malalamiko na wafanyabiashara wewe ni jukumu lako kuhakikisha unasi mamia sera nzima ya biashara. Ukifanya hivyo, utakuwa umepunguza dhana nzima ya ulalamikaji katika maeneo mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi kuna Wajumbe wamegusia suala la *General Tyre*, lakini tunacho pale Kilombero mavuno ya Matairi. Watu wa Kenya (*Firestone*) wanachukua malighafi yetu, inakwenda Kenya halafu ndiyo tunaletewa matairi.

Mheshimiwa Waziri, ukiangalia tu ni magari mangapi yanayopita kwenye nchi yetu kuzunguka wanapohitaji matairi? Kwa hiyo, ni suala ambalo ukiliangalia linaweza likatusaldia na tukapiga hatua kubwa sana katika dhana nzima ya uwajibishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la *TBS*, wawekezaji wamekuwa wakifanya *analysis* za kwanza ana kiwanda chake labda cha *Oil Mill* linachukua muda mrefu zaidi ya miezi miwili, lakini katika dhana nzima ya uwekezaji inaleta changamoto katika maeneo husika. Ningeshauri Serikali iboreshe mfumo mzima wa *TBS* ili kusudi wafanyabiashara hao wanaowekeza katika nchi yetu, wanapowapeleka *sample* yao basi ichukue angalau hata siku 30 au 20 sio kwa miezi miwili na hiyo miezi miwili inachukua muda mrefu. Wameboresha wakaweka *TFDA* sehemu ya kwanza na sehemu ya pili. Sasa nashauri watengeneze mfumo mzima wa kusaidia dhana nzima na waweke kikanda, isiwe tu Dar es Salaam peke yake wakiweka kila kanda itatusaidia kuhakikisha kwamba watu wanapiga hatua katika dhana nzima ya uwekezaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia suala la masoko, nimeligusia. Serikali yetu kuititia llani ya Chama cha Mapinduzi tulisema tutaboresha ushirika na tunavyo vyama vyta ushirika na tunavyo vinu vinachombaua pamba katika maeneo mbalimbali. Nimeona kwenye ukurasa waa kitabu

cha Mheshimiwa Waziri amezungumzia suala zima la kwamba amerudishiwa viwanda vilivyokuwa 156 na amebaki na vingapi na vingapi. Katika hali nzima ya kuhakikisha ananufaisha na kuboresha ushirika, Mheshimiwa Waziri anaweza akaniambia ni maeneo yapi ambayo ushirika umeimarika na unachakata mwenyewe bila kupitia fedha za wafanyabiashara. Naomba nalo hilo atusaidie katika majumuisho yake kwamba ameboresha hiki na amepiga hatua kufikia mahali hapa itatusaidia nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima lingine, wenzangu wamezungumza mchana hapa, kuna kiwanda cha BORA tena ni cha kizalendo cha Watanzania, Mheshimiwa Waziri atusaidie malalamiko haya watu wanayoyazungumza kulingana na uzalishaji uliopo hapa nchini, taasisi zote za kiserikali ziangalie namna gani ya kwenda kuunga jitihada hizi za wawekezaji walio kwenye maeneo yetu ili wasaidie kuongeza uchumi wa nchi na pato la Taifa, kuliko hivi sasa watu wanazalisha mali inakuwa nyangi, matokeo yake ngozi inakosa mahali pa kununuliwa ni kwa sababu mali haitoki. Mheshimiwa Waziri akitusaidi hilo atakuwa ameweka mfumo mzuri wa kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anao wataalam waliobobea kwenye eneo lake hilo la kibiashara, naamini akiyachukua haya mawazo na akitengeneza mfumo wa kufanya mazungumzo kama Waheshimiwa Mawaziri wengine wanavyofanya, *trip* ijayo hatutampigia kelele, lakini sasa hivi ni kukutana tu mitaani anakwenda huku na huku, lakini walenga hajakutana nao na wana mawazo mazuri, naamini akishirikiana nao mtu wa kilimo abakize kuzalisha, suala la biashara asimamie Mheshimiwa Waziri itatusaidia na ndio maana miaka ya nyuma Kilimo, Chakula, Ushirika na Masoko ilikuwa ni Wizara moja lakini wakaona watofautishe, sasa leo tunavutana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika hili akitufanyie utaratibu huu, biashara zitasonga mbele na shughuli zitakwenda mbele zaidi. Hilo litakuwa sehemu kubwa sana ya kuongeza uchumi katika maeneo yetu na nchi nzima

kwa ujumla. Haya akiyachukua Mheshimiwa Waziri itatusaidia sana lakini tutakapokuwa tunaendelea kupiga kelele na Mheshimiwa Waziri wa Biashara anakuwa ni sehemu, leo ameomba bilioni 100, yeye ni sehemu kubwa ya kuwezesha shughuli hizi zisitembee mara moja, kwa sababu wafanyabiashara wote anao mwenyewe, sasa sielewi ni kigugumizi gani ambacho anakipata, anashindwa kukutana nao na kupata mawazo mazuri ya kuhakikisha nchi inapiga hatua na uwekezaji unakwenda kwa kasi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri asipofanya hivyo itakuwa kila siku watu tunalamika lakini mwisho wa siku hakuna jibu lolote lile na mwisho wa siku kama walivyosema wenzangu mchana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Njalu. Tunaendelea na Mheshimiwa Riziki Lulida na baadaye Mheshimiwa Hawa Mwaifunga na Mheshimiwa Zawadi Kiteto Koshuma, wajandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika hoja iliyoko mezani. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia kupata nafasi hii. Nitaanza kuchangia katika suala la mazao mkakati ambayo unayaona hayamo ndani ya utekelezaji katika bajeti nzima ya mwaka huu. Zao la kwanza katika Tanzania ambalo linaingiza uchumi mkubwa ni zao la korosho. Hata hivyo, zao hili la korosho halimo kabisa kama ni zao ambalo linaweza kuchangia uchumi wa nchi wameliacha nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima analima, anasafisha shamba, anapulizia dawa, lakini unapofikia wakati wa kuuza anaanza kukwamishwa anaambiwa ana

*kangomba*, sasa nini maana ya *kangomba*? Ni vitu ambavyo vinajitokeza kuwakwamisha wafanyabiashara wasiweze kufanya biashara ya tasnia ya korosho. Kwenda kununua mchele Mbarali sio *kangomba*, kwenda kununua mahindi Rukwa sio *kangomba*, kwenda kununua chochote sio *kangomba*, *kangomba* inaingia kwenye zao la korosho. Tujulize swalii, je, huyo mwananchi aliyejikuwa kijijiini maporini, barabara hakuna anaipelekaje korosho yake Liwale Mjini? Mwananchi aliyejikuwa Namtumbo kijijiini anapelekaje korosho yake Namtumbo Mjini wakati hakuna barabara? Sasa iweje watu wengine wanapewa nafasi ya kuleta mazao yao wakayaauza huria lakini inapofika tasnia ya korosho tunaambiwa ni *kangomba*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wameshindwa kufanya biashara zao safari hii, wamekwamisha uchumi kwa ajili ya *kangomba*. Naiomba Serikali illiangalle neno la *kangomba* ilifute kabisa kwa vile kama wengine wanaweza kufanya biashara Tanzania nzima haina haja ya kuliweka neno la *kangomba* likawakwaza wananchi. Mwananchi amekaa Mpigamiti anataka kuja Liwale hana gari, hana usafiri, anapelekaje korosho yake. Naomba hili neno la *kangomba* lifutwe kabisa linaleta chuki na maudhi katika maeneo ya wakulima wa korosho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la korosho na mazao mengine mchanganyiko hayakutengenezea mfumo wa kibashara ambao ungeweza kusaidia mazao yao yaweze kununuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Rwanda wametengeneza *one stop center* kwa ajili ya manunuzi ya biashara zao, wamejiingiza katika *World Trade Center* mbalimbali duniani, leo sisi tunategemea mazao yote tupeleke Kenya au Uganda au Rwanda, tujulize wataalam wetu wanafanya kazi gani hapa Tanzania? Wanafanya nini kuhakikisha wana-promote mazao? Tanzania tuna mazao lakini huwezi kuuza mazao yako mpaka yapelekwe Rwanda, kwanza tujulize tumezidiwa nini na Rwanda mpaka sisi tukashindwa kufanya vile? Pana upungufu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kakunda alikuwa mjumbe mwenzangu, namfahamu, ana uwezo mkubwa sana, pale unapoona kuna watendaji ambao huwezi kufanya nao kazi, bwana mhamishe au mtoe, sasa hivi tunataka Tanzania yenye uwezo, yenye uchumi na utekelezaji katika masuala ya biashara na viwanda. Hando tunakwenda nao na unamwona Mheshimiwa Rais amesimama, ana uchungu lakini, je, unao watendaji wa kufanya nao kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja suala la *balance of trade*; leo Tanzania tunasema tunataka uchumi wa viwanda, watu wameanzisha viwanda, leo Kiwanda cha Dangote, tunaagizia katika miradi mikubwa ya *Stiegler's Gorge* na miradi mikubwa ya *SGR*, wanaagiza *cement* Tanzania walikaa nao chini wakasema jamani ongeza viwango vyako illi angalau *cement* ya Dangote iende katika uchumi wa maendeleo tunayofanya sasa hivi. Matokeo yake dola imepanda, kila kitu sasa hivi na wahujumu wanapitia humo humo kuingiza *cement* kutoka nje, nondo kutoka nje, vifaa vyote vya ujenzi vinatoka nje, tutakwenda katika uchumi ambao hauna *balance of trade*. Tuna wafanyabiashara wanaoleta vinywaji, maji yanatoka China, *juice* zinatoka China, kila kitu kinatoka nje Bakhresa atafanya kazi gani, Udzungwa atafanya kazi gani, tumefikia mahali halafu wanapewa misamaha ya ushuru, wanapewa zero VAT, matokeo yake atakwendaje mfanyabiashara wa ndani, hivyo tunavokwenda ina maana tunapingana na mifumo na sheria ambazo zinawakwaza wafanyabiashara. Wafanyabiashara kila mmoja anafunga (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mradi wa vyandarua huko Arusha, chandarua kinatoka China zero kibovu, sasa huyu atauza chandarua bei gani *A to Zameshakuja* zaidi ya mara tano anajiuiliza zinaletwa chandarua mbovu na Tanzania bado tuna *malaria*, analeta chandarua ambacho kina dawa na kila kitu anaambiwa bwana, hawasikilizwi tu! Tumefikia mahali tunajiuiliza kweli tumetaka nchi hii tuiendeleze, mifumo tuliokuwa nao uko sahihi na uchumi wetu, tumejipanga kweli ama laa. Maana yake kujipanga *at least*

10 years mbele ili angalau tujue tunafanya moja, mbili, tatu, matokeo yake pale panaachwa hapa panashikwa, matokeo yake watu wamekaa *desperate* hawajui wanafanya nini kibashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani yangu, tujipange maana yake nikiangalia nenda Temeke maduka yamefungwa, Kariakoo maduka yamefungwa, kila mahali maduka yamefungwa, leo Watanzania wanakwenda kununua bidhaa Uganda, bandari iko Dar es Salaam ukichukulia mzigo kutoka Dar es Salaam mpaka Uganda unalipwa lakini kwa nini anapata unaifuu wa kwenda Rwanda, pana kitu kimesimama hapa. Sasa nataka niorodheshe katika vitu ambavyo vinaukwamisha uchumi wa bishara na viwanda kwanza *TRA*. *TRA* ni mwiba, mwiba, mwiba wa uchumi wa Tanzania, watendaji wabovu ambaao wako ndani ya *TRA* wamejigubika wimbi la *TRA* wanaifanya nchi hii iyumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kusema ni wapi, isipokuwa waifumue *TRA* na waaangalie upungufu uko wapi, maana yake leo unafungua kampuni, hujaanza kazi wanakwambia tunakudai, watakusumbua na kesho wanakwambia tunakufungia. Mwenye kiwanda ana vurugu mara *OSHA*, pana *regulatory bodies* 47 atafanyaje kazi mtu kama huyu? Ina maana tumewakwaza wafanyabiashara wasitoke, matokeo yake tumebakia tumesimama, mbele hatuendi, nyuma hakutikisiki, mtihani kabisa mimi nauona huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuja ajira ndani ya viwanda, niilikuwa Kamati ya *P/C*, tukatembelea kiwanda cha *EPZ* cha kutengeneza *jeans*, unasema Tanzania tumeajiri watu 59,000 wameajiriwa kama vibarua, wanachukuliwa kila baada ya miezi mitatu. Baada ya pale anafukuzwa, inakuja benchi ya pili, hii huwezi kuita ajira. Ajira ambayo na analipwa mshahara mdogo kwa mwezi 100,000 na wanakimbia kuwa atalipwa haki zake za msingi. Sasa tunatakiwa tuangalie viwanda vinaendana na matatizo ya ajira, isiwe tunaleta viwanda lakini ajira tunawaletea watu wa nje na maeneo mengine kama unaenda unakuta wameja watu wa nje sio

Watanzania. Tulisimamie suala la viwanda vya ndani na ajira ya Watanzania ili kuweza kuleta tija na Watanzania hao wajione wako katika nchi yao.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa huku *CUF*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unayechangia endelea, yuko wapi simwoni Mheshimiwa Lulida naomba uendelee.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejiona Kiwanda cha Dangote kikiajiri watu kutoka nje 120 mpaka wafagiaji, sasa tunajuliza, watu wale wa Mtwara ambao tunesema tutapata *opportunity* ya kupata kazi na kupata ajira na kila kitu mpaka mfagiaji anatoka nje, tuna haja gani ya kuwa na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanzisha viwanda, tunasikia leo tumeleta matrektu, vijana hawa wadogo wanaomaliza darasa la saba ilibidi wapelekwe *VETA* wakasomee hata ufundi mchundo iwasaidie hata *trektu* likiharibika atakuwa anaweza kufanya kazi na ndio walivyotoka China, walivyotoka Thailand na nchi mbalimbali, lakini vijana wale wamekaa majumbani, wanacheza *pull*, wanakula madawa ya kulevyta, matokeo yake mfumo wa kibiashara uliotengenezwa katika kipindi kifupi umefanya nchi imedhoofika na imedorora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nasema nashukuru sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Zawadi Kiteto Koshuma na Mheshimiwa Kanal Mstaafu Masoud ajiandae.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingu wa rehema kwa kuniwezesha kusimama hapa katika Bunge hili Tukufu na kuchangia hoja ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sana nieleze kuhusu bajeti katika Wizara hii, kwa miaka mitatu mfululizo sasa bajeti ya Wizara ya Viwanda imeendelea kushuka siku hadi siku. Mwaka 2016/2017 bajeti ilikuwa ni asilimia 42.37; mwaka 2017/2018 ilikuwa asilimia 30.64; mwaka 2018/2019 ilikuwa ni asilimia 24.28, hiyo ni fedha ambayo inapelekwa katika Wizara ya Viwanda na Biashara. Kauli mbiu ya CCM ya Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Magufuli ni uchumi wa kati, Tanzania ya viwanda. Tanzania hii ya Viwanda inafikiwaje kwa bajeti ya aina hii? Hivi kweli tuko *serious* kabisa kwamba tunahitaji uchumi wa kati kwa Watanzania kama hata bajeti ya Wizara inayohusika na masuala ya viwanda na biashara bajeti inakwenda kwa kiwango hiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara na siku zote nimekuwa nikijuliza hivi wenzangu Wabunge wa CCM ambao tuko nao kwenye Kamati, hivi mko *serious* kweli kabisa kwamba hii kauli mbiu ya Mheshimiwa Rais mnaishikilia kidedea? Maana kila Mbunge wa CCM akisimama hapa ni *Stiegler's Gorge*, ni *standard gauge* ni ndege sijui hiyo haikuwa kauli ya Mheshimiwa Rais wakati anaomba kura. Haya yamejitokeza kila siku wanayasifia haya, hebu watuambie, hii Tanzania ya viwanda iko wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu anayeonekana kinara wa Tanzania ya Viwanda ni Mheshimiwa Rais peke yake. Kila anapokwenda atasimamia suala la viwanda lakini hakuna anayemsaidia kwenye suala hili. Amezungumza Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, hivi kweli Waheshimiwa Mawaziri waliopewa dhamana kwenye hii Wizara wanadhani wanaitendea haki. Hawaoni kwamba wanaenda tofauti na kauli mbiu ya Mheshimiwa Rais na kwenda tofauti na kaulimbiu ya Rais ni kukiuka maneno ya Mheshimiwa Rais. Hebu niwaombe sana tuwe *serious* kwenye hili, Wizara ya Fedha pamoja na fedha kuwa kidogo lakini hebu waangalie vipaumbele tumezidi kuwa na vipaumbele vingi, inafika mahali hata kile kipaumbele ambacho walikikusudia hakitekelezeki. Halafu tunaimba Tanzania ya Viwanda,

Mheshimiwa Rais akienda kuzindua viwanda anafurahi, lakini unashangaa anafurahi leo, kesho *TRA* wanakwenda pale kila kiwanda kinakwenda kufungwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sana tumeshindwa hata kuvilinda viwanda tulivyonyavyo nchini. Leo viwanda vilivyopo nchini vinazalisha kwa ubora wa hali ya juu, lakini utashangaa hata Serikali yenye we inapotengeneza miradi inakwenda kuagiza nje. Sasa hawa wanaotengeneza humu ndani nani atanunua bidhaa zao. Tunaagiza bidhaa nyingi kutoka nje, tunawapa *zero rate*, matokeo yake bidhaa zile zinazotoka nje zinakuwa bei ndogo kuliko bidhaa za ndani na humu ndani watu wanawachaji kodi, kuna umeme, kuna wafanyakazi, kuna *regulatory authorities* chungu nzima ambazo zote hizo wafanyabiashara hawa wanatoa fedha. Wanajikuta wanashindwa kufanya uzalishaji wa kutosha kwa sababu ya ghamama za uzalishaji na leo bado sisi kama nchi tunaendelea kuendekeza kuingiza vitu ambavyo hata Tanzania tunazalisha tena kwa kiwango cha hali ya juu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba nitoe wito kwa Serikali kama kweli tunataka Tanzania iendelee kuwa ya viwanda hivi viwanda tulivyonyavyo hebu tuvilinde tuwalinde hawa wafanyabiashara wenye viwanda waliopo nchini kwa sasa, wenye moyo ambao bado hawajakimbia. Kama hali ikiendelea namna hii, kama kiwanda kilikuwa kinazalisha kwa asilimia 80, leo kiwanda kinazalisha kwa asilimia 15, kuna tija namna hiyo jamani, halafu tunasema hii ni Serikali ya viwanda, Serikali ya viwanda ipi jamani? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumza wenzangu lakini nami naomba nikazie, *TRA* ni mwiba mchungu sana kwa wafanyabiashara. Wafanyabiashara wamelalamikia sana *TRA*, sio rafiki tena wa mlipakodi, badala yake amekuwa ni adui mkubwa sana wa mlipakodi, badala ya *TRA* na mlipakodi kuwa marafiki, kukaa, kuzungumza na kuona ni kwa namna gani ambavyo wanaweza wakalipa kodi, *TRA* wamekuwa wababe, *TRA* hawataki kusikiliza, *TRA* inatukosesha mapato, *TRA* inasababisha maduka

yanafungwa, *TRA* inasababisha viwanda vinafungwa. Leo nilikuwa namsikia mtu wa *TRA* anasema biashara zaidi ya milioni moja zimefungwa, huo ndio ukweli, kama kuna watu wamesikiliza *clouds* asubuhi, zimefungwa ndio!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tuone sasa, tunachokiangalia tuna- *target* kitu gani, tunataka kodi, lakini kama tunataka kodi na maduka yanafungwa kodi hizo tunazipata wapi? Tunataka kodi, viwanda vinafungwa kodi hizo tunazipata wapi? Leo viwanda vinapofungwa, ajira pia zinapungua, kwa hiyo tuone ni kwa namna gani tunavyoweza kuweka mfumo mzuri ama kuiangalia *TRA* kwa jicho la tatu, inawezekana wako watu ambao wana mpango wa kukwamisha hii nchi isiende mbele. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nieleze kwa masikitiko makubwa sana kuhusiana na suala zima la viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo vingi havifanyi kazi. Mara zote tumekuwa tukiipigia Serikali kelele mtueleze mna mpango gani na hivi viwanda vilivyobinafsishwa? Ukiuliza kwa watendaji wao wanafuata sheria na utaratibu lakini niwaambie Watanzania mikataba iliyoingia kuwauzia viwanda watu hawa ni mibovu ambayo inasababisha hivi viwanda sisi kama Watanzania tutashindwa tena kuvifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikumbuke kauli ya Mheshimiwa Rais amesema hawa watu ni wahujumu uchumi. Leo mtu amenunua kiwanda kazi anayofanya anapanda maua. Tumekwenda kwenye kiwanda kimoja Arusha, kiwanda kinazalisha vizuri sana, kinalipa kodi vizuri sana lakini eneo walilonalo ni dogo. Kwa muda mrefu sasa wanaiomba Serikali eneo la nyuma ya kiwanda chao ambapo kuna kiwanda kingine kinatumika kupanda maua ili waweze kuongeza uzalishaji kwenye kiwanda chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili limeshindikana na tunamuuliza Waziri tatizo ni nini na wao nafikiri bado hawajajua tatizo kwa sababu Naibu Waziri hakuwa na majibu ya kutuambia. Hata tulipokuja kwenye kikao tunamuuliza

Naibu Waziri wamefikia wapi kuhusiana na suala hilo hakuwa na majibu ya kutuambia. Leo katika Bunge hili tunaomba mtuambie Serikali mna mpango gani wa kuwapa *TBL* eneo hilo wanaloomba ili waongeze uzalishaji ili muendelee kupata kodi badala ya ilivyo hivi sasa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tangu suala la viwanda lipelekwe kwa *TR*, hili Waziri wa Fedha atuambie ni lini Waziri wa Fedha mtatusaidia kturejeshea viwanda vyetu kwa sababu viwanda vyote viko chini ya *TR*? Kama viko chini ya *TR*, Wizara ya Viwanda haina mamlaka na viwanda hivi, kwa hiyo, kila tunavyowauliza majibu yao ni kwamba wao hawana mamlaka ya viwanda hivi. Ningeomba wakati wana *windup* Wizara ya Fedha ituambie viwanda vilivyobinafishwa lini vitarudishwa Serikalini ili watu wanaovihitaji waweze kuvifanyia kazi?

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

**MHE. HAWA S. MWAFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Zawadi Kiteto Koshuma, Mheshimiwa Kanali Mstaifu Masoud na Mheshimiwa Dkt. Peter Kafumu wajiandae.

**MHE. ZAWADI K. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuendelea kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitachangia kwa utaratibu kabisa ili labda Wizara kuititia Waziri mwenye dhamana pamoja na Naibu Waziri wake waweze kunisikiliza kwa umakini na kuweza kupata kile nilichonacho kuhusu viwanda na biashara katika nchi yetu hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuanza kwa kusema kwamba kama kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa lolote lile, basi viwanda ni nguvu na kichocheo cha maendeleo ya uchumi katika Taifa lolote lile. Ili tupate mapinduzi ya viwanda pamoja na kilimo tunahitaji kuwa na teknolojia ya kisasa ili kuweza kuleta tija katika uzalishaji wa kilimo pamoja na uzalishaji wa viwandani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika nchi yetu ya Tanzania mpaka sasa tumeshindwa kufungamanisha kilimo pamoja na viwanda. Mheshimiwa Rais anayo nia njema sana anaposema anahitaji kuona Tanzania ya viwanda ili kuweza kuufikia uchumi wa kati. Sijui ni wapi tunakwama hadi tunashindwa kufikia yale malengo na azma njema ambayo viongozi wetu waliopita na waliopo sasa wamekuwa wanayo toka enzi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara, pamekuwepo na mapungufu ama changamoto ya upatikanaji wa fedha. Mimi naomba njikite katika fedha za maendeleo. Fedha za maendeleo katika Wizara hii ya Viwanda na biashara kwa mwaka 2018/2019 imepelekwa kwa asilimia 6.48 tu. Swali tu la kuijuliza sisi kama Waheshimiwa Wabunge, kweli tunaweza tukaifikia azma ya Mheshimiwa Rais ya nchi ya viwanda na kutupeleka kwenye uchumi wa kati? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo taasisi mbalimbali katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara ambazo zingeweza kusaidia uchochezi wa kuwa na kilimo cha kisasa na tekonomojo ya kisasa katika viwanda vyetu nchini Tanzania. Tunazo Taasisi kama vile *TEMDO*, *CAMARTEC*, *TIRDO* pamoja na *SIDO*. Nikiwa kama Mjumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara, Kamati ilikwenda kutemebelea miradi hii ya taasisi hizi ambazo nimezitaja, cha kusikitisha sana tulivyofika katika taasisi hizi hakuna fedha hata shilingi moja ambayo ilikuwa imeenda kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Zaidi Kamati ilifika pale na kukuta kwamba yale machache ambayo yamefanyika na ambayo ni mazuri yametumia fedha kiasi

kidogo tu ambacho kilipelekwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, naomba niwapongeze watumishi wote ambao wanafanya kazi katika Taasisi za *TEMDO*, *TIRDO* pamoja na *CAMARTEC*. Watumishi hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu lakini wameweza kujitoa katika kuhakikisha wanalisaidia Taifa hili na kumsaidia Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba azma ya viwanda inakwenda kusonga mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia katika ukurasa wa 72, 73, 74 na 75 Mheshimiwa Waziri amejinadi na kujieleza pale kwamba hizo taasisi za *TEMDO*, *TIRDO* na *CAMARTEC* ni namna gani zinaenda kutekeleza wajibu wake. Huo ndio mkakati ambao ametueleza katika kitabu chake lakini cha kusikitisha hajaweka mikakati, kama taasisi hizi hazipokei fedha unatarajia haya ambayo umeyaandika katika kitabu hiki Mheshimiwa Waziri yatakelezwa vipi kama si kwamba unatutaka sisi kuziwekea lawama taasisi hizi lakini fedha hawana? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua nitakuwa nimeongea kidogo kwa sauti iliyokuwa juu, lakini naamini kwamba ninaeleweka vizuri ninapoenda kuongelea suala hili. Kamati ilipotembelea katika taasisi zile tumekuta mambo ambayo kwa kweli yalitudhoofisha sana na tulijiona kuwa kama Kamati tumepelekwa pale kwenda kufanya nini kama sio tu kupoteza muda na kuchezea pesa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika Taasisi ya *CAMARTEC* mishahara inayolipa ni mikubwa ukilinganisha na mapato ambayo yanapatikana. Uzalishaji uliopo ni mdogo ukilinganisha na mishahara mikubwa ambayo inalipwa katika taasisi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mwaka 2016/2017, ililipwa shilingi milioni 900 ya mishahara ilhali mapato ya ndani ya mwaka huo yalikuwa ni shilingi milioni 242. Hiyo, haikutosha, mwaka 2017/2018 zimelipwa pesa milioni 864

wakati mapato ya ndani yalikuwa ni shilingi milioni 253. Mwaka 2018/2019 hadi kufikia mwezi Machi wamelipa mishahara shilingi milioni 362 wakati mapato yake hadi kufikia mwezi Machi ni shilingi milioni 214. Kwa *trend* hii siamini kama kweli tutawenza kufikia Tanzania ya viwanda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri Serikali kuhakikisha kwamba wanachukua ushauri wa Kamati ambao imeutoa kuangalia taasisi hizi zinaenda kuwekwa chini ya *management* moja. Taasisi zinapokuwa *under one management* itawenza kuangalia sasa hivi pesa ipelekwe wapi na kufanya nini. Pia wale wafanyakazi ambao wameajiriwa katika zile taasisi wanakuwa na tija. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nijielekeze katika suala la *Electronic Tax Stamp*. Naamini mfumo huu wa ukusanyaji kodi kielektroniki umelenga kuwabaini wale ambao sio waaminifu katika ulipaji kodi. Ni suala zuri na mimi naipongeza Serikali kwa kubuni mfumo huo. Hata hivyo, gharama zile ambazo zinatumika kwa ajili ya ku-*collect* ile *tax* kwa wafanyakabiashara ni kubwa sana. Kwa mfano, kijoti kile cha *juice* ya Azam, *pact* moja inatakiwa kulipa kodi ya Sh.3 lakini katika mfumo huu wa *Electronic Tax Stamp* gharama ya ku-*collect* ile Sh.3 ni Sh.9. Hebu angalia tunatumia Sh.9 kukusanya kodi ya Sh.3, hivi kweli inaingia akilini? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali watakapokuja ku-*windup* watusaidie kutuambia ni mfumo gani ambao ultumika kumpata huyu mwekezaji ambaye aliuweka huu mfumo. Hata Kamati wamesema pale kwamba, huu mfumo hauna teknolojia ambayo unaweza kusema kwamba *it is a rocket science*. Mfumo hata wewe binafsi unaweza ukaubuni. Kwa nini *TRA* haikufikiria kuwekeza wao wenyeve katika mfumo huu na kuleta mwekezaji? Naishauri Serikali iweze kukaa na huyu mwekezaji ili waweze ku-*review* zile gharama za kukusanya kodi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kiteto. Tunaendelea na Mheshimiwa Kanali Mstaafu Masoud, Mheshimiwa Dkt. Peter Kafumu na Mheshimiwa Ibrahim Raza wajiandae.

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kidogo Wizara hii ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa azma yake nzuri ya kutaka kuipeleka Tanzania katika uchumi wa kati lakini pia Tanzania ya viwanda. Kila mtu ana mtazamo wake katika jambo hili. Mimi naona tatizo tulilonalo hapa Tanzania bado Waziri hajawa na usimamizi mzuri, yeye ni baba, kama ni baba anatakiwa alee wafanyabiashara na wenye viwanda wote. Anapopelekewa matatizo ni wajibu wake kuhakikisha anayashughulikia haraka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siamini na wala siwezi kukubali kama kuna mtu anataka kuwekeza nchini aje awekeze bila kufanya utafiti kwanza. Kwa hiyo, cha kwanza anachokuja kufanya ni kuhakikisha yale mazingira wezeshi yaliyowekwa na Serikali kama ni mazuri lakini ataangalia wale walioanzisha viwanda wana changamoto gani ndipo hapo atakapoamua sasa na yeye aje awekeze. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hapa Tanzania tuna changamoto nyingi za viwanda na inaweza ikachukua miaka, Kamati itapita leo itaikuta, itapita mwakani itaikuta, itapita mwaka miwngine itaikuta bado hajitatutuliwa. Mimi nashauri sana Serikali mara nyingi wawe karibu na wafanyabiashara na wenye viwanda kuwasikiliza. Kuwasikiliza tu haitoshi, wawatatulie na matatizo yao pale yanapotokea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumeshuhudia mengi katika viwanda lakini mimi nataka niseme jambo moja ambalo linanisikitisha tuna viwanda vingi hapa nchini tayari

vina uwezo wa kuzalisha mali inayotosheleza mahitaji ya nchi lakini bado bidhaa zile zinaagizwa kutoka nje. Mimi nafikiri kama tunataka kweli tuwe na viwanda basi tuamue kuwalinda wale ambaao tayari wana uwezo wa kuzalisha mali ya kutosheleza nchi hii. Mfano mkubwa ni viwanda vya plastiki, nondo na viwanda vingine. Kuna mwekezaji amewekeza kiwanda hapa cha nondo ametumia dola milioni 30, kiwanda kina uwezo wa kuzalisha *metric tone* 200,000 lakini leo anazalisha *metric tone* 15,000 tunategemea nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotaka kukuza uchumi cha kwanza tuwalinde wenye viwanda ili kuongeza ajira kwa watu wetu. Tunaponunua bidhaa kutoka nje maana yake tunaongeza ajira kwa wenzetu wenye viwanda vya kule nje. Kwa hiyo, kama tunataka kukuza biashara kwanza tukuze viwanda, hiyo itatusaldia kuongeza wafanyakazi na ajira kwa vijana wetu. Imefika mahali sasa lazima tuamue, tusiogope. Yapo mambo tunaogopa kutatua lakini yapo mambo tunaweza tukayaamua tu na kuaona kama yataleta tija ama la. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa mfano huo mmoja wa kiwanda cha nondo lakini bado tuna viwanda vingine vinazalisha mali pia, saruji, mabati na vinginevyo, bado hatujaweka mkakati wa kuhakikisha tunapunguza uingizaji wa bidhaa hizo hapa nchini. Naiomba sana Wizara wahakikishe kama bidhaa zinazoagizwa zipo hapa nchini wapunguze uingizaji wa bidhaa hizo kutoka nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wengi wamezungumza lakini na mimi nataka niseme moja, *TIRDO*, *SIDO*, *CAMARTEC* na wengine tunawategemea ndio wazalishaji watakaowawezesha wajasiriamali wadogowadogo kule vijijini. Tunasema wao kazi yao ni kukuza teknolojia ili watu kule vijijini waweze kujitegemea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumeshuhudia kabisa wenzetu hawa mashine wanazofanyia ni za toka mimi sijamaliza shule, tukienda na mfumo huo hatutafika.

Tunachokiomba Serikali iweke mkazo wa kuungeza bajeti katika Wizara hii hasa katika bajeti ya maendeleo, kuhakikisha wanapewa teknolojia mpya, mashine mpya na wale wakufunzi wanapata mafunzo ya kisasa ili watu waweze kujiletea maendeleo kwa haraka zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata bidhaa zetu kwa mfano, tumekuta trekta pale Arusha, lakini naamini trekta lile pengine limetengenezwa siyo chini ya miezi nane au zaidi, moja tu. Sasa lile si kwamba watu hawana uwezo wa kutengeneza uwezo wanao lakini teknolojia za mashine zetu bado ni mno.

Kwa hiyo, tujaribu, yako mambo tunaweza kuyafanya wenyeewe na mengine tunaweza tukawatumia wataalam kutoka nje. Naomba sana Serikali ijithabidi katika hili lakini ifike mahali tuamue tuflikie mahali pazuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninataka kulizungumza ni hii *ETS*, kila mtu ameizungumzia. Ukiona Mheshimiwa Waziri tunaizungumzia sana maana yake inatumiza. Inatumiza kwa sababu mimi siamini, sasa hivi Kiwanda cha Bia *TBL* kwa hesabu zao za haraka kwa mwaka mmoja watalipa *ETS* shilingi bilioni saba. Wenyeewe wanasema 10% wanayolipa ambayo ni shilingi bilioni 78 lakini mimi naona wala hapajaharibika kitu, Serikali ikae kitako tu, ikae na hawa wenzenzu wazungumze wakubaliane na kama itashindikana kama walivyosema wenzangu au ilivyosema hii taarifa yetu, bora tutafute njia mbadala ya kuweza kusaidia Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa hii inayolipwa kwanza haiendi Serikalini, sisi tungefurahi tungesikia ile pesa ya *ETS* inakwenda Serikalini tunganeza kuzungumza lugha nydingine, lakini pesa hii yote inakwenda kwa mtu. Mtu tu ambaye ameweka kifaa chake pale anakusanya pesa, kwa kweli, hii inatia uchungu sana. Mimi naomba sana Mheshimiwa Waziri suala hili liangalie na ulifanyie kazi kwa sababu wenye viwanda wanalamika sana kuhusu jambo hili na jambo hili litakwenda kuleta athari kubwa siku zijazo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli sasa hivi hawajapandisha baadhi ya bei ya bidhaa zao, lakini wakianza kupandisha bei Serikali ijue kwamba itapunguza mapato kwa sababu hata hiyo *juice* inayoitwa kijoti inayokwenda kuongeza Sh.9 watu watakuwa hawanunui, watakwenda kununua matunda sokoni wakoroge basi. Kwa hiyo, tuone kwamba hapa tutakuja kupoteza siku zijazo. Naomba sana Serikali iendelee kuangalia hili na ikiwezekana ilifanyie kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalmiko makubwa kule kwa wenzetu wa *TRA* hasa katika mizigo inayoingia bandarini. Mimi nafikiri inawezekana lipo inawezekana halipo lakini sisi tunatoa tahadhari tu kwa Serikali kama kweli hili lipo linazungumzwa basi ni vizuri wakaanza kufanya mchakato wa kufuatilia na kuona kama ni tatizo gani liko bandarini kwa wenzetu wa *TRA*. Wanavyolalamika wenzetu hawa kwamba bidhaa zinaingia lakini wakati wa kuzifanyia tathmini inafanywa ndogo, kwa hiyo, zinaingia sokoni zinakuwa na bei rahisi na wengine wanasema wanaghushi risiti, vifaa vinaingia vingi vinalipiwa kidogo. Mambo kama haya ni madogomadogo sana, naomba sana Serikali iyasimamie na hatimaye tuone mafanikio gani tutayapata hapo mbele ili wote tuende kwenye huo uchumi wa viwanda tunaokusudia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kanali Masoud. Tunaendelea na Dkt. Peter Kafumu, Mheshimiwa Ibrahim Raza na Mheshimiwa Japhary Michael wajiandae.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo hoja hii ya viwanda, biashara na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Waziri kwa namna alivyowasilisha ripoti yake na alivyoisoma kwa nguvu mpya na ari mpya. Nakuombea ndugu yangu, mdogo

wangu, pambana bwana tunataka viwanda sisi. Tunataka 2025 iwe nchi ya viwanda, nchi ya kipato cha kat, kazi ni kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme Serikali ya Awamu ya Tano ilijipangia mambo kadhaa ya kufanya ili kuipeleka nchi hii kwenye viwanda. Jambo la kwanza ilisema ingeweza kuanzisha viwanda vya msingi ambavyo vinachochea viwanda vingine. Kwa mfano, viwanda vya chuma; Liganga na Mchuchuma, tumesema sana hiyo na tunaishukuru Serikali kwa kuliona kwamba hilo jambo ilikuwa la msingi. Viwanda vya magadi soda kwa mfano kule Engaruka tuliweka kama jambo la msingi. Viwanda hivi vikianzishwa, vingeweza kulipeleka Taifa mahali pazuri sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali ya Awamu ya Tano iliendeleza shughuli ya gesi na mafuta. Jambo lingine ambalo Serikali ilijiwekea ni ujenzi wa miundombinu. Tunaipongeze sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa jambo hilo, ujenzi wa reli, barabara, bandari, viwanja vya ndege, ndege zenyewe, umeme, nishati na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Serikali hii ililzungumza sana tangu iingie madarakani ni kilimo. Iilitengeneza mkakati unaoitwa *Cotton to Clothes (C2C)*, lakini ilikuwa na mkakati wa *ASDP* /na mikakati ya Sekta ya Ngozi. Kwa maandishi, Serikali imekaa vizuri sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni mazingira ya kufanya biashara iwe rahisi. Pamoja na hayo, Bunge liliendelea kuishauri Serikali, tangu mwaka 2015 nakumbuka mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Viwanda na Biashara, tumeishauri Serikali kama Bunge iyafanye haya mambo ambayo yameandikwa kwenye Mpango wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema, kwenye mazingira ya kufanya biashara, tulitaja mambo kadhaa ambayo tunahitaji Serikali iyarekebishe ili biashara iwe sawa sawa. Kwa mfano, utitiri wa kodi, wingi wa mamlaka

zinazosimamia, pia mtazamo kuhusu wafanyabiashara na wawekezaji, kuwatazama kama marafiki badala ya kuwatazama kama maadui, wezi na wanyang'anyi. Naipongeza tena Serikali, ilikubali na ilisikiliza ushauri. Natoa vithibitisho nya ushauri kusikilizwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, iliandaliwa *blue print*, ukiisoma hiyo, mambo yote haya ya uwekezaji pamoja na biashara yamesemwa vizuri sana, tena sana. Changamoto iliyopo Mheshimiwa Waziri, ni utekelezaji. Leo ni mwaka wa pili tuna *blue print* ipo kwenye shelfna wale buibui wameanza kuitanda sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule mkakati wa *ASDP I* nadhani umemaliza sijui miaka mingapi? Mitatu, minne hivi haujatekelezwa. Tunaanza kutengeneza mkakati mwingine, *ASDP II*. Changamoto kubwa tulyonayo Mheshimiwa Waziri ni kutekeleza haya mambo ambayo tulyakubali, tumeyaandika vizuri, mnataka wenzetu majirani wachukue hii mikakati wakatekeleze, sisi tunaangalia tu! Tukiweza kutekeleza hayo, Mheshimiwa Waziri, yaani hatuko mbali kabisa na mafanikio. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niseme kwamba mchango wangu mkubwa ni kuishauri Serikali sasa, naomba nitoe ushauri ufuataao: La kwanza, Wizara hizi zifanye kazi kwa ushirikiano. Niliwahi kusema zifanye kazi kwa ushirikiano; kilimo, Wizara ya Viwanda na Biashara, Nishati na Ujenzi lazima mkutane. Narudia tena, nilisema mwaka 2016 mtengeneze mkakati wa pamoja wa kutekeleza jambo hili. Wizara ya Fedha nimeisahau, ndiyo inayotoa fedha. Msipofanya hivyo, tutakuwa na mikakati na mipango lakini hatuitekelezi kwa sababu kila mtu anakwenda nya kwake. Ni muhimu sana tukawa pamoja katika mambo haya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa hizi *documents* ambazo nimezitaja hapa; *blue print, ASDP, C2C* na mikakati mingine ipo mizuri mingi kabisa, imejibu hoja zote na matatizo yote ambayo tunayasema humu Bungeni, hebu

itekelezeni. Nakumbuka kuna mkakati wa kuzalisha mbegu za mafuta nyingi hapa ili tusiwe na matatizo ya mafuta, tekelezeni. Tukiendelea kila mwaka tunakuja tunatoa *story* hapa, kwa kweli hatutafika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwininge, tuangalie baadhi ya sheria. Kuna sheria nyingine tumezitengeneza nzuri kweli, lakini mle ndani kuna maneno ambayo yamefukuza wawekezaji. Naomba kila sekta angalieni sheria zenu, mbadilishe kidogo. Ngoja nitoe mfano, mnisamehe. Sheria za *sovereignty* tulizotengeneza ni nzuri kweli zinalinda rasilimali zetu, lakini kuna vipengele mle ndani akisoma tu mwekezaji anabwaga manyanga anaondoka. Naomba sana Waziri wa Sheria na Katiba, Waziri wa Madini na Waziri wa Nishati hebu tazameni, kuna vipengele vichache siwezi kuvitaja, ukivibadilisha tu kidogo unahamasisha uwekezaji wa ndani na wa nje, utakuja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa nne, tuongeze bidii katika kujenga miundombinu. Hapa tunafanya vizuri sana, tunajenga reli, barabara, viwanja vya ndege, tunatengeneza umeme, lakini tuongeze bidii. Kuna sehemu hatujaenda vizuri. Kwa mfano, tunajenga reli kwenda Mwanza, lakini *financing* inatupa shida kidogo na Wabunge kadhaa walisema, tuna-*finance* kidogo kidogo, tutatumia miaka 20 kufika Mwanza. Hebu tutafute mkakati mzuri zaidi tuharakishe jambo hilli. Kwa kweli ni jambo zuri, lakini tulifanye kwa *speed* ya kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa tano, tujenge viwanda mama. Liganga na Mchuchuma jamani tungetumia chuma sasa hivi kujenga reli yetu, chuma cha ndani, lakini tumechelewa. Hebu tukazane kidogo hapo. Mheshimiwa Waziri wasiliana na Nishati na Madini hii rasilimali iweze kuchimbwa. Hizo changamoto zilizopo hapo tuzirekebishe, tutaenda vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa mwisho, tulifanya vizuri sana katika kuweka maeneo ya uwekezaji; *EPZ* pamoja na *SEZ*. Tume-*identify* maeneo mengi lakini kuya-*develop*

imekuwa taabu. Moja ya changamoto ni Bandari ya Bagamoyo; ni kitu kizuri kweli na kina maelezo mazuri kweli, lakini tumeenda mpaka sasa hivi kuna kzungumkuti wanasema Waswahili. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri hatuelewi kama tunaenda au hatuendi. Maeneo mengi kama Kurasini mpaka leo, yapo mengi tu, mpaka kule Igunga kuna maeneo ya uwekezaji ambayo hayajaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema, tunafanya vizuri sana katika kuandika *projects* na mikakati lakini hatufanyi vizuri katika kutekeleza. Tunaandika sheria, tunashindwa kuzitekeleza. Sheria ya PPPkwa mfano, tulitunga mwaka 2018 lakini ina vikwaruzo vingi mle ndani. Nami nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, nilisema, nilimwambia Waziri wa Fedha kama anakumbuka, kwamba hii tulivyoipitisha kama ilivyo hivi hatutapata mwekezaji hata mmoja kwenye PPPkwa miaka 20 ijayo. Lazima tuirudishe hapa tuibadilishe, kuna mambo ambayo hayakusemwa vizuri humu. (*Makofii*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana kwa kunisikiliza. Mungu awabariki. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ibrahim Raza, baadaye Mheshimiwa Japhary Michael na Mheshimiwa Raphael Chegeni wajiandae.

**MHE. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kwa mara nyingine kuchangia hii Wizara ya Viwanda na Biashara. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa pumzi zake mimi kusimama hapa nikiwa na afya, mzima, *Alhamdulillah*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nachukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Kakunda na timu yake, kwa kweli bajeti aliyowasilisha leo ni bajeti ambayo inalenga kuwasaidia wafanyabiashara na wenye viwanda na matumaini yangu mimi ni kwamba Mheshimiwa Kakunda, katika nchi hii ya Tanzania tunawategemea sana wafanyabiashara na wenye viwanda. Wao ndiyo wanatuleta *revenue* kubwa sana katika nchi hii. Kama Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kila anaposimama kwenye kiriri akiwahimiza wafanyabiashara wa nje waje Tanzania kuwekeza, hii ni kwa sababu anawatachia mema Watanzania ili Tanzania iwe nchi ya viwanda tukifika 2025 na vilevile Watanzania watakuwa wanapata ajira kuongezeka katika viwanda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nimsaidie ndugu yangu Mheshimiwa Waziri Kakunda. Kwa kweli tatizo liliokuwepo kubwa sana kwanza kwa wenzetu wa *TFDA*. *TFDA* huwa wanachukua muda mrefu kutoa ripoti ya kile kitu ambacho kimewasilishwa kwao, wanachukua miezi mitatu. Mheshimiwa Waziri mimi ninao ushahidi. Wenzetu nchi za nje kama *South Africa* hapa, *within 10 days* wanakupa ripoti kwamba kitu hiki kinafaa au hakifai. Sasa wenzetu wa *TFDA* nataka wabadiilike sana kwa sababu kumweka mtu miezi mitatu hujampa ripoti, kwanza unamvunja moyo kwamba asilete bidhaa na pili, vilevile unawarejesha nyuma wale ambaao wanataka kuleta bidhaa katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine kubwa kwanza hii ada ya dola 200 kwa kila sampuli moja Mheshimiwa Kakunda kwa kweli ni nyingi sana. Naomba Wizara yako iliangalie hili suala kwa sababu mtu kwenye kontena ameleta *item* 20 na kila *item* dola 200, fanya hesabu hapa, huyo analipa kiasi gani? Kwa hiyo, badala ya kuwa-*support* wafanyabishara tunawa-*discourage* wasilete vitu nchini na wakileta vitu nchini, Tanzania inapata *revenue*, *TRA* wanakusanya pesa. Kwa hiyo, naomba *TFDA* wabadiilike sana katika masuala haya ya haya mambo tunayokwenda nayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka wenzetu wa *TBS* na *ZBS* washirikiane, waaminiane katika kazi hii kwa sababu mzigo unaotoka Zanzibar kuja huku kwa kweli inakuwa ni shughuli kubwa sana. Kwa sababu wafanyabishara wa Zanzibar wanapoleta vitu Zanzibar wanakuwa wameshapewa kibali kule na *ZBS*, sasa unapokuja huku *TBS* nao wanaweka mguu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hili pia ni changamoto kubwa sana katika Wizara yako. Naomba *TBS* na *ZBS* washirikiane ili wafanyabiashara wawe wanafanya biashara kwa amani, wanatuingizia pesa, lakini hizi changamoto inatuletea vilevile sintofahamu katika Muungano wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nikupe taarifa kwa sababu sisi ni watu ambao tupo mjini tukaa na wafanyabiashara. Hawa *TBS* wakikupa cheti cha kwamba wewe hiki kitu unaweza ukakuza mfano, lakini wanakuja watu wa *FTC* wanaipinga *TBS*. Sasa hapo Mheshimiwa Waziri watu wanakuwa wanaonyesha mimi ni mkubwa kuliko wewe. *TBS* anasema sawa lakini anakuja *FTC* anakanusha anasema hapana, mimi sijaridhika. Sasa nani tumsikilize? Tumsikilize *FTC* au *TBS*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema nizungumzie zaidi biashara kwa sababu nakaa na wafanyabiashara wakubwa na wadogo. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mpina, juzi alikagua kiwanda cha maziwa Arusha na alihakikisha kwamba hakuna kitu kutoka nje kitakuja Tanzania ili kukilinda kile kiwanda. Wewe Mheshimiwa Waziri na hilo pia ulichukue kwamba viwanda vyetu vya ndani lazima uvilinde kwa sababu ukivilinda viwanda vya ndani ndipo ajira ya Watanzania itakapopatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Waziri, tatizo lingine kubwa lilitokuwepo ni *OSHA*. Nasema tena *OSHA*. Hawa wanakuja maofisini wanasema kwamba huu umeme haujaka sawa, hii meza haijaka sawa; hii feni haijaka sawa; hivi ni kazi ya *OSHA*, tunauliza? Kama ni kosa la umeme au nini, ni la mwenye nyumba mwenyewe aliyejenga siyo yule aliyejodi; na ushahidi ninao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kuna wafanyabiashara Dar es Salaam wametozwa shilingi 850,000/=, wengine shilingi 650,000/=, wengine wametozwa shilingi 420,000/=. Ninao ushahidi *OSHA* wamekwenda kwa sababu eti huu umeme haufai, hii meza uliyokuwa umeweke hapa siyo mahali pake, jamani hawa *OSHA* wanataka kutupeleka wapi? Hivi *OSHA* wamepewa kazi ya kwenda maofisini na kuchaji pesa nyigi kiasi hicho? Mheshimiwa Waziri, ushahidi pia ninao ukitaka, nazungumza haya kwa ushahidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri Kakunda kwa sababu upo na Mheshimiwa Kairuki kwa sababu ni Waziri wa Uwekezaji, atakusaidia sana Mheshimiwa Kairuki kukuletea wawekezaji, lakini suala la wawekezaji kupata kibali cha kufanya kazi nchini, naomba hili ulibebe kwa sababu kuna malalamiko mengi sana. Kuna watu wanaenda *ku-apply labor* hawapati, wanahangaishwa, nenda rudi, nenda rudi. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri Kakunda, hili suala uliangalie kwa sababu kuna watu wamekuja wanawekeza hapa, Watanzania wanapata ajira lakini mwisho wa siku hawapati kibali cha kufanya kazi. Kwa hiyo, nani anapata hasara? Ni wale Watanzania wanakuwa wanakosa ajira kwa yule mtu mmoja ambaye amekosa *labor*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili Mheshimiwa Waziri ulibebe sana. Nami ukitaka ushahidi wa mambo yote nitakuletea ofisini kwako. Tupo hapa kuwajenga Watanzania ili nao wapate kazi. Masuala haya ya nenda rudi haituletei sifa Tanzania. Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli anahangaika nchi nzima, anasema wawekezaji njoo, jengeni, fanyeni lakini kuna watu makusudi wanamkwamisha Mheshimiwa Rais. Hatukubali! Tunasema tena, hatukubali sisil Mheshimiwa Rais anakufa na nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Kakunda mimi hayo nilitaka niyaweke wazi na vilevile naomba Manispaa zetu watenge nafasi ili mashine/viwanda vidogo vidogo wajasiliamali wetu wapate kuwekeza kama nchi zetu za China na India, kuna Manispaa wamewekeza

nafasi maalum kwa viwanda vidogo vidogo kwa vijana wetu ili nao wachangie hii fursa ya biashara ya Tanzania ya viwanda. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na nimshukuru tena Mheshimiwa Waziri Kakunda kwa kuwasilisha hotuba yake hii nzuri. Naunga mkono hii hoja mia *fil-mia* na *Inshallah* Mungu atatusaidia. Naitakia kila la heri nchi yetu ya Tanzania, nchi ya viwanda. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nakushukuru. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ibrahim Raza. Tunaendelea na Mheshimiwa Japhary, baadaye Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Jitu Soni wajiandae.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ibrahim Raza, tunaendelea na Mheshimiwa Raphael Michael, atafuatia Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Jitu Soni ajiandae.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii ya Viwanda. Nafikiri tatizo tulilonalo katika nchi yetu ni viongozi wetu wengi na Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi muda mrefu kuishi kwa kaulimbiu bila kuwa na utekelezaji. Kwa sababu tangu awamu zilizopita zote kuacha Awamu hii ya Tano, ukiangalia mtazamo wa viongozi wakuu ilikuwa ni Tanzania ya viwanda, wala wazo hili halijaanza sasa kwa Awamu ya Tano, lakini suala ni kwamba je, katika muda wote huo ni kwa kiwango gani tumefikia kwenye malengo ambayo tumekuwa tukiyazungumza; ni utayari gani uliopo juu ya viongozi wetu wanaopewa hizo dhamana za kutekeleza hayo? Ndilo swali ambalo tunatakiwa wote tujilize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana wakati mwininge viongozi wetu wakuu wana mawazo mazuri sana

ya kutupeleka mahali, lakini inawezekana wasaidizi wao ama hawako tayari au hawana uelewa juu ya dhamira za viongozi wakuu wanazokuwa nazo juu ya safari tunayotakiwa twende. Kwa hiyo kuna haja ya kubadilisha sana mawazo na mitazamo yetu ili tufikie hapa tunapotarajia kupafikia. Vinginevyo dhana hii ya Tanzania ya viwanda itakuwa inakuwa ni wimbo tu kama ambavyo zimekuwa ni nyimbo tangu baada ya Serikali ya Awamu ya Kwanza katika nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani lilikuwa jambo jema tu kwamba Serikali ya Awamu ya Tano kwa sababu imeamua kufikia malengo ya kuwa na Tanzania ya viwanda, kufikia uchumi wa kati, basi ingerudi pale ambapo mwaka 1985 Mwalimu Nyerere aliachia wakati anaacha nchi hii. Kwa sababu miaka hiyo tayari mwelekeo wa namna gani tunatakiwa tujenge Taifa la viwanda ulishaonekana katika nchi hii. Bahati mbaya Serikali hii hii ya Chama cha Mapinduzi, viongozi waliofuata baada ya Mwalimu wakaamua kuondoa yale matumaini yote ambayo yalikuwa yamewekwa kwa Watanzania juu ya kujenga Tanzania ya viwanda. Tumerudisha wazo hilo sasa kwa Awamu hii ya Tano, je, sisi wasaidizi wa Rais tuko tayari katika kufikia malengo hayo ama tunajaribu kumwonesha Rais kwamba tuna dhamira wakati hatuna dhamira hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri unajaribu kutafakari, je, kweli tuna hiyo dhamira; tumedhamiria kufika Tanzania ya viwanda? Kwa hiyo haya ni maswali ambayo sote tunatakiwa tujiulize kwa pamoja na naflkiri kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi wanatakiwa wajiangalie sana, tusipende kuishi kwa kauli mbiu ambazo tunazi-*take by event*, kwa matukio na hatuzifanyii kazi. Tusifanye suala la viwanda kama suala la zimamoto, tudhamirie kweli kwamba tunajenga Tanzania ya viwanda kwa sababu ni ukweli kwamba ndiyo kichocheo cha maendeleo ya Taifa hili kwa sasa na kwa siku zijazo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kitabu hiki cha bajeti, ukiangalia *trend* ya bajeti ya Wizara ya Viwanda

mwaka 2017/2018, 2018/2019 na hata 2019/2020, unaona kabisa kwamba bajeti iliyotengwa inaonesha kwamba Serikali ina dhamira ya ku-*facilitate* ukuaji wa viwanda katika nchi hii na ukuaji wa biashara katika nchi hii. Hata hivyo, tofauti yake ni kwamba ukiangalia maneno ya viongozi wa Serikali, maneno hata ya kiongozi wetu mkuu, inaonekana kama vile Serikali imeamua sasa kufanya biashara yenyewe, imeamua kuendesha viwanda yenyewe, imeamua ku-*centralize* hivi vitu badala ya mfumo ambao tulishazoea kwamba tunategemea kuimarisha *Private Sector*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa matokeo yake Serikali inachukua majukumu mazito sana. Ukiangalia bajeti hii ina fedha ndogo sana lakini hushangai kwa bajeti ndogo kwa sababu dhamira ya kweli ya Serikali ilikuwa ni kusaidia kuhakikisha mazingira mazuri ya biashara katika nchi hii, mazingira mazuri ya uwekezaji katika nchi hii, mazingira mazuri ya uwepo wa viwanda katika nchi hii, lakini ukweli halisi ulioko kwenye utendaji, Serikali inaonesha wananchi kwamba yenyewe ndiyo inataka ifanye kazi ya biashara, ifanye kazi ya kujenga viwanda na vitu vingine kama hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo inaonekana kwamba wana-*discourage* sekta binafsi, hawataki kui-*encourage* sekta binafsi, ndiyo maana kila anayenyanyuka hapa anasema kuna vikwazo vingi sana kwa wafanyabiashara ambao ni ukweli ulio halisi. Leo Wabunge hapa wanalamika kuhusu hivi vi-*regulator* vingi ambavyo vimekuwepo vinavyotoza wafanyabiashara. Sasa swali langu najuliza, kama Serikali wanasilia haya Wabunge wanayolalamika, hao *regulators* wote kama *TFDA*, *TBS* na nyininge nydingi zimebekwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge, kwa nini Waziri asifanye kazi rahisi tu mpaka leo aambiwe ajiuzulu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alete sheria hapa viunganishe hivi vitu, waambiwe Wabunge wabadilishe sheria, kwa sababu hivi tunavyozungumza viko kwa mujibu wa sheria; *TFDA* wanafanya kazi kwa mujibu wa sheria, *TBS* kwa mujibu wa sheria, *OSHA* kwa mujibu wa sheria.

Bahati mbaya bado hawajaanza kutufunga, wakianza kutufunga ndiyo tutajua kwamba wapo kwa mujibu wa sheria mlizotunga ninyi wenyewe, sasa hivi bado wanatupiga tu penati, wanatuadhibu, sheria zinaruhusu watufunge, sasa siku wakianza kuwafunga hapa ndiyo tutaona kelele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo cha msingi, Serikali walete mapendekezo hapa au hoja, Wabunge wajadili, waone namna gani wanawapunguzia wafanyabiashara hizi adha. Vinginevyo watu wa *OSHA* watalalamikiwa wakati wanaangalia sheria; *TRA* watalalamikiwa wakati wanaangalia sheria na wengine wote watalalamikiwa wakati sheria mmetunga wenyewe hapa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo *TRA* wangefanya kazi kwa mujibu wa sheria ilivyo kila mtu huku ndani angekuwa amefungwa kama ni mfanyabiashara. Kwa hiyo watu wanasema *TRA* ni wabaya sana, lakini ukiniliza nitakwambia *TRA* hawajawa wabaya kwa sababu bado hawajafunga watu, bado wanakudai fedha zao ambazo hujalipa, penati kama hujalipa au umechelewa kwa muda, lakini kama unataka kufanya kazi kama ilivyo watafunga hata watu wengine hapa ndani, kila siku watu watafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nafikiri kwa sababu wanaolalamika ni Wabunge na ndio wanaomwelekeza Mheshimiwa Waziri, ni rahisi tu; alete sheria hapa zibadilishwe ziweze kusaidia nchi yetu iende mbele na tuweze kukuza viwanda vyetu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba kufanya biashara katika Tanzania ni adhabu kubwa sana. Wakati naingia kama Mbunge hapa nilikuwa nafikiri labda Wabunge humu ndani hawajui ugumu huu, lakini baadaye nikagundua viongozi wengi walikataa biashara wakaamua kuwa wakulima na kule kwenye kilimo wamejifichia huko, wana mamilioni ya pesa kibao lakini wamejifichia huko. Sasa mateso yote yako kwa wafanyabiashara, yaani ukiamua kufanya biashara wewe katika nchi hii ni umenunua mateso makubwa sana katika Taifa hili, kwa nini? Kwa sababu siku

zote wamekuwa wakiwa na *perception* ya kupata kodi, kupata fedha, lakini hawataki kumlea huyo ng'ombe ambaye wanamkamua ili wapate hiyo kodi, hawataki kabisa, yaani Serikali inafikiri kodi tu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumzia katika Taifa hili biashara zimefungwa nydingi halafu watu tumekaa kimya na kuna majibu yanakuja kwamba biashara zilizofungwa ni watu ambao wanakwepa kodi, *as if* hao sio Watanzania. Walishaenda wakaonana nao, wakafahamu kwa nini wamefunga hizo biashara? Kwa nini wafikiri tu kwamba ni kwa sababu wamekwepa kodi, kwa nini wafikiri kitu kimoja tu? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunavyozungumza kila kukicha biashara zinafungwa. Inawezekana hazijafika milioni, lakini ukweli unabaki kwamba kuna biashara kadhaa zimefungwa katika Taifa hili, zimefungwa kwa nini? Kwa sababu ya mfumo usio rafiki kwa wafanyabiashara wa nchi hii. Je, Waziri na Wizara yake wamewasaidiae wafanyabiashara? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapokaa hapa kama watetezi tusiwfanye wafanyabiashara kama watu wasiotuhusu. Tuna tatizo kubwa la nchi hii kuamini kwamba wafanyabiashara wote ni mabepari, wafanyabiashara wote wanakwepa kodi, *which is not true*. Kuna wafanyabiashara wanalipa kodi, mfumo wetu wa kodi ndiyo sio mzuri. Sasa tuwasaidie wafanyabiashara hawa na ndiyo kazi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuwasaidia wafanyabiashara. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri ili aweze kuacha *legacy* asaidie wafanyabiashara, asimwachie jukumu hili Mheshimiwa Rais peke yake. Rais mpaka aamke, akishaamka na wao ndiyo wanaamka, haiwezekani, hatuwezi kuendesha Serikali ambayo Rais ndio *everything*. Rais ana wasaidizi wake, Urais ni taasisi, lazima asaidiwe na je, wanamsaidia inavyostahili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tusipoweka dhamira ya kutosha, leo tunazungumzia habari ya viwanda

karibu 4,000 na kitu ambavyo vimekua katika nchi hii. Hata kama hivyo viwanda tunasema ni vy a vyerehani, ni vy a nini, lakini kwa mujibu wa kanuni ni viwanda vidogo. Wajibu wetu, je, tuna mkakati gani wa kuinua hawa wawekezaji wa viwanda wadogowadogo wawe wawekezaji wakubwa wa viwanda; wajibu huo tumejipangaje nao? Kwa sababu leo Wachina tunaozungumza miaka ya 2000 ukienda kwao kule Guangzhou ilikuwa watu wanazalisha bidhaa zao, chaki mtu anazalisha kwenye kibanda cha nyumbani, lakini leo Wachina hao hao wamekuwa ni mabilionea katika nchi zao. Je, sisi tunajiandaa viyi kuwa-*empower* hawa wafanyabiashara wadogowadogo wawe wafanyabiashara wakubwa ndani ya nchi yetu? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama tunataka kufikia malengo ya kuwa Tanzania ya viwanda, tuna kazi kubwa ya kufanya na tudhamirie, tuwe na viongozi wabunifu, waliodhamiria kulipeleka Taifa hili mbele. Kama viongozi watabaki kuishi maisha yaleyale waliyozoea kumdanganya Rais kwamba wanafanya wakati hawafanyi ili wapate Uwaziri, wapate Naibu Uwaziri, wapate Ukatibu Mkuu, nchi hii hatuendi popote na kila siku tutakuwa na wimbo wa Tanzania ya viwanda ambayo hatutaifikia na itakuja Serikali nyingine na wao wamesema wanataka kutawala miaka mia moja, watatawala miaka mia moja wakiwa wanaishi katika Tanzania ambayo sio ya viwanda wala sio ya kilimo, itakuwa Tanzania... (*Makof!*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Japhary.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hayo ndiyo yalikuwa maombi yangu, naomba kushauri, nashukuru sana. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Chegeni, atafuatia Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Jitu Soni ajiandae.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ili niweze kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Hotuba hii ukiisoma ni nzuri na nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kuandaa bajeti hii na hotuba hii ambayo kwa kweli inaanishi kile ambacho wanadhani wanaweza kukifanya mwaka ujao wa fedha. Naomba nianze kwanza kwa masikitiko yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania na hasa na sisi Waheshimiwa Wabunge, tusipokubaliana kwanza kubadilisha mawazo yetu kwa kuthamini kwamba biashara au *public sector* ndiyo kiini na kitovu cha ajira za Watanzania. Ndicho ambacho kinaweza kukuza uchumi wa nchi hii, *short of that* hatuwezi kutoka hapa tulipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezoea kuitana majina; fisadi, mwizi, ukimuona mtu anafanya hivi huyu ni mwizi. Hebu jiulize; kama ameweza kuiba na akawekeza hapa nchini, wizi wake uko wapi? Kwa sababu tunavunjana moyo Watanzania, sisi tukiona mtu ametajirika anaitwa fisadi, anakuwa mwizi, haya maneno hayatusaidii kutujenga Watanzania na naomba sana tufanye *a total mindset transformation*, tusipofanya hivyo Watanzania itabaki ni hadithi tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameingia na kuali mbiu sahihi kabisa, hajaianza leo, ameakisi watangulizi wake. Tunataka Tanzania ya viwanda, unapataje viwanda? Lazima kuwe na *backward and forward linkages*. Hayo unayapata kama Watanzania wameshirikishwa vizuri, lakini leo hii *Private Sector*ina matatizo chungu nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kuanzisha biashara Tanzania ni kama mzigo, utatozwa kodi kwenye mtaji ambao unataka uwekeze. Sasa *how can you invest on your capital?* Tuangalie tu, hiyo *capital* unakwenda kukopa benki, kabla hujaitumia unatandikwa kodi karibu 42, sasa unakwenda wapi. Sasa ni mambo ambayo sisi kama Watanzania lazima

tubadilike. Tusipobadilika itakuwa ni hadithi na ngonjera, tunabaki kila siku tunasema sisi tumelogwa, hakuna aliyetuloga, ni mawazo yetu yamelogana yenyewe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia vibali vyatufu kufanya kazi, unajua uchumi wowote wa nchi ni *mixture*, unaweza uka-*borrow technology*, uka-*borrow capital*/kutoka kwa watu mbalmbali uka-*invest*. Kama huna *technology* hiyo unai-*borrow from outside*, lakini sisi hapa tunaona hata wageni ni tatizo, sasa unajengaje uchumi wa kwako peke yako? Tunaomba sana katika hili tubadilike. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo ukiyaangalia, Mheshimiwa Waziri amezungumza kwenye hotuba yake, *non-tariff barriers*, wamepunguza kutoka 62 mpaka 47, *this is very good*, lakini leo hii hata kusafirisha mzigo tu ukienda kilometa kadhaa mizani unaambiwa faulisha, mara fanya kitu gani, una *waste a lot of time* barabarani kabla ya kufikisha mzigo unakokwenda; hivi ndivyo vinavyoleta uchachu katika kufanya biashara hapa nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu vilevile kuna taasisi ambazo zinapaswa kuwa *harmonized*. Namshkukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha Wizara ya Uwekezaji, nampongeza sana, angalau sasa, tena kaiweka chini ya Waziri Mkuu, kwamba angalau Waziri Mkuu moja kwa moja anawajibika katika suala la uwekezaji kupitia Waziri ambaye amepewa mamlaka hayo. Hii itasadia kutufanya Watanzania tuthamini namna ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu amepokea watalii kule Arusha, *it's a business*, utalii *is a business*. Sasa sisi hapa unaangalia kwamba tuna vituo vingi sana, lakini tunalia kwamba hatuna wawekezaji, watakujaje hatujaweka mazingira mazuri hapa kwetu?

Naomba Bunge hili litumike kuhakikisha kwamba tunaweka utaratibu mzuri wa ufanyaji biashara, bila hivyo itabaki ni ngonjera. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona na naomba nim-*quote* Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, alisema kwamba biashara nyingi zinafungwa, lakini nyingi zinafunguliwa, sio kweli. Biashara nyingi zinafungwa sasa hivi na watu wana-*scale down*, tunapaswa kama Serikali, kama nchi, tujitathmini upya, *why*, bila kufanya vile unapataje hiyo kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Watanzania tuiseme kwa sababu watu pengine wanapiga makofi huku, hoja ni kwamba lazima tutoke hapa tulipo, tufike mahali pazuri. Kwa hiyo kwa sababu unajua wakati mwingine tusipoambizana ukweli hatuwezi kusonga mbele. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Rais amempa nafasi hii, hebu atumie nafasi hii sasa kuweza kufanya mabadiliko makubwa ya kiuchumi ili Tanzania tusonge mbele, hatuwezi kila wakati kuwa tunalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukienda *by statistics* makusanyo ya kodi ya *TRA* yanazidi kushuka, wakatae wasikatae ukweli ndiyo huo, lakini yanashuka kwa sababu gani? Lazima tuchochee tupate biashara nyingi, unapata kodi hii kutoka kwenye biashara, uta-*tax* wapi kama hakuna biashara, niombe sana. Marehemu Dkt. Mengi ni mmoja wa Watanzania ambaye alijitahidi sana kufanya biashara mbalimbali, nikiuliza leo hii hapa Tanzania baada ya Dkt. Mengi kufariki, wangapi akina Mengi saa hizi, wangapi? Tukika hapa, ukiona hivi unasema wengine hapa Tanzania wapo, lakini unakuta wana *passports* zaidi ya moja au mbili, unakuta yeye peke yake akifanya biashara asilimia 75 anapeleka nje, lakini ukiwa kama mimi namna hii au wewe au ndugu yangu hapa *Mr. White*, akipata hela yake hapa ataoa mwanamke hapa, atawekeza hapahaha, hela inazunguka hapa hapa. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niseme haya kwa sababu naumia kuona kwamba *this is my country*, lakini kila siku tunalamika, tunamlalamikia nani? Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, tusaidie. Hata hivyo, lazima wasomane na wenzake, hawezo akafanya kazi *in isolation*,

wasiposomana haiwezkani, naomba apate *support* kwa Mawaziri wenzake ili tuwe na *direction* moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri sana nimemwona akizunguka, anahamasisha biashara na anasema mfanyakabiashara akiwa na shida aniambie mimi moja kwa moja. Hivi kweli wote tutamfikia Mheshimiwa Rais kumwambia matatizo yetu wakati Mawaziri wapo? Wamsaidie Mheshimiwa Rais kufanya kazi hizi, wamsaidie kabisa. Haiwezekani Mheshimiwa Rais kila wakati anazunguka anapiga kelele mpaka anasema watendaji mnaonekana hamnielewi, kama hawamwelewi basi waacie ngazi, ndiyo, *it's true*. Tunataka sisi Tanzania ambayo inasonga mbele. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba leo hii kuna miradi ya kimkakati, Mchuchuma na Liganga kila siku ni hadithi na ngonjera. Mheshimiwa Waziri atapokuwa ana-*wind up* hapa naomba nipate taarifa sahihi kwamba suala la Mchuchuma na Liganga tunatokaje hapa tulipo? Kila siku sisi tunasema, tunajadili, mwaka huu tunajadili, mwaka unaofuata tunajadili; tunafika wapi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kingine, Mheshimiwa Dkt. Kingwangala yuko hapa hivi, watu wanapoingia hapa nchini *it's part of the business. The first impression* anayoipata hapa anapoingia pale *airport*, anakuta wafanyakazi wa *airport* wamenuna kama wamekula pilipili. Wewe unamkaribisha mgeni nyumbani kwako umenuna, unaweza kum-*harass* mtu, *why?* Katika nchi nyingine unapokwenda unapewa *a very good treatment*, lakini hapa akija mgeni ni kama amekuja kwenye madaladala. (*Makof!*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** Usile pilipili.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chegeni, subiri.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kelele nashindwa kuendelea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kigwangalla unasemaje.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chegeni, subiri kidogo. Mheshimiwa Kingwangalla.

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa kuhusu utaratibu.

**MBUNGE FULANI:** Wewe vipi bwana, acha fujo.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu utaratibu.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ameshakataa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hata hamjasikia anasema nini, yeye hajasema taarifa, hajasema chochote amesimama tu, Mheshimiwa Kingwangalla unasemaje?

**WABUNGE FULANI:** Uuuuuuu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa ndogo tu Mheshimiwa Mbunge anayesema kwamba kazi ya kuwafanya watumishi wa *airport* wawe na tabasamu nzuri inaendelea kufanyika. Kwa kuanzia tu, tumeanza na watumishi wa Shirika la Ndege la Tanzania *ATCL*, tumeajiri vijana watanashati na mabinti wengi warembo na yeye mwenyewe ni shahidi. Kwa kweli wana tabasamu nzuri zinazovutia na hiyo ni katika jitihada za kuboresha huduma za ukarimu kwenye sekta ya huduma nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kingwangalla, umeeleweka, Mheshimiwa Dkt. Chegeni malizia.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie muda wangu nadhani Mheshimiwa Waziri hakunielewa.

**WABUNGE FULANI:** Kweli kabisa.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuelewa *concept* yangu mimi, siyo suala la kutabasamu na kuva *uniform* nzuri ni *culture* ya kupokea wageni. (*Makof!*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)*

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe kama Waziri mwenye zamana hii hiyo unapaswa uonyeshe kwamba, unajua sikiliza unapompokea mgeni, *its all inclusive package*, hata tabasamu ni sahihi, hata *ku-facilitate* kupata mizigo au *permit* vyote ni muhimu zaidi na kadhalika, wewe kama Waziri wa Utalii unapaswa kuibeba hiyo.

## TAARIFA

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Hakuna taarifa leo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Chegeni muda wako umemalizika.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaaa. (*Kicheko/Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Hawa Ghasia baadaye Mheshimiwa Jitu Soni.

**WABUNGE FULANI:** Chegeni, Chegeni, Chegeni, Chegeni. (*Makofi*)

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa juhudini kubwa sana anazozifanya katika kuhakikisha kwamba tunaingia katika uchumi wa viwanda na tunakua kibashara na tunaweka mazingira mazuri ya biashara. Niiombe Wizara ya Viwanda na Biashara na Serikali kwa ujumla, tupunguze muda wa majadiliano pale ambapo tunapata wawekezaji katika miradi yetu mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti wakati napitia wakati napitia kitabu cha hotuba ya bajeti malengo ya karibu kila idara, nilikuwa naangalia *NDC*, kila unapoangalia ni kuendelea na

majadiliano. Nimechanganyikiwa zaidi pale ambapo nimekuja kuangalia Mradi wa Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya bajeti ya mwaka jana walikuwa wameshafika eneo nzuri kabisa ambako mwaka huu nilikuwa na matumaini kwamba labda mradi tungeambiwa sasa hivi unakaribia kutekelezwa. Nilichokiona katika kitabu cha hotuba ni kwamba baada ya kuwa tumepitisha ile Sheria ya Kulinda Maliasili zetu inayonyesha majadiliano ya Liganga na Mchuchuma yameanza upya. (*Makofii*)

**WABUNGE FULANI:** Uuuu.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaenda mbele, tunarudi nyuma. Kwa kweli inasikitisha sana, kama majadiliano haya yangekuwa yamekwisha kwa wakati, nina uhakika kabisa *SGR* hii inayojengwa tungejenga kwa kutumia chuma cha Liganga na Mchuchuma badala ya chuma ya kutoka Japan. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Mradi wa Reli kutoka Mtwara kwenda Mbambabay na matawi kwenda Liganga na Mchuchuma. Wawekezaji wengi sana wameonyesha nia ya kujenga reli hii kwa njia ya *PPP* lakini wote wanavutiwa na makaa ya mawe na chuma iliyoko Liganga na Mchuchuma. Kama majadiliano hayataisha watafanya wale ambao wanahamu ya kujenga reli hii waondoshe ile hamu yao kwa sababu kila siku ni kujandiliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NDC* watuambie wamekwama wapi kwenye Mradi wa Liganga na Mchuchuma. Mimi nakusudia kutoa shilingi kwa sababu mradi huu ukiendelea ndiyo utaifanya Bandari ya Mtwara ifanye kazi vizuri zaidi na hata Mji wa Mtwara uwe wa viwanda kwa sababu hiyo chuma na makaa ya mawe yatawezesha *SEZ* au *EPZA* ya Mtwara kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majadiliano yanaendelea ya Kiwanda cha Mbolea kule Msanga Mkuu, huu unaingia

zaidi ya mwaka wa sita majadiliano yanaendelea. Mimi napenda kujua au Waziri wa Viwanda na Biashara au Waziri wa Fedha wakija watuamble hivi wenzetu Rwanda wao wanajadiliana kwa kwa stahili ipi ambapo anaweza akaja mwekezaji ndani ya siku tatu wameshamaliza kujadiliana, wameshakubaliana, wameshasaini mikataba na sisi haswa hicho tunachokwama ni kitu gani? Au hao wanaojadiliana wanalipwa vizuri sana, kwa hiyo, majadiliano wamefanya ni sehemu ya maisha? Hebu tuangalie suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie eneo la biashara, siyo siri sasa hivi Kariakoo kumekufa. Kariako ilikuwa inapokea wafanya biashara kutoka Congo, Zambia, Malawi, Zimbabwe mpaka Uganda, sasa hivi Watanzania tunaenda Uganda kununua bidhaa ambazo zimepita katika bandari yetu. Niiombe Serikali iangalie kuna nini kinachoua Kariakoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo siri ukienda Kariakoo maduka mengi yamefungwa na hata ukitaka banda leo Kariakoo unapata wakati zamani kupata banda Kariakoo ilikuwa ni shida. Sasa kama Serikali tujulize ni nini kimewakimbiza majirani zetu kuja kufanya biashara Kariakoo kwa sababu Karikao ilikuwa ndiyo Dubai ya Afrika Mashariki na Afrika ya Kati. Ni kitu gani sasa kinachowafanya watu waende Uganda wakimbie Kariakoo? Namuomba Waziri wa Viwanda na Biashara alifanye kazi suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine ni vizuri tu Serikali ikapokea ushauri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Kama tutakumbuka wakati tunapitisha Sheria ya Manunuzi, Kamati ya Bajeti ilikuja na mapendekezo ya kuweka kipengele cha kutumia *force account* kwenye miradi yetu, kwenye Kamati Serikali ililikataa pendekezo hilo na Kamati ikalazimika kuja kulileta pendekezo ndani ya Bunge na bahati nzuri pendekezo lili坑ita. Sasa hivi *force account* ndiyo inayotuwezesha kujenga vituo vya afya, hospitali zetu na miradi mingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaakoni ilipita kwa kutumia nguvu za ziada hapa na sasa hivi tumesahau ilipitpitaje lakini manufaa makubwa tunayapata kwa kwa

kutumia *force account* ambayo ilipita kwa shida sana ndani ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna taasisi na kodi nyingi katika biashara zetu. Sasa hivi ukiwa na kampuni yako unatakiwa ulipe *PAYE*, *Workers Compensation* na *SDL*, kwa nini hii kitu isije ikalipwa kwa wakati mmoja? Sasa hivi ukishalipa *PAYE* atakuja mtu wa *Workers Compensation* kwa wakati wake, atakuja mtu wa *SDL* kwa wakati wake, atakuja *OSHA* kwa wakati wake, atakuja *TFDA* kwa wakati wake, yaani unasikia *pressure* inapanda na kichwa kinauma. Kwa nini wasije kwa wakati mmoja halafu unalipa wenyewe wakaenda kugawana huko kwa sababu kila mtu chake kinajulikana? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ndiyo vinavyokwamisha biashara zetu na pia ndivyo vinavyokwamisha uwekezaji katika nchi yetu, ni ugumu katika ufanywaji wa biashara. Hata kuandika tu zile *return* za *VAT* kwa wakati wake, *SDL* kwa wakati wake, *PAYE* kwa wakati wake, *Workers Compensation* kwa wakati wake, navyo vinachosha na vinatia ugumu katika kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja lakini lille la Liganga na Mchuchuma lenyewe tutalijua kesho, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Ghasia. Tunamalizia na Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kunipa fursa ya kuchangia leo lakini pia nipongeze kwa jitihada mbalimbali zinazoendelea kufanywa na Serikali kuboresha sekta nzima hii ya ufanyaji biashara lakini pia kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote hapa huwa nasema pasipokuwa na *coordination*, namna ya kuhakikisha kwamba Wizara mbalimbali zinafanya kazi kwa pamoja,

suala la viwanda na biashara itakuwa ni ndoto. Kwa hiyo, ni muhimu sana Serikali ikae kama timu mojo, Wizara na Wizara ziwasiliane na kama kuna jambo lolote washirikiane kuhakikisha jambo hilo wanalitatau kwa pamoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nydingi hapa tutakuwa tunalaumu labda Wizara ya Fedha kwamba kodi ni kubwa, lakini kodi zao ni tatu tu, ukiangalia tatizo kubwa ni *regulatory authorities* kuhusiana na tozo, ada na ushuru mbalimbali zinazoenda kwenye Wizara zote. Ukiona mmoja sasa hivi anasemwa kwenye Wizara yake atanyamaza lakini wengine wote wanabaki kusubiri yale mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kumekuwa na mtindo ili Wizara fulani ionekane imekusanya mahuhuli makubwa na mengi wanapiga *fine* za ajabuajabu. Mimi nashauri zile za *fine* mngeziweka pembeni, isilsabiwe, ikipigwa *fine* iende kwenye Mfuko Mkuu isiingie kwenye hesabu ya Wizara hiyo, kwenye Wizara ibaki ile ambayo ni jukumu lake, ndiyo tutaona Wizara na hizo taasisi zinafanya vizuri siyo kwenye *fine*, kwa sababu *fine* ndiyo inawabeba kwa sehemu kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimeshauri kwamba hizi *regulatory authorities* tuziunganishe pawe na *upper stream* na *lower stream*, zifanye kazi *under umbrella* ya Tanzania *Regulatory Authority* kwa sababu ndiyo zote zimebeba hizo tozo, ada, ushuru mbalimbali. Pia nashauri kwamba pawe na ukomo wa kukusanya tozo za miaka ya nyuma. Leo anakuja mtu wa *NEMC* anakudai ya miaka kumi nyuma, anakuja mtu wa *TFDA* anakudai ya miaka kumi nyuma, hivi siku zote walikuwa wapi? Kama hii ya *TRA* miaka mitatu mwisho, siku za nyuma wasiwe na mamlaka ya kudai kwa sababu kama walilala ni makosa yao siyo makosa ya huyo mfanyabiashara. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nilikuwa nimeshauri kwamba tuwe na *One Stop Center*, Afisa Biashara iwe ya Mkoa, Wilaya au Wizarani, mimi siwezi kujua sheria zote za *regulatory authority*, leseni na tozo mbalimbali ambazo

zinafika mpaka 40. Ni vizuri tukienda Afisa Biashara anielekeze kwamba nikikata leseni natakiwa niwe na vibali vyote hivi na mlipa huyo mtu mmoja *One Stop Center* kama mwingine amesahaulika hajajulikana, Serikali ndiyo itajua namna ya kufidia huko siyo mimi mfanyakabiashara. *Ease of Doing Business*, tukiweza urahisi wa kufanya biashara ndiyo njia pekee tutaweza kuwa na mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini namna ya kulinda viwanda vya ndani, ni lazima tuwe na mifumo ya kulinda viwanda vya ndani dhidi ya bidhaa zinazotoka nje au zinazozalisha nje. Mkumbuke hawa ndiyo wanaozalisha ajira, ndiyo wanalipa kodi isije ikafika mahali sisi ikawa ni sehemu ya kuleta bidhaa kutoka nje kama Dubai, wanachukua bidhaa kutoka dunia nzima wanachukua tozo ndogo wanafanya biashara, je, sisi tunataka tuwe hivyo? Sisi tunataka tuwe na viwanda na vifanye kazi na lazima tuwe na mifumo ya kulinda viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wenye viwanda na wenye biashara wanalamika wanalipa *SDL* lakini fedha hizo hazirudi kwenda kuwasaidia kuboresha kwa mfano *SIDO, TIRDO, CAMARTEC*. Mimi nasema ile asilimia 4.5 yote ingeenda huko zikaboresha *VETA* zetu na hizi taasisi zote ili wawe na fedha za kufanya utafiti na kuandaa wataalam ambao wataweba kuja kukusaidia katika masuala ya viwanda vyetu na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lazima tuunganishe uzalishaji, sehemu kubwa ya nchi yetu ni kilimo, mifugo na uvuvi. Tusipoangalia namna ya kuunganisha bidhaa zao hatutafanikiwa. Leo hii Serikali ifanye tathmini yake, miaka mitano nyuma na leo, sekta rasmi na sekta isiyokuwa rasmi ipi inakua, asilimia kubwa ya watu wameondoka kwenye sekta rasmi wanarudi kwenye sekta isiyokuwa rasmi kutokana na tozo, ada, kodi na ushuru mbalimbali ambapo Serikali itafika mahali haitakuwa inapata ushuru wala kodi ambayo inastahili kupata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia vyuo vyetu vya elimu viangalie namna ya kutoa elimu ambayo inalingana na uhitaji wetu ndani ya nchi. Pia bidhaa nyingi zinazokuja nchini ni *substandard* lakini tunalipa kwa bei ileile ya *standard*. Kwa hiyo, ni vizuri taasisi hizo ziweze kufanya kazi vizuri na tuangalie namna ya kuondoa huu rasimu uliopo ili tuweze kufanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tuweze kuangalia namna ya kuwekeza kwenye sekta ambazo zinazalisha kama kilimo, mifugo na uvuvi ili ziweze kuzalisha bidhaa za kutosha na kwa viwango ili tuweze kuwa na viwanda. Serikali ingefanya tathmini kwamba bidhaa tunazoagiza kutoka nje ya nchi nini ambacho tunaweza kuzalisha hapa nchini, moja ikiwa ni mchele, mafuta ya kula, sukari, mbegu bidhaa hizo zote tunaweza kuzalisha humu nchini kwa nini tusiwekeze huko ili watu wetu wapate ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijue kwamba siyo kila mahali lazima upate *direct tax* kwamba lazima upate kodi au ushuru. Inawezekana katika kiwanda kimoja Serikali haipati chochote pale lakini kinaajiri watu zaidi ya 10,000 au 20,000, tayari watu wakiwa na *spending power* yaani uwezo wa kununua bidhaa Serikali itakusanya kodi kubwa kuititia *indirect taxes*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wangeangalia kwenye tozo, kodi na ada wazipunguze ziweze kulipika na *compliance* itakuwa kubwa. Badala ya watu kuwa na tamaa ya kukwepa wakizipunguza gharama hizo watu wengi zaidi wataweza kulipa na Serikali itakusanya mapato makubwa lakini uzalishaji ndani ya nchi utakuwa mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunajitahidi kuondoa baadhi ya kodi kwa kupitia Sheria ya *Finance* lakini baadaye inarudishwa kupitia Kanuni. Mimi naomba suala hili la Kanuni kama Bunge hili litaridhia badala ya Waziri kuwa na mamlaka kupeleka moja kwa moja kutangaza kwenye Gazeti la Serikali haswa popote panapohusiana na kuongeza au kupunguza tozo mbalimbali iwe ni lazima iletwe Bungeni ama kwa kupitia

Kamati husika ili zisiruhusiwe kwenda kupandishwa kiholela kwa sababu tunaweza kuondoa kodi fulani hapa baada ya muda mfupi unakuta Waziri kule kwenye Kanuni anapandisha tozo hizo na kufanya wafanyabiashara kuendelea kupata tatizo na urahisi wa kufanya biashara unakuwa mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tungkuwa na mfumo wa kuangalia namna ya kufanya uratibu. Mimi nashukuru sasa tuna Waziri wa Uwekezaji na yeze kazi yake kubwa ni kuangalia urahisi wa uwekezaji wa ndani, wa nje, mkubwa au mdogo, yeze ndiye atakuwa sasa ndiyo mratibu wa shughuli zote kwenye biashara akisaidiana na Waziri wa Viwanda na Biashara lakini na Mawaziri wengine wote ili kuangalia wapi kuna changamoto na waweze kuleta mara moja kama ni sheria ibadilishwe lakini kama kwenye Kanuni wawaagize wale Mawaziri waziondoe ili urahisi wa kufanya uweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingeweze kana kwa miaka yote michango ya Wabunge ingeangaliwa kwenye *Hansard* walichangia nini na tukaletewa hapa, naamini kila mwaka tutaendelea kusema lakini yanayotekeleza ni machache. Lengo ni kuhakikisha kwamba tunapata mafanikio, nchi yetu iende mbele na fursa zote tunazo isipokuwa utaratibu wa kuhakikisha hizo fursa zinatumika vizuri ndiyo haufanyiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ndiyo kubwa kuliko zote ambapo ndiyo inasimamia biashara na masoko yote lakini pia kuendelea kukuza viwanda vikubwa na vidogo, ni jukumu lenu kushauriana na Wizara zingine zote kuweka mazingira wezesi ili Watanzania waweze kuwekeza. Siyo kwamba Watanzania wanashindwa kuwekeza, mitaji na uwezo wanao, jukumu lenu kukaa na kuhakikisha tunaweza kufanya shughuli hizo kwa unaafuu zaidi. Badala ya kuangalia maslahi ya watu wachache tuangalie maslahi ya wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, nashukuru na naunga mkono hojo. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jitu.

Waheshimiwa Wabunge, bado tuna majina ya wachangiaji kama matano lakini kutokana na muda basi tunaweza kuomba kesho kupitia vyama vyao wakaweza kumalizia kama itapatikana nafasi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nawashukuru na nawatakia kila la kheri, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne,  
Tarehe 15 Mei, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*